




# UCHANGANUZI WA UCHAKATAJAJI WA DATA

ZA

PROGRAMU ZA MIKOPO DIJITALI  
**BARANI AFRIKA**

KAGUZI WA NCHI 19



# UCHANGANUZI WA MBINU ZA UCHAKATAJAJI WA DATA ZA PROGRAMU ZA MIKOPO DIJITALI BARANI AFRIKA

UKAGUZI WA NCHI 19

**June 2022.**

Waandishi: 'Gbenga Sesan, Bonface Witaba, Dércio Tsandanaza, Jackline Akello, Steven Akomian  
Nakili Mhariri: Nana Nwachuckwu

Paradigm Initiative  
374 Borno Way  
Yaba  
Lagos, Nigeria  
[hello@paradigmhq.org](mailto:hello@paradigmhq.org)



Creative Commons  
Attribution 4.0 International (CC BY 4.0)



PARADIGM  
INITIATIVE



@ParadigmHQ

# Yällivomio

4  
6  
10  
19  
26  
36  
51  
60  
66  
79  
88  
98  
105  
110  
118  
112  
136  
149  
158  
164  
172

Utangulizi  
Angola  
Kameruni  
Kepuvede  
Kodivaa  
Misri  
Eswatini  
Uhabeshi  
Gabon  
Ghana  
Kenya  
Mali  
Moroko  
Msumbiji  
Namibia  
Naijeria  
Afrika Kusini  
Tanzania  
Uganda  
Zimbabwe  
Hitimisho

# Utangulizi

Kwa kuenea upesi kwa muundo msingi dijitali katika mataifa ya bara la Afrika, kumekuwa na ongezeko la ufikiaji wa intaneti. Kuondolewa kwa masharti ya kudhibiti huduma za mawasiliano ya simu husababisha ubunifu na ushindani na hatua hii husaidia kupungua kwa gharama za muunganisho wa mtandao, na kuongeza idadi ya watumiaji wa intaneti. Kutokana na suala hili, kushiriki maelezo, ikiwa ni pamoja na data ya binafsi, kumerahisishwa kuenea zaidi. Kurahisishwa kwa jambo huja na masuala ya utumiaji mbaya wa haki ya kufikia data ya binafsi na makampuni, wizi wa utambulisho na watu, mashambulizi mahususi yenye nia mbaya kwa kutumia maelezo yanayoweza kumtambulisha mtu. Muungano wa Ulaya (European Union) ulishughulikia masuala haya kuhusu usalama wa data ya binafsi kwa kutunga Sheria ya Jumla ya Ulinzi wa Data (General Data Protection Regulation (GDPR)).

Ulimwenguni kote, imechochea nchi nyingi kutunga sheria madhubuti za ulinzi wa data na kubuni mamlaka za ulinzi wa data.

Ingawa nchi 32 barani Afrika zimetunga sheria za ulinzi wa data<sup>1</sup>, nchi za hivi karibuni zikiwa ni Rwanda, Afrika Kusini na Kenya, baadhi ya mapengo yaliyopo yanayapa mashirika ya kiteknolojia ufikiaji usio wa haki wa data inayovuja kupitia mifumo ya ulinzi na utekelezaji wa sheria. Bila ulinzi wa kutosha wa data ya binafsi, mashirika mapya ya fedha yanatumia upatikanaji wa data hii kulenga watumiaji wa mtandao ambao ni wenyeji na wahamiaji wanaoweza kushawishika kwa urahisi na mikopo ya ‘kulipa siku ya kulipwa mshahara’. Mikopo hii huidhinishwa bila kufanywa kwa ukaguzi wa kina wa maelezo ya msingi ili kupata data ya binafsi, ikiwa ni pamoja na, wala si tu maelezo ya mwajiri,

orodha ya anwani za mawasiliano za simu n.k. Ukusanyaji wa madeni ya mikopo hii hutumia mbinu ya ‘kudhalilisha mtu hadharani’.

Shirika la Paradigm Initiative lilifanya utafiti kuhusu ulinzi wa data na programu za kukopesha pesa katika nchi kumi na tisa (19) za Afrika. Ripoti inaeleza kwa kina sheria za ulinzi wa data za nchi hizi, mianya ya ulinzi inayotumiwa na mifumo hili ya mikopo ya kupeana dijitali, na aina ya data ya binafsi inayopatikana na kukusanywa na mashirika haya ya programu za kukopesha pesa.

Katika nchi ambako utafiti ulifanywa, nchi 12 zina sheria za wastani za ulinzi wa data na zinatoa utaratibu dhahiri wa kisheria na kishirika wa kudhibiti data ya binafsi ilhali nchi 7 zilizosalia ziko katika mchakato wa kutunga sheria za ulinzi wa data au zinategemea sheria mahususi za sekta kwa udhibiti na uelekezaji. Jambo la kufurahisha, nchi kama vile Ghana na Naijeria hudhibiti sekta za teknolojia ya fedha kupitia sheria za benki na sheria za Benki Kuu (Central Bank) ambazo zinahitaji tekonomi hizo kupitia hatua na kanuni zilizowekwa za kutambuliwa rasmi. Suala la kuzingatiwa kwa data ya mteja halitiliwi maana zaidi na sheria hizo.

Programu hizi zisizo za kawaida za kukopesha pesa na huduma za fedha za simu za mikononi zilizofanyiwa utafiti, zilikusanya maelezo yanayoweza kumtambulisha mtu licha ya kiwango cha ruhusa zinazoruhusiwa na mtumiaji. Hata kwa kuwepo kwa sheria za ulinzi wa data katika nchi ambako utafiti ulifanywa, programu za simu za mikononi hupata njia za kukwepa maandishi ya sheria kwa kutumia neno ‘ruhusa za jumla’. Kulikuwa na matukio ambapo data ya mahali ya mtumiaji ilinekodiwa na programu ya kukopesha pesa

<sup>1</sup> Shirika la Paradigm Initiative na Olumide Babalola LP. Mamlaka za Ulinzi wa Data (Data Protection Authorities (DPA) Barani Afrika: Ripoti kuhusu kuanzhishwa, uhuru, uadilifu na ufanisi wa mamlaka za usimamizi wa ulinzi wa data katika miongo miwili ya kuwepo kwake barani. (2021)

kwa njia ya simu bila ruhusa wala ufahamu. Programu hizi hushiriki maelezo yanayoweza kumtambulisha mtu ikiwa ni pamoja na data ya mahali na wahusika wengine bila chaguo la mtumiaji kujiondoa katika hali hii ya kushiriki maelezo. Programu hizi hazielezi muda ambao data hii hushirikiwa na wahusika wengine. Programu hasidi iliyofichwa kwenye programu zingine huidhinisha kiotomatiki malipo ambayo hayajaidhinishwa kwa niaba ya watumiaji na kuiba maelezo nyeti ya binafsi na kifedha pia. Nchi zilizo na mbinu madhubuti za udhibiti kama vile Angola, ziliweza kufunga biashara za baadhi ya Programu kama vile programu ya kukopesha pesa ya Xikhila.

Kitu kimoja ni wazi kutoka kwenye utafiti: ingawa programu za kukopesha pesa kwa njia ya simu hubainisha maelezo zinazokusanya, maelezo haya si bayana kwa kiwango cha kuweka sahihi na mara nyingi hufichwa katika maandishi madogo. Pia, kuna maelezo machache mno au hakuna maelezo yoyote

kuhusu kiwango cha ufikiaji au udhibiti ambao mtumiaji anao kuhusu data yake iliyohifadhiwa. Ni muhimu kwa Mamlaka za Ulinzi wa Data (Data Protection Authorities) katika nchi mbalimbali kuzingatia kosa la utumiaji mbaya wa data linaloendelezwa kwenye programu za mikopo dijitali ili kuchukua hatua inayofaa ili kulinda wamiliki wa data, na kushirikiana pia na wadau wengine ili kutoa uhamasisho unaohitajika zaidi kuhusu ulinzi wa data.

# Angola



## Maelezo ya Nchi

Ikiwa inapatikana katika eneo la Kusini mwa Afrika, Angola ni nchi inayotumia lugha ya kireno iliyo na idadi inayokadiriwa ya watu milioni 31<sup>2</sup> na kadirio la GDP la bilioni 208.034 kufikia mwaka wa 2019. Nchi hii ya Kusini mwa Afrika inayotumia lugha ya Kireno ilipata uhuru wake kutoka kwa Ureno mwaka wa 1975.<sup>3</sup>

Rais wa sasa, João Lourenço, alichaguliwa mwaka wa 2017, baada ya kuongozwa kwa zaidi ya miaka 30 na Rais wa zamani, José Eduardo dos Santos.

<sup>2</sup> Takkumu za nchi ya Angola, World Bank <https://data.worldbank.org/country/AO> > ilifikiwa tarehe 15 Agosti 2021.

<sup>3</sup> Barrow Munslow, 'Angola: Siasa za Maendeleo Yasiyo ya Kudumu' (1999) 20(3) Third World Quarterly 551-568.

## Ulinzi wa Data Nchini Angola

Kulingana na DLA Pipen,<sup>4</sup> Angola hudhibiti masuala ya ulinzi na faragha ya data chini ya Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Law (Sheria nambari 22/11, tarehe 17 Juni 2011),<sup>5</sup> Sheria ya Huduma za Muungano wa Habari na Mawasiliano ya Kielektroniki (Electronic Communications and Information Society Services Law (Sheria nambari 23/11, tarehe 20 Juni 2011)<sup>6</sup>, na Sheria ya Ulinzi wa Mitandao na Mifumo ya Habari (Protection of Information Systems and Networks Law (Sheria nambari 7/17, tarehe 16 Februari 2017).<sup>7</sup>

Madokezo ya Mwongozo wa Data (Data Guidance)<sup>8</sup> yanabainishwa kuwa Amri ya Rais (Presidential Decree) ya 214/16 ya tarehe 10 Oktoba 2016 inabainisha kanuni ambazo zinasimamia muundo na utendakazi wa mamlaka ya usimamizi, Shirika la Ulinzi wa Data (Data Protection Agency (APD) la kitaifa.<sup>9</sup> Angola imetunga pia Sheria ya 11/20 ya tarehe 23 Aprili 2020 kuhusu Utambulisho na Data ya Mahali ya Simu za Mkononi (Identification and Location of Cellular Phones)<sup>10</sup>, na Upelelezi wa Kielektroniki (Electronic Surveillance)<sup>11</sup> unaofanywa na

<sup>4</sup> <https://www.dlapiperdataprotection.com/index.html?t=law&c=AO> > ilifikiwa tarehe 15 Agosti 2021.

<sup>5</sup> [https://platform.dataguidance.com/sites/default/files/lei\\_de\\_proteccao\\_de\\_dados\\_pessoais\\_v.pdf](https://platform.dataguidance.com/sites/default/files/lei_de_proteccao_de_dados_pessoais_v.pdf) > ilifikiwa tarehe 15 Agosti 2021.

<sup>6</sup> [https://minttcs.gov.ao/fotos/frontend\\_10/gov\\_documentos/lei\\_das\\_comunicacoes\\_electro\\_19324146535f1886da78b9b...s\\_sociedade\\_da\\_informacao.pdf](https://minttcs.gov.ao/fotos/frontend_10/gov_documentos/lei_das_comunicacoes_electro_19324146535f1886da78b9b...s_sociedade_da_informacao.pdf) > ilifikiwa tarehe 15 Agosti 2021.

<sup>7</sup> [https://minttcs.gov.ao/fotos/frontend\\_10/gov\\_documentos/redes\\_e\\_sistemas\\_informaticos\\_20864175955f109a14374be.pdf](https://minttcs.gov.ao/fotos/frontend_10/gov_documentos/redes_e_sistemas_informaticos_20864175955f109a14374be.pdf) > ilifikiwa tarehe 15 Agosti 2021.

<sup>8</sup> <https://www.dataguidance.com/notes/angola-data-protection-overview> > ilifikiwa tarehe 12 Agosti 2021.

<sup>9</sup> <https://apd.ao/ao/> > ilifikiwa tarehe 13 Agosti 2021.

<sup>10</sup> [https://apd.ao/fotos/frontend\\_1/editor2/200420\\_lei\\_11-20\\_de\\_23\\_abril-identificacao\\_ceular\\_vigilancia\\_electronica.pdf](https://apd.ao/fotos/frontend_1/editor2/200420_lei_11-20_de_23_abril-identificacao_ceular_vigilancia_electronica.pdf) > ilifikiwa tarehe 13 Agosti 2021.

<sup>11</sup> [https://apd.ao/fotos/frontend\\_1/editor2/200222\\_lei\\_2-20\\_de\\_22\\_janeiro-videovigilancia.pdf](https://apd.ao/fotos/frontend_1/editor2/200222_lei_2-20_de_22_janeiro-videovigilancia.pdf) > ilifikiwa tarehe 13 Agosti 2021.

Polisi (Police Authorities).

Angola ina kampuni tatu za huduma za simu za mkononi, Movicel, Unitel na kampuni inayomilikiwa na serikali ya Angola Telecom, ambayo ilikuwa ni kampuni ya pekee ya kutoa huduma za simu za mkononi hadi mwaka wa 2005.

Kiwango cha muunganisho wa Intaneti nchini Angola ni 31%, ilhali idadi ya watumiaji wa simu za mkononi ni zaidi ya watumiaji milioni 15, idadi inayowakilisha 46% ya jumla ya idadi ya watu.

<sup>12</sup>

Ripoti ya Freedom on the Net 2020<sup>13</sup> inakadiria "Hali ya uhuru wa Intaneti" ya taifa la Angola kama "huru kwa kiwango fulani."<sup>14</sup>

Hakuna vizuizi vya serikali kuhusu ufikiaji wa Intaneti. Kando na maudhui ya ponografia ya watoto na nyenzo zinazolindwa na hakimiliki, serikali haizui au kuchuja maudhui ya Mtandaoni. Hakuna vizuizi kuhusu aina ya maelezo ya kushirikiwa mtandaoni.

## Mfumo wa Fedha na Teknolojia ya Fedha Nchini Angola

Mfumo wa Fedha na Teknolojia za Fedha Nchini Angola

Benki Kuu ya Angola (National Bank of Angola (BNA) ni shirika kuu ambalo hudhibiti sekta ya fedha nchini Angola. Kuhusu shughuli za kutuma na kupokea pesa kidijitali, suala la kuangaziwa ni Sheria ya Uzuiaji na Kupambana na Ulanguzi wa Pesa (Law for the Prevention and Combat of Money Laundering), Ufadhilli wa Shughuli za Kigaidi (Terrorist Financing), na Uenezaji wa Silaha za Maangamizi Makubwa (Proliferation of Weapons of Mass Destruction).<sup>15</sup> Inaeleza kwamba mashirika ya fedha ambayo yanaruhusu shughuli za kutuma na kupokea pesa kupitia benki/uhawilishaji wa pesa yanapaswa kujumuisha maelezo yaliyothibitishwa ipasavyo kwenye ujumbe au fomu ya malipo inayoambatana na shughuli ya kutuma pesa, ikijumuisha jina kamili, nambari ya benki, anwani, na panapohitajika, jina la shirika linalotuma pesa. Kuna masharti machache kuhusu programu za simu kama vile Xikila Money.

Tarehe 26 Julai 2021, shirika la AllAfrica liliripoti<sup>16</sup> kwamba Angola ilikuwa imeibuka kama nchi inayoweza kuathiniwa kwa urahisi zaidi kwa sababu wahalifu wa mtandaoni wataalamu duniani kote wanalenga idadi ya watu inayozidi kuongezeka ya watumiaji wa simu za mkononi barani Afrika. Kulingana na ripoti ya "State of Mobile Fraud in Africa",<sup>17</sup> Angola ni mojawapo ya nchi zinazowenza kuathiriwa kwa urahisi zaidi barani Afrika, ambapo asilimia 34 ya shughuli za kutuma na kupokea kupitia simu za mkononi ni za kutiliwa shaka.

The report also explained<sup>18</sup> kwamba programu hasidi zina programu fiche hatari na zimesanidiwa ili kufanya malipo kwa niaba ya watumiaji bila ufahamu wao.

Kuna pia tukio la kuteka mibofyo, ambapo mlaghia huzuia mbofyo halali na kumwelekeza mtumiaji bila kujua kwenye tovuti ya wizi. Tovuti hii inaweza kuiba maelezo nyeti ya fedha na maelezo mengine ya binafsi.

Shirika la Statista liliripoti<sup>19</sup> kwamba kufikia Machi 2021, shughuli milioni 29.4 za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya simu zilirekodiwa nchini Angola, ambalo ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na mwezi kama huo mwaka uliotangulia. Watu walitekeleza shughuli milioni 7.4

<sup>12</sup> Digital 2021 in Angola – Hootsuite <https://datareportal.com/digital-in-angola>, ilifikiwa tarehe 20 Mei 2021.

<sup>13</sup> Freedom House Angola <https://freedomhouse.org/country/angola/freedom-net/2020>, ilifikiwa tarehe 1 Juni 2021.

<sup>14</sup> Angola ilipata pointi 62/100 <https://freedomhouse.org/country/angola/freedom-net/2020> > ilifikiwa tarehe 14 Agosti 2021

<sup>15</sup> Sheria Nambari 05/2020 ya tarehe 27 Januari <https://www.bna.ao/uploads/%7B5ff3bf3f-eba6-4b79-94e4-f16d8a01e74c%7D.pdf> > ilifikiwa tarehe 12 Agosti 2021

<sup>16</sup> <https://allafrica.com/stories/202107260738.html> > ilifikiwa tarehe 13 Agosti 2021.

<sup>17</sup> <https://www.techfinancials.co.za/2021/07/26/mobile-fraud-continues-to-hit-africa-hard/> > ilifikiwa tarehe 15 Agosti 2021.

<sup>18</sup> <https://www.bizcommunity.africa/Article/410/793/218325.html> > ilifikiwa tarehe 15 Agosti 2021.

<sup>19</sup> <https://www.statista.com/statistics/1228848/number-of-transactions-with-mobile-banking-in-angola/> > ilifikiwa tarehe 15 Agosti 2021.

za kutuma na kupokea pesa kupitia benki kwa kutumia simu ya mkononi mwezi wa Machi 2020 kwenye App Multicaixa Express, iliyozinduliwa mwaka wa 2019. Baada ya kuweka kadi moja au zaidi za benki kwenye Programu, mtumiaji anaweza kutumia simu ya mkononi kufanya malipo ya mtandaoni, ununuzi na kutuma na kupokea pesa.

## **Xikila Money: Programu ya Simu za Mkononi ya Kukopesha Pesa**

Ikiwa ilizinduliwa mwaka wa 2017 na shirika la Banco Postal,<sup>20</sup> Xikila Money ulikuwa mfumo ulioruhusu kutumia simu ya mkononi kama pochi dijitali na, kwa msingi huo kufanya malipo mbalimbali kupitia simu ya mkononi. Programu hii hutumia simu za mkononi kama akaunti za benki ili kufanya shughuli za kifedha na kukopesha pesa.<sup>21</sup> Ili kuanza kutumia huduma ya Xikila Money, unahitaji kufungua akaunti katika tawi la shirika la Xikila Money na kuweka pesa kwenye akaunti. Programu hii inapatikana kwa watumiaji wa vifaa vya Android na iOS.<sup>22</sup>

## **Kusimamishwa kwa huduma za Programu**

Mfumo huu ulionekana kuwa umefaulu nchini Angola. Katika ripoti ya habari iliyochapishwa mwaka wa 2017,<sup>23</sup> shirika la Angola Journal lilitaja kuwa Programu hiyo tayari ilikuwa imefikisha wateja 100,000 ndani ya miezi saba na kuongeza idadi ya zaidi ya akaunti 40,000 ndani ya miezi miwili tu. Hata hivyo, uamuzi uliofanywa na Benki Kuu ya Angola (Central Bank of Angola (BNA) ulibadilisha mambo mwaka wa 2019.

Sababu kuu iliyotangazwa na BNA ilikuwa ni shirika la Banco Postal kushindwa kutii sera ya fedha ya urahisi wa hisa au mali kubadilishwa katika pesa taslimu inayohitajika ili kufanya kazi nchini Angola.<sup>24</sup> Shirika la Banco Postal lilikuwa na matawi 200 ya nchini ya mtandao wa huduma ya Xikila Money katika jiji kuu la Luanda, na jiji la Huambo<sup>25</sup> na benki hiyo ilidai kuwa na zaidi ya wateja 250,000 kabla ya kufungwa. Kwa sasa, tovuti ya Xikila Money haifanyi kazi tena.<sup>26</sup>

## **Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali**

Xikila Money	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	Kwa sababu programu hiyo ilihuushwa na Benki, moja ya ruhusa kuu iliyohitajika ilikuwa kitambulisho cha binafsi cha mteja na historia yake ya shughuli za kifedha.
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Kusoma hali ya simu na utambulisho Data ya mahali pasipo mahususi (inayotokana na mtandao) Data ya mahali mahususi (inayotokana na GPS na mtandao) Kutafuta akaunti zilizo kwenye kifaa Kusoma anwani za mawasiliano za mtumiaji Kutafuta akaunti zilizo kwenye kifaa

20 https://www.menosfios.com/conheca-xikila-money-um-servico-permite-efectuar-pagamentos-via-mobile/ > ilifikiwa tarehe 11 Agosti 2021.

21 Xikila Money – mabadiliko mapya ya huduma ya fedha yabadilisha muundo wa huduma za benki nchini Angola https://www.youtube.com/watch?v=PW392kJVm7w > ilifikiwa tarehe 14 Agosti 2021.

22 https://play.google.com/store/apps/details?id=tagattitude.mwallet.app.xikila na https://appadvice.com/game/app/xikila-money/1261392972 > ilifikiwa tarehe 14 Agosti 2021.

23 https://www.jornaldeangola.ao/ao/noticias/detalhes.php?id=393253 > ilifikiwa tarehe 14 Agosti 2021.

24 https://novojornal.co.ao/sociedade/interior/bna-tambem-fechou-o-xikila-money-um-servico-bancario-inovador-em-angola-e-de-utilidade-confirmada-pelos-utilizadores-65247.html > ilifikiwa tarehe 16 Agosti 2021.

25 Ripoti ya habari https://sol.sapo.pt/artigo/650953/joao-loureiro-limpa-sistema-bancario > ilifikiwa tarehe 12 Agosti 2021.

26 http://www.xikilamoney.co.ao/ > ilifikiwa tarehe 14 Agosti 2021.

	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Kupokea data kutoka kwenye Intaneti Kuangalia miunganisho ya mtandao Kufikia mtandao kikamilifu Kufunga programu zingine Kudhibiti mtetemo Kuzuia kifaa kuingia katika hali tuli
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kusoma hali ya simu na utambulisho Kuangalia miunganisho ya Wi-Fi Kunekodi sauti – Programu inahitaji Maikrofoni ili kuthibitisha shughuli za kifedha kwa usalama
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Maelezo ya kitambulisho Akaunti ya benki Shughuli za fedha unazofanya na watumiaji wengine

Kubatilishwa kwa leseni ya Postal Bank na kupigwa marufuku kwa programu ya Xikila Money kunatuzuia kufanya uchanganuzi zaidi. Hata hivyo, tuliweza kutambua kupitia Google Play kuwa Programu hiyo ilisasishwa mara mwisho mwezi wa Mei 2018, karibu mwaka mmoja kabla ya kupigwa marufuku na serikali ya Angola, hasa kwa sababu sheria na masharti ya matumizi yanayopaswa kuwa na sera ya faragha hayaweza kufikiwa.<sup>27</sup> Kwa upande mwingine, hali ya ukosefu wa tovuti haikuruhusu kupata data zaidi kuhusu jinsi wahusika wengine huthibitisha vidakuzi au kufuatilia maelezo ya mtumiaji.

Ingawa iliendelea kuwa sokoni nchini Angola kwa muda mfupi, huduma ya Xikila Money ilikuwa njia mpya ya kusambaza fedha nchini Angola. Kutokana na maelezo yaliyokusanywa kutoka kwenye kilichobaki kuwa kama programu hiyo, tunatambua idadi kubwa ya data iliyokusanywa kutoka kwa watumiaji wake. Jambo muhimu la kuzingatia ni Shirika la Ulinzi wa Data kutotoa taarifa yoyote wakati huduma ya Xikila Money ilipokuwa inafanya kazi nchini. Hakuna rekodi yoyote inayoonyesha kuwa DPA iliwhi kutoa maoni yoyote kuhusu jinsi Programu hiyo ilivyokusanya na kutumia maelezo ya wateja.

Kwa mfano, mojawapo ya tatizo kuu ambalo bado lipo hadi sasa ni kuwa baadhi ya wateja na wafanyakazi walipoteza akaunti zao na bado wanasubiri kufidiwa na shinika la Banco Postal.<sup>28</sup> Kifungu cha 16 cha Sheria ya Ulinzi wa Data kinaeleza kuwa “uchakataji wa data ya binafsi kuhusiana na mkopo na uwezo wa kulipa madeni unaweza tu kutekelezwa kwa ruhusa ya mmiliki wa data na kwa idhini ya Shirika la Ulinzi wa Data.” Hata hivyo, hili halikutendeka, na wateja wa Xikila Money bado hawafahamu kitakachotendeka kwa data yao baadaye baada ya kupigwa marufuku kwa shinika la Banco Postal.

<sup>27</sup> <http://www.xikilamoney.co.ao/TermosUtilizacao > ilifikiwa tarehe 17 Agosti 2021>.

<sup>28</sup> <https://www.novagazeta.co.ao/artigo/1186 / https://valoreconomico.co.ao/artigo/80-dos-trabalhadores-do-extinto-banco-postal-continuam-no-desemprego > ilifikiwa tarehe 17 Agosti 2021>.

# Kameruni



## Maelezo ya Nchi

Ikiwa inapatikana katika eneo la Katikati mwa Afrika, Kameruni, au Jamhuri ya Kameruni, ina idadi ya watu 25,876,380<sup>29</sup>. Inapakana na Naijeria, Chad, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Kongo, Gabon, Ginekweta (Equatorial Guinea), na lango la bahari kwenye Ghuba ya Gine (Guinea). Lughu mbili rasmi: Kifaransa na Kiingereza, zinatumika huko. GDP yake inakadiriwa kuwa Dola za Marekani bilioni 39.01 (2019) na inawakilisha zaidi ya 40% ya Jumuiya ya Fedha na Uchumi ya Afrika ya Kati (Economic and Monetary Community of Central Africa), ambapo ni mwanachama. Ina mfumo wa uongozi wa urais.

<sup>29</sup> countryeconomy.com. 2022. Kameruni. [mtandaoni] Inapatikana katika: <<https://fr.countryeconomy.com/pays/cameroun>> [ilifikiwa tarehe 11 Februari 2022].

## Ulinzi wa Data Nchini Kameruni

Nchi ya Kameruni haina utaratibu mahususi wa kisheria unaofuatwa ili kulinda data ya binafsi. Ikiwa bado inasubiri kutungwa kwa sheria na kuteuliwa kwa mamlaka huru inawajibika na masuala ya ulinzi wa data ya binafsi, ni huduma ya mawasiliano ya kielektroniki na soko la ICT ndivyo tu vinavyodhibitiwa. Sheria za udhibiti zinazotokana na maandishi yafuatayo:

- Sheria nambari 2010 / 012 ya tarehe 21 Desemba 2010, inayohusiana na usalama na uhalifu wa mtandaoni,
- Sheria nambari 2010 / 013 ya tarehe 21 Desemba 2010, inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki,
- Sheria nambari 2010/021 ya tarehe 21 Desemba 2010, inayosimamia biashara za kielektroniki,
- Sheria nambari 2006/018 ya tarehe 29 Desemba 2006, inayosimamia matangazo, na
- Sheria nambari 2011/012 ya tarehe 6 Mei 2011, inayohusu ulinzi wa mteja.
- Katika kiwango cha udhibiti, Amri nambari 2013/0399 / PM ya tarehe 27 Februari 2013 inabainisha sheria na masharti ya kulinda watumiaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroniki.
- Nchi ya Kameruni imeidhinisha Mapatano ya Umoja wa Afrika (AU) kuhusu Usalama wa Mtandaoni na Ulinzi wa Data ya Binafsi ya tarehe 27 Juni 2014, katika kiwango cha bara.
- Na katika kiwango cha jamii, Kameruni inatumia Amri Nambari 07/08-UEAC-133-CM-18 and Sheria Nambari 03/16-CEMAC-UMAC-CM of December 21, 2016, inayohusiana na mifumo na matukio ya malipo ambayo inashughulikia maswali yanayohusiana maelezo ya binafsi yanayokusanya wakati wa mawasiliano, shughuli za fedha zinazohusiana na

huduma mbalimbali za mawasiliano ya kielektroniki.

Shirika la Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (Telecommunications Regulatory Agency (ART)<sup>30</sup> na Shirika la Kitaifa la Teknolojia za Habari na Mawasiliano (National Agency for Information and Communication Technologies (ANTIC)<sup>31</sup> hudhibiti sheria hizi tofauti.

Bado, kuna pengo kubwa katika kuchukua hatua kuhusu ulinzi wa data ya binafsi ya kompyuta. Kweli, ulinzi wa data ya binafsi ya kompyuta unaotekelawa na ART unaonekana kuwa hatua katika dhamira yake ya usimamizi na unaendelea kushughulikia tu sekta ya mawasiliano ya simu, ambayo si sekta ya pekee ambapo data ya binafsi inaweza kudhibitiwa. ANTIC inapata mwanzo wake katika sheria kuhusu mawasiliano ya kielektroniki, ingawaje sheria imebainisha sehemu yake ya udhibiti wa usalama na uhalifu wa mtandaoni.

Uchanganuzi wa dhamira hizi unaonyesha kwamba zinashughulikwa ulinzi wa data ya binafsi ya kompyuta katika kazi zake pana. Hata hivyo, kwa kuchunguza kwa ukaribu, dhamira hizi hazibainishi kazi mahususi ya ANTIC katika ulinzi wa data ya binafsi. Sheria kuhusu usalama na uhalifu wa mtandaoni ya mwaka wa 2010 inashughulikia tu ulinzi wa data ya binafsi katika kiwango cha uhalifu. Kizuizi hiki kimewekwa kwa sababu ni vigumu kuingilia kati iwapo shughuli yenye utata inayohusiana na ulinzi wa data binafsi itatokea, kwa majaji wa makosa ya uhalifu na wa mahakamani<sup>32</sup>. Mchakato huu unaodhibitiwa unaonyesha matumizi mabaya katika uchakataji wa data ya binafsi nchini Kameruni.

## **Utangulizi**

Ukuaji ambao karibu ni wa jumla wa Huduma za Kutuma na Kupokea Pesa Kupitia Simu (Mobile Money (MM) katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara (Sub-Saharan Africa (SSA) unatatizika kukua katika eneo la Afrika ya Kati<sup>33</sup>. Kulingana na ripoti ya mwaka wa 2019 kutoka kwa Muungano wa Kimataifa wa watumiaji wa simu za mkononi(GSMA), katika karibu idadi ya akaunti milioni 400 zinazotumika katika eneo la SSA, chini ya 10% zilipatikana katika eneo la Afrika ya Kati. Kameruni inaoongoza nchi zingine kuhusiana na suala la ukuaji wa huduma ya MM katika eneo hili. Kiwango chake cha ukuaji wa huduma ya MM ni 15%, na idadi ya shughuli husika za fedha iliwalilisha 76% kati ya FCFA bilioni 7,964 zilizopatikana mwaka wa 2018 katika eneo la Afrika ya Kati.

Kwa sababu ya shughuli za huduma ya MM, shughuli za fedha hutekelezwaa hasa na watoa huduma za simu za mkononi, ambao ni Orange Cameroon na MTN Cameroon.

Kampuni hizi mbili ambazo zinaoongoza katika soko la huduma za simu nchini Kameruni zilipata mapato ya jumla ya FCFA bilioni 500.3 katika mwaka wa 2020. Kulingana na Orange Cameroon, huduma ya Orange Money iliyoziinduliwa mwaka wa 2011 inawakilisha mapato ya jumla ya FCFA bilioni 9,600 kila mwaka, hiyo ni kumaanisha kuwa ni karibu mara mbili ya bajeti ya Taifa la Kameruni katika mwaka wa fedha wa 2021. Mwisho wa mwaka wa 2020, kampuni ya MTN Cameroon ilipata mapato ya jumla ya randi bilioni 1.73 (karibu FCFA bilioni 66). Watoa huduma hawa wawili hutoa shughuli za kuweka na kutoa pesa, kutuma pesa, kulipa bili, mishahara na shughuli zote zinazohusiana na malipo ya kibiashara n.k, kwa zaidi

30 Shirika la Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (ART) ni shirika la usimamizi la umma linalotambulika kisheria na linalojisimamia kifedha, liliobuniwa na sheria inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki. Kama shirika la usimamizi la umma, ART liko chini ya uchunguzi wa usimamizi wa Wizara ya Barua na Mawasiliano ya Simu (Ministry of Posts and Telecommunications (MINPOSTEL) na chini ya uchunguzi wa fedha wa Wizara ya Fedha (Ministry of Finance (MINFI). Kubuniwa kwake kunasimamiwa na Amri nambari 2012/092 na nambari 2012/180 ya Aprili 2012 kuhusu kubuniwa, mpangilio na utendakazi wa Shirika la Kitaifa la Teknolojia za Habari na Mawasiliano (National Agency for Information and Communication Technologies)

31 ANTIC ni shirika la usimamizi la umma linalotambulika kisheria na kujisimamia kifedha ambalo dhamira zake kuu ni kuhakikisha kwa niaba ya Serikali: kuendelezwa na kufuatiliwa kwa vitendo vya mamlaka za umma kuhusu masuala ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (Technologies Information and Communication (ICT); usimamizi, udhibiti na ufuatiliaji wa shughuli zinazohusiana na usalama wa mifumo ya habari na mitandao ya mawasiliano ya kielektroniki pamoja na uthibitishaji wa kielektroniki kwa kushirkiana na shirika la ART.

32 Kifungu cha 74 cha Sheria nambari 2010/012 ya tarehe 21 Desemba 2010 inayohusiana na usalama na uhalifu wa mtandaoni.

33 Eneo la Afrika ya Kati linaleta pamoja nchi 6 za Jumuiya ya Fedha na Uchumi ya Afrika ya Kati (Central African Economic and Monetary Community (CEMAC): Kameruni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Kongo, Gabon, Ginekweta (Equatorial Guinea) na Chad. Na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Democratic Republic of Congo (DRC ).

ya watumiaji milioni 20 wa simu za mkononi nchini Kameruni, kutoka kwenye akaunti zao kupidia huduma ya MM. Kwa kufahamu fursa iliyotolewa na soko hili, waliamua kuanza kutoa huduma za kupeana mikopo midogo. Kampuni ya Orange Money Cameroon, kwa hivyo, ilituma ombi la kuidhinishwa mwaka wa 2019 ili kukuza huduma zake kwa kuanza kutoa huduma ya kupeana mikopo midogo. Kampuni ya MTN Cameroon inakamilisha mbinu kama hiyo mwisho wa mwaka wa 2020. Teknolojia za fedha na kampuni za mfumo wa benki na biashara ambazo hazipatikani nchini Kameruni zinasimamia mikopo hii inayotolewa kupidia programu za simu za mkononi. Programu hizi ni Treoloans App<sup>34</sup>, Cameroon Direct Loan Hub<sup>35</sup> na Kiva<sup>36</sup>.

Katika mazingira ya uchumi mkubwa yasiyo na utaratibu mkuu wa usimamizi wa ulinzi wa data ya binafsi, kuenea kwa huduma hizi, zaidi ya manufaa yanayotarajiwa katika ujumuishwaji kwenye fursa za kupata fedha, kunaweza kusababisha matatizo ya faragha ya watumiaji wake. Swali ni iwapo mbinu za uchakataji wa data za programu hizi, kama inavyoelezwa katika sera na masharti yake ya matumizi, zinazingatia maslahi ya kuheshimu ulinzi wa faragha? Utafiti huu unalenga kuchanganua sera za faragha na sheria na masharti ya programu hizi na kuchunguza jinsi zinavyotii sheria mbalimbali zinazohusiana na ulinzi wa wateja (watumiaji) nchini Kameruni. Sehemu ya kwanza inajumuisha muhtasari wa data inayokusanywa na programu hizi.

Sehemu ya pili inachunguza shughuli zake za uchakataji kuhusiana na sheria mbalimbali zinazohusiana na ulinzi wa wateja. Sehemu ya mwisho inakamilika kwa kuonyesha iwapo programu hizi zinatii sheria inayolinda data ya binafsi au la.

## **Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali**

Programu ya TreoLoans <sup>37</sup>	Maelezo yanayokusanywa na kuchakatwa na programu
Kiungo cha kupakua: Google Play Store	

34 Programu ya Treoloans ni programu ya simu za mkononi ya kupata mikopo isiyo na dhamana ya kati ya FCFA 5,000 na 30,000 (karibu Dola 9 za Marekani) na kwa viwango vya riba ya kila mwezi vya kati ya 10% na 30% nchini Kameruni. Hutolewa kwa watu walio na akaunti za huduma ya MM zinazotolewa na watoa huduma za simu za mkononi amba ni Orange Money Cameroon na MTN Money Cameroon kuanzia Aprili 2019.

35 Cameroon Direct Loan Hub ni huduma ya EasyLoan ya mikopo ya kidijitali. Kwa kawaida, EasyLoan haikopeshi fedha zake lakini hutoa tu mfumo kwa watoa huduma za mikopo na waombaji kuwasiliana. Lengo lake ni kuondoa utaratibu wa kawaida wa shughuli za benki kati ya maajenti wanaohitaji ufadhilli na maajenti wenye uwezo wa kutoa ufadhilli.

36 Programu ya Kiva ni huduma ya Kiva US ya mikopo ya kidijitali.

Kiva ni mfumo wa kutoa mikopo kwa watu wengi amba unaruhusu watoa huduma za mikopo na waombaji kuuungana na kuwasiliana kwa urahisi. Lengo lake ni kuondoa utaratibu wa kawaida wa shughuli za benki kati ya maajenti wanaohitaji ufadhilli na maajenti wenye uwezo wa kutoa ufadhilli. Wateja wa huduma ya Kiva wanaweza kunaufaika na mikopo inayoanzia \$ 25. Kwa sasa, jumuiya ya huduma ya Kiva ina idadi ya hadi watu milioni 1.9 amba wamenufaika na huduma ya kutoa mikopo kwa watu wengi inayokadiriwa kuwa Dola bilioni 1.4 za mikopo iliyotolewa kwa waombaji milioni 3.4 katika zaidi ya nchi 90.

37 Sheria na Masharti ya Programu ya TreoLoans. Sera ya Faragha ya Programu ya TreoLoans inapatikana katika Sheria na Masharti.

	Ruhusa Zinazotakikana	<p>Unapowasha programu, Programu ya TreoLoans huomba: Kufikia data ya mahali mtumiaji alipo, data ya mahali mahususi (GPS na mtandao) na data ya eneo la karibu (mtandao).</p> <p>Kufikia kamera ili kupiga picha na kurekodi video</p> <p>Kufikia maelezo ya utambulisho wa mtumiaji na kutafuta akaunti zilizo kwenye kifaa cha mtumiaji</p> <p>Kufikia Picha / Maudhui anuai / Faili, kubadilisha au kufuta maudhui ya nafasi ya hifadhi ya USB na kucheza maudhui ya nafasi ya hifadhi ya USB.</p> <p>Kufikia nambari za simu za mtumiaji, kuangalia na kubadilisha anwani za mawasiliano, kutafuta akaunti zilizo kwenye kifaa na kupiga simu kwa nambari za simu moja kwa moja.</p> <p>Kufikia hifadhi, kubadilisha au kufuta maudhui ya nafasi ya hifadhi ya USB na kucheza maudhui ya nafasi ya hifadhi ya USB.</p> <p>Kufikia Maikrofoni na kurekodi faili ya sauti.</p> <p>Kufikia maelezo ya muunganisho wa Wi-Fi na kuangalia miunganisho ya Wi-Fi</p> <p>Kutekeleza vitendo fulani: kupokea data kwa kutumia muunganisho wa intaneti, kufunguka kifaa kinapowashwa, kuzuia kifaa kuingia katika hali tuli, kubadilisha mipangilio ya sauti, kuangalia miunganisho ya mtandao na kuwa na uwezo kamili wa kufikia mtandao</p>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Wakati wa kujisajili kwenye huduma ya mkopo, Programu ya TreoLoans hukusanya maelezo ya binafsi kuhusu mtumiaji bila kubainisha aina au ubora wa data hii.
	Maelezo Yanayokusanywa kutoka kwenye Kifaa cha Mtumiaji Maelezo yanayokusanywa kwa kutumia tovuti	<p>Programu ya TreoLoans hukusanya maelezo mbalimbali kuhusu kifaa cha mtumiaji bila kubainisha aina ya data hiyo.</p> <p>Programu ya TreoLoans haitoi maelezo yoyote kuhusu tovuti</p>
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Programu haitoi Maelezo yoyote kuhusu data inayokusanywa kutoka kwa wahusika wengine mbalimbali.
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Sera ya faragha ya Programu ya TreoLoans inaeleza kwamba inakusanya data ya mtumiaji kwa madhumuni mbalimbali ambayo hayajabainishwa katika sera yake ya faragha.

	Maelezo Yanayoshirikiwa na Wahusika Wengine Muda Ambao Data Inafikiwa na Wahusika Wengine	Programu ya TreoLoans inashiriki maelezo ya mtumiaji na wahusika wengine mbalimbali ambao hawajabainishwa katika sera yake ya faragha.  Sera ya faragha ya Programu ya TreoLoans inaeleza kwamba inashiriki maelezo na wahusika wengine bila kubainisha muda wa ufikiaji wa data waliopewa.
	Teknolojia za Ufutiliaji / Vidakuzi vya Tovuti	Sera ya faragha ya Programu ya TreoLoans na tovuti havitoi maelezo yoyote kuhusu matumizi ya vidakuzi.
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Sera ya Faragha ya Programu ya TreoLoans inaeleza kwamba wanachukua kila hatua ili kuhakikisha usalama wa data inayokusanywa kuhusu watumiaji. Hata hivyo, hawakutoa maelezo yoyote kuhusu muda wa kuhifadhiwa kwa data iliyokusanywa.
Cameroon Direct Loan Hub <sup>38</sup> Kiungo cha Nje cha Kupakua na Google Play Store	Maelezo yanayokusanywa na kuchakatwa na programu	
	Ruhusa Zinazotakikana	Unapoawasha programu, programu ya Cameroon Direct Loan Hub huomba: Kuangalia miunganisho ya mtandao na kupata uwezo kamili wa kufikia mtandao
	Maelezo Yanayokusanywa Kutoka kwa Mtumiaji	Sera ya faragha ya Programu ya Cameroon Direct Loan Hub haitoi maelezo yoyote kuhusu maelezo inayokusanya kutoka kwa watumiaji.
	Maelezo Yanayokusanywa Kutoka Kwenye Kifaa cha Mtumiaji	Sera ya faragha ya Programu ya Cameroon Direct Loan Hub haitoi maelezo yoyote kuhusu maelezo yanayokusanywa kwenye kifaa cha mtumiaji.
	Maelezo Yanayokusanywa Unapotumia Tovuti ya Cameroon Direct Loan Hub	Sera ya faragha ya Programu ya Cameroon Direct Loan Hub haitoi maelezo yoyote kuhusu maelezo yanayokusanywa kwenye tovuti yake. Kando na hayo, tovuti ya mto huduma za programu haiwezi kufikiwa.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Sera ya faragha ya Programu ya Cameroon Direct Loan Hub haitoi maelezo yoyote kuhusu maelezo yanayokusanywa kutoka kwa wahusika wengine mbalimbali.

Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Sera ya faragha ya Programu ya Cameroon Direct Loan Hub haitoi maelezo yoyote kuhusu madhumuni ya data inayokusanywa kutoka kwa watumiaji.
Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Sera ya faragha ya Programu ya Cameroon Direct Loan Hub haitoi maelezo yoyote kuhusu maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine.
Muda ambao data inafikiwa na wahusika wengine	Sera ya faragha ya Programu ya Cameroon Direct Loan Hub haitoi maelezo yoyote kuhusu muda ambao wahusika wengine wanaweza kufikia maelezo ya binafsi ya mtumiaji na muda ambao wanayahifadhi.
Teknolojia za Ufutiliaji / Vidakuzi vya Tovuti	Sera ya faragha ya Programu ya Cameroon Direct Loan Hub haitoi maelezo yoyote kuhusu matumizi ya "vidakuzi". Kando na hayo, tovuti inayohusishwa na programu haifanyi kazi.
Jinsi Programu inayohifadhi maelezo ya mtumiaji	Sera ya faragha ya Programu ya Cameroon Direct Loan Hub haitoi maelezo yoyote kuhusu usalama, usiri na muda wa kuhifadhiwa kwa data iliyokusanywa.

Kiva <sup>39</sup>	Maelezo yanayokusanywa na kuchakatwa na programu
Kiungo cha Kupakua: Google Play Store na Apple Store	Ruhusa Zinazotakikana Unapowasha programu, Programu ya Kiva huomba: Kupokea data kutoka kwenye Intaneti . Kuangalia miunganisho ya mtandao . Kupata uwezo kamili wa kufikia mtandao . Kuzuia kifaa kuingia katika hali tuli  Programu ya Kiva inahifadhi pia haki ya kuongeza maombi zaidi ya ruhusa za kiolesura chake.
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji Wakati wa kujisajili kwenye huduma ya mkopo, Programu ya Kiva hukusanya maelezo ya mtumiaji: jina la kwanza na la mwisho, picha, anwani ya barua pepe na anwani ya mahali, nambari ya simu, maelezo ya kampuni na fedha, mapendeleo ya kibinafsi, sheria na mashanti ya mkopo yanayopendelewa, akaunti ya malipo na baadhi ya maelezo ya takwimu, maelezo ya mitandao ya kijamii ya mtumiaji.

	Maelezo Yanayokusanya kutoka Kwenye Kifaa cha Mtumiaji  Maelezo Yanayokusanya Unapotumia tovuti ya Kiva	Programu ya Kiva hukusanya maelezo yafuatayo kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji: maelezo ya kifaa ikijumuisha aina ya simu ya mkononi na nambari ya simu data ya mahali mahususi inayotolewa na teknolojia ya GPS na huduma zingine za mahali Kitambulisho cha akaunti ya malipo ya mtumiaji  Mtumiaji anapotumia tovuti ya Programu ya Kiva kwenye simu yake ya mkononi, jina lake, anwani ya barua pepe na njia ya kuthibitisha akaunti ya mtumiaji (kwa mfano, nenosiri) hukusanya. Maelezo na maoni yanayochapishwa kwenye ukurasa mwengine wowote wa wavuti unaosimamiwa na Kiva (kama vile ukurasa wa mikopo, blogu, au jukwaa la watu wa kujitolea) au kupitia kipengele cha Kiva Lender Mail hukusanya pia.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine Programu hukusanya maelezo kutoka kwa huluki nydingine za Kikundi, Kiva (kampuni tanzu), Ofisi za Utathmini wa Mikopo (Credit Assessment Bureaus (BIC), Watoa huduma za mtandao wa simu, mashirika ya ukusanyaji wa madeni, washirika wa kibashara, n.k.
	Jinsi Programu Inavyotumia Maelezo ya Mtumiaji	Sera ya faragha ya Programu ya Kiva inaeleza kwamba hukusanya data ya watumiaji kwa madhumuni yafuatayo: Kuthibitisha utambulisho wa mtumiaji Kushughulikia shughuli za kifedha za mtumiaji Kutoa mikopo na kubuni miundo ya Utoaji wa alama za mikopo na ukusanyaji wa malipo  Kutekeleza majukumu ya Kiva kwa watumiaji Kutii sheria husika zinazohusiana na masharti ya KYC “Know Your Customer”, AML “Anti-money laundering”, na CFT (Combating the Finance of Terrorism) Kutoa huduma za matangazo na mawasiliano kuhusu ofa
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine  Muda ambao data inafikiwa na wahusika wengine	Programu ya Kiva hushiriki maelezo ya mtumiaji na: Kampuni zake tanzu, kampuni yake kuu na kampuni zingine tanzu za kampuni yetu kuu (“kikundi chake”) Mtu ye yeyote anayewakilisha mtumiaji Ofisi za masuala ya mikopo au taasisi nydingine za fedha . Washirika wa kibashara katika hali za uhamishaji, uuzaaji, muungano na ununuzi wa biashara, nk.  Watoa huduma wengine ikiwa ni pamoja na GAFA (Google, Facebook, nk.) na Twitter.  Sera ya faragha inaeleza kwamba inashiriki maelezo na wahusika wengine kwa muda unaofaa bila kubainishwa kwa uwazi urefu wa muda huu.

	Teknolojia za Ufutiliaji / Vidakuzi vya Tovuti	<p>Huduma ya Mikopo ya Kiva (Kiva Lending Service) hutumia vidakuzi, bikoni za wavuti na mifumo mingine ya kiotomatiki ili kukusanya data kuhusu vitendo vya mtumiaji. Programu inabainisha vipengele hivi katika sera yake ya vidakuzi.</p> <p>Kwa kutumia zana hizi, Programu ya Kiva na tovuti yake hupata maelezo kivyake na kupitia programu na zana za wahusika wengine (kama vile Google Analytics). Data inayokusanya inajumuisha maelezo fulani ya kiufundi (k.m. Njia unayotumia kufikia tovuti, kurasa ulizotembelea, anwani halisi ya IP, aina ya kifaa, aina ya kivinjani, lugha ya kivinjani, aina ya muunganisho wa mtandao, na tarehe na saa uliyotembelea tovuti).</p>
	Jinsi Programu Inavyohifadhi Maelezo ya Mtumiaji	<p>Shirika la Kiva hukusanya na kuhifadhi data yote ya watumiaji nchini Marekani. Shirika la Kiva, washirika wake, watoa huduma, maajenti na wawakilishi wake nchini Marekani au kwangineko duniani wanaweza kuona maelezo haya ya binafsi. Shirika la Kiva imejitolea pia kuheshimu sera yake ya faragha, bila kujali mahali ambapo maelezo yako ya binafsi yanachakatwa au yalichakatwa.</p> <p>Sera ya faragha ya Programu ya Kiva inaeleza pia kwamba inachukua hatua zinazofaa ili kudumisha usalama halisi, wa kiufundi na kiusimamizi unaofaa ili kusaidia kuzuia kupotea, kutumiwa vibaya na ufikiaji ambao haujaidhinishwa, kufichuliwa au kubadilishwa kwa maelezo.</p>

## **Uchunguzi Kifani: Kuunda na kuwezesha upatikanaji wa hifadhidata kuhusu historia ya mikopo ya wateja wa Kiva.**

Muundo wa ukuaji wa Kiva unawezesha utoaji wa mikopo midogo katika zaidi ya nchi 80 kwa kuunganisha watu wanaohitaji ufadhili na wenye uwezo wa kutoa ufadhili. Ili kufanya hivyo, shirika la Kiva huwezesha upatikanaji wa hifadhidata za historia za mikopo za wateja kama sehemu ya mfumo mpana wa mtandaoni wa utoaji wa mikopo. Hifadhidata hizi, ambazo zinaweza kupatikana bila malipo, zinatokana na ukusanyaji wa data ya binafsi (jina la ukoo, majina ya kwanza, jinsia, historia ya mikopo, n.k.) ya watumiaji. Mbinu hii haijabainishwa kwa uwazi katika sera za faragha za Kiva na inaweza kusababisha utumiaji mbaya. Pia, ruhusa inayotolewa na watumiaji wanaposjisajili kwenye huduma ya mikopo ya Kiva haipaswi kutumiwa kama kigezo cha kushirikiwa kwa data yao na watumiaji wengine. Kwa hivyo, Taifa la Kameruni linapaswa kutunga sheria na mamlaka iliyoteuliwa ili kulinda data ya binafsi.

Kando na suala la kushiriki maelezo kuhusu historia ya mikopo ya wateja wa Kiva, wanasheria wa taifa la Kameruni wanapaswa pia kushughulikia suala la uhusiano kati ya Kiva na makampuni fulani makubwa ya huduma za dijitali: Facebook, Google na Apple. Kweli, sera ya faragha ya Kiva inaeleza kwamba watumiaji wanapoingia katika tovuti yake kupitia akaunti ya Facebook, maelezo ya akaunti (anwani ya barua pepe, picha ya akaunti, orodha ya marafiki wa Facebook ambao pia hutumia huduma ya Kiva) hukusanya. Kupitia mbinu hii, Facebook inaweza kupata historia ya mikopo ya wateja wa Kiva bila mtumiaji kutoa idhini ya wazi. Mbinu hii pia hutendeka kwenye akaunti za Google na Apple.

## **Uchanganuzi wa Desturi za Data za Programu za Mikopo Dijitali Dhidi ya Sheria Zinazohusiana na Ulinzi wa Haki za Mteja nchini Kameruni**

Kwa sababu nchi ya Kameruni haina sheria iliyotungwa ili kulinda data ya binafsi, si nahisi kuchanganua desturi za programu za mikopo dijitali kwa kutegemea maelezo yaliyopo. Sheria zinazohusiana na ulinzi wa mteja na zinazohusiana na usalama wa mawasiliano ya kielektroniki hazitekelezi madhumuni ya sheria ya masuala ya dijitali. Ukosefu huu unatoa msingi thabiti wa uchakataji haramu wa data ya binafsi na ukiukaji wa haki za dijitali za watumiaji wa programu za mikopo dijitali na shughuli zingine zote za aina hii.

Vipengele mbalimbali vya mbinu za uchakataji wa data za programu za mikopo dijitali za nchini Kameruni havitii kanuni na viwango vya kimataifa vya ulinzi wa data ya binafsi. Sheria na mamlaka maalum vinahitajika ili kulazimisha wadhibiti wa data wa programu hizi kuanza kutumia sera za faragha za data zinazofaa. Pindi mamlaka inayoungwa mkononi na sheria itakapoundwa kwa madhumuni haya, inapaswa kuwa na nyenzo na ujuzi wa kiufundi unaohitajika ili kutekeleza majukumu yake. Nyenzo hizi zitaiwezesha kufuatilia moja kwa moja ukubwa, ubora na wingi wa data inayokusanywa na wadhibiti wa data wa programu za simu za mkononi na wachakataji wengine wa data.

# Kepuvede (Cape Verde)

## Maelezo ya Nchi



Ikiwa na idadi inayokadiriwa ya watu 550,000 na GDP ya bilioni 4.323 kufikia mwaka wa 2019, nchi ya Kabovede (Cabo Verde), inayojulikana pia kama Kepuvede (Cape Verde), ina visiwa kumi vya volkano ambavyo vinapatikana maili 385 (kilomita 620) kutoka pwani ya magharibi mwa Afrika. Jiji la Praia, linalopatikana kwenye kisiwa cha Santiago, ni mji mkuu wa Kepuvede (Cape Verde). Kepuvede (Cape Verde) ina visiwa tisa ambapo watu wanaishi, kisiwa kimoja ambapo watu hawaishi, na visiwa mbalimbali vidogo. Visiwa hivi viliendelea kuwa chini ya ukoloni wa Ureno hadi mwaka wa 1975<sup>40</sup>.

40 Carling, Jørgen, and Luís Batalha. 'Cape Verdean Migration and Diaspora' in Transnational Archipelago: Perspectives on Cape Verdean Migration and Diaspora, Carling Jørgen and Batalha Luís (eds) (Amsterdam University Press, 2008) 13-32.

## Ulinzi wa Data Nchini Kepuvede (Cape Verde)

Nchi ya Kepuvede (Cape Verde) inawapa watu haki kadhaa za kikatiba na kisheria za ulinzi wa data ya binafsi. Katiba ina vifungu vingi vya sheria ya ulinzi wa data na inatoa safu ya ziada ya sheria ya ulinzi. Nchi ya Kepuvede (Cape Verde) ina sheria mbili muhimu kuhusu ulinzi wa data: Sheria ya 133-V-2001 kuhusu Ulinzi wa Data ya Binafsi (kama ilivyorekebishwa na Sheria Nambari 41/VIII/2013 - Sheria Rasmi ya Jumla ya Ulinzi wa Data ya Binafsi ya Watu (inapatikana tu kwa Kireno hapa) na Sheria Nambari 121/IX/2021 ya tarehe 17 Machi 2021. Mwaka wa 2001, nchi ya Kepuvede (Cape Verde) ilipitisha sheria yake kuu ya ulinzi wa data, Seria Nambari 133.

Tangu wakati huo, sheria hiyo imefanyiwa mabadiliko kadhaa. Mwaka wa 2013, bunge ilipitisha Sheria Nambari 41 ya kuongezea na kubadilisha Sheria Nambari 133. Hivi karibuni zaidi, mnamo Machi 2021, bunge ilipitisha Sheria Nambari 121 ya kuelezea kwa kina majukumu ya mamlaka ya ulinzi wa data ya Kepuvede, inayojulikana kama Comissão Nacional de Proteção de Dados Pessoais (CNPD). Sheria rasmi ya ulinzi wa data ya Kepuvede (Cape Verde) inaiga mfano kutoka Ulaya.<sup>41</sup>

Sheria ya Ulinzi wa Data ('Sheria') inashughulikia suala la uchakataji data kupitia njia za kiotomatiki na zisizo za kiotomatiki na mashirika yanayotambulika nchini Kepuvede (Cape Verde) au kukusanya au kutuma data ya binafsi kupitia njia yoyote nchini.

41 <https://dataprotection.africa/cape-verde/> na <https://www.dataguidance.com/notes/cape-verde-data-protection-overview> > ilifikiwa tarehe 2 Agosti 2021.

## Teknolojia za Fedha na Mifumo ya Fedha Nchini Kepuvede (Cape Verde)

Hatua ya kwanza iliyochukuliwa na Benki ya Kepuvede (Bank of Cape Verde) kama msimamizi wa mfumo wa malipo ilikuwa mwaka wa 2018 wakati ambapo Benki hiyo ilizindua programu ya simu ya mkononi ya kukopesha pesa ya Makeba. Mageuzi ya mfumo wa usimamizi wa Mfumo wa Malipo wa Kepuvede, Amri-Sheria Nambani 7/2018, ya tarehe 28 Novemba,<sup>42</sup> ilidhibiti masuala yanayohusiana na kanuni kuu kwamba mfumo wowote wa malipo unaofanya kazi nchini lazima uzingatie kuhakikisha ufanisi na usalama. Mojawapo ya kanuni zilizobainishwa kwenye Kifungu cha 10 cha amri-sheria hiyo kinarejelea kufafanua sera za usalama na mbinu za kuhakikisha utendakazi wa kutegemewa katika mfumo wa malipo, ikiwa ni pamoja na malipo ya simu za mkononi.

Tarehe 17 Juni 2021, Bank of Cape Verde<sup>43</sup> ilichapisha sheria ya kubainisha masharti ya msingi ya kuboresha utendakazi na usalama katika utekelezaji wa Huduma za Malipo ya Simu za Mkononi nchini Kepuvede (Cape Verde).<sup>44</sup> Kifungu cha 1 kinaeleza kuwa inalenga kubainisha masharti ya msingi na ya wastani ya usalama yanayotumika kwa usalama wa malipo ya simu za mkononi ambayo lazima yafuatwe na Watoa Huduma za Maipo (Payment Service Providers (PSP)).

Kifungu cha 4 kinarejelea masuala ya usalama na kinabainisha kwamba muundo wa Huduma ya Malipo ya Simu za Mkononi unapaswa kuelnga mbinu ambazo zinaruhusu utumaji, uchakataji na kuhifadhi maelezo nyeti kwa usalama. Kinafafanua pia sera na matumizi ya mbinu za kuzuia na kugundua matukio ya ubadilishaji au kuathiriwa kwa maelezo. Kiliongezea kwamba Watoa Huduma za Malipo (Payment Service Providers (PSP)) wanapaswa kutekeleza tanatibu za kutegemewa za kufuatilia shughuli za kifedha na mifumo ya kutambua akaunti zisizo za kawaida za malipo na kuzuia vitendo vya ulaghaji.

Mojawapo ya vifungu vilivytuvutia ni Kifungu cha 6 cha sheria hiyo. Bank of Cape Verde inaeleza kwamba mtohuduma za malipo ya simu za mkononi lazima ahakikishe kuna tanatibu thabiti za uthibitishaji wa mteja kwa ajili ya uidhinishaji wa malipo kulingana na ufanuzi uliotolewa katika sheria hii. Benki hiyo inabainisha kwamba watoa huduma za malipo lazima wahakikishe kuwa huduma inayotolewa inajumuisha mbinu salama za kurekodi data ya shughuli ya kifedha. Mbinu hiyo inapaswa kujumuisha marejeleo ambayo yanaruhusu kutambuliwa kwa shughuli ya malipo, tarehe na saa ya kutekelezwa, mabadiliko ya mipangilio ya vipimo na ufikiaji wa data, hatua ambayo inaruhusu uwezo wa kufuatiliwa kwa shughuli za kifedha wakati wowote.

Hatimaye, mbinu zilizotekeliza na faili za kumbukumbu zinapaswa kutambua na kufuatilia chanzo kilichotekeliza malipo (mahali, intaneti) na mnufaishwa (muuzaji). Tunatambua kuwa ni mbinu ambayo inawapa watoa huduma uwezo kupita kiasi wa kufuatilia maelezo ya wateja wao.

### Makeba: Programu ya Simu za Mkononi ya Kukopesha Pesa

Programu hii ilingia katika soko la fedha nchini Kepuvede mwaka wa 2018.<sup>45</sup>

Watumiaji wanaweza kupakua Programu hii kwenye vifaa vya iOS au Android.<sup>46</sup> Ni

<sup>42</sup> Amri-Sheria Nambani 7/2018, ya tarehe 28 Novemba [https://www.bcv.cv/pt/O%20Banco/Sectores/Documents/2018/Bo\\_28-11-2018\\_78.pdf](https://www.bcv.cv/pt/O%20Banco/Sectores/Documents/2018/Bo_28-11-2018_78.pdf) > ilifikiwa tarehe 29 Julai 2021.

<sup>43</sup> Bank of Cape Verde <https://www.bcv.cv/pt/Paginas/Homepage.aspx> > ilifikiwa tarehe 2 Agosti 2021.

<sup>44</sup> Sheria nambari 3/2021 ya tarehe 17 Juni kuhusu Huduma za Malipo ya Simu za Mkononi [https://www.bcv.cv/pt/O%20Banco/Sectores/Documents/2021/Legis%203.07.2021/Aviso\\_3-2021.pdf.pdf#search=aplica%C3%A7%C3%B5es%20m%C3%B3veis](https://www.bcv.cv/pt/O%20Banco/Sectores/Documents/2021/Legis%203.07.2021/Aviso_3-2021.pdf.pdf#search=aplica%C3%A7%C3%B5es%20m%C3%B3veis) > ilifikiwa tarehe 28 Julai 2021.

<sup>45</sup> <https://www.makeba.money/cv-pon/howitworks.html> > ilifikiwa tarehe 1 Agosti 2021.

<sup>46</sup> iOS – <https://itunes.apple.com/pt/app/makeba-money/id1458893785> and Android – [https://play.google.com/store/apps/details?id=money.makeba.makebamoney&hl=pt\\_cv](https://play.google.com/store/apps/details?id=money.makeba.makebamoney&hl=pt_cv) > ilifikiwa tarehe 3 Agosti 2021.

programu ambayo inaruhusu watumiaji kutoa na kukopa pesa au kutuma pesa kwenye BAICV<sup>47</sup> au kwa Wauzaji wa Bidhaa wanaotumia programu ya Makeba. Kama inavyoonyeshwa na programu, Programu ya Makeba hufanya kazi kwa kusoma msimbo wa QR au data ya kielektroniki. Bado, haibainishi data ya binafsi inavyofikiwa, hasa kwa sababu Ajenti anayesimamia programu ndiye husoma data na wala si lazima awe mteja. Yaani, lazima mtumiaji apeane simu yake ya mkononi kwa msimamizi ili asome data iliyopo kabla ya kutuma au kukopesha pesa.

Wakati wa uzinduzi huu, Afisa Mkuu Mtendaji wa Makeba, Yamandou Alexander alieleza<sup>48</sup> kwamba Programu hii italeta mabadiliko na kurahisisha zaidi biashara. Hata hivyo, zaidi ya miaka miwili baadaye, hakuna ushahidi unaoonyesha kuwamba inaleta mabadiliko katika soko la fedha nchini Kepuvede (Cape Verde), bado kukiwa na shaka kuhusu jinsi Programu hii inavyofanya kazi. Idadi ya wateja wake na kiasi chake cha sasa cha pesa za kutumika hakijulikani tangu ilipoanza kutumiwa nchini Kepuvede (Cape Verde).

## **Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali**

Makeba <sup>49</sup>	Maeleo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu
Ruhusa zinazotakikana	Kwa kukubali mkataba, BAICV inaahidi kutoa huduma ya MAKEBA kwa mtumiaji chini ya sheria na masharti yaliyobainishwa katika vifungu vya mkataba. Mtumiaji huidhinisha kiasi cha malipo kwenye akaunti yake ya sasa ya Benki. Kiasi hiki cha malipo kinaonyesha kiasi kinacholingana na malipo anayolipa kupitia huduma ya MAKEBA na kiasi cha malipo ya mkopo cha kiasi kinachohusiana na kiasi cha pesa zinazotumwa kupitia benki anachopokea au kuagiza, mtawalia, kupitia huduma ya MAKEBA. Maeleo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji

47 https://www.bancobai.cv/particulares/produtos-e-servicos/servico-de-pagamento/makeba > ilifikiwa tarehe 3 Agosti 2021.

48 https://expressodasilhas.cv/eitec/2018/12/14/app-que-permite-transferir-dinheiro-e-pagar-online-e-lancada-para-a-semana/61403 > ilifikiwa tarehe 28 Julai 2021.

49 Sera ya Faragha – https://www.makeba.money/cv-por/terms.html / https://www.makeba.money/app/terms/terms-money-cv-por.html > ilifikiwa tarehe 10 Agosti 2021.

	<p>Maelezo yanayokusanya kutoka kwa mtumiaji</p>	<p>Kadi ya Kitambulisho. Kadi ya Kitambulisho cha Kitaifa, Pasipoti, Kibali cha Mkazi. Nambari ya Kitambulisho cha Mlipa Ushuru, nchi/jiji la kuzaliwa, anwani, mji, sanduku la posta, nambari ya simu, nambari ya simu ya mkononi na barua pepe</p> <p>Wajibu wa kutoa huduma ya MAKEBA utaanza kutekelezwa tu baada ya kuthibitishwa, na BAICV au mhusika mwingine anayetenda kwa niaba yake na kwa jina lake. Uthibitishaji huu utaonyesha kwamba huduma ya MAKEBA imewezeshwa (kupitia kwa mawasiliano na mtumiaji kwamba huduma ya MAKEBA imewezeshwa). BAICV itatoa thibitisho baada ya mtumiaji kukubali sheria na masharti. Thibitisho hili hutumwa kupitia nambari ya simu iliyotolewa na mtumiaji wakati wa kujisajili kwenye huduma ya MAKEBA</p> <p>Ili BAICV itoe huduma ya MAKEBA kwa mtumiaji, mtumiaji anapaswa kupata idhini ya utumiaji na kusakinisha programu ya MAKEBA kwenye simu ya mkononi ya iOS au Android.</p> <p>Wajibu wa kutoa huduma ya MAKEBA unashurutisha tu iwapo na mradi mteja:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>a) Ataendelea kutumia nambari ya simu aliyotoa kwenye simu yake ya mkononi.</li> <li>b) Ataendelea kutumia kitambulisho ambacho yeeye hutumia kufanya shughuli za kifedha kwenye huduma ya MAKEBA kila wakati.</li> <li>c) Atahakikisha kuwa anapokea arifa ya programu inayoomba uthibitishaji wa shughuli ya kifedha ya huduma ya MAKEBA kwenye simu ya mkononi ambapo mtumiaji amesakinisha programu ya MAKEBA.</li> </ul>
--	--	---

	<p>Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji</p> <p>Mtumiaji huidhinisha BAICV kuchakata maelezo ya binafsi yaliyotolewa na Mtumiaji kwa BAICV. Uidhinishaji huu unahusiana na utekelezaji na udumishaji wa mkataba huu. Inajumuisha maelezo yaliyotolewa wakati wa kusakinisha na kutumia programu ya MAKEBA, moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, ambapo madhumuni yake ni kutoa huduma ya MAKEBA na BAICV kwa mtumiaji.</p> <p>Data ya binafsi hukusanywa kwa kutumia utaratibu wa KYC (Jua Mteja Wako) unaofuata Sheria ya Ulinzi wa Data ya Binafsi na sheria nyingine husika inayotumika nchini Kepuvede (Cape Verde).</p> <p>Uchakataji wa data ya binafsi iliyotolewa na mtumiaji kwa Benki kuhusiana na utekelezaji na udumishaji wa mkataba hufanywa pia chini ya Sheria ya Ulinzi wa Data ya Binafsi inayotumika nchini Kepuvede (Cape Verde).</p> <p>Ingawa mmiliki wa programu ya MAKEBA hutekeleza shughuli ya uchakataji wa data, ni huduma ya MAKEBA ndio hubainisha madhumuni na njia za uchakataji, kwa sababu ndilo shirika linalowajibika na shughuli hiyo.</p> <p>Watumiaji wanakubali kwamba, ndani ya vizuizi vya sheria, rekodi zinazotolewa na mfumo wa kompyuta ambazo hutumika kutoa huduma ya MAKEBA na ambazo zinahusiana na shughuli zinazotekelawa na mtumiaji zitatumia na BAICV kwa madhumuni ya uthibitishaji, utoaji wa maelezo ya takwimu au yaliyojumlishwa, au mengineyo.</p>
<p>Maelezo yanayokusanywa kutokana na kutumia tovuti ya Makeba</p>	<p>Tovuti haiombi mtumiaji kukubali au kukataa matumizi ya vidakuvi.</p>
<p>Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine</p>	<p>Maelezo ya fedha (akaunti ya benki) Nambari ya Kitambulisho cha Kulipa Ushuru (Tax Identification Number(TIN)).</p>

	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kila mtumiaji anahusishwa na nambari moja ya simu ya mkononi na Nambari moja ya Kitambulisho cha Kulipa Ushuru (Tax Identification Number (TIN). Katika shughuli za kutuma pesa katika huduma ya MAKEBA zinazoagizwa na mtumiaji, mtumiaji anathibitisha kuwa mpokeaji atapokea tu pesa zilizotumwa ikiwa tayari ni mtumiaji au akiwa mtumiaji kwa madhumuni haya.  Mtumiaji anaiddhinisha BAICV kutuma maelezo yake kwa kampuni ya MAKEBA INC, yenye ofisi zake zilizosajiliwa nchini Marekani, na kampuni za kundi la BAI. Kuna tahadhari inayozuia kampuni kutumia maelezo hayo kwa madhumuni mengine kando na yaliyobainishwa na kuyalinda dhidi kufichuliwa au kufikiwa bila idhini. Inazuia pia uwezo wa Mmiliki kufikia maelezo yaliyo hapo juu kwa ajili ya urekebishaji, ubadilishaji au uondoaji chini masharti ya sheria.
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Watumiaji wanakiri kwamba wanaiddhinisha BAICV kutuma maelezo yao ya binafsi kwa wahusika wengine wanaoiwakilisha, ambao ni muhimu kwa ajili ya uvezeshaji, kutoa huduma ya usaidizi, usimamizi na udumishaji wa huduma ya MAKEBA na uendelezaji wa shughuli zozote zinazohusiana nayo.
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	a) Kwa muda usio chini ya miaka 7 (saba) kuanzia kwa shughuli ya mwisho ya kifedha au mwisho wa uhusiano wa kimkataba. b) Wakati hakuna wajibu wowote unaotokana na uhusiano wa kimkataba. c) Wakati haki za BAICV zinabatilishwa.
	Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuvi vya tovuti	Tovuti haiombi mtumiaji kukubali au kukataa matumizi ya vidakuvi.
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Maelezo ya fedha Maelezo ya mawasiliano

Makeba ni programu yenye mawasiliano ya kistaarabu kwa wateja wake. Tovuti yake inatoa mafunzo yanayoeleweka kuhusu jinsi wateja wanavyoweza kujisajili kwenye huduma, na ufanuzi wa kina wa hatua kwa hatua, kuanzia kwa upakuaji hadi kwa utumiaji. Ingawa kuna sehemu ya mawasiliano, haifanyi kazi kwa sababu huwezi kujuia iwapo wasimamizi wa mfumo wamepokea ujumbe kwa sababu hakuna arifa zozote. Katika sehemu moja, Programu inaeleza kwamba huduma ya Makeba inakusudiwa kutumiwa na watu na biashara ambazo zinaaminiana. Masharti ya msingi ya kutumia programu hii ni kuthibitisha utambulisho, angalau kuweka kadi ya kitambulisho kwenye mfumo, kunaonyesha kwa uwazi utumiaji wa data ya binafsi.<sup>50</sup>

Sehemu ya Maswali Yanayoulizwa Sana (FAQ)<sup>51</sup> inaonekana bila kuangazia chochote, na inaeleza kwamba mtumiaji hawezi kughairi shughuli za kifedha baada ya kuidhinishwa. Inaeleza kwamba inatumia teknolojia mpya zaidi ya usimbaji ili kulinda akaunti za wateja na kuhakikisha kuwa data yao ni ya siri. Ikiwa watumiaji watashuku kuwa akaunti zao zimeathiriwa, lazima wawasiliame na wasimamizi wa programu.

Kando na hayo, si wazi kuhusu jinsi teknolojia ya usimbaji inavyotumika ili kulinda data ya wateja, kwa sababu kwa kutumia programu, huwezi kuona maelezo yanayokusanywa. Programu inaeleza kwamba pesa zinazotumwa kwenye huduma ya Makeba hulindwa na mshirika wa huduma za benki ambaye ni Banco BAI Cabo Verde kuhusiana na data ya binafsi. Programu pia ilieleza kwamba wateja wanahitaji kutumia NIB yao ili kufikia akaunti ya huduma ya Makeba ili kuhamisha pesa zilizo kwenye akaunti yao ya benki. Si wazi jinsi NIB hii inavyohifadhiwa na kiwango ambacho Banco BAI-CV inaweza kudhibiti au kufikia data ya mteja, hasa kwa sababu inahusu maelezo nyeti kuhusu akaunti za benki za mteja.

One case that gained visibility in the media was related to a fine that the Data Protection Agency (CNPD) imposed on the Central Bank of Cape Verde and a commercial bank called Novo Banco Cabo Verde.<sup>52</sup> Faini hii ilikuwa ni kwa sababu ya kufichuliwa kwa orodha ya wadeni 50 wa Benki ya biashara kwa vyombo vya habari. Faini zilihusiana na ukweli kwamba benki hizo hazikuchukua hatua mwafaka za kulinda data ya binafsi. Benki Kuu (Central Bank) na Benki ya biashara zimekata rufaa mahakamani.

Orodha hiyo ilipotolewa hadharani, Benki ya Kepuvede (Bank of Cape Verde) na Wizara ya Fedha (Ministry of Finance) zilijitenga na suala hilo. Lengo la uchunguzi wa CNPD halikuwa kutambua jinsi orodha hiyo ilivyotolewa hadharani, lakini ilikuwa ni kuhusu iwapo kulikuwa na ukiukaji wa sheria ya ulinzi wa data ya mteja na Benki hiyo.<sup>53</sup>

Tunatambua kuwa tukio hili linaonyesha udhaifu wa kutumia programu kama vile Makeba kulinda data ya wateja wao. Hata hivyo, linaonyesha pia baadhi ya hatua zinazochukuliwa na shirika la ulinzi wa data.

Kwa kuzingatia kuwa nchi ya Kepuvede (Cape Verde) ni nchi ya kwanza kutunga sheria ya ulinzi wa data barani Afrika, tunatambua lengo dhahiri la Shirika la Ulinzi wa Data (Data Protection Agency) kuhusu kufuutilia jinsi sekta ya fedha hutumia data ya watumiaji. Hata hivyo, hatukuweza kuthibitisha jinsi wasimamizi wanavyoweza kuchukua hatua kama hizo kwa programu za simu za mkononi za kukopesha pesa kama vile Makeba. Hakuna mifano thabiti ya shughuli zinazofanywa na CNPD ili kulinda data ya watumiaji kwenye programu hizi, hali ambayo inaonyesha upungufu.

Kwa upande mwingine, hatuoni hatua zaidi zinazochukulia na Benki ya Kepuvede (Bank of Cape Verde), ambayo kimsingi inapaswa kuwa taasisi kuu ya kusimamia jinsi programu hizi zinavyotumiwa, hasa kwa sababu hakuna programu nyinginezo kando na programu ya Makeba.

51 <https://www.makeba.money/cv-pon/faq.html> > ilifikiwa tarehe 30 Julai 2021.

52 Inajulikana kuwa faini hiyo karibu \$30,000 <https://www.voaportugues.com/a/banco-de-cabo-verde-e-novo-banco-multados-violar-lei-proteccao-de-dados/3898368.html> > ilifikiwa tarehe 29 Julai 2021.

53 <https://www.dn.pt/lusa/banco-central-e-novo-banco-de-cabo-verde-multados-por-falha-na-protecao-de-dados-8563648.html> > ilifikiwa tarehe 28 Julai 2021.

# Kodivaa (Côte d'Ivoire)



## Maelezo ya Nchi

Jamhuri ya Kodivaa (Côte d'Ivoire) ni nchi inayotumia lugha ya Kifaransa katika eneo la Afrika Magharibi yenyewe idadi ya zaidi watu milioni 26 kufikia mwaka wa 2020.<sup>54</sup> Nchi hii inapakana na mataifa ya Mali, Burkina Faso (Burkina Faso), Ghana, Liberia na Gine (Guinea), inayowakilishwa 40% ya uchumi wa Muungano wa Kiuchumi wa Mataifa ya Afrika Magharibi (Economic Union of West African States' (UEMOA). Kadirio la GDP la nchi hii ni Dola bilioni 58.54 za Marekani, na ina mfumo wa utawala wa urais.

54 Chanzo. Karatasi ya Maelezo ya Nchi ya Kodivaa (Ivory Coast) iliyotolewa na Atlas of the Countries and Populations of the World na inapatikana katika kiungo kifuatacho:  
<https://www.populationdata.net/pays/cote-divoire/>

## Ulinzi wa Data Nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire)

Ulinzi wa data ya binafsi nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire) unasimamiwa na Sheria nambari 2003-450.<sup>55</sup>

Sheria hii inatumika kwa uchakataji wowote wa kiotomatiki au usiofanyika nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire)<sup>56</sup>. Si wazi iwapo sheria hii inatumika kwa data ya raia wa Kodivaa wanaoishi nje ya nchi. L'Autorité de Régulation des Télécommunications de Côte d'Ivoire (ARTCI) ni shirika la kitaifa la DPA nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire). Amri nambari 2012-293 ya tarehe 25 Juni 2013, iliunda shirika hili lakini lilipewa mamlaka ya kusimamia uchakataji wa data ya binafsi na Sheria nambari 2003-450 ya tarehe 16 Juni 2013.<sup>57</sup>

Linawajibika katika kuhakikisha utiifu wa vifungu vya sheria vinavyohusiana na uchakataji wa data ya binafsi na kuhakikisha kuwa shughuli mbalimbali za uchakataji haziingilii uhuru na faragha<sup>58</sup>.

## Utangulizi

Ikiwa na mgawo wa soko wa 70.9%, Biashara ya Kutuma na Kupokea Pesa Kupitia Simu

55 Sheria nambari 2003-450 ya tarehe 16 Juni 2013 kuhusu ulinzi wa data ya binafsi nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire). < [https://www.artci.ci/images/stories/pdf/lois/loi\\_2013\\_450.pdf](https://www.artci.ci/images/stories/pdf/lois/loi_2013_450.pdf) > ilifikiwa tarehe 7 Mei 2021.

56 Kifungu cha 3 cha Sheria nambari 2003-450 ya tarehe 16 Juni 2013  
 57 Kifungu husika?

58 Kifungu cha 47 cha Sheria nambari 2003-450.

(Mobile Money)<sup>59</sup> inanawini nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire). Inaendeshwa na mashinika makuu ya kutoa huduma za simu za mkononi<sup>60</sup>, ambayo yanagawana idadi yawatumiaji 20,789,662. Kwa kufahamu uwezo unaotolewa na soko hili, wawili (2) kati ya watoa huduma hawa, wanaojulikana kama Orange na MTN, wameanza kutoa huduma za kukopesh pesa kidijitali, huduma ya fedha ambayo inaruhusu raia wa Kodivaa kupata mikopo ya hanaka na ya muda mfupi kupitia programu za simu za mkononi. Huduma hii ya kupata mkopo hanaka inatoa na kuboresha hali ya watu wasiopokea huduma bora za benki kuwa na uwezo na fursa sawa ya kufikia huduma za fedha, inawasaidia kukidhi għarama zao, na inatoa fursa kwa watu kuwa chanzo kinachoweza kukuza sekta ya fedha nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire). Kweli, huduma ya kwanza ya kutoa mkopo dijitali iliyozinduliwa tarehe 16 Februari 2018, na kampuni ya MTN na Bridge Microfinance Côte d'Ivoire ilivutia wateja 1,900,000 ndani ya mwaka mmoja.

Mnamo Julai 2020, shirika la Orange lilianzisha huduma kama hiyo. Kati ya Julai 2020 na tarehe 31 Mei, huduma yake ya kutoa mikopo midogo iliunda kiasi cha FCFA bilioni 44 kutokana na mikopo iliyotolewa kwa wateja wa Kodivaa, ikiwa ni pamoja na maombi milioni 1.2 ya mikopo iliyoshughulikiwa ya kiasi cha kati ya FCFA 5,000 na 250,000. Idadi ya wateja wa shirika la Orange ilikuwa watu 600,000 mwisho wa mwezi wa Mei 2021, na pesa za kuweka akiba zilipokea riba ya kiwango cha 3.5%, iliyotokana na FCFA bilioni 1.5. Kwa ukusanyaji wa madeni ya mikopo na ufuutiliжи wa mipango ya kuweka akiba, watoa huduma hawa hukusanya data ya binafsi kutoka kwa wateja wao kupitia programu za simu za mkononi<sup>61</sup> ambazo zinatumika kama kiolesura.

Mbinu hii inaweza kuingilia faragħa ya mtumiaji na inapaswa kuchunguzwa kwa uadilifu. Huduma hizi za kutoa mikopo kupitia Programu ya simu ya mkononi zilianza kutumika baada ya kutii Sheria inayohusu ulinzi wa data ya binafsi nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire)<sup>62</sup>. Kwa hivyo, ni muhimu kujua iwapo mbinu za uchakataji wa data za programu hizi, kama inavyoelezwa katika sera na sheria na masharti yake ya matumizi, zinazingatia sheria za ulinzi wa faragħa. Utafiti huu unalenga kuchanganua sera za faragħa na sheria na masharti ya programu hizi na kuchunguza jinsi zinavyotii sheria ya ulinzi wa wateja nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire). Sehemu ya kwanza inajumuisha muhtasari wa data inayokusanywa na programu hizi. Sehemu ya pili inachunguza shughuli zake za uchakataji chini ya Sheria ya ulinzi wa data ya binafsi. Sehemu ya mwisho inakamilika kwa kuonyesha iwapo programu hizi zinatii Sheria inayolinda data ya binafsi au la.

## **Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali**

59 Huduma ya Kutuma na Kupokea Pesa Kupitia Simu za Mkononi ni pesa za kielektroniki zilizoundwa na watoa huduma za mawasiliano ya simu na kuhifadhiwa kwenye pochi la kielektroniki linalosimamiwa na mpango wa huduma ya simu. Teknolojia hii inaruhusu watu kutuma au kupokea pesa dijitali kupitia simu zao. Unahitaji tu kujua nambari ya simu ya mpokeaji ili kumtumia pesa. Kwa hivyo, nambari ya simu imekuwa, kwa namna fulani, nambari ya akaunti ya benki bila kuwa na akaunti ya benki. Hata hivyo, għarama za huduma ya kutuma na kupokea pesa kupitia simu ya mkononi bado ziko chini zaidi kuliko za akaunti ya benki. Jambo ambalo limefanya huduma hii kuwa maarufu na kuperdelewa zaidi na watu.

60 Orange, MTN na Moov ni mashirika 3 ya kutoa huduma za simu za mkononi nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire).

61 Huduma ya kutoa mikopo midogo na kuweka akiba ndogo ya MTN Mobile Money inayojulikana kama MOMO KASH inatolewa kulingana na msimbo wa USSD unaohusishwa na nambari ya simu na programu ya simu za mkononi ya MyMTN CI. Zote zinahusishwa na akaunti ya mteja ya huduma ya MTN Mobile Money. Kwa upande mwiegħine ħuduma ya kutoa mikopo midogo na kuweka ndogo ndogo ya Orange Côte d'Ivoire, inayojulikana kama Tik-Tak inahusishwa pia na msimbo wa USSD na programu ya simu za mkononi: Orange Bank Africa. Zote zinahusishwa na akaunti ya mteja ya huduma ya Orange Money.

62 LSheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013 kuhusu ulinzi wa data ya binafsi nchini Kodivaa (Ivory Coast)

Orange Money Africa <sup>63</sup>  Kiungo cha kupakua : Google Play Store na Apple Store	Maelezo yanayokusanywa na kuchakatwa na programu
	Ruhusa zinazoombwa  Wakati wa kufunguka, programu ya Orange Money Africa huomba:  <ul style="list-style-type: none"> <li>· Kudhibiti simu za mtumiaji</li> <li>· kufikia SMS za mtumiaji: Huonyesha SMS za mtumiaji ili kukusanya maelezo ya fedha na data ya shughuli za kifedha ili kukusanya maelezo kuhusu historia ya fedha ya mtumiaji na kubainisha ufaafu wake wa kupokea mikopo</li> <li>· Kufikia anwani za mawasiliano za mtumiaji</li> <li>· Kufikia data ya mahali, kifaa na matumizi: Programu ya Orange Money hutumia teknolojia ya GPS au huduma zingine za mahali kubainisha mahali mahususi alipo mtumiaji</li> </ul>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji  Wakati wa kujisajili, programu ya Orange Money hukusanya maelezo ya mtumiaji: jina, anwani, anwani ya barua pepe na nambari ya simu, nambari ya simu ya kifaa, maelezo ya SIM kadi, umni, jina la mtumiaji, nenosiri, data ya fedha na mikopo, maelezo ya binafsi na picha na maelezo mengine ya usajili
Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji  Maelezo yanayokusanywa unapotumia tovuti ya Orange Côte d'Ivoire	Programu ya Orange Money Africa hukusanya maelezo yafuatayo kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji: Muundo wa kifaa cha mkononi, nambari ya IMEI ya kifaa au nambari ya utambulisho, maelezo ya SIM kadi, maelezo ya mtandao wa simu, mfumo wa uendeshaji wa kifaa, aina ya kivinjari, data ya mahali ya kifaa na mipangilio ya saa za eneo  Maelezo yaliyohifadhiwa kwenye kifaa: orodha ya anwani za mawasiliano, nekodi za nambari za simu, rekodi za SMS, anwani zilizo kwenye akaunti za mitandao ya kijamii, picha, video au maudhui yoyote dijitali husika. Mtumiaji anapotumia tovuti ya Orange Côte d'Ivoire kwenye simu yake ya mkononi, programu ya Orange et Moi <sup>64</sup> hukusanya maelezo yafuatayo kiotomatiki na kuyahifadhi kwenye faili za rekodi zake: Anwani ya IP ya mtumiaji, aina ya kivinjari, Mto Huduma za Intaneti (ISP), kurasa za uelekezaji / kuondoka, mfumo wa uendeshaji, muhuri wa muda na maudhui ya kuvinjari. Kisha maelezo haya huchanganywa kwa madhumuni ya uchanganuzi au matangazo na kufichuliwa kwa Orange Bank.

63 Sera ya faragha kuhusu data ya binafsi kwenye huduma ya Orange Money na Sheria na Masharti ya Jumla ya Matumizi (T & Cs) ya huduma za Mikopo na Akiba za Benki ya Orange (Orange Bank Savings and Loan)

64 Orange et moi ni programu ya Orange Côte d'Ivoire inayotumika kama kiolesura cha wateja wake wanaotumia simu za android.

Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Maelezo hupatikana kutoka kwa mashirika mengine ya Orange Group: Orange Money Côte d'Ivoire na Orange Côte d'Ivoire, Ofisi za Utathmini wa Mikopo (Credit Assessment Offices (BIC), Watoa huduma za mtandao wa simu na mashirika ya ukusanyaji wa madeni.
Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Sera ya faragha ya Programu ya Orange Money Africa inaeleza kwamba hukusanya data ya watumiaji kwa madhumuni yafuatayo: kushughulikia shughuli za kifedha za mtumiaji Kuthibitisha utambulisho wa mtumiaji Kutoa mikopo na ukusanyaji wa malipo, kutoa alama za mikopo na kuunda mifumo ya kutoa mikopo kuchanganua tabia za mkopaji Wajibu wa Programu ya Orange Money kwa watumiaji kutii · kutii sheria, vifungu na kanuni zinazohusiana na mchakato wa "jua mteja wako" na kanuni za kupinga ulanguzi wa pesa Kuzuia ulaghai, Huduma za matangazo
Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Programu ya Orange Money hushiriki maelezo ya mtumiaji na: Wanachama wake, maajenti, watoa huduma, mashirika ya Orange Money Group, na mashirika ambayo hupewa kandarasi ya kushughulikia data iliyokusanywa. Mtu ye yeyote anayewakilisha taasisi ya fedha ya mtumiaji, mashirika na ofisi za usimamizi wa mikopo (BIC) Washirika wa kibashara katika hali za uhamishaji, uuzaaji, muungano na ununuzi wa biashara, nk Watoa huduma wengine Mashirika ya utekelezaji wa sheria (Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano ya Simu / ICT ya Kodivaa (Côte d'Ivoire) (ARTCI)4), maofisa wa serikali, kulingana na:
Muda ambao data inafikiwa na wahusika wengine	Ombi rasmi au agizo la mahakama Kutii Sheria au Kuripoti Shughuli za Kinyume cha Sheria Zinazoshukiwa  Sera yake haitoi maelezo yoyote kuhusu muda ambao wahusika wengine wanaweza kufikia maelezo ya binafsi ya mtumiaji na kuyahifadhi.
Teknolojia za Ufuatiliaji / Vidakuzi vya Tovuti	Programu ya Orange Money Africa hutumia teknolojia za ufuatiliaji wa simu na vidakuzi vya tovuti ili kutofautisha watumiaji wa Programu.

	Jinsi Programu Inavyohifadhi Maelezo ya Mtumiaji	Programu ya Orange Money Africa huhifadhi data ya watumiaji nje ya nchi ya Kodivaa (Ivory Coast). Maelezo pia huchakatwa na wafanyakazi wa Orange Money Côte d'Ivoire, Orange Bank Africa, na CECOM yake inayopatikana nchini Madagaska inayofanya kazi njie ya nchi ya Kodivaa (Côte d'Ivoire). Programu haikutoa maelezo kuhusu muda wa kuhifadhiwa kwa data na shirika la Orange Côte d'Ivoire.
--	---	--

<p>MyMTN CI<sup>65</sup></p> <p>Kiungo cha kupakua : Google Play Store na Apple Store</p>	Maelezo yanayokusanywa na kuchakatwa na programu	
	Ruhusa zinazoombwa	<p>Wakati wa kufunguka, programu ya MyMTN CI huomba:</p> <p>Kudhibiti simu za mtumiaji kufikia SMS za mtumiaji: Huonyesha SMS ya mtumiaji ili kukusanya maelezo ya fedha na ya shughuli za fedha ili kukusanya maelezo kuhusu historia ya fedha ya mtumiaji na kubainisha ufaafu wake wa kupokea mikopo</p> <p>Kufikia anwani za mawasiliano za mtumiaji Kufikia data ya mahali, kifaa na matumizi: Programu ya MyMTN CI hutumia teknolojia ya GPS au huduma zingine za mahali ili kutambua mahali mahususi alipo mtumiaji</p>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	<p>Wakati wa kujisajili, programu ya MyMTN CI hukusanya maelezo ya mtumiaji: utambulisho wa mteja (jina, jina la kwanza, jinsia, tarehe ya kuzaliwa), maelezo haya ya mawasiliano (anwani ya posta, anwani ya barua pepe, nambari za simu), data ya mahali (hali ya kijografija) na uhusiano katika njia hizi za malipo zilizochaguliwa (hundi, pesa taslimu, kadi ya benki, kutuma na kupokea pesa kupitia simu ya mkononi)</p>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	<p>Maelezo yanayokusanywa na Programu ya MyMTN CI kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji: Mbinu ya Utashi wa Kompyuta (Artificial Intelligence (AI): muundo wa simu, nambari ya IMEI au nambari ya kitambulisho, maelezo ya SIM kadi, maelezo ya mtandao wa simu, mfumo wa uendeshaji wa kifaa, aina ya kivinjari, data ya mahali ya kifaa na mipangilio ya saa za eneo</p>
	Maelezo yanayokusanywa unapotumia tovuti ya MTN Côte d'Ivoire	<p>Maelezo yaliyohifadhiwa kwenye kifaa: orodha ya anwani za mawasiliano, rekodi za nambari za simu, rekodi za SMS, anwani zilizo kwenye akaunti za mitandao ya kijamii, picha, video au maudhui yoyote dijitali husika. Mtumiaji unapotumia tovuti ya MTN Côte d'Ivoire, shirika la MyMTN CI hukusanya kiotomatiki maelezo yafuatayo na kuyahifadhi kwenye faili za rekodi zake: Anwani ya IP ya mtumiaji, aina ya kivinjari, mtohuduma za intaneti (ISP), kurasa za uelekezaji / kuondoka, mfumo wa uendeshaji, muhuni wa muda na maudhui ya kuvinjari. Maelezo haya huunganishwa kwa madhumuni ya kufanya uchanganuzi au kuonyesha matangazo.</p>
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Maelezo yanayopatikana kutoka kwa mashirika mengine ya MTN Group: MTN Côte d'Ivoire na MTN Mobile Financial Services Côte d'Ivoire, Ofisi za Utathmini wa Mikopo (Credit Assessment Offices (BIC), Watoa huduma za mtandao wa simu na mashirika ya ukusanyaji wa madeni.

65 Sera ya faragha, sheria na masharti (T & C) ya Programu za MyMTN CI na Masharti ya Jumla ya Matumizi () ya akaunti za MTN Mobile Money Ivory Coast

	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Sera ya faragha ya Programu ya MyMTN CI inaeleza kwamba hukusanya data ya mtumiaji kwa madhumuni yafuatayo: <ul style="list-style-type: none"> <li>· Kushughulikia shughuli za kifedha za mtumiaji</li> <li>· Kuthibitisha utambulisho wa mtumiaji</li> <li>· Kutoa mikopo na ukusanyaji wa malipo</li> <li>· kutoa mikopo na kuunda mifumo ya kutoa mikopo</li> <li>· kuchanganua tabia za mkopaji</li> <li>· Wajibu wa Programu ya Orange Money kwa watumiaji</li> <li>· kutii · kutii sheria, vifungu na kanuni zinazohusiana na mchakato wa “jua mteja wako” na kanuni za kupinga ulanguzi wa pesa</li> <li>· Kuzuia ulaghai,</li> <li>· Huduma za matangazo</li> </ul>
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Programu ya MyMTN CI hushiriki maelezo ya mtumiaji na: Wanachama wake, maajenti, watoa huduma, mashirika ya MTN Group, na mashirika yanayopewa kandarasi ndogo ya kusimamia data iliyokusanywa. Mtu yejote anayewakilisha mtumiaji taasisi za fedha, ofisi za mikopo na mashirika (BIC) Washirika wa kibashara katika hali za uhamishaji, uuzaji, muungano na ununuzi wa biashara, nk. Watoa huduma wengine Mashirika ya utekelezaji wa sheria (Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano ya Simu / ICT ya Kodivaa (Côte d'Ivoire) (ARTCI) <sup>4</sup> ), maofisa wa serikali, kulingana na:
	Muda ambao data inafikiwa na wahusika wengine	Ombi rasmi au agizo la mahakama Kutii Sheria au Kuripoti Shughuli za Kinyume cha Sheria Zinazoshukiwa  Sera yake haitoi maelezo yoyote kuhusu muda ambao wahusika wengine wanaweza kufikia maelezo ya binafsi ya mtumiaji na kuyahifadhi.
	Teknolojia za Ufutiliaji / Vidakuzi vya Tovuti	Programu ya MyMTN CI hutumia teknolojia za ufuutiliaji wa simu na vidakuzi vya tovuti ili kutofautisha watumiaji wa Programu.
	Jinsi Programu Inavyohifadhi Maelezo ya Mtumiaji	Programu ya MTN CI huhifadhi maelezo ya mtumiaji nje ya nchi ya Kodivaa (Ivory Coast). Maelezo pia yanaweza kuchakatwa na wafanyakazi wa shirika la MTN Côte d'Ivoire nje ya nchi ya Kodivaa (Côte d'Ivoire). The privacy policy of MyMTN CI indicates that the maximum retention period for the data collected is ten years from the end of the contractual relationship and may be extended in the event of legal or administrative proceedings.

## **Uchunguzi Kifani: Orange Money Africa: Swali la muda wa kuhifadhiwakwa data ya mtumiaji**

Sera ya usiri, sheria na masharti ya jumla ya matumizi (T & C) ya akaunti za programu ya Orange Money Côte d'Ivoire na sera ya utiifu wa umma ya programu ya Orange Côte d'Ivoire, inayohusishwa na Programu za Orange Money Africa haitoi maelezo yoyote kuhusu muda wa kuhifadhi data ya mtumiaji. Ukosefu huu unasababisha ukiukaji wa sheria ya ulinzi wa data nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire), ambayo inahitaji kuwa data ikusanywe kwa kipindi maalum<sup>66</sup>.

## **Uchanganuzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu za Mikopo Dijitali Kuhusiana na Sheria Inayohusiana na Ulinzi wa Data Binafsi**

Sheria ya ulinzi wa data ya binafsi nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire) imebainisha kwa uwazi wajibu wa kutekeleza katika sheria za faragha, zinazotumika kwa uchakataji wowote, uwe ni wa kiotomatiki au la<sup>67</sup>. Kwa kufanya hivyo, programu za mikopo dijitali pia zimejumuishwa. Hata hivyo, kutokana na kuanzishwa kwake hivi karibuni, hatari za ulinzi wa faragha ni mpya. Sehemu hii inaangazia vifungu husika vya Sheria ili kutambua iwapo Programu hizi zinatii vifungu hivi.

### **Haki ya Faragha**

Sheria ya ulinzi wa data inahitaji wadhibiti na wachakataji wa data (katika hali hii, programu za mikopo dijitali) washughulikie data ya binafsi kwa njia ambayo inaheshimu haki ya faragha.<sup>68</sup> Katika hali hii, Sheria inazitaka programu hizi zihakikishe kuwa haki ya faragha ya mkopaji inazingatiwa kwanza wakati wa kuchakata data yake. Programu zilizofanyiwa utafiti zinakiuka haki hii na zinachakata data ambayo inaingilia faragha ya mtumiaji na isiyohusiana na madhumuni ya ukusanyaji wa data. Kwa mfano, programu hizi hukusanya maelezo kama vile anwani za mawasiliano zilizohifadhiwa kwenye kifaa cha mkopaji, maelezo ya kuingia katika akaunti kwenye mifumo ya mitandao ya kijamii, na data sahihi ya moja kwa moja ya mahali, ambayo inaingilia faragha ya mtumiaji na haihusiani na madhumuni ya ukusanyaji wa data.

### **Uhalali, Haki na Uwazi**

Sheria ya ulinzi wa data inahitaji programu hizi zichakate data kwa njia halali, ya haki na uwazi.<sup>69</sup> All applications must inform their data subjects clearly and concisely on how their data will be processed and that all the parameters of the Law are respected in such processing.<sup>70</sup>

Katika hali hii, programu zinapaswa kuwafahamisha watumiaji kwa nini data yao inakusanywa, jinsi kampuni itakavyotumia data yao na, ikiwa itashirikiwa na wahusika wengine, ni nani ambao kampuni itashiriki nao data yao na muda ambao watahifadhi data hiyo. Inaweza kusemekana kuwa programu zilizofanyiwa utafiti zinaeleza kwa uwazi kwa nini zinakusanya data ya mtumiaji na wahusika zinaoshiriki nao data hiyo. Hata hivyo, hazielezi muda ambao wahusika wengine watafikia data hiyo na muda ambao wataihifadhi.

### **Kikomo cha Madhumuni, Ufaafu na Utoshelevu**

Programu za mikopo dijitali zinahitajika chini ya sheria ya ulinzi wa data kuchakata data ya binafsi baada ya ukusanyaji wa data.<sup>71</sup>

66 Kifungu cha 16 na 43 vya Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

67 Kifungu cha 3 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

68 Kifungu cha 3 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

69 Kifungu cha 14, 15 na 16 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

70 Kifungu cha 28 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

71 Kifungu cha 14 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

Hii inamaanisha kuwa Programu zinapaswa tu kukusanya data inayohusiana na madhumuni ya kutoa mikopo dijitali wala si data isiyohusiana na madhumuni hayo. Programu zinapaswa kukusanya tu data inayohusika, ya kutosha na inayohusiana na madhumuni ya ukusanyaji wa data.<sup>72</sup>

Programu zilizochunguzwa hukusanya data ya binafsi ambayo haihusiki na madhumuni ya ukusanyaji wa data.

Hukusanya maelezo ya wakopaji, kama vile nambani za kadi za mikopo, shughuli za kifedha, maelezo ya kuingia katika akaunti ya mitandao ya kijamii, anwani za mitandao ya kijamii, anwani za simu, picha na video, nk, ambayo hayahusiki katika utoaji wa mikopo dijitali.

## **Kushiriki Maelezo na Wahusika Wengine**

Sheria ya ulinzi wa data ya Kodivaa (Côte d'Ivoire's) inaeleza kwamba programu hizi lazima ziwafahamishe watumiaji kuhusu wahusika wengine ambao zitashiriki nao data yao, ikijumuisha mbinu zilizowekwa ili kulinda usalama wa data yao kabla ya kukusanywa.<sup>73</sup>

Katika hali mahususi ya Programu za Orange Money Africa, ukosefu wa kipindi maalum cha uchakataji wa data unasababisha ukiukaji wa haki za faragha<sup>74</sup>.

Programu zilizokaguliwa hushiriki maelezo ya mtumiaji/mkopaji na ofisi ya maelezo ya mikopo (Credit Information Office (CIO), washirika wa kibiashara, wataalamu wa washauri, serikali na mashirika ya utekelezaji wa sheria, nk., na hazielezi mbinu za ulinzi zinazotumika ili kulinda data ya mkopaji. Programu hizi pia hazielezi muda ambao wahusika hawa wataweza kufikia data na muda watakaoihifadhi.

## **Uhamishaji wa data ya binafsi nje ya nchi ya Kodivaa (Côte d'Ivoire)**

Kifungu kinachofuata na watoa huduma za programu mbalimbali

## **Usiri Kimuundo na kwa Chaguomsingi**

Sheria inaeleza kwamba mdhibiti wa data lazima aweke mikakati yote ya uchakataji wa data ya mtumiaji<sup>75</sup>.

Programu hizi zina mbinu za usimbaji zinazotumika ili kulinda mawasiliano na maudhui ya siri ya watumiaji wake—ambacho ni kiwango cha usalama kinachohitajika ili kulinda data ya mtumiaji. Hata hivyo, kiwango cha usalama kilicho jumuishwa hakiwezi kuzuia mto huduma ya Programu kukusanya maelezo ya ziada.

## **Haki ya Kufikia na Kufuta Data ya Binafsi**

Watumiaji wa programu hizi wana haki ya kufikia data yao inayohifadhiwa na programu hizi<sup>76</sup> na wana haki ya kuomba kufutwa au kuharibiwa kwa data yao ambayo programu haziruhusiwi tena kuhifadhi. Watumiaji pia wana haki ya kuomba kufutwa kwa data ambayo haihusiki, ni ya ziada au iliyopatikana kwa njiaharamu<sup>77</sup>. Watoa huduma za programu wamewe ka huduma maalum za kupokea maombi ya watumiaji kuhusiana na suala hili.

## **Kuhamishika kwa Data**

Sheria inawapa wamiliki wa data haki ya kupokea data yao kwa muundo uliopangwa na unaoweza kusomeka na mashine.<sup>78</sup> Inawapa pia haki, panapowezekana kiufundi, kuhamishia

72 Kifungu cha 16 na 43 vya Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

73 Kifungu cha 16 na 43 vya Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

74 Kifungu cha 49 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

75 Kifungu cha 39, 40, 41 na 44 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

76 Kifungu cha 49 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

77 Kifungu cha 30, 31, 3 , 33, 34, 35 na 36 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

78 Kifungu cha 49 cha Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013

data moja kwa moja kwa wadhibiti au wachakataji wengine wa data.

<sup>79</sup> Programu zinazochunguzwa haziwapi watumiaji njia za kutekeleza haki hii.

## **Utathmini wa Athari ya Ulinzi wa Data (Data Protection Impact Assessment (DPIA))**

Sheria inahitaji ripoti kuhusu mchakato wa uchakataji wa data itolewe kila mwaka na kutumwa kwa shirika la ARTCI. Kando na hayo, mamlaka za kuidhinisha uhamishaji wa data zimebainisha haja ya wadhibiti wa data kutekeleza Utathmini wa Athari ya Ulinzi wa Data (Data Protection Impact Assessment (DPIA)). Hata hivyo, hamna yeyote katи ya wadhibiti wa data wa programu hizi mbili ambaye ametoa au kuchapisha ripoti zake.

Mbinu za uchakataji wa data za programu za mikopo dijitali nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire) haziheshimu Sheria ya kanuni za ulinzi wa faragha.

Tathmini za athari ya ulinzi wa data (DPIA) lazima utekelezwe na wanaowajibika kwa uchakataji wa maombi haya ya dijitali ili kulazimisha utiifu mkali wa wajibu wa kisheria katika sehemu hii.

Kando na hayo, marekebisho ya Sheria nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013, yanayohusiana na ulinzi wa data ya binafsi lazima yazingatiwe, kwa kuzingatia hatani zinazoweza kujitokeza kwa suala la faragha. Zaidi ya hayo, ni muhimu pia kwa shinika la ARTCI kupata ujuzi na nyenzo za kiufundi za kufuatilia moja kwa moja ukubwa, ubora na wingi wa data inayokusanywa na wadhibiti hao wa data kwa uchakataji wa maombi ya mikopo dijitali.

# Misri



## Maelezo ya Nchi

Ikiwa inapatikana katika eneo la Kaskazini Mashariki mwa Afrika, Misri, au Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, ilikuwa na idadi ya zaidi watu milioni 106 mwaka wa 2021. It is located on the southern coast of the Eastern Mediterranean, bordered by Israel, Libya, Sudan and is part of the group of countries of the Middle East and North Africa (MENA). Ni nchi yenye GDP ya pili kubwa zaidi barani Afrika na ilikuwa karibu Dola bilioni 362 mwaka wa 2019/20. Ina mfumo wa utawala wa rais na wazini mkuu.

## Ulinzi wa Data Nchini Misri

Ulinzi wa faragha unasimamiwa na Sheria Nambari 151 ya tarehe 15 Julai 2020, ya ulinzi wa data ya binafsi. Sheria hii inatumika kwa shughuli yoyote ya uchakataji, iwe ni ya kiotomatiki au la, inayofanyika nchini au nje ya nchi ya Misri<sup>80</sup>. Kituo cha Ulinzi wa Data (Data Protection Center ('DPC') ni DPA ya Misri. Kiliundwa na Sheria Nambari 151 ya tarehe 15 Julai 2020, na kilianza shughuli zake mnamo Aprili 2021. Kimepewa mamlaka ya kusimamia na kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Data, ikiwa ni pamoja na, wala si tu, kutoa leseni, idhini na vyeti vinavyohitajika chini ya Sheria ya Ulinzi wa Data<sup>81</sup>.

## Utangulizi

Mwaka wa 2020, bara la Afrika lilikuwa na akaunti milioni 562 za Huduma ya Kutuma na Kupokea Pesa Kupitia Simu za Mkononi (Mobile Money), idadi inayowakilisha 45% ya akaunti za Huduma ya Kutuma na Kupokea Pesa Kupitia Simu za Mkononi (Mobile Money) zilizofunguliwa duniani kote, yaani, bilioni 1.2. Idadi kubwa ya akaunti hizi imegawanywa katika eneo la Afrika Mashariki (milioni 293) na Afrika Magharibi (milioni 198), na zinatumiwa angalau kufanya shughuli za malipo ya aina mbalimbali. Tunatambua pia ongezeko kubwa zaidi la idadi ya akaunti la nambari kamili kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita katika eneo la Afrika Kaskazini kwa sababu ya juhudhi mpya na zilizofufuliwa katika sekta ya eneo hili. Kweli, katika eneo la Afrika Kaskazini, akaunti milioni 14 za huduma ya kutuma na kupokea pesa kupitia simu ya mkononi zilisajiliwa mwaka wa 2020 kwa shughuli milioni 248 za kifedha, kiasi

<sup>80</sup> Kifungu cha 1 na 2 cha Sheria Nambari 151 ya tarehe 15 Julai 2020

<sup>81</sup>

Kifungu cha 19 cha Sheria Nambari 151 ya tarehe 15 Julai 2020

kinacholingana na zaidi ya Dola bilioni 3 za Manekani (\$), ongezeko la 24% ikilinganishwa na mwaka wa 2019. Mojawapo ya nchi zinazoongoza katika mabadiliko haya yanayoendelea ni Misri, ambapo huduma nne za kutuma na kupokea pesa kuitia simu za mkononi zimetolewa kwa wanainchi tangu Aprili 2013. Huduma hizi zinahusu (i) kufanya malipo kuitia simu za mkononi (malipo ya bili, malipo ya kikundi na malipo ya ununuzi wa bidhaa), kutuma pesa (kutuma pesa kitaifa na kimataifa), kulipa mishahara (Kulipa wafanyakazi mishahara) na huduma za benki (kuweka pesa, kutoa pesa, akaunti ya akiba, mikopo dijitali, nk.). Kutokana na huduma zake, Misri ilitekeleza karibu shughuli milioni 4.5 za kifedha kielektroniki kila mwezi, zilizofanywa na pochi milioni 13.5 za mtandaoni za akaunti za simu za mkononi (pochi za mtandaoni) zinazotumika nchini, kulingana na takwimu za hivi karibuni zaidi kutoka kwa shinika la Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (National Authority of Telecommunications Regulation (NTRA), zilizochapishwa Juni 2020. Kampuni kuu za kutoa huduma za simu za mkononi pia zinatoa huduma ya pochi za mtandaoni, yaani, teknolojia ya fedha. Kampuni ya Vodafone Egypt inaendelea kuongoza katika kitengo hiki, ikiwakilisha 62.7% ya jumla ya pochi za mtandaoni na 86.5% ya shughuli za kifedha za pochi za mtandaoni, ikifuatwa na kampuni ya Orange Egypt (25% ya pochi za mtandaoni na 8.5% ya shughuli za kifedha), Etisalat Misr (12% ya pochi za mtandaoni na 4.5% ya shughuli za kifedha) na We (0.3% na 0.5%). Huduma zinazotumika zaidi na watumiaji ni huduma ya kuweka na kutoa pesa (35% ya jumla ya shughuli za kifedha zinazofanywa kuitia pochi ya mtandaoni), kutuma pesa (33%) na kuweka mjazo wa simu za mkononi (26%).

Kuhusu huduma ya kutoa mikopo dijitali, ilianzishwa mara ya kwanza nchini Misri na Kampuni mpya ya Kayshat<sup>82</sup> mnamo Februari 2020 wa makubaliano ya Mamlaka ya Usimamizi wa Fedha Nchini Misri (Financial Regulatory Authority of Egypt). Programu hii inawezesha watu kupata mikopo ya kati ya pauni za Misri 100 na 1,500 (EGP). Biashara inayonawiri kwa nchi ambayo karibu 70% ya idadi ya watu hawana akaunti za benki na, zaidi ya yote, ni soko kwa wadau wa sekta ya benki na fedha. Kweli, kwa kufahamu faida inayoweza kupatikana kutokana na aina hii ya huduma, huduma kadhaa (Shahry<sup>83</sup>, MNT Halan<sup>84</sup> na MoneyFellows<sup>85</sup>) zilibuniwa. Kuongezeka kwa huduma hizi kuliko athari zake za manufaa ya uwezo wa kufikia huduma za fedha na kuboresha viwango vya maisha ya watu kunasababisha changamoto kuhusiana na suala la ulinzi wa data ya binafsi nchini Misri.

Kwa hivyo, je, mbinu za uchakataji wa data za programu hizi, kama inavyoelezwa katika sera na sheria na masharti yake ya matumizi, zinazingatia sheria za ulinzi wa faragha?

Utafiti huu unalenga kuchanganua sera za faragha na sheria na masharti ya programu hizi na kuchunguza jinsi zinavyotii sheria ya ulinzi wa wateja nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire). Sehemu ya kwanza inajumuisha muhtasari wa data inayokusanywa na programu hizi, na sehemu ya pili inachunguza shughuli zake za uchakataji chini ya Sheria ya ulinzi wa data ya binafsi. Sehemu ya mwisho inakamilika kwa kuonyesha iwapo programu hizi zinatii sheria inayolinda data ya binafsi au la.

<sup>82</sup> Kashat ni programu ya kwanza ya simu za mkononi ya Kukopesha pesa bila kuhitaji dhamana yoyote nchini Misri, ambayo inatoa mikopo ya muda mfupi ambayo inaanzia EGP 100 hadi EGP 1500 na mpango wa malipo wa hadi siku 61.

<sup>83</sup> Programu ya Shahry iliwezesha wanainchi wa Misri kupata mikopo ya papo hapo na ya muda mfupi ya kununua bidhaa na huduma nchini.

<sup>84</sup> Programu ya Halan ni programu ya huduma nydingi ambayo inawezesha wanainchi wa Misri kupata mikopo ya papo hapo kando na usafirishaji na ununuzi wa bidhaa. Huduma ya kutoa mikopo dijitali ambayo inatokana na ushirikiano kati ya kampuni ya Uholanzi, MNT Investments BV na kampuni ya kutoa mikopo kwa biashara ndogo ya Tasaheel. Kimahususi, inaruhusu wafanyakazi kupata mikopo ya kuanzia EGP 3,000 hadi EGP 200,000 kwa urahisi. Ilianzishwa mnamo tarehe 24 Juni 2021.

<sup>85</sup> Programu ya MoneyFellows inatoa aina nydingi ya chaguo cha mikopo ya pesa ambayo kila mtumiaji anaweza kuchagua. Kulingana na mwenendo wa kulipa, mtumiaji anaweza kupata mikopo ya papo hapo. Ada zinaanza 8% na zinapungua polepole kulingana na mikopo uliochagua, hadi sufuri. Uteuzi wa aina ya mikopo na kiasi kinachotolewa kwa watumiaji hufanywa kuitia mchakato wa kutathmini ufaafu wa mtumiaji kuidhinishwa kupata mikopo unaofanywa na timu ya programu ya MoneyFellows.

## Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali

Kashat <sup>86</sup>	Maelezo yanayokusanywa na kuchakatwa na programu
Kiungo cha kupakua: Google Play Store na HUAWEI AppGallery	<p>Ruhusa zinazotakikana</p> <p>Wakati wa kufunguka, Programu ya Kashat huomba: Kudhibiti simu na kufikia anwani za mawasiliano za mtumiaji, kutafuta akaunti zilizo kwenye kifaa, kusoma anwani zako, kusoma rekodi za nambari za simu, kupiga simu moja kwa moja kwa nambari za simu na kusoma hali ya simu na kitambulisho.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>. kufikia SMS za mtumiaji: Huonyesha SMS na au MMS za mtumiaji ili kukusanya maelezo fulani ya fedha na ya shughuli za fedha ili kukusanya maelezo kuhusu historia ya fedha ya mtumiaji na kubainisha ufaafu wake wa kupokea mikopo</li> <li>. Kufikia data iliyohifadhiwa kwenye simu ya mtumiaji, kubadilisha, kusoma au kufuta maudhui yaliyo kwenye nafasi ya hifadhi ya USB</li> </ul> <p>kufikia data ya mahali, kifaa na matumizi: Programu ya Kashat hutumia teknolojia ya GPS na huduma zingine za data ya mahali ili kubainisha mahali mahususi.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>. Kuangalia miunganisho ya Wi-Fi</li> <li>. Kufikia natiba ili kusoma matukio ya kalenda pamoja na maelezo ya siri, kuongeza au kubadilisha matukio ya kalenda, na kutuma barua pepe kwa wageni bila ufahamu wa mmiliki.</li> <li>. Kutekeleza vitendo mbalimbali: kuunganisha kwenye huduma inayoweza kufikiwa, kupokea data kutoka kwenye intaneti, kuchomoza juu ya programu zingine, kusoma mipangilio ya huduma ya Google, kuangalia miunganisho ya mtandao, kufunguka baada ya kuwasha kifaa, ufikiaji kamili wa mtandao na kuzuia kifaa kuingia katika hali tuli</li> </ul>
	<p>Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji</p> <p>Wakati wa kujisajili kwenye huduma ya mikopo, Programu ya Kashat hukusanya maelezo ya mtumiaji: jina, anwani, nambari ya simu, anwani ya barua pepe, kadi ya kitambulisho cha kitaifa, picha yako, jina la mtumiaji na nenosini., na maelezo mengine ya usajili: hali ya kazi na sekta, hali ya ndoa, maelezo ya fedha na mikopo.</p>

	Maelezo Yanayokusanywa Kutoka Kwenye Kifaa cha Mtumiaji	Programu ya Kashat hukusanya maelezo yafuatayo kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji: maelezo ya kifaa ya kifaa, ikijumuisha aina ya simu, vitambulisho maalum vya kifaa (IMEI au nambari ya kitambulisho), mfumo wa uendeshaji wa kifaa na data ya mahali ya kifaa na saa za eneo maelezo ya mtandao wa simu
Kuhusu nchi ya Eswatini kimahususi, hali ya ukosefu wa sheria ya utaratibu kuhusu ulinzi wa faragha hairuhusu kampuni ya MTN kutotekeleza wajibu wake. Kuwepo kwake katika zaidi ya nchi 22 barani Afrika na Mashariki ya Kati na uzito wake wa kiuchumi na kifedha unapaswa kuiwezesha kuunganisha programu zake za simu za mkononi na sera za kisheria za usini zinazotumika kwenye miktadha ya nchi mbalimbali.

## Uchanganuzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu za Mikopo Dijitali Dhidi ya Sheria Inayohusiana na Ulinzi wa Data Binafsi

Ukosefu wa sheria ya utaratibu kuhusu ulinzi wa faragha nchini Eswatini ni hatari kwa wanainchi wake. Hata hivyo, wadhibiti wa data wa kampuni zinazotoa programu za mikopo dijitali zinapaswa kutii sheria ya ulinzi wa mtumiaji. Katika kifungu chake cha 14, sheria hii imetoe vifungu vinavyohusu ulinzi wa faragha ikisubiri kupitishwa kwa sheria mpya na kuanzishwa kwa 'Tume ya Mawasiliano ya Eswatini (Communication Eswatini Commission

("ECC")<sup>114</sup>. Pia, Mswada wa Ulinzi wa Data (Data Protection Bill), 2020 (Rasimu) unaelezwa wajibu wa kisheria kuhusu ulinzi wa faragha, unaotumika kwa uchakataji wowote wa kiotomatiki au la<sup>115</sup>. Programu za mikopo dijitali zinapaswa kutii sheria hiyo ili kupunguza hatari kuhusu suala la ulinzi wa faragha.

Kuhusu vifungu husika vinavyohusu kutii faragha nchini Eswatini, ni vyema kusema kwamba programu zinazochunguzwa zimekiuka kabisa kanuni za msingi. Ukiukaji huu unahusu haki ya faragha, usawa, haki na uwazi, kushiriki maelezo na wahusika wengine, usiri kimuundo na kwa chaguomsingi, haki ya kufikia na kufutwa kwa data ya binafsi na kuhamishika kwa data. Kando an hayo, baadhi ya programu hizi hazina sera za faragha za data zinazochakata. Mbinu za ushughulikiaji wa data za programu za mikopo dijitali nchini Eswatini ni muhimu kwa ulinzi wa faragha. Ikiwa inakabiliwa na mabadiliko ya aina hii ya maendeleo ya huduma, mamlaka za kisiasa na usimamizi nchini lazima zijitahidi kuanzisha Mamlaka ya Ulinzi wa Data. Baada ya kuanzishwa, mamlaka hiyo itapaswa kutekeleza ukaguzi wa utiifu wa sheria wa shughuli za wajibu wa uchakataji na itapaswa kupewa nyenzo za kuiwezesha kufuatilia data inayokusanywa na Programu za simu za mkononi.

---

<sup>114</sup> Mamlaka ya usimamizi iliundwa na inapaswa kuwajibika kwa uchapishaji wa mwongozo wa data.

<sup>115</sup> Kifungu cha 3 cha Mswada wa Ulinzi wa Data, 2020

# Uhabeshi (Ethiopia)



## Maelezo ya Nchi

Ikiwa inapatikana katika eneo la Kaskazini Mashariki mwa Afrika (yaani., Pembe ya Afrika (Horn of Africa)),<sup>116</sup> Ethiopia, inayojulikana pia kama Shirikisho la Kidemokrasia la Jamhuri ya Ethiopia, inapakana na nchi ya Eritrea, Jibuti, Somalia, Kenya, Sudan Kusini na Sudan.<sup>117</sup> Ina ukubwa wa 1,112,000 km<sup>2</sup> na ina idadi ya watu milioni 110.14.<sup>118</sup> Ina karibu makabila 80, ambapo mengi ya Amhara na Oromo.<sup>119</sup> Jiji lake kuu ni Addis Ababa ambalo pia ni jiji lake kubwa zaidi.<sup>120</sup>

<sup>116</sup> Kuhusu Ethiopia <https://ethiopianembassy.org/overview-about-ethiopia/>

<sup>117</sup> Ethiopia <https://www.britannica.com/place/Ethiopia>

<sup>118</sup> Kuhusu Ethiopia <https://ethiopianembassy.org/overview-about-ethiopia/>

<sup>119</sup> Ibid

<sup>120</sup> Ethiopia <https://www.britannica.com/place/Ethiopia>

## Ulinzi wa Data Nchini Ethiopia

Hakuna utaratibu unaosimamia programu za mikopo dijitali nchini Ethiopia kwa sasa. Nchi hii pia haina sheria ya ulinzi wa data ya kudhibiti mbinu za kutoa mikopo za programu hizi.<sup>121</sup> Hata hivyo, vifungu vya faragha na ulinzi wa data vinaweza kupatikana kwenye sheria nyingine nchini, muhimu kati yake ikiwa ni Katiba ya Shirikisho la Kidemokrasia la Jamhuri ya Ethiopia (Constitution of the Federal Democratic Republic of Ethiopia) ya 1995<sup>122</sup>. Katiba inahakikisha haki ya faragha na inawapa maofisa wa umma jukumu la kuheshimu na kulinda haki hii.<sup>123</sup>

Sheria ya Ulinzi wa Data ya Ethiopia bado iko katika awamu ya rasimu. Utafiti huu utachunguza sera za faragha za programu za mikopo dijitali (mahususi) nchini Ethiopia ili kutambua iwapo zinatii haki ya faragha ya watumiaji wa programu.

## Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali

Programu ya Dashen Amole[5]	Maelezo yanayokusanywa na kuchakatwa na Programu[1]
-----------------------------	---

<sup>121</sup> Ethiopia-Muhtasari wa Ulinzi wa Data Ulinzi wa Faragha na data ya binafsi barani Afrika: Utafiti kuhusu haki wa sheria katika nchi nane (Mei 2021) ukurasa wa 27

<sup>122</sup> Ethiopia-Muhtasari wa Ulinzi wa Data

<sup>123</sup> Kifungu cha 26, Katiba ya Shirikisho la Kidemokrasia la Jamhuri ya Ethiopia (Constitution of the Federal Democratic Republic of Ethiopia) <https://www.refworld.org/docid/3ae6b5a84.html>

	Ruhusa zinazotakikana	Huomba kufikia: barua pepe, ujumbe (SMS), mifumo ya mitandao ya kijamii au programu za simu. Wakati ambapo mtumiaji hataki tena programu hii kufikia maelezo haya, anaweza kuwasiliana na huduma kwa wateja ili kukomesha matumizi ya huduma ya programu hii
	Maelezo Yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Programu hukusanya jina la mtumiaji, anwani, anwani ya barua pepe na nambari ya simu wakati wa kujisajili
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	
	Matumizi ya maelezo ya mtumiaji	Utekelezaji wa wajibu kwa mtumiaji Kufuata maagizo ya mtumiaji Kufungua na kudumisha akaunti ya mtumiaji, kuwezesha shughuli za kifedha, kudhibiti madai na hatari Madhumuni ya uchanganuzi na takwimu Matangazo Kutii sheria husika
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Hukusanya maelezo kutoka kwa wahusika wafuatao: Mashirika ya ripoti za mikopo Mashirika ya serikali Hushiriki maelezo na: Watu wanaotoa huduma za usaidizi Washirika na mashirika yake tanzu
	Ufichuzi wa maelezo ya binafsi	Hufichua maelezo ya mtumiaji chini ya hali zifuatazo: Panapohitajika na sheria Yanapotakikana na NBE Chini ya wajibu wake wa umma wa kufichua maelezo Wakati maslahi ya kisheria ya mtumiaji au kampuni yanahitaji ufichuzi wa maelezo Mtumiaji anapokubali Ikiamrishwa na mahakama
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	Haijabainishwa
	Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuvi vya tovuti	Aina za vidakuvi vinavyotumika: Vidakuvi vya kipindi: Ni vya muda mfupi na hutumika tu wakati mtumiaji anavinjani tovuti Vidakuvi vya kudumu: Ni vya kudumu na huhifadhiwa kwenye kifaa cha mtumiaji hadi muda wa mwisho wa kutumika au kufutwa na mtumiaji Vidakuvi vya mhusika wa kwanza: Vinamilikiwa na kuundwa na shinika la Dashen Vidakuvi vya mhusika mwingine: Vinamilikiwa na kuundwa na watoa huduma za programu ya Dashen

	Kuhifadhiwa kwa maelezo ya mtumiaji	
Programu ya HelloCash[6]	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
Ruhusa zinazotakikana		
Data Inayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Maelezo ya mawasiliano Nambari ya simu na mengineyo	
Data inayokusanywa kutoka kwa kifaa cha mtumiaji	Anwani ya Internet Protocol (IP), jina la kifaa, mfumo wa uendeshaji, mipangilio ya programu, tarehe na saa ya mtumiaji kutumia huduma	
Matumizi ya maelezo ya mtumiaji	Hakuna maelezo dhahiri kuhusu matumizi ya maelezo husika Sera inaeleza tu kwamba maelezo ya mtumiaji yatashirikiwa na wahusika wengine ili kusaidia katika utambulisho wa watumiaji	
Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Utambulisho wa watumiaji: Programu hutumia huduma za wahusika wengine ili kusaidia katika utambulisho wa watumiaji	
Jinsi wahusika wengine wanavyotumia maelezo/ Kufichuliwa kwa maelezo	Hushiniki maelezo na wahusika wengine kwa madhumuni yafuatayo: Kuwezesha huduma za programu ya HelloCash Kutoa huduma za HelloCash kwa niaba yake Kuchanganua huduma za programu ya HelloCash Wahusika wengine hawapaswi kufichua au kutumia maelezo ya mtumiaji kwa madhumuni mengine yoyote Haijabainishwa	
Muda wa wahusika wengine kufikia data		
Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuvi vya tovuti	Sera inaonyesha kwamba programu haitumii vidakuvi (hili linapaswa kuthibitishwa) Sera pia inaeleza kwamba programu hutumia vidakuvi vya wahusika wengine	
Kuhifadhiwa	Hawakikishii watumiaji usalama wa data yao	

Programu ya Mikopo ya Benki ya Biashara ya Ethiopia (Commercial Bank of Ethiopia Lending App)[7]	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	Huomba kufikia: anwani za mawasiliano za simu,na vipengele vingine (sera haibainishi vipengele hivi)
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Programu hukusanya maelezo kuhusu simu ya mtumiaji (sera haibainishi maelezo haya)
	Matumizi ya maelezo ya mtumiaji	Sera haielezi jinsi maelezo ya mtumiaji yanavyotumika
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Haijabainishwa
	Jinsi wahusika wengine wanavyotumia maelezo/ kufichuliwa kwa maelezo	Hushiriki maelezo ya mtumiaji chini ya hali zifuatazo: Mtumiaji anapotoa idhini yake Kwa kufanikisha maslahi yake ya kisheria Kwa utekelezaji wa mkataba na mtumiaji Kutimiza wajibu wa kisheria - yaani., kutii sheria, maombi ya serikali, kesi za mahakama, amri za mahakama, taratibu za kisheria Kwa upelelezi na uzuiaji wa ulaghai au shughuli haramu  Haijabainishwa
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Teknolojia za ufuatilaji/ vidakuvi tovuti	Haijabainishwa
	Jinsi programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Haijabainishwa

Programu ya TeleBirr ya kampuni ya EthioTelecom[9]	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	
	Maelezo Yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Hukusanya maelezo yafuatayo kutoka kwa watumiaji: Data iliyio kwenye maoni ya watumiaji waliyotoa kwenye tovuti, ikijumuisha anwani ya IP ya mtumiaji na kivinjari
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Haijabainishwa
	Jinsi programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Haijabainishwa
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Haijabainishwa
	Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuzi vya tovuti	Wanapotoa maoni kwenye tovuti, watumiaji wanaweza kuhifadhi maelezo yao kwenye vidakuzi vya tovuti, yaani., jina, anwani ya barua pepe n.k Vidakuzi vya muda mfupi: hufutwa mtumiaji anapofunga kivinjari Vidakuzi ambavyo huhifadhi maelezo ya kuingia katika akaunti ya mtumiaji wakati wa kuingia kwenye tovuti Vidakuzi vinavyohifadhiwa kwenye kivinjari cha mtumiaji anapohariri au kuchapisha makala kwenye tovuti
	Kuhifadhiwa kwa maelezo ya mtumiaji	Haikubainishwa.

## Uchanganuzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu Hizi

Ethiopia haina sheria ya jumla ya ulinzi wa data na faragha ya kuchunguza iwapo programu hizi zinatii sheria chini ya utafiti huu. Hata hivyo, nchi hii ina haki ya faragha iliyotolewa kwenye Katiba, ambapo kila mtu anahakikishiwa haki ya kutosakwa, kufanya msako nyumbani kwake au kwa mali yake. Katiba pia inawahakikishia watu haki ya faragha ya mawasiliano yao wanayofanya kwa kutumia simu au mawasiliano wanayofanya kwenye vifaa vya kielektroniki. Inawapa maofisa wa umma jukumu la kuheshimu na kulinda haki hii.<sup>124</sup>

Utafiti huu utaangalia mbinu za uchakataji wa data za programu hizi dhidi ya viwango vinavyohitajika vya ulinzi wa faragha na data ya binafsi.

<sup>124</sup> Kifungu cha 26, Katiba ya Shirikisho la Kidemokrasia la Jamhuri ya Ethiopia (Constitution of the Federal Democratic Republic of Ethiopia)

<https://www.refworld.org/docid/3ae6b5a84.html>

## **Uwazi wa Sera za Faragha**

Sera za faragha zinazochunguzwa hazina maelezo ya kutosha kuhusu mbinu zake za uchakataji. Hazimpi mtumiaji maelezo ya kutosha kuhusu data inayokusanywa, jinsi inavyokusanywa na matumizi yanayokusudiwa. Hazibainishi pia wahusika wengine watakaofikia data na muda watakaoifikia. Ni muhimu kutambua kuwa hakuna mbinu za ulinzi zinazotajwa ambazo zimekekwa ili kulinda data inayoshirikiwa na wahusika wengine, kipindi cha muda wa kuhifadhiwa kwa data hiyo, na mbinu za usalama zilizowekwa ili kulinda data wanayomiliki. Angalau, sera ya faragha inapaswa kutoa maelezo kuhusu masuala haya muhimu. Inapaswa kuwezesha mtumiaji kujua jinsi kampuni (kampuni ya programu ya mikopo dijitali) inalenga kutumia data yake na haki zake za kufikia na kurekebisha data yake.<sup>125</sup>

Sera za faragha za programu zinazochunguzwa katika utafiti huu zinaweza kusababisha wasiwaso kwa watumiaji kwa sababu ya ukosefu wa uhakika kuhusu jinsi zinavyotumia na kuhifadhi data yao. Hazitoi maelezo ya kutosha ili kuwezesha watumiaji kufanya maamuzi ya busara kuhusu matumizi yao ya programu.

## **Udhibiti wa Mtumiaji**

Mashirika yanayomiliki programu za mikopo dijitali yanapaswa kuruhusu watumiaji kudhibiti data yao. Yanapaswa kuwapa uwezo wa kujiondoa katika huduma ya kupokea ujumbe wa matangazo na kuawezesha kufikia na kuomba kurekebishwa na kufutwa kwa data yao. Ufikiaji wa data ya binafsi ni muhimu kwa sababu wamiliki wa data wana haki za kudhibiti data yao. Hata hivyo, uchunguzi wa programu hizi unaonyesha kwamba programu nyingi haziwawezeshi watumiaji kudhibiti data yao. Kwa mfano, programu ya mikopo ya Commercial Bank of Ethiopia na programu ya HelloCash hazitoi haki zozote kwenye sera zake. Ni programu ya Ethio Telecom na DashenBank ndizo tu zinawawezesha watumiaji kufikia data yao na kuomba kufutwa au kurekebishwa kwa data yao. Programu ya DashenBank inaendelea zaidi na kuwaruhusu watumiaji kujiondoa katika huduma ya kupokea ujumbe wa matangazo.

## **Usalama**

Usalama wa data ni muhimu zaidi, hasa wakati ambapo data nyingi ya binafsi inachakatwa. Programu za mikopo dijitali, kwa mfano, hukusanya data nyingi, na ufikiaji wa huduma zake unategemea data ya mtumiaji. Lazima ziweke mbinu thabiti za usalama ili kuzuia matukio ya ufichuzi haramu wa data na ufikiaji wa data ya mtumiaji na wahusika wenye nia mbaya. Baadhi ya programu hizi hazina vifungu vya usalama vinavyoonyesha mbinu za usalama zinazolenga kuweka.

## **Ufikiaji wa Data na Wahusika Wengine**

Programu hizi hazibainishi wahusika wengine wanaofikia data ya mtumiaji, maelezo wanayofikia, muda wanaoweza kufikia data hiyo, na mbinu ambazo programu hizi zimekekwa ili kuhakikisha usalama wa data inayofikiwa na wahusika wengine. Programu ya DashenBank ndio programu pekee inayobainisha wahusika wengine wanaofikia maelezo ya binafsi ya mtumiaji.

## **Kuhifadhiwa kwa Data**


Programu zinazochunguzwa hazielezi muda ambaa zinalenga kuhifadhi data ya mtumiaji na vigezo zinavyotumia ili kubainisha kipindi hicho cha muda wa kuhifadhi. Zinaacha watumiaji bila uhakika kuhusu muda ambaa mashirika haya yatahifadhi data yao na iwapo shughuli hiyo ya kuhifadhi itaendelea hata baada ya kuondoa programu hizi kwenye vifaa vyao. Madhumuni ya ukusanyaji wa data

Mhusika anayechakata data ya binafsi ya mmiliki wa data anapaswa kubainishwa moja kwa moja aina ya data inayokusanywa na madhumuni ya ukusanyaji wa data. Sera za faragha za programu zinazochunguzwa kwenye utafiti huu hazibainishi madhumuni ya ukusanyaji wa data kwa watumiaji. Programu pekee inayotoa maelezo haya ni programu ya Dashen Bank, ambayo inaorodhesha maelezo yanayokusanywa na matumizi yake.<sup>126</sup>

---

<sup>126</sup> Sera ya Faragha ya programu ya Dashen Bank: Kifungu cha Ukusanyaji  
<https://dashenbanksc.com/privacy-and-security/>

# Gabon



## Maelezo ya Nchi

Katika Jamhuri ya Gabon, Gabon ni nchi inayotumia lugha ya Kifaransa inayopatikana katika eneo la Afrika ya Kati yenye idadi ya watu 2,172,579<sup>127</sup>. Mstari wa ikweta umepita nchini na inapakana na Jamhuri ya Kongo, Ginekweta (Equatorial Guinea) na Kameruni. Ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Kiuchumi na Fedha ya Mataifa ya Afrika ya Kati (Economic and Monetary Community of Central African States (CEMAC)<sup>128</sup> ina GDP ya Dola biliioni 16.87 za Marekani (2019)<sup>129</sup> na ina mfumo wa utawala wa rais na waziri mkuu<sup>130</sup>.

127 <https://fr.coutryeconomy.com/pays/gabon>

128 Jumuiya ya Kiuchumi na Fedha na Mataifa ya Afrika ya Kati (Economic and Monetary Community of Central African States (CEMAC) ni shirika la kimataifa linaloleta pamoja nchi kadhaa za eneo la Afrika ya Kati, lilloundwa kuchukua nafasi ya shirika la Muungano wa Kiuchumi na Forodha wa Afrika ya Kati (Economic Union of Central Africa (UDEAC). Makao makuu yake yanapatikana Bangui, Jamhuri ya Afrika ya Kati. Linaleta pamoja nchi zifuatazo: Kameruni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Kongo-Brazzaville, Gabon, Ginekweta (Equatorial Guinea) na Chad.

129 <https://www.google.com/search?client=avast-a-1&q=le+GDP+du+gabon&oq=le+PIB+du+gabon&aqs=avast..69i57j0l6.9968j0j4&ie=UTF-8> (Source World Bank)

130 [http://archive.ipu.org/parline-fr/reports/CtrParlementaire/1115\\_F.htm](http://archive.ipu.org/parline-fr/reports/CtrParlementaire/1115_F.htm)

## Ulinzi wa Data Nchini Gabon

Ulinzi wa data ya binafsi nchini Gabon unasimamiwa na sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011<sup>131</sup>. Sheria hii inatumika kwa uchakataji wowote wa kiotomatiki au usio wa kiotomatiki unaofanywa nchini Gabon<sup>132</sup>. Tume ya Kitifa ya Ulinzi wa Data ya Binafsi (National Commission for the Protection of Personal Data (CNPDCP)<sup>133</sup> ndio DPA ya Gabon. Iliundwa na sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011, na inawajibika katika kuhakikisha kuwa uchakataji wa data ya binafsi unaheshimu faragha ya watu<sup>134</sup>. Pia, shughuli za kifedha za kielektroniki zinasimamiwa na Amri Nambari 00000014 / PR / 2018 ya tarehe 23 Februari 2018.

## Utangulizi

Kulingana na ripoti ya pamoja "Stimulating Electronic Commerce in Central Africa: Role of Mobile Services and Policy Implications" ya shirika la Global Grouping of Mobile Telephone Operators (GSM Association) na Economic Commission for Africa (ECA), mataifa ya Afrika ya Kati yameachwa nyuma na mataifa ya maeneo mengine ya Afrika kuhusiana na ufikiaji wa huduma ya intaneti ya simu za mkononi. Kweli, data kutoka shirika la GSMA Intelligence inaonyesha kuwa kiwango cha kupenya kwa huduma ya intaneti ya simu za

131 <https://www.afapdp.org/wp-content/uploads/2012/01/Gabon-Loi-relative-%c3%a0-la-protection-des-donn%c3%a9es-personnelles-du-4-mai-2011.pdf>

132 Kifungu cha 2 na 4 vya Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

133 Kwa maelezo zaidi: <https://www.cnpdcp.ga/presentation/>

134 Kifungu cha 11 cha Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

mkononi ndani ya Jumuiya ya Kiuchumi na Fedha ya Mataifa ya Afrika ya Kati (Economic Community of Central African States (ECCAS) kilifika 23% mwaka wa 2019, dhidi ya 43% katika eneo la Afrika Kaskazini., 29% katika Muungano wa Kiuchumi wa Mataifa ya Afrika Magharibi (Economic Community of West African States (ECOWAS), 26% katika jumuiya ya Afrika Kusini na 21% katika Afrika Mashariki. Kando na hayo, eneo hili bado linakabiliwa na changamoto kubwa kama vile upungufu wa maarifa ya ICT na uwezo dhaifu wa kishirika wa kukuza biashara bunifu. Mambo yote ambayo hayawezeshi ukuaji wa Huduma ya Kutuma na Kupokea Pesa kwa Njia ya Simu (Mobile Money). Hata hivyo, ndani ya ECCAS, Gabon ni ya kwanza kuhusiana na suala la kupenya kwa huduma ya intaneti, ikiwa na kiwango cha 38%. Pia, kiwango cha kupenya kwa huduma ya kutuma na kupokea pesa kupitia simu kilikuwa juu nchini Gabon (43% ya idadi ya watu wenye umri wa zaidi ya miaka 15 walikuwa na akaunti mwaka wa 2017 ikilinganishwa na kiwango cha 6.7% mwaka wa 2017) lakini kilibaki kuwa cha juu kuliko katika mataifa mengiye ya eneo hilo 15% nchini Kameruni na Chad, na 6% nchini Kongo na chini ya kiwango cha nchini Kenya 73%.

Zaidi ya hayo, huduma ya kutuma na kupokea pesa kupitia simu katika Afrika ya Kati na Gabon inaendelea kuhusishwa na huduma rahisi kama vile kuweka na kutoa pesa kwenye simu za mkononi. Kampuni za simu za mkononi hutekeleza shughuli hizi: Airtel Mobile Gabon, Moov Africa Gabon, benki fulani (BGFI Bank, Ecobank Gabon, nk.) zinazotoa huduma dijitali kwa wateja wake wa kawaida na FinTechs (E-Doley Finance, Fedha Finance, nk.) zenyе huduma za fedha za kielektroniki. Kwa sababu ya kampuni hizi, huduma za kutuma na kupokea pesa kupitia simu zinakuruhusu kulipia usajili wako wa huduma ya televisheni kwa mbali, bili zako za maji na stima, karo yako ya shulenii na chuo kikuu, na pia kodi za mali yako nk.

Licha ya uwezo huu unaotolewa kwa watu, shughuli za mikopo na mikopo dijitali bado hazijaimarika zaidi nchini Gabon kama vile katika eneo la Afrika Mashirika. Ni huduma mbili pekee za mikopo dijitali zinazotolewa nchini Gabon na kampuni za nje ya nchi. Viva PS inatoa huduma ya kwanza kupitia huduma yake ya Open Loans Gabon<sup>135</sup>. Huduma hii inawezesha mtu kupata mikopo ya binafsi bila dhamana moja kwa moja na kuunganisha wakopaji na wakopeshaji wanaopatikana nchini Gabon. Lengo lake ni kuunda soko fanisi na linalofanya kazi la mikopo ya papo hapo kati ya watu nchini Gabon. Mikopo inayotolewa inatozwa niba ya kiwango cha kati ya 12% na 15%, kiasi cha chini zaidi cha malipo na kipindi cha malipo cha siku 90 na siku 365, mtawalia. Huduma hizi pia zinapatikana katika nchi za Afrika kama vile Ghana, Kenya, Naijeria na Tanzania. Spectro Coin inatoa huduma ya pili ya usambazaji wa sarafu dijitali kupitia huduma ya Crypto Loans kwenye huduma yake ya Bitcoin Wallet inayotolewa na programu ya SpectroCoin. Huduma hii, iliyoanzishwa mwaka wa 2013, inaruhusu wamiliki wa akaunti za sarafu dijitali (Bitcoin, Ethereum nk.) nchini Gabon kupata na kuhakikishiwa mikopo inayoweza kubadilishwa kwenye sarafu mbalimbali kama vile Euro (€) au dola (\$). Mikopo hii inaanzia € 25 hadi zaidi ya € 15,000 () (FCFA 16,000 hadi zaidi ya FCFA 9,000,000). Kwa sababu ya kuanza kutumika polepole kwa sarafu dijitali duniani kote, aina hii ya huduma itaendelea kuzidi kusambaa. Ingawa zinaongeza uwezo wa kufikia huduma za fedha kwa raia na hasa kwa wakopaji wa kibinafsi, tofauti hizi zinawezesha watoa huduma kukusanya data kuhusu wateja wao ili kufuatilia shughuli za kifedha na kukusanya madeni. Mbinu hii inaweza kuingilia faragha ya mtumiaji na lazima ichunguzwe kwa uadilifu. Aina hii ya huduma ya mikopo inayotolewa kupitia programu za simu ilianzishwa baada ya sheria ya ulinzi wa data kuanza kutekelezwa nchini Gabon<sup>136</sup>. Je, mbinu za uchakataji wa data za programu hizi, kama inavyoelezwa katika sera na sheria na masharti yake ya matumizi, zinazingatia sheria za ulinzi wa faragha?

Utafiti huu unalenga kuchanganua sera za faragha na sheria na masharti ya programu

<sup>135</sup> Open Loans Gabon a été lancé en Janvier 2018

<sup>136</sup> Loi n°001/2011 du 25 septembre 2011 relative à la protection des données à caractère personnel au Gabon.

hizi na kuchunguza jinsi zinavyotii sheria ya ulinzi wa data nchini Gabon. Sehemu ya kwanza inajumuisha muhtasari wa data inayokusanywa na programu hizi. Sehemu ya pili inachunguza shughuli zake za uchakataji chini ya sheria ya ulinzi wa data ya binafsi. Sehemu ya mwisho inakamilika kwa kuonyesha iwapo programu hizi zinatii sheria inayolinda data ya binafsi au la.

## Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali

Open Loans Gabon <sup>137</sup> Kiungo cha kupakua : Google Play Store <sup>138</sup>	Maelezo yanayokusanywa na kuchakatwa na programu	
	Ruhusa zinazoombwa	<p>Wakati wa kufunguka, Programu ya Open Loans Gabon huomba:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>· Kudhibiti simu za mtumiaji · kufikia SMS za mtumiaji: Huonyesha SMS za mtumiaji ili kukusanya maelezo ya fedha na data ya shughuli za kifedha ili kukusanya maelezo kuhusu historia ya fedha ya mtumiaji na kubainisha ufaafu wake wa kupokea mikopo</li> <li>Kufikia anwani za mawasiliano za mtumiaji</li> <li>Kufikia data ya mahali, kifaa na matumizi: Programu ya Open Loans Gabon hutumia teknolojia ya GPS au huduma zingine za data ya mahali ili kubainisha mahali mahususi alipo mtumiaji</li> <li>. Kufikia Kalenda ya Mtumiaji, Programu ya Open Loans Gabon husoma matukio ya kalenda pamoja na maelezo ya siri, kuongeza au kubadilisha matukio ya kalenda na kutuma barua pepe kwa wageni bila mtumiaji kujua.</li> <li>. Kufikia Picha / Maudhui anuai / Faili, Programu ya Open Loans Gabon husoma maudhui ya nafasi yako ya hifadhi ya USwB, kubadilisha au kufuta maudhui ya nafasi yako ya hifadhi ya USB, inaweza kusoma maudhui ya nafasi ya hifadhi ya USB, kubadilisha au kufuta maudhui ya nafasi yako ya hifadhi ya USB</li> <li>. Programu ya Open Loans Gabon inaweza pia kupokea data kutoka kwenye intaneti, kuangalia miunganisho ya mtandao, ufikaji kamili wa mtandao, kufunguka kifaa kinapowashwa, kuchomoza juu programu zingine, kudhibiti mtetemo, kuzuia kifaa kuingia katika hali tuli na kuweka kengele.</li> </ul>
	Maelezo Yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	<p>Wakati wa kujisajili, programu ya Open Loans Gabon hukusanya maelezo ya mtumiaji: anwani ya barua pepe, jina na nambari ya simu, maelezo ya fedha na malipo, kitambulisho, anwani zinazotolewa na mtumiaji, marejeleo ya mikopo na nchi anakoishi.</p>

137 Sera ya Faragha ya Mikopo

138 <https://play.google.com/store/apps/details?id=com.viva.openloansglobal>

	Maelezo Yanayokusanywa Kutoka Kwenye Kifaa cha Mtumiaji	Tovuti ya Open Loans Gabon hukusanya maelezo yafuatayo kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji: Mbinu ya Utashi wa Kompyuta (Artificial Intelligence (AI): muundo wa simu, nambari ya IMEI au nambari ya kitambulisho, maelezo ya SIM kadi, maelezo ya mtandao wa simu, mfumo wa uendeshaji wa kifaa, aina ya kivinjari, data ya mahali ya kifaa na kuweka mipangilio ya saa za eneo
	Maelezo Yanayokusanywa Unapotumia Tovuti	Maelezo yaliyohifadhiwa kwenye kifaa: orodha ya anwani za mawasiliano, nekodi za nambari za simu, rekodi za SMS, anwani zilizo kwenye akaunti za mitandao ya kijamii, picha, video au maudhui yoyote dijitali husika.
		Baada ya mtumiaji kuunganisha kifaa kwenye mtandao, data ya programu hutumwa kuititia HTTPS. Kisha maelezo haya huchanganywa kwa madhumuni ya uchanganuzi au matangazo na kufichuliwa kwa Orange Bank.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Programu ya Open Loans Gabon hupokea sajili kutoka kwa wakopeshaji katika kila nchi ambapo programu hizo zinatumika: Kenya, Ghana, Naijeria na Tanzania ili kuwapa wakopaji chaguo nyingi za huduma kadri iwezekanavyo wanapotafuta ufadhili.
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Sera ya faragha ya Programu ya Open Loans Gabon inaeleza kwamba hukusanya data ya watumiaji kwa madhumuni yafuatayo: <ul style="list-style-type: none"> <li>· kushughulikia shughuli za kifedha za mtumiaji</li> <li>· Kuthibitisha utambulisho wa mtumiaji</li> <li>· Kutoa mikopo na ukusanyaji wa malipo</li> <li>· Kutoa mikopo na kuunda mifumo ya kutoa mikopo</li> <li>· kuchanganua tabia za mkopaji</li> <li>· kutii · kutii sheria, vifungu na kanuni zinazohusiana na mchakato wa “jua mteja wako” na kanuni za kupinga ulangizi wa pesa</li> <li>· Kuzuia ulaghaji,</li> <li>· Huduma za matangazo</li> <li>. Wajibu wa Programu ya Open Loans Gabon kwa watumiaji</li> </ul> <p>Data nyeti na ya binafsi ya mtumiaji inayokusanywa na programu kwa ruhusa ya mtumiaji na kulindwa na sera hii inajumuisha tu maelezo yanayoweza kumtambulisha mtu, maelezo ya fedha na malipo, maelezo ya uthibitishaji, anwani zinazotolewa na mtumiaji, manejeleo ya mikopo na nchi anakoishi.</p>

	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine  Muda ambao data inafikiwa na wahusika wengine	Programu ya Open Loans Gabon hushiriki maelezo ya mtumiaji na wakopeshaji wengine ili kuchanganua hatari ya kutoa mkopo na kufanya maamuzi ya kutoa mikopo. Maelezo kuhusu wanaotembelea tovuti wasiotambulika yanaweza kutolewa kwa wahusika wengine kwa madhumuni ya matangazo, utangazaji au madhumuni mengine. Wahusika hawa wanakubali kudumisha usiri wa maelezo haya na hawapaswi kuyafichua.  Sera yake haitoi maelezo yoyote kuhusu muda ambao wahusika wengine wanaweza kufikia maelezo ya binafsi ya mtumiaji na kuyahifadhi. Wahusika walijotajwa hawaruhusiwi kufuatilia tabia za mtumiaji.
	Vidakuzi/ teknolojia za ufuatiliaji za tovuti	Programu ya Open Loans Gabon inaeleza kuwa haitumii vidakuzi kwa madhumuni ya ufuatiliaji. Kwa miunganisho ya kompyuta, mtumiaji hypokea onyo vidakuzi vinapotumwa. Kwa hivyo, mtumiaji ana uhuru wa kuamua kukubali au kukataa vidakuzi vyote.
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Maelezo ya binafsi ya mtumiaji huhifadhiwa kwenye mitandao salama. Yanafikiwa tu na watu wachache walio na haki maalum za kufikia mifumo hii na lazima wadumishe faragha ya maelezo haya. Kando na hayo, maelezo yote nyeti / ya mikopo yanayotolewa husimbwa kwa kutumia teknolojia ya Secure Socket Layer (SSL). Shughuli zote za kifedha huchakatwa kuitia mtoa huduma za malipo na hazihifadhiwi wala kuchakatwa kwenye seva za huduma ya Open Loans Gabon. Kando na hayo, mbinu mbalimbali za usalama huwekwa wakati mtumiaji anaweka, kutuma au kufikia maelezo yake ili kudumisha usalama wa data yake.

Programu ya Bitcoin Wallet ya SpectroCoin <sup>139</sup>  Kiungo cha kupakua : Google Play Store na Apple Store	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu
---	--

Ruhusa Zinazotakikana	<p>Wakati wa kufunguka, programu ya Bitcoin Wallet huomba:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>· Kudhibiti maelezo ya utambulisho wa mtumiaji, kutafuta akaunti zilizo kwenye kifaa na kuongeza au kuondoa akaunti.</li> <li>. Kufikia data ya mtumiaji</li> <li>. Kufikia Picha za mtumiaji / Maudhui anuai / Faili na maudhui mengine, kusoma maudhui ya nafasi yako ya hifadhi ya USB na kubadilisha au kufuta maudhui ya nafasi yako ya hifadhi ya USB.</li> <li>. Kufikia kamera ili kupiga picha na video na maikrofoni ili kurekodi sauti.</li> </ul> <p>Kufikia Data ya Mahali Mtumiaji Alipo, Kifaa na Matumizi: Programu ya Bitcoin Wallet hutumia teknolojia ya GPS au huduma zingine za data ya mahali ili kubainisha mahali mahususi alipo mtumiaji</p> <p>. Inaweza pia kuangalia miunganisho ya mtandao, kuunda akaunti na kuweka manenosini, kufikia mtandao kikamilifu, kubadilisha mipangilio ya sauti ya mtumiaji na kuzuia vifaa kuingia katika hali tuli.</p> <p>. Vipengele vinaweza kuongezwa kiotomatiki ndani ya kila kikundi katika tukio la sasisho la programu ya Bitcoin Wallet ya SpectroCoin</p>
Maelezo Yanayokusanywa Kutoka kwa Mtumiaji	<p>Wakati wa kujisajili, programu ya Bitcoin Wallet hukusanya maelezo yafuatayo kuhusu watumiaji: (i) Data ya jumla ya utambulisho: jina la kwanza, jina la katikati, jina la zamani, majina bandia, jina la ukoo, jinsia, tarehe ya kuzaliwa, anwani ya makazi, barua pepe, nambari ya simu, picha ya kujipiga (na hati ya utambulisho), video ya moja kwa moja; (ii) data ya hati ya utambulisho: Aina ya Kitambulisho (Pasipoti / Kadi ya Kitambulisho / Kibali cha Mkazi), nakala yake, MRZ, nambari ya hati, tarehe ya kutolewa, tarehe ya mwisho wa matumizi; (iii) Maelezo mengine ya Wasifu wa mtumiaji: aina ya wasifu, kitambulisho cha mwanachama, msimbo wa kuelekezwa, hali ya kuingia katika akaunti, hali ya kuthibitishwa kwa barua pepe, hali ya kuthibitishwa kwa simu, maelezo ya maswali ya siri; (iv) Data ya mitandao ya kijamii: aina ya kuingia katika mitandao ya kijamii, picha ya wasifu wa mtandao wa kijamii, jina, jina la ukoo, maoni yako, hisia na vitendo vingine unavyoonyesha kuititia akaunti yetu ya mitandao ya kijamii, maelezo mengine ya mitandao ya kijamii uliyotoa; na (v) Maelezo kuhusu Kazi ya mteja na vyanzo vya mapato: kazi maalum, sekta kuu za Kazi ya mteja, chanzo cha mali na fedha zilizo katika Akaunti ya mteja, chanzo cha mapato yasiyobadilika, maelezo kuhusu asilimia ya mapato katika Shughuli ya mteja iliyoitajwa iliyoshughulikiwa kwa pesa taslimu.</p>

<p>Maelezo Yanayokusanywa Kutoka Kwenye Kifaa cha Mtumiaji</p> <p>Maelezo Yanayokusanywa Unapotumia Tovuti ya <a href="https://spectrocoin.com">https://spectrocoin.com</a></p>	<p>Programu ya Bitcoin Wallet hukusanya maelezo yafuatayo kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji: Mbinu ya Utashi wa Kompyuta (Artificial Intelligence (AI): muundo wa simu, nambari ya IMEI au nambari ya kitambulisho, maelezo ya SIM kadi, maelezo ya mtandao wa simu, mfumo wa uendeshaji wa kifaa, aina ya kivinjari, data ya mahali ya kifaa na mipangilio ya saa za eneo</p> <p>Maelezo yaliyohifadhiwa kwenye kifaa: orodha ya anwani za mawasiliano, rekodi za nambari za simu, rekodi za SMS, anwani zilizo kwenye akaunti za mitandao ya kijamii, picha, video au maudhui yoyote dijitali husika.</p> <p>Mtumiaji anapotumia tovuti ya Spectro Coin, Programu ya Bitcoin Wallet hukusanya kiotomatiki maelezo yafuatayo na kuyahifadhi kwenye faili zake za kumbukumbu:</p> <p>Anwani ya IP ya mtumiaji, aina ya kivinjari, mto huduma za intaneti (ISP), kurasa za uelekezaji / kuondoka, mfumo wa uendeshaji, muhuri wa muda na maudhui ya kuvinjari.</p> <p>Kisha maelezo haya huchanganywa kwa madhumuni ya uchanganuzi au matangazo.</p>
<p>Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine</p>	<p>Kampuni hukusanya data yako moja kwa moja kutoka kwako au wahusika wengine wakati: unatumia au kutembelea Mfumo; unajisajili kwenye Mfumo; unatumia Huduma zetu; unaomba usaidizi kwenye Huduma; tunafanya ukaguzi wa historia ya mteja au ukaguzi wa historia unaoendelea; tunafuutilia shughuli zako za kifedha; tunaangalia iwapo huhuishwi na shughuli ya ulaghai; tunapokea maombi, maagizo, maamuzi, nk ya wahusika wengine kukuhusu.</p> <p>Kampuni inaweza pia kukusanya data yako kutoka kwa kampuni zingine za SpectroCoin, kama inavyoelezwa katika Sheria na Masharti ya Mfumo unapobadilisha kampuni ya Spectro Coin kama mto huduma wako.</p>

	<p>Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji</p> <p>Sera ya faragha ya programu ya Bitcoin Wallet inaeleza kwamba inakusanya data ya mtumiaji ili: Kufungua akaunti ya mtumiaji; . Kutekeleza Huduma (kama vile kuuza na kununua, kutoa pesa, kuweka pesa, kubadilisha shughuli za kifedha); . Kuzuia ulangizi wa pesa na ufadhilli wa shughuli za kigaidi (kutekeleza kanuni ya "Jua Mteja Wako"); . Kuzuia uhalifu; . Kutii na kutekeleza vikwazo vyta kimataifa; . Kutoa huduma za usaidizi; . Kuhakikisha ubora; . Kusajiliwa kwenye orodha ya wanaosubiri kupokea Huduma; . Kutuma matangazo moja kwa moja na matumizi ya akaunti za mitandao ya kijamii za Kampuni; . Kuhakikisha utendakazi sahihi na salama wa Mfumo wa Bitcoin Wallet.</p>
<p>Maelezo Yanayoshinikiwa na Wahusika Wengine</p> <p>Muda Ambao Data Inafikiwa na Wahusika Wengine</p>	<p>Programu ya Bitcoin Wallet hushiriki maelezo ya mtumiaji na mashinika mengine ya kundi la Spectrocoin katika nchi 40 ili kusaidia shughuli ya ufuatiliaji wa wateja na mamlaka za kimataifa zinazosimamia vita dhidi ya uhalifu wa mtandaoni, ulangizi wa pesa, ulinzi wa data ya binafsi, ofisi za usimamizi wa mikopo,nk</p> <p>Kulingana na aina ya data ya binafsi na madhumuni ya uchakataji wake, kipindi cha kuhifadhiwa kwa data yako huwekwa na Kampuni, kama inavyohitajika na sheria au desturi za biashara, ili kuhakikisha utoaji wa Huduma ipasavyo</p>
<p>Teknolojia za Ufuatiliaji / Vidakuzi vya Tovuti</p>	<p>Programu ya Bitcoin Wallet hutumia teknolojia za ufuatiliaji wa simu na vidakuzi vya tovuti ili kutofautisha watumiaji wa Programu. Sera ya Vidakuzi (inayojulikana kuanzia sasa kama "Sera ya Vidakuzi") inatumika kwa ufikiaji wa tovuti (<a href="https://spectrocoin.com">https://spectrocoin.com</a>) na vikoa/vikoa vidogo vingine vyetu kama vile <a href="https://spectrocoin.com/crypto-loans/app">https://spectrocoin.com/crypto-loans/app</a>, <a href="https://exchange.spectrocoin.com">https://exchange.spectrocoin.com</a> au tovuti, ukurasa, kipengele au maudhui mengine yoyote na inaeleza aina za vidakuzi husika.</p>

Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Programu ya Bitcoin Wallet huchakata data ya binafsi ili kufanikisha madhumuni yaliyobainishwa kwenye sera hii. Ili kuweka vipindi nya muda wa kuhifadhiwa kwa data iliyokusanywa, Kampuni ilirejelea vifungu nya sheria na mapendekezo ya umma kama vile kutii vipindi nya kisheria nya kikomo na desturi za sasa za biashara. Kampuni hutumia taratibu na teknolojia mbalimbali za kuhakikisha usalama ili kulinda data yako dhidi ya uchakataji haramu au ambao haujaidhinishwa, kupotea kiajali, kutumiwa vibaya, kufikiwa bila idhini, kutumiwa kinyume cha sheria, kuhanibowi, kufichuliwa, nk. Hii inajumuisha mbinu za usalama za kisheria, kishirika, kiufundi na halisi, kama vile mifumo mipyä zaidi ya usalama, manenosiri, uwezo wa kutambua mashambulizi ya uhalifu wa mtandaoni na vitisho vingine kwa uadilifu wa Mfumo, kufanya kazi na huduma za kuaminika za watoa huduma, nk. Hata hivyo, hakuna shughuli yoyote ya utumaji wa maelezo kuititia barua pepe au njia nyingine za mawasiliano ya simu au ufikiaji wako wa Mfumo au Huduma kuititia intaneti ambayo ni salama kabisa. Kwa hivyo, unapaswa kutahadhari unapotumia Mfumo au kutumia Huduma kuititia intaneti au kushiriki maelezo ya siri kuititia barua pepe au njia nyingine za mawasiliano ya simu.
--	---

## **Uchunguzi Kifani: Suala la iwapo uchakataji wa kiotomatiki wa data hufanywa nje ya nchi ya Gabon na mahali ambapo wadhibiti wa data wanapatikana**

Sheria ya tarehe 25 Septemba 2011, kuhusu ulinzi wa data ya binafsi katika vifungu vyake vya 2, 3 na 4 inaeleza kwamba inatumika kwa uchakataji wote wa kiotomatiki au usio wa kiotomatiki wa data ya binafsi unaofanywa nchini Gabon. Kuhusiana na programu hizi mbili, hata kama kampuni zinazotoa huduma zake zinapatikana nje ya nchi ya Gabon, sheria iliyotajwa inatumika kwa kampuni hizo. Hata hivyo, sera za faragha zilizotolewa na kampuni hizi mbili hazielezi uhusiano wowote na Tume ya Kitaifa ya Ulinzi wa Data ya Binafsi (National Commission for the Protection of Personal Data (CNPDCP). Hali hii inazua swali la kufuatilia mbinu za uchakataji wa data za kampuni zinazopatikana nje ya nchi au data inayokusanywa.

## **Uchanganuzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu za Mikopo Dijitali Kuhusiana na Sheria Inayohusiana na Ulinzi wa Data Binafsi**

Sheria ya ulinzi wa data ya Gabon imebainisha kwa uwazi wajibu wa kisheria kuhusiana na ulinzi wa faragha, unaotumika katika uchakataji wowote, iwe ni wa kiotomatiki au la<sup>140</sup>. Kwa kufanya hivyo, programu za mikopo dijitali zinahusika. Hata hivyo, kutoptaka na kuanzishwa kwake hivi karibuni, hatari za ulinzi wa faragha ni mpya. Sehemu hii inaangazia vifungu husika nya Sheria ili kutambua iwapo Programu hizi zinatii vifungu hivi.

## **Haki ya Faragha**

Sheria ya ulinzi wa data inahitaji wadhibiti na wachakataji wa data (katika hali hii, programu za mikopo dijitali) washughulikie data ya binafsi kwa njia ambayo inaheshimu haki ya faragha

ya wahusika.<sup>141</sup> Katika hali hii, Sheria inazitaka kampuni zinazotoa huduma za programu hizi zihakikishe kuwa haki ya faragha ya mkopaji inazingatiwa kwanza wakati wa kuchakata data yake. Programu zilizofanyiwa utafiti zinakiuka haki hii na zinachakata data ambayo inaingilia faragha ya mtumiaji na isiyohusiana na madhumuni ya ukusanyaji wa data. Kwa mfano, programu hizi hukusanya maelezo kama vile anwani za mawasiliano zilizohifadhiwa kwenye kifaa cha mkopaji, maelezo ya kuingia katika akaunti kwenye mifumo ya mitandao ya kijamii, na data sahihi ya moja kwa moja ya mahali, Picha/Maudhui/Faili za mtumiaji nk. Mwenendo ambao unasababisha ukiukaji wa sheria za ulinzi wa data ya binafsi na madhumuni ya ukusanyaji wake.

## **Uhalali, Haki na Uwazi**

Sheria ya ulinzi wa data inahitaji programu zikusanye na kuchakata data kwa njia ya haki na ya kisheria.<sup>142</sup> Kulingana na kifungu hiki, lazima kampuni zipate idhini ya watumiaji.<sup>143</sup>, Wamiliki wa data lazima wajulishwe kwa uwazi na kwa ufupi kuhusu jinsi data yao itakavyotumika na kuhakikisha kuwa vifungu vyote vya sheria vinafuatwa katika uchakataji huo.<sup>144</sup>

Katika hali hii, programu zinapaswa kufahamisha watumiaji kwa nini data yao inakusanywa, jinsi data yao itakavyotumiwa na, ikiwa itashirikiwa na wahusika wengine, ni nani ambao data yao itashirikiwa nao na muda ambao watahifadhi data hiyo. Inaweza kusemekana kuwa programu zilizofanyiwa utafiti zinaleza kwa uwazi kwa nini zinakusanya data ya mtumiaji na wahusika zinaoshiriki nao data hiyo. Hata hivyo, hazielezi muda ambao wahusika wengine watafikia data hiyo na muda ambao watahifadhi.

## **Kikomo cha Madhumuni, Ufaafu na Utoshelevu**

Programu za mikopo dijitali zinahitajika chini ya sheria ya ulinzi wa data kuchakata data ya binafsi baada ya ukusanyaji wa data.<sup>145</sup> Hii inamaanisha kuwa zinapaswa tu kukusanya data iliyo ndani ya vikomo vya kutoa mikopo dijitali wala si data isiyohusiana na madhumuni hayo. Programu pia zinahitajika kukusanya tu data husika, ya kutosha na inayohusiana na madhumuni ya ukusanyaji.<sup>146</sup>

Programu zilizochunguzwa hukusanya maelezo ya binafsi ambayo hayahusiki na ya kinyume cha madhumuni ya ukusanyaji wa data. Hukusanya maelezo kuhusu wakopaji kama vile maelezo yao ya mitandao ya kijamii, anwani za mawasiliano za simu, picha na video, ambayo hayahusiki na utoaji wa mikopo dijitali.

## **Kushiriki Maelezo na Wahusika Wengine**

Sheria ya ulinzi wa data inaeleza kwamba programu hizi lazima ziwafahamishe watumiaji kuhusu wahusika wengine<sup>147</sup> ambao zitashiriki nao data yao, ikijumuisha mbinu zilizowekwa ili kulinda usalama wa data yao kabla ya kuikusanya.<sup>148</sup> Ukosefu wa kipindi maalum cha muda wa kuchakata na kuhifadhi data kinasababisha ukiukaji wa haki ya faragha.

Katika mchakato wa ulinzi na uzuiaji wa ulangazi wa pesa, programu zilizokaguliwa hushiriki maelezo ya mtumiaji/mkopaji na wahusika wengine kama vile washirika wake, washirika wa kibiasara na mashirika ya serikali na ya utekelezaji wa sheria. Data ya binafsi nk, haibainishi mbinu za ulinzi zilizowekwa ili kulinda data ya mkopaji. Programu hizi pia hazielezi muda ambao wahusika hawa wataweza kufikia data na muda watakaoihifadhi. Kando na hayo,

<sup>141</sup> Vifungu vya 2,3 na 4 vya Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>142</sup> Kifungu cha 45 cha Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>143</sup> Kifungu cha 46 cha Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>144</sup> Kifungu cha 8, 66, 68 na 69 vya Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>145</sup> Kifungu cha 45 cha Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>146</sup> Kifungu cha 45 cha Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>147</sup> Kifungu cha 13 cha Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>148</sup> Kifungu cha 14, 48, 60 na 66 vya Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

kanuni za faragha za programu hizi mbili hazibainishi uhusiano wake maalum na DPA ya Gabon.

## **Usiri Kimuundo na kwa Chaguomsingi**

Sheria inaeleza kwamba mdhibiti wa data lazima aweke mikakati yote ya kuchakata data ya mtumiaji<sup>149</sup>. Programu hizi zina mbinu za usimbaji zinazotumika ili kulinda mawasiliano na maudhui ya siri ya watumiaji wake—ambacho ni kiwango cha usalama kinachohitajika ili kulinda data ya mtumiaji. Hata hivyo, kiwango cha usalama kilichojuishwa hakiwezi kuzuia mtoa huduma ya Programu kukusanya maelezo ya ziada.

## **Haki ya Kufikia na Kufuta Data ya Binafsi**

Watumiaji wa programu wana haki ya kufikia data yao inayohifadhiwa na programu hizi na kuomba kufutwa au kuharibiwa kwa data yao ambayo programu hizi haziruhusiwi tena kuihifadhi, au haihusiki, ni ya ziada au ilipatikana kwa njia haramu<sup>150</sup>. Watoa huduma za programu wameweka huduma maalum za kupokea maombi ya watumiaji kuhusiana na suala hili.

## **Kuhamishika kwa Data**

Sheria inawapa wamiliki wa data haki ya kupokea data yao kwa muundo uliopangwa na unaoweza kusomeka na mashine. Inawapa pia haki, panapowezekana kiufundi, kuhamishia data moja kwa moja kwa wadhibiti au wachakataji wengine wa data.

<sup>151</sup> Programu zinazochunguzwa haziwapi watumiaji njia za kutekeleza haki hii.

## **Kanuni za kufuata kabla ya kutekeleza uchakataji wa data ya binafsi**

Sheria inaeleza kwamba uchakataji wa data ya binafsi kiotomatiki lazima ubainishwe kwa Tume ya Kitaifa ya Ulinzi wa Data ya Binafsi (National Commission for the Protection of Personal Data (CNPDCP)<sup>152</sup>. Sheria ilitoa mamlaka ya kuteua ofisa wa ulinzi wa data. Kifungu hiki kilitungwa kimsingi kwa sababu ya makao ya watoa huduma za programu zinazochunguzwa<sup>153</sup>. Ukaguzi wa hati za mapendekezo kutoka kwa shirika la CNPDCP haubainishi kuwa kampuni zinazochunguzwa zilipata idhini hizi.

Mbinu za uchakataji wa data za programu za mikopo dijitali nchini Gabon zinasimamiwa na vipengele tofauti vya sheria inayotumika kuhusu ulinzi wa faragha. Tathmini za athari ya ulinzi wa data (DPIA) lazima zitekelezwe na wanaowajibika kwa uchakataji wa maombi ya mikopo dijitali. Utathmini huu utawezesha kufuatwa kikamilifu kwa wajibu wa kisheria. Kando na hayo, marekebisho ya Sheria Nambari 2013-50 ya tarehe 19 Juni 2013, kuhusu ulinzi wa data ya binafsi lazima yazingatiwe, kwa kuzingatia hatari mpya za faragha. Zaidi ya hayo, ni muhimu pia kwa shirika la CNPDCP kupata nyenzo na mbinu za kiufundi za kufuatilia ukubwa, ubora na wingi wa data inayokusanywa na wanaowajibika kwa uchakataji wa maombi ya mikopo dijitali. Bila kusahau hitaji la shirika la CNPDCP kuhakikisha ufuatiliaji wa kudumu wa kiteknolojia kwa kujitokeza kwa mashinika mapya ambayo shughuli zake za msingi zinahitaji ukusanyaji na uchakataji wa data ya binafsi.

<sup>149</sup> Kifungu cha 66, 68, 69 na 70 vya Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>150</sup> Kifungu cha 7, 8, 9, 10, 11, 12, 13 na 14 vya Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>151</sup> Kifungu cha 14 cha Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>152</sup> Kifungu cha 51 cha Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

<sup>153</sup> Kifungu cha 51 cha Sheria ya 001/2011 ya tarehe 25 Septemba 2011

# Ghana



## Maelezo ya Nchi

Ghana, inayojulikana pia kama Jamhuri ya Ghana, inapatikana katika eneo la Afrika Magharibi.<sup>154</sup> Inapanuka hadi kufikia Ghuba ya Gine (Gulf of Guinea) na Bahari ya Atlantiki katika upande wa kusini. Ghana inapakana na mataifa ya Kodivaa (Ivory Coast), Burkinafaso na Togo<sup>155</sup> na ina mandhari ya kupendeza ambayo yanajumuisha maeneo tambarare yenyε kinzo za vilima, mito na Ziwa Volta, linalojulikana kama ziwa bandia kubwa zaidi duniani.<sup>156</sup> Nchi hii ina ukubwa wa 238,533km<sup>2</sup><sup>157</sup> na ina idadi ya zaidi ya watu milioni 31<sup>158</sup>. Jiji lake kuu ni Accra, na Kiingereza ni mojawapo ya lugha zinazozungumzwa zaidi, ikifuatwa na Kiakani na lugha zingine za nchini.<sup>159</sup>

<sup>154</sup> Ghana <https://www.britannica.com/place/Ghana>

<sup>155</sup> Ghana <https://www.nationsonline.org/oneworld/ghana.htm>

<sup>156</sup> Ghana <https://www.nationsonline.org/oneworld/ghana.htm>

<sup>157</sup> Maelezo ya Nchi ya Ghana <https://www.bbc.com/news/world-africa-13433790>

<sup>158</sup> Worldometer <https://www.worldometers.info/world-population/ghana-population/>

<sup>159</sup> Kuhusu Ghana <https://www.nationsonline.org/oneworld/ghana.htm>

## Ulinzi wa Data Nchini Ghana

Biasara ya mikopo dijitali nchini Ghana ina utaratibu mbalimbali wa kisheria. Mifumo ya kukopesha pesa inasimamiwa na mamlaka kadhaa zilizoanzishwa chini ya sheria mbalimbali zinazoisimamia. Sheria kuu kati yazo ni Sheria ya Mifumo wa Malipo na Huduma (Payment System and Services Act), ya 2019, ambayo inaipa Benki ya Ghana (Bank of Ghana) mamlaka ya kuisimamia na kuidhibiti.<sup>160</sup> Chini ya sheria hii, lazima mifumo hii itume maombi ya kusajiliwa na Benki ya Ghana (Bank of Ghana)<sup>161</sup>, inayowajibika kwa utoaji wa leseni<sup>162</sup>. Hatua ya kushindwa kutuma maombi ya kusajiliwa ni kosa na linaweza kusababisha watoa huduma za mfumo husika kupigwa faini au kufungwa gerezani kwa kipindi maalum cha muda baada ya kushtakiwa.<sup>163</sup>

Kwa sababu ya wingi wa data inayokusanya, mifumo ya kukopesha pesa inasimamiwa pia na Tume ya Ulinzi wa Data (Data Protection Commission) iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012.<sup>164</sup> Sheria hii inaanzisha Tume ya kulinda faragha ya watu na kuhakikisha ulinzi wa data ya binafsi.<sup>165</sup> Chini ya Sheria hii, watoa huduma za mikopo

<sup>160</sup> Kifungu cha 3 (1), Sheria ya Mifumo ya Malipo na Huduma (Payment Systems and Services Act), ya 2019

<sup>161</sup> Kifungu cha 8 (1), Sheria ya Mifumo ya Malipo na Huduma (Payment Systems and Services Act), ya 2019

<sup>162</sup> Kifungu cha 3 (2)(l), Sheria ya Mifumo ya Malipo na Huduma (Payment Systems and Services Act), ya 2019

<sup>163</sup> Kifungu cha 9, Sheria ya Mifumo ya Malipo na Huduma (Payment Systems and Services Act), ya 2019

<sup>164</sup> Kifungu cha 2, Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012

<sup>165</sup> Kifungu cha 2, Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012

dijitali lazima wasajiliwe na Tume hiyo<sup>166</sup>, ambayo inasimamia shughuli zao za uchakataji wa maelezo ya binafsi<sup>167</sup>. Sheria hii inalazimu mifumo hiyo kujisajili, ambapo hatua ya kutojisajili inaweza kusababisha watoa huduma za mifumo hii kupigwa faini au kufungwa gerezani kwa kipindi maalum cha muda baada ya kushtakiwa.

Tatu, kwa sababu ya vitisho vinavyoletwa na mifumo ya kompyuta, mifumo hii pia inapatikana chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Usalama wa Mtandaoni (Cyber Security Authority) ilioanzishwa chini ya Sheria ya Usalama wa Mtandaoni (CyberSecurity Act), ya 2020.<sup>168</sup> Mamlaka hii inasimamia shughuli za usalama wa mtandaoni nchini na inashughulikia matukio na vitisho vya usalama wa mtandaoni.<sup>169</sup> Lengo muhimu kati ya malengo yake ni kuwajibisha wamiliki wa muundo msingi wa maelezo muhimu kuhusiana na shughuli za usalama wa mtandaoni, watoa huduma za usalama wa mtandaoni na madaktari nchini Ghana.<sup>170</sup>

Nne, mifumo hii iko chini ya Sheria ya Uzuiasi wa Ulanguzi wa Pesa (Anti-Money Laundering Act), ya 2020, inayoizua kutekeleza shughuli za ulanguzi wa pesa. Sheria hii inaanzisha Kituo cha Ujasusi wa Kifedha (Financial Intelligence Center), ambacho hutambua shughuli haramu na kukabiliana na shughuli za ulanguzi wa pesa na ufadhili wa shughuli za ugaidi.<sup>171</sup>

Hatimaye, mifumo hii iko chini ya Sheria ya Shughuli za Kifedha za Kielektroniki (Electronic Transactions Act), ambayo inalenga kuondoa na kuzuia vizuizi vya biashara ya mtandaoni na kukuza mazingira bora na salama kwa wateja, biashara na Serikali kufanya na kutumia shughuli za kifedha za kielektroniki.<sup>172</sup> Sheria hii inalenga kuunda mazingira bora na salama kwa mifumo ya kukopesha pesa.<sup>173</sup>

Utafiti unalenga zaidi udhibiti wa mifumo hii kuhusiana na shughuli zake za uchakataji wa data. Unaangalia mfumo wa udhibiti wa mifumo hii kuhusiana suala la ulinzi wa data. Unaanza kwa kueleza aina ya data inayochakatwa na mifumo hii na vile vile kuchanganua iwapo shughuli zake za uchakataji zinalingana na Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act). Utafiti huu unalenga mifumo minne mikuu ya kukopesha pesa nchini Ghana, yaani., Airtel Money Bosea, MTN Qwik Loan, FIDO Micro Finance na EcoBank Mobile Money.

<sup>166</sup> Kifungu cha 27 (1), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012

<sup>167</sup> Kifungu cha 2 (a) Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012

<sup>168</sup> Kifungu cha 2, Sheria ya Usalama wa Mtandaoni (Cyber Security Act), ya 2020 (Sheria ya 1038)

<sup>169</sup> Kifungu cha 3 (a)&(b), Sheria ya Usalama wa Mtandaoni (Cyber Security At), ya 2020 (Sheria ya 1038)

<sup>170</sup> Kifungu cha 3 (c) cha Sheria ya Usalama wa Mtandaoni (Cyber Security At), ya 2020 (Sheria ya 1038)

<sup>171</sup> Kifungu cha 7 (a)(b)(i)(ii), Sheria ya Usalama wa Mtandaoni (Cyber Security Act), ya 2020 (Sheria ya 1038)

<sup>172</sup> Kifungu cha 1, Sheria ya Shughuli za Kifedha za Kielektroniki (Electronic Transactions Act), ya 2008 (Sheria ya 772)

<sup>173</sup> Sheria na Mbinu: Soko la Teknolojia ya Fedha (Kanuni ya 2.2) <https://practiceguides.chambers.com/practice-guides/comparison/626/6478/10265-10267-10280-10284-10289-10292-10295-10305-10310-10314-10317-10320-10329>

## Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali

Airtel Money	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
Bosea	Ruhusa zinazotakikana	
-Hakuna Sheria na Masharti	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	
-Hakuna sera ya faragha	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji na	
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	
MTN Qwik Loan	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	Sera ya Faragha ya mfumo wa MTN Qwik Loan haipatikani. Sera pekee inayopatikana ni Sera ya Faragha ya Jumla ya MTN Group <sup>174</sup>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	

174 Sera ya Faragha ya MTN Group <https://www.mtn.com/privacy-policy/>

	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	
	Teknolojia ya Ufutiliaji na Vidakuzi	.
FIDO Micro Credit <sup>175</sup>	Maelezo Yanayokusanya na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	Huomba ruhusa ya kufikia: Akaunti ya mitandao ya kijamii ya mtumiaji
	Maelezo yanayokusanya kutoka kwa mtumiaji	Mfumo wa FIDO hukusanya maelezo yafuatayo ya mtumiaji kutoka kwenye Programu na tovuti yake: Maelezo ya binafsi: maelezo ya usajili, maelezo ya bili na malipo, maelezo yanayotokana na mawasiliano ya mtumiaji. Maelezo ya kifaa hukusanya kiotomatiki kuitia Programu na tovuti: data ya faili za rekodi, data ya matumizi ya bidhaa, programu zilizosakinishwa (kwenye kifaa cha mtumiaji), rekodi za SMS, orodha ya anwani za mawasiliano, anwani ya barua pepe, akaunti ya mhusika mwingine na nambari ya simu ya kifaa. Wahusika wengine (wanaoshiriki maelezo na FIDO): Ofisi za rekodi za mikopo na sajili za utambulisho, akaunti za mitandao ya kijamii na watoa huduma wengine wa data
	Maelezo yanayokusanya kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Maelezo ya kifaa yanayokusanya kiotomatiki kuitia Programu na tovuti: data ya faili za rekodi, data ya matumizi ya bidhaa, programu zilizosakinishwa, rekodi za SMS, orodha ya anwani za mawasiliano, anwani ya barua pepe, akaunti ya mhusika mwingine na nambari ya simu ya kifaa.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Mfumo wa FIDO hukusanya maelezo kutoka kwa wahusika wengine wafuatao: Ofisi za rekodi za mikopo na sajili za utambulisho, akaunti za mitandao ya kijamii na watoa huduma wengine wa data.

	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kuboresha bidhaa na huduma za kukopesha pesa za FIDO na hali ya utumiaji Utafiti na ukuzaji Bili na malipo Kuwasiliana na mtumiaji Matangazo Kutoa ripoti ya mteja Uchanganuzi wa mikopo Uthibitishaji wa utambulisho wa mtumiaji Kutii masharti ya kisheria au maombi ya mamlaka za usimamizi Kushtaki au kutetea haki za FIDO katika kesi za kisheria Kutoa maelezo kwa wahusika wengine walioidhinishwa
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Hushiriki maelezo na wahusika wengine wafuatao: Washirika wa FIDO, yaani, wakurugenzi, maofisa, wafanyakazi na wadau Watoa huduma za FIDO, wakandarasi, wauzaji wa bidhaa, maajenti, huduma na watoa huduma za malipo Watu wanaowakilisha watumiaji kama vile wapokeaji wa malipo, wanufaishwa, walioteuliwa kusimamia akaunti, watu wa kati (mabroka), watu wa kuwasiliana nao na maajenti wa benki Waelekezaji wa FIDO Washirika wa kibashara katika hali za kuuzwa, kuungana, kuhamishwa au kununuliwa kwa biashara Ofisi za rekodi za mikopo Mashirika ya utekelezaji wa sheria, mahakama au maofisa wa serikali Haijabainishwa
	Muda wa Wahusika Wengine Kufikia Data	Teknolojia ya Secure Layer Socket (SLS) hulinda maelezo ya binafsi ya mtumiaji yanayotumwa kuitia Programu
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji  Vidakuzi na teknolojia za ufuatiliaji	
EcoBank Mobile App <sup>176</sup>	Maelezo Yanayokusanya na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	

<sup>176</sup> Taarifa ya Faragha ya EcoBank Mobile App <https://www.ecobank.com/privacy-centre/personal-banking-privacy-notice/mobile-app>

	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Hukusanya maelezo yafuatayo kutoka kwa watumiaji baada ya kujisajili: Jina Anwani ya barua pepe Nambari ya simu Tarehe ya kuzaliwa Jinsia Anwani ya makazi Nambari za kitambulisho Kitambulisho cha kifaa Data ya mahali ya kifaa
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Anwani ya IP Maelezo ya vidakuzi Vitambulishi vya kifaa na matangazo Toleo la kivinjari Toleo na aina ya mfumo wa uendeshaji Maelezo ya mtandao wa simu Mipangilio ya kifaa, na Data ya programu Hukusanya pia maelezo ya mtumiaji kutoka kwa wahusika wengine ili kuthibitisha akaunti ya mtumiaji na kifaa
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Uthibitishaji na uidhinishaji wa idhini ya mtumiaji kufikia huduma kwenye Programu Kuwasiliana na mtumiaji, yaani., kupitia barua pepe, SMS, kupiga simu nk Kuwaonyesha watumiaji matangazo Kutangaza bidhaa zake Uchunguzi na utatuzi wa malalamiko ya mteja Uchunguzi wa ulaghai na ukiukaji wa sera ya faragha
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine/ Kushiriki maelezo ya binafsi	Programu ya EcoBank inaweza kushiriki maelezo ya mtumiaji na wahusika wengine wafuatao: Washirika wake Kampuni zake tanzu za teknolojia na usalama Watoa huduma wake na washirika wa matangazo
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji  Vidakuzi na teknolojia za ufuutiliaji	Maelezo huendelea kuhifadhiwa mradi akaunti ya mtumiaji inatumika au iwapo yanahitajika ili kutoa huduma za ExpressPay, kutii wajibu wa kisheria, kutatua migogoro na kutekeleza mkataba.

## **Uchanganuzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu za Mikopo Dijitali Dhidi ya Sheria ya Ulinzi wa Data ya 2012**

Sheria ya Ulinzi wa Data ya Ghana ina vifungu muhimu, kuanzia Kifungu cha 18 hadi 24, vinavyodhibiti mbinu za ulinzi wa data za Programu za mikopo dijitali zinazofanya kazi nchini Ghana. Sheria hii inabainisha kanuni zinazopaswa kuzingatiwa na Programu hizi na wajibu wake kuhusu faragha na ulinzi wa maelezo ya binafsi ya wakopaji. Sehemu hii inaangazia vifungu husika vya Sheria ili kutambua iwapo Programu hizi zinatii vifungu hivi.

### **Ukosefu (Kutopatikana) wa Sera za Faragha**

Sera za faragha ni muhimu kwa mifumo dijitali ya kukopesha pesa kwa sababu ya wingi wa data inayokusanya. Huwapa watumiaji maelezo muhimu kuhusu data inayochakatwa na mifumo hii, madhumuni ya matumizi ya data, wahusika wengine wanaoweza kufikia data, kipindi cha kuhifadhiwa kwa data na iwapo data itahimishwa nje ya nchi ya mtumiaji. Huwezesha watumiaji kujua jinsi mifumo ya kukopesha pesa inakusudia kushughulikia data yao na iwapo wana haki ya kudhibiti data yao, yaani., haki ya kufikia, kurekebisha, kufuta au kuhamisha data ya binafsi.<sup>177</sup>

Mifumo miwili mikuu ya kukopesha pesa inayochunguzwa kwenye utafiti huu, yaani, Airtel Money Bosea na MTN Qwik Loan, haina sera za faragha. Ukosefu huu ni kinyume na wajibu wake chini ya Sheria ya Ulinzi wa Data, ya 2012, ambayo inahitaji mifumo hii iwafahamishe watumiaji kuhusu yafuatayo.

- aina ya data inayochakatwa,
- jina na anwani ya mfumo wa kukopesha pesa,
- madhumuni ya ukusanyaji wa data, iwapo ukusanyaji huo ni wa hiari au wa lazima,
- athari za kukosa kutoa data,
- wapokeaji wa data na haki ya mmiliki wa data ya kufikia na,
- kuomba urekebishaji wa data kabla ya kukusanywa.<sup>178</sup>

### **Udhibiti wa Mtumiaji**

Mifumo ya kukopesha pesa inapaswa kuruhusu watumiaji kuwa na uwezo wa kudhibiti data yao kwa kuwapa nafasi ya kufikia, kurekebisha na kuhamishia data kwa watoa huduma wengine.<sup>179</sup> Haki hii inapaswa kupewa kipaumbele kwa sababu watumiaji ndio wamiliki wa data yao. Sheria ya Ulinzi wa Data inabainisha masharti haya na inatoa mwongozo wa kina kuhusu jinsi mifumo hiyo inavyoweza kuwezesha watumiaji kutekeleza haki yao ya ufikiaji wa data.<sup>180</sup>

Mifumo ya kukopesha pesa kama vile Airtel Money Bosea na MTN Qwik Loan haiwapi watumiaji haki ya kudhibiti data yao kwa sababu ya kukosa sera za faragha, ambazo zinawawezesha watumiaji kujua kwamba haki kama hizo zinaweza kutekelezwa. Mifumo ya FIDO na EcoBank Mobile Money inawapa watumiaji njia za kutekeleza haki hizi. Mfumo wa EcoBank Mobile Money hauruhusu watumiaji kuomba kuhamisha maelezo yao ya binafsi.

### **Madhumuni ya Ukusanyaji wa Data**

Mifumo ya mtandaoni ya kukopesha pesa inapaswa tu kukusanya na kutumia data ya mtumiaji kwa madhumuni ya kutoa huduma ya kukopesha pesa.<sup>181</sup> Inapaswa kuzingatia faragha ya mtumiaji<sup>182</sup> na kuhakikisha kuwa shughuli za uchakataji wa data binafsi ni muhimu, zinafaan hazikiuki faragha ya mtumiaji<sup>183</sup>. Ukusanyaji wa maelezo ya mtumiaji

<sup>177</sup> Kituo cha Uwezo wa Kufikia Huduma za Fedha (Center of Financial Inclusion) ukurasa wa 1

<sup>178</sup> Kifungu cha 27, Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012

<sup>179</sup> [Lengo la Kufanya Data Ifae Wasiojiweza] ukurasa wa 2

<sup>180</sup> Kifungu cha 32-35, Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012.

<sup>181</sup> [Lengo la Kufanya Data Ifae Wasiojiweza] ukurasa wa 10

<sup>182</sup> Kifungu cha 17 (c) Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012

<sup>183</sup> Kifungu cha 19, Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012.

kama vile data ya faili za nekodi, programu zilizosakinishwa, nekodi za SMS, orodha za anwani za mawasiliano na maelezo ya akaunti za mitandao ya kijamii ni kinyume na madhumuni ya biashara ya kukopesha pesa mtandaoni.<sup>184</sup>

Maelezo kama hayo ni ya ukiukaji na yanaingilia faragha ya mtumiaji. Kumekuwa na wasiwasi kwamba data ya watumiaji, kama vile maelezo yanayokusanya kwenye akaunti zao za mitandao ya kijamii kwa ajili ya kutoa alama za mikopo, yanaweza kutumiwa visivyo au kuuzwa bila idhini yao.<sup>185</sup> Wakopeshaji wanapaswa kuhakikisha kuwa data inatumia kwa maslahi bora ya mteja na wala si kwa namna ya kumdhuru.<sup>186</sup>

## **Kufanya Maamuzi Kiotomatiki**

Mifumo dijitali ya kukopesha pesa hutumia mifumo mbadala ya kutoa alama za mikopo ambayo inategemea teknolojia ya AI ili kubaini ufaafu wa mtumiaji kupokea mikopo. Mifumo ya teknolojia ya AI hufikia maudhui yaliyohifadhiwa kwenye kifaa cha mtumiaji kama vile kamera, anwani za mawasiliano, hifadhi na mengineyo, ili kumpa mteja alama.<sup>187</sup> Alama zinazotolewa na mifumo hii kutokana na kutathmini data ya mtumiaji wakati mwengine zinaweza kuwa si za haki. Zinaweza kuendeleza zaidi ukosefu wa usawa wa kupokea huduma. Mashirika haya ya kukopesha pesa yanapaswa kubuni mifumo hii ili kuhakikisha haki na kutokuwa na mapendeleo.<sup>188</sup> Kwa kufanya hivyo, mashirika haya yanapaswa kuajini wafanyakazi ambao wanafuatilia mara kwa mara na kutathmini alama zinazotolewa na mifumo hii ya teknolojia ya AI ili kuhakikisha kuwa mifumo hii haisababishi ukosefu wa usawa wa kupokea huduma za fedha.<sup>189</sup>

## **Mbinu za Usalama**

Chini ya Sheria ya Ulinzi wa Data, mifumo dijitali ya kukopesha pesa inapaswa kuchukua hatua muhimu za kuhakikisha usalama wa data iliyokusanya kwa kuweka mbinu mwafaka, zinazofaa, za kiufundi na za kishirika.<sup>190</sup> Ulinzi huu unahitajika ili kulinda data kutokana na kupotea, kufikiwa na kuchakatwa kinyume cha sheria.<sup>191</sup> Kwa kufanya hivyo, lazima kwanza programu zitambue hatari yoyote inayoweza kutokea kwa data ya binafsi. Pili, lazima ziweke na kudumisha mbinu mwafaka za ulinzi za kulinda data dhidi ya hatari zilizotambulika na kuthibitisha mara kwa mara kwamba mbinu hizi za usalama zinatekelezwa ipasavyo. Hatimaye, zinapaswa kuhakikisha kuwa mbinu hizi za usalama zinasasishwa mara kwa mara kulingana na vitisho vipyta.<sup>192</sup>

Kwa sababu ya kiasi kikubwa cha data inayochakatwa na mifumo dijitali ya kukopesha pesa, hatua ya kutii kikamilifu kifungu hiki inahitajika ili kuhakikisha usalama wa data. Programu zinazochunguzwa zinazua wasiwasi mwangi mno kuhusu mbinu zake za usalama. Baadhi ya programu hizi, hasa programu ya Airtel Money Bosea na MTN Qwik Loan, hazina sera za faragha ambazo ni muhimu katika suala hili katika kuwalishya watumiaji mbinu za usalama zinazotumiwa na mifumo hii. Programu zingine, kama vile FIDO Microcredit, hazina vifungu kuhusu mbinu za usalama zinazotumika, hali ambayo haiwapi watumiaji maelezo yoyote kuhusu jinsi mfumo utakavyohifadhi data yao.

## **Uchakataji wa Data kutoka kwa Ofisi za Mikopo**

<sup>184</sup> Sera ya Faragha ya FIDO - 'Maelezo Tunayokusanya' <https://www.fidocredit.com/privacy.html>

<sup>185</sup> John Owens, Huduma Wajibikaji ya Mikopo Dijitali: Huduma Wajibikaji ya Mikopo Dijitali Inaonekanaje? (Julai 2018) ukunasa wa 25 [https://content.centerforfinancialinclusion.org/wp-content/uploads/sites/2/1970/01/Responsible\\_Digital\\_Credit\\_FINAL\\_2018.07.18.pdf](https://content.centerforfinancialinclusion.org/wp-content/uploads/sites/2/1970/01/Responsible_Digital_Credit_FINAL_2018.07.18.pdf)

<sup>186</sup> [Lengo la Kufanya Data Ifae Wasiojiweza] ukurasa wa 2

<sup>187</sup> Je, Uchanganuzi wa Hatari ya Kutoa Mkopo wa AI Utakuza Kweli Uwezo wa Kufikia Huduma za Mikopo Barani Afrika? <https://www.theafricanreport.com/107432/will-ai-risk-analysis-really-expand-access-to-credit-in-africa/>

<sup>188</sup> [Lengo la Kufanya Data Ifae Wasiojiweza] ukunasa wa 2

<sup>189</sup> [Lengo la Kufanya Data Ifae Wasiojiweza] ukurasa wa 3

<sup>190</sup> Kifungu cha 28 (1), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012

<sup>191</sup> Kifungu cha 28 (1), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012

<sup>192</sup> Kifungu cha 28 (2), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2012

Programu za mikopo dijitali hufikia data kutoka kwa wahusika wengine kama vile ofisi za rekodi za mikopo kwa madhumuni ya kutathmini ufaafu wa mkopaji kupokea mkopo. Programu hizi, zisipozuiwa, zinaweza kufikia data ya binafsi ya ziada ambayo hailingani na madhumuni ya huduma ya utoaji mikopo dijitali. Sheria, katika hali hii, inadhibiti kikomo cha data ambayo programu hizi zinaweza kufikia kutoka kwa ofisi za rekodi za mikopo ili kuzuia tukio la ukichuzi haramu wa data. Inabainisha kwamba data inayofikiwa na programu hizi kutoka kwa ofisi za mikopo inapaswa kuhusiana tu na rekodi ya kifedha na historia ya mmiliki wa data ya kipindi kinachotangulia miezi 12 baada ya kuchukua mkopo.<sup>193</sup>

# Kenya



## Maelezo ya Nchi

Kenya ni nchi inayopatikana katika eneo la Afrika Mashariki.<sup>194</sup> Ina ukubwa wa 580,000 Km<sup>2</sup><sup>195</sup> na inapakana na mataifa ya Somalia, Ethiopia na Sudan katika upande wa kaskazini na Uganda na Tanzania katika upande wa magharibi na kusini.<sup>196</sup> Jiji lake kuu ni Nairobi, ambayo ni kaunti iliyoendelea zaidi. Kulingana na ripoti ya Hesabu ya Watu ya Kitaifa (National Census) ya 2019, Kenya i idadi ya watu milioni 47,000,000.<sup>197</sup>

194 Kuhusu Kenya <https://www.britannica.com/place/Kenya>

195 <https://www.nationsonline.org/oneworld/kenya.htm>

196 <https://www.un.int/kenya/kenya/general-information-about-kenya>

197 Idadi ya Watu na Nyumba Nchini Kenya ya 2019 Toleo la I: Idadi ya Watu Kulingana na Kaunti na Maeneo Bunge

<https://www.knbs.or.ke/?wpdmpro=2019-kenya-population-and-housing-census-volume-i-population-by-county-and-sub-county>

## Ulinzi wa Data Nchini Kenya

Programu za mikopo dijitali zimetoa njia rahisi ya kupata mikopo ya haraka na ya muda mfupi kwa Wakenya. Zinarahisisha huduma ya kupata mikopo kwa watu ambao hawana akaunti za benki na vyanzo vya kawaida vya mapato vinavyohitajika ili kupata mkopo kutoka kwa taasisi za fedha.<sup>198</sup> Urahisi wake umeziwezesha kupata umaarufu nchini Kenya. Utafiti uliofanywa na shirika la FSD Kenya unabainisha kwamba zaidi ya idadi ya Wakenya milioni 6 wamepata mikopo kuititia programu hizi kwa miaka iliyopita.<sup>199</sup>

Hata hivyo, programu hizi zinaendelea kutodhibitiwa kimsingi, hali ambayo inazipa nafasi ya kutoza riba za juu na kutekeleza mbinu ambazo zinakiuka haki za watumiaji. Serikali inajaribu kukabiliana na suala hili kuititia Mswada wa Benki Kuu ya Kenya (Marekebisho), wa 2021, ambao unajadiliwa Bungeni kwa sasa.<sup>200</sup> Mswada huu, ukipitishwa, utafanikiwa kufanya programu za mikopo kufuata kanuni za Benki Kuu ya Kenya (Central Bank of Kenya (CBK) na utazihitaji zipokee leseni kutoka kwa Benki hiyo.<sup>201</sup> Mswada huu utaipa CBK mamlaka ya kusimamia shughuli za programu hizi<sup>202</sup> na utaipa, mionganini mwa mambo mengine, CBK uwezo wa kutunga Sheria kuhusu: usajili wa programu hizi, usimamizi wake, shughuli zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa, shughuli zake kushiriki maelezo na ofisi za rekodi za

198 Kenya Inajitayarisha Kufanya Msako kuhusu Kufurika kwa Programu za Mikopo Zinazotoza Riba ya Juu <<https://qz.com/africa/1975202/kenya-prepares-to-crack-down-on-high-interest-loan-apps/>> Ilifikiwa tarehe 26/7/2021

199 Fsd Kenya, Ripoti ya Ukaguzi wa Mikopo Dijitali: Kutathmini Maadili na Desturi za Programu za Mikopo Dijitali nchini Kenya (Septemba 2019) ukurasa wa iv

<http://www.fsdkenya.org/wp-content/uploads/2019/11/19-09-10-Regulation-Digital-credit-audit.pdf>

200 Mswada wa Benki Kuu ya Kenya (Marekebisho) wa 2021

[http://kenyalaw.org/kl/fileadmin/pdfdownloads/bills/2021/TheCentralBankofKenya\\_Amendment\\_Bill\\_2021.pdf](http://kenyalaw.org/kl/fileadmin/pdfdownloads/bills/2021/TheCentralBankofKenya_Amendment_Bill_2021.pdf)

201 Kifungu cha 33 (S) (1), Mswada wa Benki Kuu ya Kenya (Marekebisho) wa 2021

202 Kifungu cha 3 (da), Mswada wa Benki Kuu ya Kenya (Marekebisho) wa 2021

mikopo, shughuli zake za ulinzi wa data, ulinzi wa wateja na masharti yake ya kunipoti.<sup>203</sup>

Ni muhimu kutambua kwamba baada ya Mswada huu kupidishwa, programu zitashiriki na kupokea maelezo kutoka kwa ofisi za nekodi za mikopo. Haikuwa hivyo mwaka uliopita wakati ambapo Serikali ilifanikiwa kuzifungia nje ya mifumo ya ofisi za nekodi za mikopo baada ya kutokea kwa janga la COVID-19.<sup>204</sup>

Kwa sasa, programu hizi zinakusanya maelezo mengi mno ya binafsi zinapotoa huduma za mikopo hii. Kiasi cha data inayokusanywa na programu hizi nydingi ni ya ziadi ikilinganishwa na madhumuni ya uchakataji, hali ambayo inasababisha ukiukaji wa faragha ya watumiaji. Sheria ya Ulinzi wa Data, ya 2019 inabainisha vifungu vikuu ambavyo ni muhimu kwa ushughuli za uchakataji za programu hizi.

Utafiti huu unalenga kuchanganua sera za faragha na sheria na masharti ya programu hizi na kuchunguza jinsi zinavyotii Sheria ya Ulinzi wa Data. Sehemu ya kwanza inajumuisha muhtasari wa data inayokusanywa na programu hizi. Sehemu ya pili inachunguza shughuli zake za uchakataji dhidi ya Sheria ya Ulinzi wa Data. Sehemu ya mwisho inahitimisha kwa kubainisha iwapo programu hizi zinatii Sheria ya Ulinzi wa Data au la.

## **Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali**

Tala <sup>205</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu
Ruhusa zinazotakikana	Kudhibiti simu za mtumiaji Kufikia SMS za mtumiaji Kufikia anwani za mawasiliano za mtumiaji Kufikia data ya mahali ya mtumiaji (kwa kutumia teknolojia ya GPS) na data ya mtumiaji
Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Jina la mtumiaji, anwani, anwani ya barua pepe na nambari ya simu, nambari ya simu ya kifaa, SIM kadi, umri, jina la mtumiaji, nenosiri, maelezo ya fedha na mikopo, maelezo ya binafsi na picha na maelezo mengine ya usajili
Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Data ya kiufundi: Muundo wa simu, IMEI ya kifaa au nambari ya kitambulisho, maelezo ya SIM kadi, maelezo ya mtandao wa simu, mfumo wa uendeshaji wa kifaa, aina ya kivinjari, data ya mahali ya kifaa na mipangilio ya saa za eneo Maelezo yaliyohifadhiwa kwenye kifaa: orodha ya anwani za mawasiliano, rekodi za nambari za simu, rekodi za SMS, anwani zilizo kwenye akaunti za mitandao ya kijamii, picha, video au maudhui yoyote dijitali husika.
Maelezo yanayokusanywa kutokana na kutumia tovuti ya Tala	Anwani ya IP ya mtumiaji, aina ya kivinjari, mtoa huduma za intaneti (ISP), kurasa za uelekezaji/kuondoka, mfumo wa uendeshaji, muhuri wa saa/tarehe na maudhui ya kuvinjari. Maelezo haya huhifadhiwa kwenye faili za rekodi za Tala na kutumiwa kwa uchanganuzi au matangazo

203 Kifungu cha 6 (3), Mswada wa Benki Kuu ya Kenya (Marekebisho) wa 2021

204 624 Mashirika ya Mikopo Dijitali Yazuiwa Kushiriki Data ya Mteja na Mashirika ya CRB

<https://www.businessdailyafrica.com/bd/markets/market-news/624-digital-loan-from-sharing-client-data-with-crbs-3416546>

205 Sera ya Faragha ya Tala <https://tala.co.ke/privacy-policy-ke/>

	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Hupokea maelezo kutoka kwa ofisi za rekodi za mikopo, watoa huduma za mtandao wa simu na mashirika ya ukusanyaji wa madeni
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kuchakata shughuli za kifedha Uthibitishaji Kutoa mikopo Kutoa alama za mikopo Uchanganuzi wa tabia ya mkopaji Kutimiza wajibu wa mkopeshaji Kutii kanuni za KYC (Masharti ya Jua Mteja Wako) na kuzuia ulanguzi wa pesa Kuzuia ulaghaji Matangazo
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Hushiriki maelezo ya mtumiaji na wafuatao: Wanachama wake, maajenti, watoa huduma na mtu ye yeyote aliyepewa kandarasi nayo Watu wanaowakilisha mtumiaji Taasisi za Fedha, ofisi za rekodi za mikopo Washirika wa kibiashara katika hali za uhamishaji, uuzaji, muungano na ununuzi wa biashara, nk. Watoa huduma wengine Mashirika ya utekelezaji wa sheria, maofisa wa serikali, kwa msingi wa: Ombi rasmi au agizo la mahakama Kutii sheria au kuripoti shughuli za kinyume cha sheria zinazoshukiwa Haijabainishwa
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Teknolojia za ufuutiliaji/vidakuzi vya tovuti	Teknolojia za ufuutiliaji wa simu na vidakuzi hutumika ili kutofautisha watumiaji wa Programu
	Kuhifadhiwa kwa maelezo ya mtumiaji	Huhifadhi maelezo ya watumiaji nje ya nchi ya Kenya na huchakatwa na wafanyakazi wanaishi nje ya nchi ya Kenya.
Branch <sup>206</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	Ufikiaji wa: Anwani za mawasiliano SMS Simu Data ya mahali: Kwa kutumia teknolojia ya GPS
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	jina, anwani, anwani ya barua pepe na nambari ya simu, maelezo ya SIM kadi, umri, jina la mtumiaji, nenosini, maelezo ya fedha na mikopo na maelezo mengine ya usajili.

	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Maelezo ya Kiufundi: Muundo wa simu, IMEI ya kifaa au nambari ya kitambulisho, maelezo ya SIM kadi, maelezo ya mtandao wa simu, mfumo wa uendeshaji wa kifaa, aina ya kivinjari kinachotumiwa na mtumiaji, data ya mahali ya kifaa na mipangilio ya saa za eneo Maelezo yaliyohifadhiwa kwenye kifaa: orodha ya anwani za mawasiliano, rekodi za nambari za simu, rekodi za SMS, anwani zilizo kwenye akaunti za mitandao ya kijamii, picha, video au maudhui yoyote dijitali husika. Data kutoka kwa programu yoyote ya mhusika mwingine inayotumiwa na mtumiaji kwenye kifaa
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Maelezo hypokewa kutoka kwa wahusika wengine kama vile ofisi za rekodi za mikopo, watoa huduma za mtandao wa simu na mashirika ya ukusanyaji wa madeni.
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kubainisha ufaafu wa kupokea mikopo Sera yake ya faragha pia inabainisha kwamba inashiriki maelezo ya mtumiaji kwa kutii tu agizo la mahakama, Jopo la Upatanishi, Mahakama, Amri au Agizo la Usimamizi, au wajibu mwingine wowote wa kisheria au usimamizi.
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Hushiriki maelezo ya mtumiaji na wafuataao: Ofisi za rekodi za mikopo Wanachama wake, yaani, kampuni tanzu, washirika, kampuni za kumiliki hisa Washirika wa kibashara wakati wa mauzo ya biashara au mali Mamlaka za kisheria, kutii wajibu wa kisheria au usimamizi Haijabainishwa
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Kuhifadhiwa kwa maelezo ya mtumiaji	Huhifadhi maelezo ya mtumiaji nje ya nchi ya Kenya, ambapo wafanyakazi wake huyachakata nje ya nohi.
	Teknolojia ya Ufuatiliaji na Vidakuzi	Teknolojia za ufuatiliaji wa simu/ vidakuzi hutumika ili kutofautisha watumiaji wa Programu

LionCash <sup>207</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	Ufikiaji wa: SMS Data ya mahali: Hutumia maelezo ya moja kwa moja ya mahali mahususi Simu: Ili kusoma hali ya simu na utambulisho Anwani za mawasiliano
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Jina la mtumiaji, cheo cha kazi, jina la kampuni, anwani, anwani ya barua pepe, nambari ya simu, jinsia, umri, tarehe ya kuzaliwa, utaifa, miungano ya kitaalamu na nambari za usajili, maelezo kuhusu jinsi mtumiaji anavyotumia bidhaa za LionCash, taarifa za shughuli za kutuma na kupokea pesa kuitia simu ya mkononi, maelezo ya benki au akaunti, maelezo ya kuingia katika akaunti za mitandao ya kijamii za mtumiaji, anwani za mawasiliano zilizo kwenye kifaa cha mtumiaji.
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Maelezo ya Kiufundi: Aina ya simu ya mkononi, anwani ya IP, mfumo wa uendeshaji wa kifaa na kitambulisho cha kifaa. Maelezo haya hukusanya kiotomatiki kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji na vivinjari vya wavuti kuitia vidakuzi Data ya matumizi ya Programu ya mtumiaji na matumizi ya matangazo dijitali Data ya mahali: Hukusanya maelezo ya moja kwa moja ya mahali mahususi kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Hupokea maelezo kutoka kwa washirika wake wa kibiashara kama vile; jina la mtumiaji, jina la kampuni, cheo cha kazi, anwani, anwani ya barua pepe na nambari ya simu kwa madhumuni ya uthibitishaji Inaweza pia kukusanya maelezo yanayopatikana hadharani au ya kibiashara kutoka kwa wahusika wengine.
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Utoajia wa huduma Kutoa maelezo kuhusu bidhaa na huduma Kuboresha tovuti, Programu, bidhaa na huduma Matangazo Kutetea madai ya kisheria, kutii sheria na maagizo ya mahakama na uzuiaji wa ulaghai
Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Hushiriki maelezo ya mtumiaji na: Watoa huduma Washirika wa kibiashara ambao huwasaidia kutoa bidhaa na huduma kwa watumiaji Mamlaka za kisheria, kutii sheria, kanuni na maagizo ya mahakama na uzuiaji wa ulaghai Washirika wa kibiashara katika hali za muungano, mauzo au kuvunjwa kwa biashara nk
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	Haijabainishwa

	Kuhifadhiwa kwa maelezo ya mtumiaji	Huhifadhi maelezo ya mtumiaji kwenye hifadhidata na seva za nje ya nchi ya Kenya
Timiza <sup>208</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	Huomba kufikia: Data ya mahali - hufikia maelezo ya moja kwa moja ya mahali mahususi Simu - Ili kusoma hali ya simu na utambulisho Anwani za mawasiliano
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Hupata maelezo kutoka kwa wafuatao: Safaricom: Ikijumuisha nambari ya simu ya mtumiaji, jina, tarehe ya kuzaliwa, nambari ya kitambulisho/ pasipoti na maelezo mengine husika Hufikia maelezo kuhusu jinsi mtumiaji anavyotumia huduma za MPESA na Safaricom Mfumo wa IPRS wa serikali. Ofisi za rekodi za mikopo na hushiriki maelezo ya mikopo ya mtumiaji na ofisi hizo
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Utoajia wa huduma Kwa madhumuni ya matangazo Uboreshaji wa tovuti, Programu, bidhaa na huduma Kutetea madai ya kisheria, kutii sheria na maagizo ya mahakama na kuzuia ulaghai
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine/ Kushiriki maelezo ya binafsi	Hushiriki maelezo ya mtumiaji na: Watoa huduma wake, wauzaji wa bidhaa na maajenti Washauri wake wa kitaalamu, ikijumuisha mawakili na wakaguzi Safaricom kuhusiana na huduma za MPESA Mashirika ya nchini na ya kimataifa ya utekelezaji wa sheria na mashirika ya serikali katika uzuiaji wa ulaghai na kuripoti shughuli za kihalifu
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	

<sup>208</sup> Sheria na Masharti ya Akaunti ya Timiza ya Absa <https://www.absabank.co.ke/content/dam/kenya/absa/pdf/Terms-of-use/timiza-account-terms-and-conditions.pdf>

O-Kash <sup>209</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	Huomba kufikia: · Picha na maudhui yaliyo kwenye kifaa cha mtumiaji · Data ya mahali ya kifaa
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Nambari ya MPESA, nambari ya simu, jina la mkopaji, umri, anwani ya barua pepe na maelezo mengine ya mawasiliano. Anwani za mawasiliano ya dharura zinaweza kutumika kuthibitisha utambulisho wa mtumiaji
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	muundo wa kifaa, mfumo wa uendeshaji, programu na kitambulisho maalum cha mtumiaji. Anwani za mawasiliano za barua pepe na simu, rekodi za nambari za simu, SMS na maelezo ya mahali ya GPS.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Hukusanya maelezo kutoka kwenye ofisi za nekodi za mikopo na taasisi za fedha.
	Matumizi ya maelezo ya mtumiaji	Uthibitishaji na utoaji wa alama za mikopo
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Hushiriki maelezo ya mtumiaji na: Ofisi za rekodi za mikopo Mashirika ya ukusanyaji wa madeni Mashirika ya serikali na ya utekelezaji wa sheria Washauri wa kitaalamu Washirika wa biashara wakati wa muungano, ununuzi na ufilisi wa biashara
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Huhamishia data ya mtumiaji kwenye nchi zingine, ikijumuisha nchi ambazo hazina sheria za ulinzi wa data

## Uchunguzi Kifani: O-Kash: Uaibishaji wa Walioshindwa Kulipa Madeni

Programu ya O-Kash imetambulika sana kwa vitendo vya kuaibisha wakopaji walioshindwa kulipa madeni kwenye mfumo wake. Programu hii hutegemea anwani za mawasiliano zilizo kwenye kifaa cha mtumiaji na maelezo ya mawasiliano ya anwani za mawasiliano ya dharura/mtu wa kurejelea.<sup>210</sup> Programu hii, baada ya kusakinishwa, huomba kufikia anwani za mawasiliano za mkopaji na inahitaji kutolewa kwa anwani ya mawasiliano ya dharura baada ya mtumiaji kuomba mkopo.<sup>211</sup>

Sheria na masharti yake yanahitaji mkopaji atoe idhini ya moja kwa moja ya kuwasiliana na mtu wa kurejelea wa mkopaji wakati ambapo mkopaji anashindwa kulipa deni.<sup>212</sup> Kutokana na suala hili, Programu imekuwa ikiwapigia simu kwa fujo watu wa kurejelea na watu ambao wakopaji huwasiliana nao na, wakati mwengine kutoa vitisho ili kuwafanya walipe.<sup>213</sup>

Vitendo kama hivyo ni ukiukaji wa faragha ya mkopaji. Ni kinyume na vifungu vya Sheria ya

209 Sera ya Faragha ya O-Kash <https://ke.o-kash.com/kenya/en/privacy-policy/>

210 Sera ya Faragha ya O-Kash <https://ke.o-kash.com/kenya/en/privacy-policy/>

211 Sera ya Faragha ya O-Kash <https://ke.o-kash.com/kenya/en/privacy-policy/>

212 Kifungu cha 8, Sheria na Masharti ya Programu ya O-Kash <https://ke.o-kash.com/kenya/en/Terms-for-Kenya/>

213 Programu Hii ya Kukopesha Pesa Hukuaibisha Hadharani Ukielewa Kulipa Malipo ya Mkopo <https://restofworld.org/2020/okash-microlending-public-shaming/>

Ulinzi wa Data, ambavyo vinahitaji data ya binafsi ya wamiliki wa data ichakatwe chini ya haki yao ya faragha.<sup>214</sup>

## **Uchanganuzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu za Mikopo Dijitali Dhidi ya Sheria ya Ulinzi wa Data ya 2019**

Sheria ya Ulinzi wa Data ya Kenya ina vifungu muhimu vinavyodhibiti mbinu za ulinzi wa data za Programu za mikopo dijitali zinazofanya kazi nichini Kenya. Sheria hii inabainisha kanuni zinazopaswa kuzingatiwa na Programu hizi na wajibu wake kuhusu faragha na ulinzi wa maeleo ya binafsi ya wakopaji. Sehemu hii inaangazia vifungu husika vya Sheria ili kutambua iwapo Programu hizi zinatii vifungu hivi.

### **Haki ya Faragha**

Sheria ya Ulinzi wa Data inahitaji wadhibiti na wachakataji wa data (katika hali hii, Programu za mikopo dijitali) wachakate data ya binafsi kwa njia ambayo inaheshimu haki ya faragha ya mamiliki wa data.<sup>215</sup> Katika hali hii, Sheria inazitaka Programu hizi zizingatie zaidi haki ya faragha ya mkopaji wakati wa kuchakata data yake.

Programu zinazochunguzwa zinakiuka haki hii na zinachakata data ambayo inaingilia faragha ya mtumiaji na isiyohusiana na madhumuni ya ukusanyaji wa data. Kwa mfano, programu hizi hukusanya maeleo kama vile anwani zilizohifadhiwa kwenye kifaa cha mkopaji, maeleo ya kuingia katika akaunti za mitandao ya kijamii, maeleo ya moja kwa moja ya mahali mahususi na mengineyo, ambayo yanaingilia faragha ya mkopaji na ya ziada kuhusiana na madhumuni ya ukusanyaji wa data. Programu kama vile O-Kash imetambulika sana kwa vitendo vya kuaibisha wakopaji wanaoshindwa kulipa deni kwa kuwapigia simu na kuwasumbua wadhamini wao na kuwasiliana na anwani za mawasiliano zilizohifadhiwa kwenye vifaa vyao ili kuwafanya walipe deni.<sup>216</sup> Vitendo kama hivyo vinaingilia faragha ya wakopaji.

### **Uhalali, Haki na Uwazi**

Sheria ya Ulinzi wa Data inahitaji programu hizi zichakate data kwa njia halali, ya haki na uwazi.<sup>217</sup> Hii inahusu Programu hizi kuhakikisha kwamba wamiliki wa data wamejulishwa kwa uwazi na kwa ufupi jinsi data yao itakavyotumiwa na kuhakikisha kwamba masharti yote ya sheria yametimizwa katika uchakataji huo.<sup>218</sup> Sheria hii inazidi kuhitaji Programu hizi kuhakikisha kwamba idhini ya mkopaji imetolewa kabla ya kuchakata data yao.<sup>219</sup>

Katika hali hii, Programu zinapaswa kufahamisha watumiaji kwa nini data yao inakusanywa, jinsi data yao itakavyotumiwa na, ikiwa itashirikiwa na wahusika wengine, ni nani amba data yao itashirikiwa nao na muda amba watahifadhi data hiyo. Programu zinazochunguzwa zinaweza kuwa na uwazi kuhusu kukusanya data ya mtumiaji na kuishiriki. Hata hivyo, zinashindwa kubainisha muda amba wahusika wengine watafikia data hiyo na muda amba watahifadhi.

### **Kikomo cha Madhumuni, Ufaafu na Utoshelevu**

Programu za mikopo Dijitali zinahitajika chini ya Sheria ya Ulinzi wa Data kuchakata data ya binafsi kulingana na madhumuni ya ukusanyaji wa data, kumaanisha kuwa zinapaswa tu kukusanya data inayohusiana na madhumuni ya utoaji wa mikopo dijitali wala si data ya ziada. Programu pia zinahitajika kukusanya data husika, ya kutosha na inayohusiana na

214 Kifungu cha 25 (a) Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

215 Kifungu cha 25 (a) Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

216 Kuaibisha Walioshindwa Kulipa Deni: Jinsi Watoa Huduma za Mikopo Dijitali Wahuni Hutumia Mbinu Zisizo za Kawaida Kukusanya Madeni ya Mikopo <https://www.instagram.com/p/CRgoT7OM8hy/>

217 Kifungu cha 25 (b) Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

218 Mwongozo wa Kimataifa wa Faragha kwa Ulinzi wa Data

219 Kifungu cha 30 (1), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

madhumuni ya ukusanyaji.<sup>220</sup>

Programu zinazochunguzwa hukusanya maelezo yasiyohusika na yanayoingilia faragha kama vile; anwani za mawasiliano za wakopaji, nambari za kadi za mikopo, maelezo ya kuingia katika akaunti za mitandao ya kijamii na anwani, picha na video.

## **Kushiriki Maelezo na Wahusika Wengine**

Sheria ya Ulinzi wa Data inaeleza kwamba Programu hizi zinapaswa kuwafahamisha watumiaji kuhusu wahusika wengine ambao zitashiriki nao data yao, ikijumuisha mbinu zilizowekwa ili kulinda usalama wa data yao kabla ya kuikusanya.<sup>221</sup>

Programu zinazochunguzwa hushiriki maelezo ya mtumiaji/mkopaji na ofisi za rekodi za mikopo, washirika wa kibiashara, wataalamu wa ushauri, kampuni za huduma za mawasiliano ya simu kama vile Safaricom, serikali na mashirika ya utekelezaji wa sheria, nk, na zinashindwa kubainisha mbinu za ulinzi wa usalama zilizowekwa ili kulinda data ya mkopaji. Programu hizi pia zinashindwa kubainisha muda ambao wahusika hawa wataweza kufikia data na muda watakaoihifadhi.

## **Uhamishaji wa Data ya Binafsi Nje ya Nchi ya Kenya**

Sheria ya Ulinzi wa Data inaeleza kwamba Programu hizi zinapaswa kuhakikisha kuwa data ya binafsi haihamishiwi nje ya nchi ya Kenya isipokuwa mbinu za kutosha za ulinzi wa data ziwe zimewekwa na idhini ya mmiliki wa data imetolewa.<sup>222</sup> Inaeleza pia kwamba Programu hizi zinapaswa tu kuhamishia data kwenye nchi zingine wakati ambapo zimetoa thibitisho kwa mkuu wa data kuhusu mbinu mwafaka za ulinzi zilizowekwa kuhusiana na usalama na ulinzi wa data ya binafsi.<sup>223</sup> Sheria inazidi kueleza kwamba Programu hizi zinaweza tu kuhamishia data ya binafsi kwenye nchi zingine wakati ambapo zimetoa thibitisho kwa Mkuu wa Data kuhusu mbinu mwafaka za usalama na ulinzi wa data binafsi na mbinu mwafaka za ulinzi zilizowekwa, ikijumuisha nchi zenye sheria zinazofaa za ulinzi wa data.<sup>224</sup>

Kampuni nydingi zinazomiliki Programu zinazochunguzwa zinapatikana nje ya nchi ya Kenya na zina hifadhidata na seva zinazohifadhi maelezo ya binafsi ya mkopaji nje ya nchi ya Kenya. Suala hili linasababisha hatari ya usalama kwa wakopaji kuhusiana na data yao. Kwa mfano, Programu za Tala, Branch na O-Kash zina makao makuu yake nje ya nchi na zinahifadhi maelezo ya binafsi ya mkopaji kwenye seva zinazopatikana nje ya nchi.<sup>225</sup> Baadhi ya Programu zinahifadhi data katika nchi ambazo hazina sheria zinazofaa za ulinzi wa data kama Kenya. Programu ya O-Kash, kwa mfano, huhamishia data ya binafsi kwenye nchi ambazo hazina kiwango sawa cha ulinzi wa data kama Kenya.<sup>226</sup>

## **Faragha Kimuundo na kwa Chaguomsingi**

Sheria ya Ulinzi wa Data inahitaji Programu hizi zitekeleze mbinu mwafaka za kiufundi na kishirika zilizobuniwa ili kutekeleza ipasavyo kanuni za ulinzi wa data na kujumuisha mbinu muhimu za ulinzi kwa uchakataji.<sup>227</sup>

Sheria inazidi kueleza kwamba programu hizi zinapaswa kutekeleza mbinu za kiufundi na kishirika ambazo zinahakikisha, kwa chaguomsingi, kuwa data ya binafsi inayohitajika pekee

220 Kifungu cha 25 (d), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

221 Kifungu cha 29 (d), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act) ya 2019

222 Kifungu cha 25 (h), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act) ya 2019

223 Kifungu cha 48 (a) Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

224 Kifungu cha 48 (b) Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act) ya 2019

225 Sera ya Faragha ya Programu ya Tala: <https://tala.co.ke/privacy-policy-ke/>; Sera ya Faragha ya Programu ya Branch: <https://branch.co.ke/pp>; Sera ya Faragha ya Programu ya O-Kash: <https://ke.o-kash.com/kenya/en/privacy-policy/>

226 Sera ya Faragha ya O-Kash, Kifungu cha C

227 Kifungu cha 41 (a) na (b), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act) ya 2019

ndio inachakatwa.<sup>228</sup> Sheria inaeleza kwamba Sheria inapaswa kuzingatia kiasi cha data ya binafsi inayokusanywa, upeo wa uchakataji, kipindi cha kuhifadhiwa, uwezo wa ufikiaji wa data na gharama ya uchakataji wa data na teknolojia zinazotumika.<sup>229</sup>

Programu zinazochunguzwa zinapaswa kuwa zilibuniwa ili kuzuiwa kukusanya maelezo ya ziada na zinapaswa kuwa zilidhibitiwa kukusanya maelezo yanayohitajika tu kwa madhumuni ya utoaji wa mikopo dijitali.

## **Haki ya Kufikia na Kufuta Data ya Binafsi**

Wakopaji wamepewa haki ya kufikia data yao inayohifadhiwa na Programu hizi<sup>230</sup> na haki ya kuomba kufutwa au kuharibiwa kwa data yao ambayo Programu hizi haziruhusiwi tena kuihifadhi, au haihusiki, ni ya ziada au ilipatikana kwa njia haramu<sup>231</sup>.

Programu hizi, hata hivyo, hazitoi nafasi ambapo wakopaji wanaweza kutekeleza haki hizi. Programu ya Tala, kwa mfano, huendelea kuhifadhi maelezo ya mtumiaji hata kama mtumiaji ameondoaa Programu hiyo kwenye kifaa.<sup>232</sup>

## **Kuhamishika kwa Data**

Sheria inawapa wamiliki wa data haki ya kupokea data yao kwa muundo uliopangwa na unaoweza kusomeka na mashine.<sup>233</sup> Inawapa pia haki, panapowezekana kiufundi, kuhamishia data moja kwa moja kwa wadhibiti au wachakataji wengine wa data.

<sup>234</sup> Programu zinazochunguzwa haziwapi watumiaji namna ya kutekeleza haki hii.

## **Utathmini wa Athari ya Ulinzi wa Data (Data Protection Impact**

### **Assessment (DPIA)**

Sheria inahitaji Utathmini wa Athari ya Ulinzi wa Data (Data Protection Impact Assessment (DPIA) utekelezwe wakati ambapo uchakataji wa data ya binafsi unaweza kusababisha hatari ya kiwango cha juu kwa haki na uhuru wa mmiliki wa data.<sup>235</sup> Hakuna programu yoyote kati ya zilizochunguzwa ambayo imetekeliza DPIA licha ya kiasi kikubwa zaidi cha data inayochakatwa.

Programu za mikopo dijitali nchini Kenya huenda zinachakata data kinyume na Sheria ya Ulinzi wa Data, ya 2019. Mbinu zake, kwa sababu hiyo, zinakiuka faragha ya watumiaji na haki ya ulinzi wa data yao. Serikali inapaswa kuziamnisha programu hizi kurekebisha sera zake za faragha ili zilingane na Sheria ya Ulinzi wa Data.

228 Kifungu cha 41 (3), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

229 Ibid

230 Kifungu cha 26 (b) Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act) ya 2019

231 Kifungu cha 40 (1) (b), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act) ya 2019

232 Sera ya Faragha ya Tala <https://tala.co.ke/privacy-policy-ke/>

233 Kifungu cha 38 (1), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

234 Kifungu cha 38 (3), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

235 Kifungu cha 31 (1), Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Act), ya 2019

# Mali



## Maelezo ya nchi

Ikiwa ni nchi isiyo na bandari inayotumia lugha ya Kifaransa inayopatikana katika eneo la Afrika Magharibi, Jamhuri ya Mali inapakana na mataifa ya Mauritania, Aljeria, Nijeri (Niger), Burkinafaso, Kodivaa (Côte d'Ivoire), Gine (Guinea) na Senegali. Ikiwa na idadi ya zaidi ya watu milioni 19, ina GDP ya Dola bilioni 17.28 za Marekani (2019) na ina mfumo wa utawala wa rais na waziri mkuu<sup>236</sup>. Mnamo Mei 2013, serikali ya Mali ilitunga Sheria nambari 2013-015 kuhusu ulinzi wa data ya binafsi katika Jamhuri ya Mali<sup>237</sup>. Sheria hii inatumika kwa uchakataji wa kiotomatiki au usio wa kiotomatiki unaofanyika kwa ujumla au kwa sehemu nchini Mali<sup>238</sup>. The Autorité de Protection des Données à Caractère Personnelles (APDP) ni DPA ya Mali<sup>239</sup>. Lengo lake kuu ni kulinda data ya binafsi na kudhibiti sekta dijitali ya Jamhuri ya Mali.

236 Katiba ya Mali iliyotungwa mnamo tarehe 25 Februari 1992 inabainisha kwamba inategemea mfumo wa utawala wa rais na waziri mkuue. Kweli, katiba inabainisha ugawanaji wa mamlaka na wajibu wa Serikali mbele ya Bunge la Kitaifa (Sheria ya 54, 78 na 79). Cf: <https://mjp.univ-perp.fr/constit/ml1992.htm#3>

237 Loi no 2013-015 du 21 mai 2013 relative à la protection des données personnelles (Sheria Nambari 2013-015 ya tarehe 21 Mei 2013 kuhusu ulinzi wa data ya binafsi) <<https://apdp.ml/wp-content/uploads/pdf/Loi-sur-la-protection-des-donnees-personnelles-du-21-mai-2013.pdf>> 2 May 2021.

238 Kifungu cha 4 cha Sheria nambari 2013-015

239 Tovuti: <https://apdp.ml/>

## Ulinzi wa Data Nchini Mali

Ukuaji wa huduma ya kutuma na kupokea pesa kupitia simu za mkononi umeanzisha huduma mpya ambazo hazijawahi kugunduliwa. Mojawapo ya huduma hizi mpya ni kutoa mikopo dijitali, sehemu ya huduma dijitali za fedha za kizazi kipya. Inarahisisha kuwapa watu mikopo ya papo hapo kwa mahitaji yao mahususi—ambayo ni njia mbadala ya huduma ya kutoa mikopo ya kawaida ambayo imefaulu zaidi katika nchi zinazotumia lugha ya Kiingereza barani Afrika.

Katika nchi zinazotumia lugha ya Kifaransa, hasa eneo la Afrika Magharibi, majaribio ya kwanza ya huduma ya kutoa mikopo dijitali yalianza mwaka wa 2018 na huduma ya 'Momo Kash' kutoka kwa kampuni ya MTN & Bridge Bank nchini Kodivaa (Côte d'Ivoire) na nchini Mali na huduma ya Singa Ni Mara<sup>240</sup> kutoka kwa shirika la First Microfinance Agency (PAMF-M)

240 SINGA NI MARA ni huduma ya kutoa huduma za akiba na mikopo midogo kwa watu, kwa ushirikiano na taasisi ndogo ya fedha ya PAMF (Première Agence de Microfinance) iliyoanzishwa mnamo Jumatano, tarehe 13 Juni 2018. Inaruhusu watu kunufaika papo hapo na bidhaa za mikopo na akiba, ambazo zinawasaidia kushughulikia haraka na kwa urahisi mahitaji ya ghafla au kuweka akiba. Inapatikana kwa kutumia msimbo wa USSD kwa wateja wa Orange Money wa huduma ya Orange Mali na hupitia programu yake ya simu za mkononi ya Orange Mali Sugu.

na Orange nchini Mali. Kwa kufahamu uwezo wa kubadilika wa aina hii ya huduma, huduma nyiningine ya kutoa bima ndogo ilianzishwa kati ya shirika jipya la OKO<sup>241242</sup> na Orange Mali. Huduma hii inategemea data ya setilaiti na huduma za kutuma na kupokea pesa kuitia simu za mkononi ili kubuni bidhaa za kiotomatiki za bima kwa wakulima. Kuhusu huduma ya Singa Ni Mara, huduma ya Oko inapatikana kwenye simu za mkononi za watu wanaotumia msimbo wa USSD na kwenye programu ya simu za mkononi ya Orange Money Mali: Orange Mali Sugu. Ni programu ya simu za mkononi ambayo kando na data inayokusanywa na akaunti za Orange Money Mali zilizohusishwa pia na zile za Oko na Singa Ni Mara, hutoa; kiasi kikubwa cha data, ambapo uchakataji wake unaweza kusababisha hatani kwa haki ya faragha ya watumiaji hawa na ambao lazima uchanganuliwe. Zaidi ya yote, aina hii ya uchakataji wa data unaofanywa na programu za simu za mkononi ulianzishwa baada ya kutungwa kwa sheria ya ulinzi wa data ya binafsi nchini Mali. Kwa hivyo, ni muhimu kujua iwapo mbinu za uchakataji wa data za programu ya simu za mkononi ya Orange Mali Sugu, kama inavyoolezwa kwenye sera na masharti yake ya matumizi, unazingatia kanuni za ulinzi wa faragha.

Utafiti huu unalenga kuchanganua sera za faragha na sheria na masharti ya programu hizi na kuchunguza jinsi zinavyotii sheria ya ulinzi wa data nchini Mali. Sehemu ya kwanza inajumuisha muhtasari wa data inayokusanywa na programu hizi. Sehemu ya pili inachunguza shughuli zake za uchakataji chini ya sheria ya ulinzi wa data ya binafsi. Sehemu ya mwisho inakamilika kwa kuonyesha iwapo programu hizi zinatii sheria inayolinda data ya binafsi au la.

## **Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali**

Orange Mali Sugu <sup>243</sup>	Maelezo yanayokusanywa na kuchakatwa na programu	
Kiungo cha kupakua : Google Play Store na Apple Store	Ruhusa zinazombwa	<p>Wakati wa kufunguka, Programu ya Orange Mali Sugu huomba:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>· Kudhibiti simu za mtumiaji · kufikia SMS za mtumiaji: Huonyesha SMS za mtumiaji ili kukusanya maelezo ya fedha na data ya shughuli za kifedha ili kukusanya maelezo kuhusu historia ya fedha ya mtumiaji na kubainisha ufaifu wake wa kupokea mikopo</li> <li>Kufikia anwani za mawasiliano za mtumiaji</li> <li>Kufikia data ya mahali, kifaa na matumizi: Programu ya Orange Mali Sugu hutumia teknolojia ya GPS au huduma zingine za mahali kubainisha mahali mahususi alipo mtumiaji</li> </ul>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	<p>Wakati wa kujisajili, programu ya Orange Mali Sugu hukusanya maelezo ya mtumiaji: jina, anwani, anwani ya barua pepe na nambari ya simu, nambari ya simu ya kifaa, maelezo ya SIM kadi, umri, jina la mtumiaji, nenosiri, data ya fedha na mikopo, maelezo ya binafsi na picha na maelezo mengine ya usajili</p>

241 <https://fr.oko.finance/mali>

242 Huduma ya bima ya kilimo ya OKO ilianzishwa mnamo Jumanne, tarehe 21 Januari 2020

243 Programu ya Orange Money Sugu haina Sera ya Ulinzi wa Data ya Binafsi. Yanayopatikana pekee ni, masharti ya matumizi ya programu ya Orange Money Mali ambayo yanashughulikia suala la uchakataji wa data katika kifungu cha 12.

	<p>Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji</p> <p>Maelezo yanayokusanywa unapotumia tovuti ya Orange Mali</p>	<p>Programu ya Orange Mali Sugu hukusanya maelezo yafuatayo kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji: Mbinu ya Utashi wa Kompyuta (Artificial Intelligence (AI): muundo wa simu, nambari ya IMEI au nambari ya kitambulisho, maelezo ya SIM kadi, maelezo ya mtandao wa simu, mfumo wa uendeshaji wa kifaa, aina ya kivinjari, data ya mahali ya kifaa na mipangilio ya saa za eneo</p> <p>Maelezo yaliyohifadhiwa kwenye kifaa: orodha ya anwani za mawasiliano, nekodi za nambari za simu, nekodi za SMS, anwani zilizo kwenye akaunti za mitandao ya kijamii, picha, video au maudhui yoyote dijitali husika.</p> <p>Mtumiaji anapotumia tovuti ya Orange Mali kwenye simu yake ya mkononi, Programu ya Orange Mali Sugu hukusanya kiotomatiki maelezo yafuatayo na kuyahifadhi kwenye faili zake za kumbukumbu.</p> <p>Anwani ya IP ya mtumiaji, aina ya kivinjari, Mto Huduma za Intaneti (ISP), kurasa za uelekezaji / kuondoka, mfumo wa uendeshaji, muhuri wa muda na maudhui ya kuvinjari.</p> <p>Kisha maelezo haya huchanganywa kwa madhumuni ya uchanganuzi au matangazo na kufichuliwa kwa mashirika ya Orange Money Mali, Oko Israel na PAMF.</p>
	<p>Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine</p>	<p>Maelezo hupatikana kutoka kwa mashirika mengine ya Orange Group: Orange Money Mali na Orange Finances Mobile Mali, Ofisi za Utathmini wa Mikopo (Credit Assessment Offices (BIC), Watoa huduma za mtandao wa simu na mashirika ya ukusanyaji wa madeni.</p>
	<p>Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji</p>	<p>Sheria na masharti ya matumizi ya Orange yanabainisha kwamba hukusanya data ya mtumiaji kwa madhumuni yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>· Kushughulikia shughuli za kifedha za mtumiaji</li> <li>· Kuthibitisha utambulisho wa mtumiaji</li> <li>· Kutoa Mikopo na ukusanyaji wa malipo</li> <li>· Kutoa mikopo na kuunda mifumo ya kutoa mikopo</li> <li>· kuchanganua tabia za mkopaji</li> <li>· Wajibu wa Programu ya Orange Mali Sugu kwa watumiaji</li> <li>· kutii · kutii sheria, vifungu na kanuni zinazohusiana na mchakato wa “jua mteja wako” na kanuni za kupinga ulanguzi wa pesa</li> <li>· Kuzuia ulaghai,</li> <li>· Huduma za matangazo</li> </ul>

	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Programu ya Orange Mali Sugu hushiriki maelezo ya mtumiaji na: Wanachama wake, maajenti, watoa huduma, mashirika ya Orange Money Group, na mashirika ambayo hupewa kandarasi ya kushughulikia data iliyokusanywa. · Mtu yejete anayewakilisha mtumiaji · taasisi za fedha, ofisi za mikopo na mashirika (BIC) · Washirika wa kibashara katika hali za uhamishaji, uuzaaji, muungano na ununuzi wa biashara, nk. Watoa huduma wengine Mashirika ya utekelezaji wa sheria (Mamlaka ya Ulinzi wa Data ya Binafsi (Authority for the Protection of Personal Data (APDP)), maofisa wa serikali, kwa msingi wa: Ombi rasmi au agizo la mahakama Kutii Sheria au Kuripoti Shughuli za Kinyume cha Sheria Zinazoshukiwa  Sera yake haitoi maelezo yoyote kuhusu muda ambao wahusika wengine wanaweza kufikia maelezo ya binafsi ya mtumiaji na kuyahifadhi.
	Teknolojia za Ufuatiliaji / Vidakuvi vya Tovuti	Programu ya Orange Mali Sugu hutumia teknolojia za ufuatiliaji wa simu na vidakuvi vya tovuti ili kutofautisha watumiaji wa Programu.
	Jinsi Programu Inavyohifadhi Maelezo ya Mtumiaji	Programu ya Orange Mali Sugu huhifadhi maelezo ya mtumiaji nje ya nchi ya Mali. Data inaweza pia kuchakatwa na wafanyakazi wa Orange Money Mali, Orange Mali. Hakuna maelezo yanayotolewa pia kuhusu kipindi cha muda wa kuhifadhiwa kwa data na Standard Bank.

## **Uchunguzi Kifani: Orange Mali Sugu (Swali la kipindi cha kuhifadhiwa kwa data ya mtumiaji)**

Sheria na masharti ya akaunti za Orange Money Mali zilizohusishwa na Programu za Orange Mali Sugu hazitoi maelezo kuhusu kipindi cha kuhifadhiwa kwa data ya mtumiaji. Ukosefu huu unasababisha ukiukaji wa sheria ya ulinzi wa data nchini Mali, ambayo inahitaji kuwa data ikusanywe kwa kipindi maalum.<sup>244</sup> Kando na hayo, programu ya Orange Mali Sugu haina sera maalum ya faragha.

## **Uchanganzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu za Mikopo Dijitali Kuhusiana na Sheria Inayohusiana na Ulinzi wa Data Binafsi**

Sheria ya Mali ya ulinzi wa data ya binafsi imebainisha kwa uwazi wajibu wa kutekelezwa katika sheria za faragha, unaotumika katika uchakataji wowote, iwe ni wa kiotomatiki au la<sup>245</sup>. Kwa kufanya hivyo, programu za mikopo dijitali pia zimejumuishwa. Hata hivyo, kutokana na kuanzishwa kwake hivi karibuni, hatari za ulinzi wa faragha ni mpya. Sehemu hii inaangazia vifungu husika vya Sheria ili kutambua iwapo Programu hizi zinatii vifungu hivi.

244 Kifungu cha 15 cha Sheria nambari 2013-015  
245 Kifungu cha 5 na 6 vya Sheria nambari 2013-015

## Haki ya Faragha

Sheria ya ulinzi wa data inahitaji wadhibiti na wachakataji wa data (katika hali hii, programu za mikopo dijitali) washughulikie data ya binafsi kwa njia ambayo inaheshimu haki ya faragha.<sup>246</sup> Katika hali hii, sheria inazitaka programu hizi zihakikishe kuwa haki za faragha za wakopaji inazingatiwa kwanza wakati wa kuchakata data yao. Programu zilizofanyiwa utafiti zinakiuka haki hii na zinachakata data ambayo inaingilia faragha ya mtumiaji na isiyohusiana na madhumuni ya ukusanyaji wa data. Kwa mfano, programu hizi hukusanya maelezo kama vile anwani za mawasiliano zilizohifadhiwa kwenye kifaa cha mkopaji, maelezo ya kuingia katika akaunti kwenye mifumo ya mitandao ya kijamii, na data sahihi ya moja kwa moja ya mahali, ambayo inaingilia faragha ya mtumiaji na haihusiani na madhumuni ya ukusanyaji wa data.

## Uhalali, Haki na Uwazi

Sheria ya ulinzi wa data inahitaji programu hizi zichakate data kwa njia halali, ya haki na uwazi.<sup>247</sup> Hii inamaanisha kwamba programu hizi zihakikishe kwamba wamiliki wa data wamejulishwa kwa uwazi na kwa ufupi jinsi data yao itakavyotumiwa na kwamba masharti yote ya sheria yametimizwa katika uchakataji huo.<sup>248</sup>

Katika hali hii, programu zinapaswa kufahamisha watumiaji kwa nini data yao inakusanywa, jinsi data yao itakavyotumiwa na, ikiwa itashirikiwa na wahusika wengine, ni nani ambao data yao itashirikiwa nao na muda ambao watahifadhi data hiyo. Inaweza kusemekana kuwa programu zilizofanyiwa utafiti zinaeleza kwa uwazi kwa nini zinakusanya data ya mtumiaji na wahusika zinaoshiriki nao data hiyo. Hata hivyo, hazielezi muda ambao wahusika wengine watafikia data hiyo na muda ambao watahifadhi.

## Kikomo cha Madhumuni, Ufaafu na Utoshelevu

Programu za mikopo dijitali zinahitajika chini ya sheria ya ulinzi wa data kuchakata data ya binafsi baada ya ukusanyaji wa data.<sup>249</sup> Hii inamaanisha kuwa zinapaswa tu kukusanya data inayohusiana na madhumuni ya kutoa mikopo dijitali wala si data isiyohusiana na madhumuni hayo. Programu zinapaswa kukusanya tu data inayohusika, ya kutosha na inayohusiana na madhumuni ya ukusanyaji wa data.<sup>250</sup>

Programu Orange Mali Sugu hukusanya maelezo ya binafsi ambayo hayahusiki na madhumuni ya ukusanyaji wa data. Hukusanya maelezo ya wakopaji, kama vile nambari za kadi za mikopo, shughuli za kifedha, maelezo ya kuingia katika akaunti ya mitandao ya kijamii, anwani za mitandao ya kijamii, anwani za simu, picha na video, nk, ambayo hayahusiki katika utoaji wa mikopo dijitali.

## Kushiriki Maelezo na Wahusika Wengine

Sheria ya ulinzi wa data ya Mali inaeleza kwamba programu hizi lazima ziwafahamishe watumiaji kuhusu wahusika wengine ambao zitashiriki nao data yao, ikijumuisha mbinu zilizowekwa ili kulinda usalama wa data yao kabla ya kukusanya.<sup>251</sup> Katika hali mahususi ya Programu za Orange Mali Sugu, ukosefu wa kipindi maalum cha uchakataji wa data unasababisha ukiukaji wa haki za faragha<sup>252</sup>.

Programu za Orange Mali Sugu hushiniki maelezo ya mtumiaji/mkopaji na ofisi ya maelezo ya mikopo (Credit Information Office (CIO), washinika wa kibashara, wataalamu wa ushauni, serikali na mashirika ya utekelezaji wa sheria, nk. Hazibainishi mbinu zilizowekwa ili kulinda

246 Kifungu cha 8 cha Sheria nambari 2013-015

247 Kifungu cha 7 cha Sheria nambari 2013-015

248 Kifungu cha 15 cha Sheria nambari 2013-015

249 Kifungu cha 15 cha Sheria nambari 2013-015

250 Kifungu cha 15 cha Sheria nambari 2013-015

251 Kifungu cha 11 na 15 vya Sheria nambari 2013-015

252 Kifungu cha 8 cha Sheria nambari 2013-015

data ya mkopaji. Programu za Orange Mali Sugu pia hazielezi muda ambao wahusika hawa wataweza kufikia data na muda watakaoihifadhi.

## **Uhamishaji wa Data ya Binafsi Nje ya Nchi ya Mali**

Kifungu kinachofuata na watoa huduma za programu mbalimbali

### **Usiri Kimuundo na kwa Chaguomsingi**

Sheria inaeleza kwamba mdhibiti wa data lazima aweke mikakati yote ya uchakataji wa data ya mtumiaji<sup>253</sup>. Programu za Orange Mali Sugu zina mbinu za usimbaji za kulinda mawasiliano ya wateja wake na maudhui ya siri. Kiwango cha usalama kinachohitajika ili kulinda data ya mtumiaji. Hata hivyo, kiwango cha usalama kilicho jumuishwa hakiwezi kuzuia mto huduma ya Programu kukusanya maelezo ya ziada.

### **Haki ya Kufikia na Kufuta Data ya Binafsi**

Watumiaji wa Programu za Orange Mali Sugu wana haki ya kufikia data yao inayohifadhiwa na programu hizi<sup>254</sup> na wana haki ya kuomba kufutwa au kuharibiwa kwa data yao ambayo programu haziruhusiwi tena kuhifadhi. Watumiaji pia wana haki ya kuomba kufutwa kwa data ambayo haihusiki, ni ya ziada au iliyopatikana kwa njia<sup>255</sup> haramu.

### **Kuhamishika kwa Data**

Sheria inawapa wamiliki wa data haki ya kupokea data yao kwa muundo uliopangwa na unaoweza kusomeka na mashine.<sup>256</sup> Inawapa pia haki, panapowezekana kiufundi, kuhamishia data moja kwa moja kwa wadhibiti au wachakataji wengine wa data.

<sup>257</sup> Programu za Orange Mali Sugu zinazochunguzwa haziwapi watumiaji njia za kutekeleza haki hii.

### **Utathmini wa Athari ya Ulinzi wa Data (Data Protection Impact**

#### **Assessment (DPIA)**

Sheria inahitaji ripoti kuhusu mchakato wa uchakataji wa data itolewe kila mwaka na kutumwa kwa Mamlaka ya Ulinzi wa Data ya Binafsi (Personal Data Protection Authority (APDP). Kando na hayo, mamlaka za kuidhinisha uhamishaji wa data zimebainisha haja ya wadhibiti wa data kutekeleza Utathmini wa Athari ya Ulinzi wa Data (Data Protection Impact Assessment (DPIA). Hata hivyo, programu ya Orange Mali Sugu hajatoa wala kuchapisha ripoti zake.

### **Hitimisho**

Mbinu za uchakataji wa data za programu za mikopo dijitali nchini Mali hazitii kanuni za msingi za sheria ya ulinzi wa faragha. Tathmini za athari ya ulinzi wa data (DPIA) lazima zifanywe ili kushinikiza wanaowajibika na uchakataji wa data wa programu hizi kutii wajibu wa kisheria kikamilifu kuhusiana na suala hili. Kando na hayo, marekebisho ya sheria nambari 2013-015 ya tarehe 21 Mei 2013, kuhusu ulinzi wa data ya binafsi lazima yazingatiwe, kwa kuzingatia hatari zinazoweza kujitokeza kwa suala la faragha. Zaidi ya hayo, ni muhimu pia kwa shirika la APDP Mali kupata ujuzi na nyenzo za kiufundi za kufuatilia moja kwa moja ukubwa, ubora na wingi wa data inayokusanywa na wadhibiti hao wa data kwa uchakataji wa maombi ya mikopo dijitali.

<sup>253</sup> Kifungu cha 8 cha Sheria nambari 2013-015

<sup>254</sup> Kifungu cha 12,13,14,18 na 18 vya Sheria nambari 2013-015

<sup>255</sup> Kifungu cha 12,13,14,18 na 18 vya Sheria nambari 2013-015

<sup>256</sup> Kifungu cha 12 cha Sheria nambari 2013-015

<sup>257</sup> Kifungu cha 12 cha Sheria nambari 2013-015

# Moroko



## Maelezo ya Nchi

Ufalme wa Moroko unapatikana katika eneo la kaskazini magharibi mwa Afrika na ina idadi ya watu milioni 37<sup>258</sup> na GDP inayokadiriwa ya Dola Bilioni 117 za Marekani mwaka wa 2021.<sup>259</sup> Nchi hii ina mfumo wa utawala wa kifalme na wabunge wanaochaguliwa. Kulingana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (African Development Bank (2018), uchumi wa Moroko unazingatiwa kuwa uchumi thabiti zaidi barani Afrika. Sekta ya kutoa huduma inaongoza katika uchumi wa Moroko, kwa kuchangia karibu 55% ya GDP.<sup>260</sup>

258 Atlas monde <https://www.atlas-monde.net/afrique/maroc/> > ilifikiwa tarehe 23 Agosti 2021.

259 Uchumi wa biashara <https://tradingeconomics.com/morocco/gdp> > ilifikiwa tarehe 25 Agosti 2021.

260 <https://thefintechtimes.com/fintech-africa-morocco/> > accessed on 25 August 2021.

## Ulinzi wa Data Nchini Moroko

Kulingana na shirika la Freedom House (2020), Uhuru wa matumizi ya intaneti nchini Moroko unazingatiwa kuwa dhaifu huku msako wa waandishi wa habari wa mtandaoni wanaokusanya habari kuhusu maandamano ukiendelea, na tovuti zinazounga mkono serikali zikichapisha habari za uongo kuhusu wanaharakati na waandishi wa habari. Ufikiaji wa huduma za intaneti unapozidi kuongozeka kwa ujumla, serikali inaendelea kudumisha mifumo mikali ya upelelezi.<sup>261</sup>

Sheria ya Moroko kuhusu ulinzi wa data ilitungwa mnamo tarehe 18 Februari 2009.<sup>262</sup> Sheria hii inatumika kwa mbinu za kiotomatiki au zisizo za kiotomatiki za uchakataji wa data ya binafsi kwa ujumla au kwa sehemu, kwa data ya binafsi inayohifadhiwa au inayokusudiwa kuhifadhiwa kwenye faili za kawaida.<sup>263</sup> Nchi hii ina Shirika la Ulinzi wa Data – DPA – Tume ya Kitaifa ya Usimamizi na Ulinzi wa Data ya Binafsi (National Commission for the Supervision Protection of Personal Data (CNPD))<sup>264</sup> ilianzishwa kwa Amri ya tarehe 21 Mei 2009.

## Mfumo wa Fedha na Teknolojia ya Fedha Nchini Moroko

Benki, ambazo zinadhibitiwa na Benki Kuu ya Moroko (Central Bank of Morocco) (Bank Al Maghreb – BAM),<sup>265</sup> zinachangia karibu nusu ya mfumo wa fedha wa nchi.<sup>266</sup> Kati ya benki 19 zilizopo, benki tatu maarufu zinachangia zaidi ya thuluthi mbili za amana na mali zote za

261 Freedom House 2020 <https://freedomhouse.org/country/morocco/freedom-net/2020> > ilifikiwa tarehe 25 Agosti 2021.

262 Sheria ya 09-08 ya tarehe 18 Februari 2009 <https://www.cndp.ma/images/lois/Loi-09-08-Fr.pdf> > accessed on 10 May 2021.

263 Sheria ya 09-08 ya tarehe 18 Februari 2009, kifungu cha 1, aya ya 1, kifungu cha 2.

264 <https://www.cndp.ma/fr/> > ilifikiwa tarehe 24 Agosti 2021.

265 <https://www.bkam.ma/> > ilifikiwa tarehe 24 Agosti 2021.

266 <https://thefintechtimes.com/fintech-africa-morocco/> > ilifikiwa tarehe 22 Agosti 2021.

benki. Tangu mwaka wa 2007, BAM imefanya juhudzi za kutambulika katika kubonesha uwezo wa kufikia huduma za fedha.<sup>267</sup>

Mwaka wa 2014, ilibuni sheria mpya (Nambari 103-12), iliyochapishwa kwenye Journal Officiel mnamo Machi 2017 (Banking Law).<sup>268</sup> Inatumika kwa mashirika (ikijumuisha Benki za Kiislamu (Islamic Banks) zinazoshiriki): yanayopokea fedha kutoka kwa umma, yanayotekeleza huduma za mikopo, yanayowapa wateja huduma yoyote malipo au usimamizi.

Sheria hii inaunda aina mbinu za watoa huduma za fedha, hivyo basi kuongeza ushindani ndani ya sekta ya huduma za malipo. Aina mpya, inayotafsiriwa kwa urahisi kama ‘huduma za benki za kiushiriki’, inaruhusu mashirika ambayo si benki kutoa huduma za fedha, hatua ambayo inawezesha shughuli za kutuma na kutoa pesa kutoka kwa akaunti za malipo.

Kulingana na shirika la Fintechnews Middle East (Aprili 2021),<sup>269</sup> Moroko ni kitovu cha tatu kikubwa zaidi cha teknolojia ya fedha katika Ulimwengu wa Kiarabu, ikiwa inamiliki 13% ya huduma zote 400 za teknolojia ya fedha, au karibu huduma 40 za teknolojia ya fedha. Inarekodiwa kuwa kiwango cha jumla cha ukuaji wa huduma za benki nchini Moroko kilikuwa 28.6% mwaka 2017, na uchumi unaendelea kutegemea hasa shughuli za kibashara za pesa taslimu, na karibu 80% ya shughuli za kifedha zikifanywa kwa kutumia pesa taslimu.

Kiwango cha juu cha huduma za simu inaripotiwa kuwa zinatumia mfumo wa Teknolojia ya Fedha wa Morocco. Shirika la Fintech News Middle East kwanza liliripoti kuwa kati ya huduma 40 zinazotumika za teknolojia ya fedha nchini Moroko, huduma ya malipo, kutuma pesa na mifumo ya kulipia bidhaa dukani (POS) ni sekta iliyoendelea zaidi.<sup>270</sup> Miundo mingine ya Teknolojia ya Fedha inayokua kwa maarufu ni ya kuchangisha pesa kutoka kwa watu wengi, huduma za fedha za kibinafsi, mifumo ya kukopesha pesa na takwimu za kina za data. Kwa mfano, Cotizi<sup>271</sup> unaripotiwa kuwa ni mfumo wa kwanza wa kuchanganisha pesa kutoka kwa watu nchini.

## **Wafacash/Jibi: Programu ya Simu za Mkononi ya Kukopesh Pesa**

Jibi<sup>272</sup> ni programu ya huduma ya kutuma na kupokea kuitia simu za mkononi inayopatikana wakati wowote ambayo inaruhusu wateja kufanya shughuli za kifedha mtandaoni au kwenye simu ya mkononi ya mtumiaji. Kwa kutumia programu ya Jibi, wateja wanaweza: kulipia bidhaa wanazonunua kwa kutumia simu ya mkononi kutoka kwa mtandao mkubwa wa wafanyakilishi; kuweka na kutoa pesa popote na wakati wowote wanapotaka kuitia mtandao wetu mkubwa wa matawi ya Wafacash na maajenti wa rejaneja kote nchini Moroko.

Hutuma pia pesa kutoka kwenye simu zao za mkononi hadi kwenye akaunti ya simu ya mkononi ya Jibi, akaunti ya benki au tawi la Wafacash. Mtu pia anaweza kutumiwa pesa kutoka kwa mojawapo ya matawi ya Wafacash, kulipa bili au kufanya ununuzi mtandaoni bila kutoa maelezo ya benki au kuweka mjazo kwenye simu yake mkononi.

Kwa ushirikiano na Wafasalaf, Wafacash hutoa huduma ya mikopo kwa wateja ambayo inaruhusu kupokea mkopo wa muda mfupi kwa ajili ya mradi au kushughulikia gharama

267 Idem

268 Sheria Nambari 103-12 – Kwa Mashirika ya Mikopo na Mashirika Ya Kutoa Huduma Kama Hizo (Banking Law) <https://dfsobservatory.com/sites/default/files/Parliament%20of%20Morocco%20-%20Law%20No.%20103-12%20-%20On%20Credit%20Institutions%20and%20Similar%20Business%20%28Banking%20Law%29.pdf> > ilifikiwa tarehe 22 Agosti 2021.

269 Ripoti ya habari <https://www.moroccoworldnews.com/2021/01/331921/cmi-chief-moroccos-2020-e-commerce-transactions-rose-43/> > ilifikiwa tarehe 22 Agosti 2021.

270 Ripoti ya habari <https://www.crowdfundinsider.com/2021/04/174365-morocco-is-now-home-to-many-fintech-services-crowdfunding-lending-advanced-data-analytics-platforms-report/> > ilifikiwa tarehe 22 Agosti 2021.

271 <http://www.cotizi.com/> > ilifikiwa tarehe 22 Agosti 2021.

272 Inapatikana kwenye Google Play – <https://play.google.com/store/apps/details?id=com.b3g.wafacash.jibi&hl=fr&gl=US> and iOS – <https://apps.apple.com/fr/app/jibi-pro/id1371478054>

yoyote. Wafacash hutoa huduma za kutimiza mahitaji ya wateja wake, kuanzia kwa huduma ya kutoa mikopo ya kawaida hadi mikopo midogo kwa ushirikiano na Wafasalaf na Al Amana Micro Finances – inatumika kama programu ya kukopesha pesa.<sup>273</sup>

## Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali

Wafacash/Jibi <sup>274</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu <sup>275</sup>
Ruhusa zinazotakikana	Kutafuta akaunti zilizo kwenye kifaa Kutafuta akaunti zilizo kwenye kifaa Kupiga picha na video Kuangalia miunganisho ya Wi-Fi Kusoma hali ya simu na utambulisho Kusoma maudhui ya nafasi ya hifadhi ya USB ya mteja Kubadilisha au kufuta maudhui ya nafasi ya hifadhi ya USB ya mteja
Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Data ya binafsi: cheo, jina la ukoo, jina la kwanza Nambari ya simu Mtoa huduma za simu Anwani ya barua pepe
Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Data ya mahali pasipo mahususi (inayotokana na mtandao) Data ya mahali mahususi (inayotokana na GPS na mtandao) Kusoma hali ya simu na utambulisho Wajibu wa mteja ni kulinda simu yake ya mkononi ipasavyo, kuhifadhi nakala ya data yake na kifaa, na kuchukua hatua mwafaka na zinazofaa za tahadhari ili kutambua virusi na vitu vingine viharibifu. Wafacash haitawajibika kwa hasara zozote ambazo mteja anaweza kupata kwa sababu ya matukio ya hapo. Shughuli zote zinazotekelizwa na mteja kuitia "Programu ya Simu za Mkononi ya Jibi" na "Tovuti ya Jibi", ambacho zimethibitishwa, zinachukuliwa kuwa zimefanywa na mteja. Mteja anakubali moja kwa moja na anaahidi kutopinga.

273 <https://www.wafacash.com/cr%C3%A9dit-micro-cr%C3%A9dit/> / <https://www.alamana.org.ma/fr/alamana/tout-savoir-sur-le-micro-credit> > ilifikiwa tarehe 23 Agosti 2021.

274 <https://www.wafacash.com/mentions-legales> > ilifikiwa tarehe 22 Agosti 2021.

275 Sheria na Masharti (yalianza kutumika tarehe 4 Julai 2018) [https://www.jibi.co.ma/DocReadme/CG\\_JIBI\\_VF\\_04072018\\_Valide.pdf](https://www.jibi.co.ma/DocReadme/CG_JIBI_VF_04072018_Valide.pdf)

/ Sera ya Faragha <https://www.jibi.co.ma/DocReadme/PROPRIETE%20INTELLECTUELLE%20JIBI.pdf> > ilifikiwa tarehe 25 Agosti 2021.

	Maelezo yanayokusanywa kutokana na kutumia tovuti ya Jibi	Matumizi ya tovuti ya www.wafacash.com hayadhibitiwi na ni huru kwa kila mtu. Wafacash inahifadhi haki, kwa sababu mabadiliko ya kudumu ya intaneti na bidhaa na huduma, kubadilisha au kufuta, wakati wowote na bila kutoa notisi ya mapema, masharti ya matumizi yaliyopendekezwa na maelezo yanayopatikana kwenye tovuti ya www.wafacash.com. Kulingana na sheria ya 09-08 ya ulinzi wa watu kuhusu uchakataji wa data ya binafsi, mtumiaji anafahamishwa kwamba kwa kukubali masharti ya jumla, mtumiaji wa tovuti anakini kuwa data yake inaweza kuchakatwa kwa kutumia kompyuta. Kwa hali yoyote, wafacash hukusanya tu maelezo ya binafsi yanayohusiana na mtumiaji wa huduma fulani zinazotolewa na tovuti ya www.wafacash.com. Mtumiaji hutoa maelezo haya kwa kufahamu kikamilifu maelezo wanayoweka.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Maelezo yanayokusanywa yanaweza kuchakatwa kwa kutumia kompyuta. Yanakusudiwa kutumiwa na Wafacash, kikundi chake na mashirika yake tanzu, ambayo, kwa makubaliano ya moja kwa moja, yana idhini ya kuendelea na shughuli zake za uchakataji wa kiotomatiki au usio wa kiotomatiki, kuyafichua kwa mashirika halali ya kikundi chake, washirika na watoa huduma. Wafacash, kikundi chake na mashirika yake tanzu husika yanaahidi kutumia maelezo yaliyokusanywa kwa madhumuni ya kutimiza wajibu wa kisheria na usimamizi pekee. Yanaweza pia kutumika kuendelea kufahamisha mteja kuhusu huduma, matukio, vitendo au machapisho mapya ambayo yanaweza kumvutia.
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kupokea data kutoka kwenye intaneti Kutambua vyanzo vya data ya mahali vya kujaribu Kuangalia miunganisho ya mtandao Kufikia mtandao kikamilifu Kuzuia kifaa kuingia katika hali tuli Kusoma mipangilio ya huduma ya Google

	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Maelezo ya binafsi yanakusanywa yanakusudiwa kutumiwa na idara za Wafacash zinazowajibika kwa kushughulikia maombi ya mteja ya kudhibiti programu za HR, malalamiko na rufaa, na programu za ushirika. Hutumiwa na Wafacash, Attijariwafa Bank Group <sup>276</sup> na washirika wake na yanaweza kufichuliwa kwa mamlaka yoyote ya usimamizi au ya mahakama kwa kuwa na haki ya kutuma maelezo.
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	Sheria na masharti ya jumla hayabainishi kipindi mahususi cha muda. Huanza kutekelezwa mteja anapotia sahihi ya makubaliano ya akaunti. Wafacash ina haki ya kubadilisha sheria na masharti ya jumla, kuyaongeza au kuyafuta, kushughulikia vyema hali ya kuridhishwa kwa mteja, na mabadiliko ya masharti ya sheria, usimamizi na kiufundi.
	Teknolojia za ufuatiliaji/vidakuzi vya tovuti	Matumizi ya vipengele vya tovuti ya www.wafacash.com yanaweza kuhitaji kuwekwa kwa vidakuzi. Tovuti ya www.wafacash.com hutumia vidakuzi kukumbuka mapendeleo yaliyochaguliwa na mtumiaji wakati wa kutembelea tovuti na kwa madhumuni ya uchanganuzi na vipimo vya watumiaji.

## Hitimisho

Moroko ni mojawapo ya nchi ambayo zimeshuhudia ukuaji wa haraka wa mifumo dijitali katika sekta ya fedha na biashara. Utafiti wetu unatambua kuwa muktadha unaonyesha kuwa nchi hii ina utaratibu wa sheria uliopangwa vizuri unaoleza wazi kuhusu jinsi huduma hizi dijitali/programu zinapaswa kufanya kazi. Isitoshe, tangu mwaka wa 2007, Benki Kuu ya Moroko (Central Bank of Morocco) (Bank Al Maghreb – BAM) imekuwa ikijitahidi sana kuboresha huduma za ufikiaji wa fedha. Mwaka wa 2014, ilibuni sheria mpya (Nambari 103-12), iliyochapishwa mnamo Machi 2017 (Banking Law).

Mojawapo ya hitimisho kuu linalohusiana na uwepo wa programu dijitali ambazo, katika wingi wake, hazidhibitiwi kwanza nchini Moroko, kwa sababu zinaundwa na kampuni za kigeni. Kwa upande mwingine, tunatambua ukosefu wa hali thabiti. Shirika la Ulinzi wa Data tayari limechukua hatua za kulinda haki za watumiaji, hata baada ya kutangaza matukio ya wizi wa data ya wateja kwenye Intaneti mwezi wa Julai mwaka huu.<sup>277</sup>

276 [> ilifikiwa tarehe 25 Agosti 2021.](https://www.attijariwafabank.com/fr)

277 Ripoti ya habari [> ilifikiwa tarehe 25 Agosti 2021.](https://www.zdnet.fr/actualites/un-pirate-accuse-de-fraude-bancaire-arrete-au-maroc-39925899.htm)

# Msumbiji



## Maelezo ya Nchi

Maputo ni jiji kuu la Msumbiji. Nchi hii ina zaidi ya watu milioni 30, na Kineno ni lugha nasi ya taifa.<sup>278</sup> Nchi ya Msumbiji inapatikana katika eneo la Kusini mwa Afrika, na inapakana na taifa la Eswatini katika eneo la kusini.<sup>279</sup> Kulingana na miundo mikubwa ya kimataifa ya Trading Economics na matarajio ya wachanganuzi, kufikia mwisho wa mwaka wa 2021, GDP inatarajiwa kufikia Dola Bilioni 14.30 za Marekani.<sup>280</sup>

278 <http://www.ine.gov.mz/iv-rgph-2017/mocambique/censo-2017-brochura-dos-resultados-definitivos-do-iv-rgph-nacional.pdf> > ilifikiwa tarehe 15 Julai 2021.

279 <https://www.britannica.com/place/Mozambique> > ilifikiwa tarehe 17 Julai 2021.

280 <https://tradingeconomics.com/mozambique/gdp> > ilifikiwa tarehe 17 Julai 2021.

## Ulinzi wa Data Nchini Msumbiji

Utangulizi wa Katiba ya Msumbiji ya 2004, kama ilivyorekebishwa, unasisitiza haja ya kukubaliwa kwa maoni mengi na heshima na mahakikisho ya haki za msingi za binadamu.<sup>281</sup> Kifungu cha 48 kinatoa haki ya uhuru wa kujieleza, vyombo vya habari na haki ya kufikia maelezo ambayo haitadhibitiwa. Inclusive Internet Index 2020<sup>282</sup>, ambayo hutathmini upatikanaji wa intaneti, unafuu, ufaafu na utayari, inaorodhesha nchini ya Msumbiji katika nafasi ya 94 katи ya nchi 100. Kulingana na Faharasa hiyo, alama za chini za nchi ya Msumbiji katika vigezo vyote vinne vya utathmini zinahusishwa na viwango vya chini vya elimu, usambazaji wa chini wa umeme na muundo msingi wa mtandao.<sup>283</sup>

Msumbiji kwa sasa inaorodhesha katika nafasi ya 45 katи ya nchi 61 katika unafuu wa upatikanaji wa huduma ya intaneti.<sup>284</sup> Bado hakuna sheria maalum kuhusu ulinzi wa data na faragha. Kanuni za mwongozo zinatolewa na katiba, sheria ya umma na vifungu mbalimbali vya sheria ya kisekta ambavyo vinasimamia ulinzi wa data katika sekta maalum. Mwaka wa 2020, marekebisho mapya<sup>285</sup> yaliyofanywa kwenye Kanuni ya Adhabu ya Msumbiji (Mozambican Penal Code)<sup>286</sup> yaliwekwa ili kulinda faragha. Shirika la Media Institute of Southern Africa (MISA) liliikutana na serikali ya Msumbiji ili kujadili juhudhi za pamoja za ulinzi

281 [https://cdn.accf-francophonie.org/2019/03/mozambique\\_const-en.pdf](https://cdn.accf-francophonie.org/2019/03/mozambique_const-en.pdf) > ilifikiwa tarehe 19 Julai 2021.

282 <https://theinclusiveinternet.eiu.com> > ilifikiwa tarehe 22 Julai 2021.

283 <https://theinclusiveinternet.eiu.com/explore/countries/MZ/?category=affordability> > ilifikiwa tarehe 24 Julai 2021.

284 <https://a4ai.org/affordability-report/report/2019/#annexes> > ilifikiwa tarehe 25 Julai 2021.

285 <https://advox.globalvoices.org/2020/01/17/new-privacy-law-in-mozambique-threatens-freedom-of-expression-activists-say/> > ilifikiwa tarehe 26 Julai 2021.

286 <https://acjr.org.za/news/mozambique-promulgates-new-penalty-code> > ilifikiwa tarehe 27 Julai 2021.

wa data na kukabiliana na uhalifu wa mtandaoni katika kipindi hicho.<sup>287</sup>

Tarehe 26 Juni 2018, Msumbiji ilitia sahihi Makubaliano ya Umoja wa Afrika kuhusu Usalama wa Mtandaoni na Ulinzi wa Data ya Binafsi (African Union Convention on Cyber Security and Personal Data Protection)<sup>288</sup> ('Makubaliano ya AU'). Msumbiji bado haijaidhinisha Makubaliano ya AU, na hali hii inaweza kuonyesha mwelekeo wa jumla wa jinsi utaratibu wa ulinzi wa data unaweza kujitokeza katika mamlaka.<sup>289</sup>

## **Mfumo wa Fedha na Teknolojia ya Fedha Nchini Msumbiji**

Sekta ya fedha nchini Msumbiji inasimamiwa na Benki Kuu (Central Bank (Banco de Moçambique)).<sup>290</sup> Sheria Nambari 14/2013 ya tarehe 12 Agosti inaweka<sup>291</sup> utaratibu wa kisheria wa uzuaiji na udhibiti wa matumizi ya mfumo wa fedha kwa utekelezaji wa vitendo vya ulangazi wa pesa, bidhaa au haki zinazotokana na shughuli za uhalifu zinazolezwa chini ya sheria, na hii inatumika kwa Programu za Simu za Mkononi za Kukopesha Pesa. Kifungu cha 17 cha Sheria kinaleza kuwa taasisi za fedha na mashirika ya fedha yanayodhibitiwa na sheria yanapaswa kuhifadhi hati za utambulisho na shughuli za kifedha kwa miaka 15 kuanzia tarehe ya kufungwa kwa akaunti za mteja husika au kukomeshwa kwa mkataba.

Sheria hiyo inasimamiwa na Amri ya 66/2014, ya tarehe 29 Oktoba.<sup>292</sup> Katika kifungu chake cha 2, Amri hii inaelezwa kuwa taasisi zote za fedha, benki au mshirika ya programu za simu za mkononi, yanapaswa kuwa na angalau utambulisho wa wateja, ambao unathibitishwa na kadi ya kitambulisho au hati nyingine ya utambulisho inayotumika nchini Msumbiji. Mwaka wa 2020, Msumbiji ilipitisha Sheria Nambari 20/2020 ya tarehe 31 Desemba, ambayo inatambua Taasisi za Mikopo na Kampuni za Fedha.<sup>293</sup> Sheria ya Shughuli za Kifedha za Kielektroniki (Sheria Nambari 03/2017, ya tarehe 9 Januari), kwa mfano, inatoa masharti yanayohusiana na biashara ya mtandaoni.<sup>294</sup>

## **M-Pesa: Programu ya Simu za Mkononi ya Kukopesha Pesa**

M-Pesa<sup>295</sup> ni huduma kubwa zaidi ya huduma za fedha za simu nchini Msumbiji ambayo inaruhusu wateja kutuma na kutoa pesa, kununua mjazo wa simu, kulipia bili ya stima na kulipia huduma zingine kuitia simu za mkononi.<sup>296</sup> Kampuni ya Vodafone M-Pesa SA iliunda huduma hii.<sup>297</sup> Ilianzzishwa tarehe 16 Januari 2013 na inasimamiwa na Benki ya Msumbiji (Bank of Mozambique). Idadi ya wateja wanaotumia huduma hii hawajulikani. Hivi karibuni, M-Pesa ilianzisha huduma inayojulikana kama "Txuna", ambayo itaangaziwa kwenye utafiti wetu. Txuna M-Pesa ni huduma ya fedha – programu ya simu za mkononi ya kukopesha pesa ambayo inaruhusu wateja kukopa pesa kutoka kwenye Benki na kupokea pesa kuitia huduma ya M-Pesa kwenye simu zao bila kuhitaji kuwa na akaunti ya benki. Huduma hii inatolewa kwa wateja wote wa Vodacom walio na akaunti ya M-Pesa ambayo imetumika kwa

287 Ripoti ya vyombo vya habari <https://www.misa.org.mz/index.php/destaques/noticias/85-government-and-misa-mozambique-explore-synergies-for-cyber-security> > accessed on 27 July 2021.

288 <https://platform.dataguidance.com/legal-research/african-union-convention-cyber-security-and-personal-data-protection-27-june-2014-0> > ilifikiwa tarehe 25 Julai 2021.

289 <https://www.dataguidance.com/jurisdiction/mozambique> > ilifikiwa tarehe 26 Julai 2021.

290 [https://www.salcaldeira.com/index.php/pt/component/docman/cat\\_view/32-legislacao/77-bancario](https://www.salcaldeira.com/index.php/pt/component/docman/cat_view/32-legislacao/77-bancario) > ilifikiwa tarehe 24 Julai 2021.

291 <http://www.minec.gov.mz/index.php/documentos/legislacao/131-lei-14-2013-lei-de-branqueamento-de-capitais/file> > ilifikiwa tarehe 24 Julai 2021.

292 Amri ya 66/2014, ya tarehe 29 Oktoba <https://www.standardbank.co.mz/en/content/download/94383/2328657/file/Decreto%20n%C2%BA66-2014%20-%20Regulamento%20da%20Lei%2014-2014%20-%20Branqueamento%20de%20Capitais.pdf> > ilifikiwa tarehe 20 Julai 2021.

293 [https://www.salcaldeira.com/index.php/pt/publicacoes/artigos/doc\\_download/1205-lei-n-20-2020-de-31-de-dezembro-de-2020-lei-das-instituicoes-de-credito-e-sociedades-financeiras-e-revoga-as-leis-n-15-99-de-1-de-novembro-e-n-9-2004-de-21-de-julho](https://www.salcaldeira.com/index.php/pt/publicacoes/artigos/doc_download/1205-lei-n-20-2020-de-31-de-dezembro-de-2020-lei-das-instituicoes-de-credito-e-sociedades-financeiras-e-revoga-as-leis-n-15-99-de-1-de-novembro-e-n-9-2004-de-21-de-julho) > ilifikiwa tarehe 23 Julai 2021.

294 <http://www.oam.org.mz/wp-content/uploads/2017/07/Lei-das-Transac%C3%A7%C3%B5es-eletr%C3%B3nicas.pdf> > ilifikiwa tarehe 23 Julai 2021.

295 <https://www.vm.co.mz/M-Pesa2> > ilifikiwa tarehe 23 Julai 2021.

296 Programu ya Kupakuliwa kwa Vifaa vya iOS <https://apps.apple.com/pt/app/meu-m-pesa-mo%C3%A7ambique/id1442121355>; Pakua kwenye Google Play [https://play.google.com/store/apps/details?id=com.vodafone.mpesa.mozambique&hl=en\\_US&gl=US](https://play.google.com/store/apps/details?id=com.vodafone.mpesa.mozambique&hl=en_US&gl=US) > ilifikiwa tarehe 20 Julai 2021.

297 <https://www.vm.co.mz/> > ilifikiwa tarehe 23 Julai 2021.

miezi mitatu.

Ili kuomba mkopo, lazima mteja afikie menu ya M-Pesa kwa kubonyeza \*150# au atue chaguo la “Txuna M-Pesa” kwenye Programu kisha afuate hatua zilizopo. Mikopo inaweza kulipwa ndani ya siku 7 (na ada ya huduma ya 10%), siku 14 (na ada ya huduma ya 12%) na siku 30 (na ada ya huduma ya 15%). Huduma hii inatumika na benki mbili za Msumbiji, ABC<sup>298</sup> (African Banking Corporation) na MozaBanco.<sup>299</sup>

## Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali

	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
Txuna M-Pesa <sup>300</sup>	Ruhusa zinazotakikana	<p>Sheria na masharti (T&amp;C) yanaeleza kwamba mkataba unaeleza kanuni na wajibu uliopo kati ya Mteja, M-Pesa, MozaBanco na BancABC katika kipindi cha mkopo. Hakuna tarehe ya mara ya mwisho ya kusasishwa kwa sheria na masharti na benki hizi mbili.</p> <p>Kwa kukubali Sheria na Masharti (T&amp;C) haya, mteja anaidhinisha BancABC kufikia data ya nambari yake ya Vodacom na akaunti ya M-Pesa ili kubainisha kiwango cha ustahiki.</p>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	<p>Huduma ya Txuna M-Pesa inaahidi kukusanya maelezo muhimu ya binafsi yaliyoidhinishwa na yanayodhibitiwa. Inaweza kukusanya maelezo ya binafsi ya mteja wakati: Unanunua au kupata bidhaa au huduma kutoka M-Pesa (ikijumuisha kununua bidhaa mtandaoni, kwa kutumia simu au kwenye duka la Vodacom au duka jingine). Unajisajili kupata bidhaa au huduma (ikijumuisha wakati ambapo mteja anasajili jina lake na maelezo ya anwani au kufungua akaunti ya barua pepe na Vodacom). Unajisajili kwenye huduma ya kupokea taarifa, arifa au huduma zingine kutoka Vodacom.</p> <p>Unaomba kupata maelezo zaidi kuhusu bidhaa au huduma yoyote, au kuwasiliana na Vodacom ukiwa na maswali au malalamiko yoyote.</p> <p>Unashiriki katika shindano, mchezo wa bahati nasibu au utafiti wowote.</p> <p>Unatumia bidhaa na huduma za M-Pesa.</p> <p>Baada ya kupokea ruhusa au idhini yako na kama inavyoruhusiwa na sheria, tunaweza pia kukusanya maelezo yako kutoka kwa mashirika mengine au wahusika wengine ikiwa inafaa na inaruhusiwa na sheria. Hii inajumuisha kuzuia ulaghai, mashirika ya kuzuia ulaghai, saraka za biashara, mashirika ya nekodi za mikopo na kampuni zingine.</p>

298 <https://www.bancabc.co.mz/en/index.html/> > ilifikiwa tarehe 23 Julai 2021.

299 <https://www.mozabanco.co.mz/> > ilifikiwa tarehe 23 Julai 2021.

300 Sera ya Faragha – <https://www.vm.co.mz/M-Pesa2/Termos-e-Condicoes/Politica-de-Privacidade> > ilifikiwa tarehe 4 Agosti 2021. Ilifurahisha kutambua kwamba kwenye tovuti, huduma ya M-Pesa ina anwani ya barua pepe ya kutuma Maoni na Malalamiko: M-PESA. Privacy@vm.co.mz.

	<p>Ufikiaji na unekebishaji wa maelezo ya binafsi</p>	<p>Chini ya masharti yaliyobainishwa na sheria, mteja ana haki ya kufikia, kusahihisha, kurekebisha na kufuta maelezo yake ya binafsi au kukataa yasichakatwe.</p> <p>Baada ya kupokea ombi kwa maandishi, na maelezo ya kutosha ili kuwezesha huduma ya M-Pesa kutambua maelezo ya binafsi, watafichua maelezo yote ya watumiaji yaliyohifadhiwa na M-Pesa. Wanaweza kutoza mteja, kama inavyoruhusiwa na sheria.</p>
	<p>Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji</p>	<p>Maelezo yanayokusanywa na kampuni kuhusu watumiaji yanategemea bidhaa na huduma za M-Pesa ambazo mteja anatumia na kujisajili kwazo. Hii ni pamoja na (wala si tu) zifuatazo:</p> <p>Jina la mteja, tarehe ya kuzaliwa, aina ya kitambulisho na nambari, mahali pa kuzaliwa na utaifa, ulezi, hali ya ndoa na mfumo wa ndoa, anwani, maelezo ya akaunti ya mteja na anwani ya barua pepe na aina ya mapato.</p> <p>Mapendeleo ya mteja ya bidhaa, huduma au shughuli fulani, yaliyonipotiwa na mteja – au wakati ambapo huduma ya Vodacom inayakisia, kulingana na jinsi mtumiaji anatumia bidhaa na huduma zetu.</p> <p>Mawasiliano ya mteja na huduma ya M-Pesa – kama vile madokezo au rekodi zozote za simu ambazo mteja apige kwenye mojawapo ya vituo vya mawasiliano vya Vodacom, barua pepe au barua iliyotumwa kwa Vodacom, au rekodi zingine zozote za mawasiliano ambayo mteja amefanya na huduma ya Vodacom.</p> <p>Maelezo ya akaunti ya mteja yanajumuisha nambari za simu za mtumiaji, tarehe za shughuli za kutuma pesa na malipo yaliyofanywa au kupokewa, au maelezo mengine yoyote husika.</p> <p>Ununuzi</p> <p>Maelezo ya fedha</p> <p>Maelezo ya mawasiliano</p> <p>Anwani za mawasiliano</p> <p>Nenosini</p> <p>Vitambulisho</p> <p>Data ya matumizi</p> <p>Utambuzi wa hitilafu</p>

	Maelezo yanayokusanywa kutokana na kutumia tovuti ya M-Pesa	Vidakuzi nya mhusika wa kwanza vinatoka kwenye kikoa sawa na tovuti unayotembelea kwa sasa (katika hali hii, vodafone.com).  Vidakuzi nya mhusika mwengine vinatoka kwenye kikoa tofauti na tovuti inayotembelewa. Kwa mfano, wateja wanapotembelea tovuti ya M-Pesa, wanawenza kuunganisha kwenye tovuti ya kampuni nyingine – kama vile akaunti zao za Facebook au Twitter au video kwenye ukurasa wao wa YouTube.  Kwa hivyo, mteja anapoweza alama ya 'Kupenda' au 'Kuandika ujumbe wa Twitter' kuhusu kipengee kutoka kwenye tovuti ya M-Pesa, tovuti hizi wakati mwengine zinaweza kuweka vidakuzi kwenye kompyuta ya mtumiaji. M-Pesa inaeleza kuwa haidhibiti vidakuzi vyake, kwa hivyo inapendekeza kuwa watumiaji waangalie tovuti yao ili kuona jinsi wanavyovitumia na jinsi ya kuvidhibiti.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Washirika wa Vodafone Group wenyewe jina tofauti la kikoa wanawenza pia kuweka vidakuzi kwenye tovuti zao ili kuonyesha watumiaji matangazo au kurasa za kampuni zingine za Vodafone Group ambazo zinaweza kuwavutia. Maelezo kuhusu washirika hawa – na jinsi ya kujiondoa – yamejumuishwa kwenye tovuti.
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Maelezo ya fedha Kitambulisho – hati za binafsi (pasipoti au kitambulisho cha nchini) Anwani za mawasiliano

	Maelezo ya fedha Kitambulisho (Benki huwalazimu wateja kutoa nakala ya hati zao)
Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	<p>Maelezo yanaweza kushirikiwa na: Kampuni za kikundi cha Vodacom (Vodafone Group Plc na kampuni nyingine ambapo kampuni ya Vodafone Group Plc inamiliiki zaidi ya 15% ya hisa) Washirika au maajenti wanaohusika katika kutoa huduma ulizoomba au unazotumia</p> <p>Washirika au maajenti ambao hufanya tafiti za kutathmini hali ya kuridhishwa kwa wateja na bidhaa na huduma unazopokea</p> <p>Kampuni zinazohusika katika utoaji wa huduma kwa niaba ya kampuni ya Vodacom (Pty) Ltd, ikijumuisha Vodafone Limited au kampuni nyingine za Vodafone Group Panapowezekana, mashirika ya rekodi za mikopo, uzuiaji wa ulaghai, mashirika ya utathmini wa biashara au mashirika mengine ya utathmini wa mikopo.</p> <p>Kampuni za ukusanyaji wa madeni au kampuni zingine za urejeshaji wa pesa</p> <p>Ikiwa inahitajika au inaruhusiwa na sheria, mamlaka za utekelezaji wa sheria, wasimamizi, mahakama, au mamlaka zingine za umma.</p> <p>Huduma za dharura (ikiwa mteja atapiga simu ya dharura) Kampuni hufichua maelezo ndani ya vikomo vinavyofaa kwa ulinzi dhidi ya ulaghai, kulinda haki au mali ya M-Pesa au kulinda maslahi ya wateja wetu.</p> <p>Ikiwa huduma ya Vodafone M-Pesa itabadilishwa au kununuliwa na kampuni au kikundi kingine, tunaweza kuhamishia maelezo yako yoyote binafsi tuliyohifadhi kwa kampuni au kikundi hicho.</p>
Muda wa wahusika wengine kufikia data	Si wazi jinsi data hii inavyotumiwa na muda wa kutumiwa ikiwa mkataba utakomeshwa kati ya Benki, M-Pesa Txuna na mteja.
Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuzi vya tovuti	M-Pesa Txuna inaeleza kwamba vidakuzi vyake havihifadhi maelezo ya binafsi kama vile jina. M-Pesa huruhusu watumiaji kupata maelezo baada ya kuingia katika akaunti au kusaidia kuunganisha maelezo yao ya kuvunjani kwenye data yao wateja wanapoamua kujisajili kwenye huduma, kupokea ripoti ya usimamizi au taarifa.
Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Maelezo ya fedha Maelezo ya mawasiliano

Mikopo inaweza kuanzia Metacais 70 (MT) hadi MT 3,500 (karibu Dola 1 hadi Dola 60). Kiasi hiki kinaweza kubadilika kulingana na kiwango cha ustahiki wa mteja na rekodi za historia yake. Sheria na masharti ya Bank ABC yameandikwa<sup>301</sup> katika muundo usio wa kitaalamu.

<sup>301</sup> <http://www.vm.co.mz/content/download/106232/706643/version/1/file/Termos+e+Condicoes+Txuna+M-Pesa+BancABC.pdf> > ilifikiwa tarehe 23 Julai 2021.

Haionekani kama hati ya mkataba kati ya wahusika wawili. Hati inaeleza maana ya neno data ya mteja, ambayo ni maelezo yanayotolewa na M-Pesa kwa Benki na NANO (Global Holdings Limited) ili kuwezesha kuweka nekodi ya Mteja na utoaji wa huduma hii.

Hati hiyo pia inaeleza kwamba NANO ni kampuni ya teknolojia ambayo inatoa mfumo wa kiufundi wa kubainisha ustahiki wa Mteja kutumia huduma. Inasemekana kuwa ikiwa sheria na masharti yamekubaliwa, mteja: a) anathibitisha kuwa maelezo yote (ikijumuisha hati zozote) anayotoa kwa kampuni ya Vodafone M-Pesa SA ni sahihi, kamili na si ya kupotosha; na b) anaidhinisha kampuni ya Vodafone M-Pesa SA kufichua, kuthibitisha na kushiriki maelezo yoyote ya utambulisho na shughuli za kifedha na taasisi ya fedha inayowajibika kwa utoaji wa huduma ya mikopo na wahusika wengine wanaotoa huduma za kiufundi na mamlaka za usimamizi.

Tunatambua kwamba kati ya benki hizi mbili, ABC na MozaBanco, kuna tofauti fulani kuhusu jinsi sheria na masharti haya yamefanuliwa. Kwa mfano, MozaBanco<sup>302</sup> hutumia mfumo tofauti wa udhibiti wa data, FICO, kampuni mshirika/mhusika anayeshughulikia huduma za mikopo/fedha, uchanganuzi, vigezo na huduma husika. Hata hivyo, mfumo wa uidhinishaji wa data ya binafsi/maelezo unafanana kati ya benki hizi mbili.

Tulitambua pia kwamba sehemu ya Maswali Yanayoulizwa Sana – hati ya Maswali na Majibu<sup>303</sup> inayopatikana kwenye tovuti haikubainisha mara ya mwisho iliposasishwa. Hati hiyo pia haitaji chochote kuhusu ulinzi wa data au matumizi ya maelezo. Maswali yanayoulizwa kimsingi husaidia programu ya simu ya mkononi ya kukopesha pesa kuboresha huduma yake na wala si wateja hasa. Hata hivyo, mojawapo ya vipengele vizuri ambavyo tuliweza kupata ni kwamba M-Pesa huchapisha<sup>304</sup> ripoti zake za fedha za kila mwaka, na ripoti ya mwisho ilichapishwa mnamo Desemba 2020.

Tanehe 7 Machi 2019, tulitambua kwamba kampuni ya Vodafone M-Pesa, S.A. ilipigwa faini<sup>305</sup> ya shilingi MT milioni 10 (karibu Dola 157,240) na Benki Kuu ya Msumbiji (Central Bank of Mozambique), baada ya ukiukaji wa sheria zauzuiaji wa ulanguzi wa pesa – kifungu cha 77 cha Sheria ya 14/2013. Kosa hilo lilitokana na hitilafu ya mfumo ambayo imetatuliwa kwa sasa. Hitilafu hiyo mfumo<sup>306</sup> iliyotokea haijulikani. Bado, inaeleweka kwamba lilikuwa tukio la ufhuzi haramu wa data ambalo lilifichua data ya watumiaji kwa wahusika wengine amba wanaweza kufikia data ya binafsi na kutekeleza kitendo cha ulaghai wa kifedha kuitia programu hiyo.

## **Uchunguzi Kifani: Watumiaji Wawili wa M-Pesa**

Gilberto Manhiça<sup>307</sup> amekuwa akitumia huduma ya M-Pesa tangu mwaka wa 2017. Kwanza, alipeana data yake (utambulisho/kitambulisho cha binafsi) kwa kampuni ya huduma za simu alipofungua akaunti yake na kusasisha maelezo yake ya binafsi ili kuongeza kiasi cha pesa kinachoruhusiwa kwenye akaunti. Kuhusu faragha ya data, anasema kwamba huduma ya Txuna ilikuwa salama mwaka wa 2020 wakati M-Pesa ilipobadilisha kanuni ili kuficha jina la mteja wakati wa mchakato wa kutuma maelezo. Kama mteja wa huduma ya Txuna, hana ufahamu kamili kuhusu usalama wa data yake. Bado, hata kama angekuwa anafahamu kuhusu data yake, hana shaka kuwa iwapo mamlaka za utekelezaji wa sheria (polisi) zinataka maelezo yake, zitayatapa kila wakati kwenye kampuni ya huduma za simu. Gilberto

302 <http://www.vm.co.mz/content/download/106233/706647/version/1/file/Termos+e+Condicoes+Txuna+M-Pesa+Moza+Banco.pdf> > ilifikiwa tarehe 25 Julai 2021.

303 <http://www.vm.co.mz/content/download/106095/705913/version/1/file/Perguntas+Frequentes+Txuna+M-Pesa.pdf> > ilifikiwa tarehe 24 Julai 2021.

304 <https://www.vm.co.mz/M-Pesa2/Relatorios-Financeiros> > ilifikiwa tarehe 24 Julai 2021.

305 Ripoti [http://www.vm.co.mz/content/download/103501/690546/version/1/file/M-Pesa++Relat%C3%B3rio+Disciplina+de+Mercado\\_d-Junho\\_2019.pdf](http://www.vm.co.mz/content/download/103501/690546/version/1/file/M-Pesa++Relat%C3%B3rio+Disciplina+de+Mercado_d-Junho_2019.pdf) > ilifikiwa tarehe 24 Julai 2021.

306 [http://www.vm.co.mz/content/download/103501/690546/version/1/file/M-Pesa++Relat%C3%B3rio+Disciplina+de+Mercado\\_d-Junho\\_2019.pdf](http://www.vm.co.mz/content/download/103501/690546/version/1/file/M-Pesa++Relat%C3%B3rio+Disciplina+de+Mercado_d-Junho_2019.pdf) > ilifikiwa tarehe 24 Julai 2021.

307 Mahojiano ya Tarehe 22 Julai 2021, Maputo (Msumbiji, kuptitia Zoom).

hajawahi kusoma sheria na mashanti lakini anakumbuka mkataba wake na ABC Bank ambao unaruhusu kampuni ya Vodacom na Txuna M-Pesa kushiriki data yake na Benki. Ana wasiwasi fulani kuhusu usalama, lakini alisema kuwa “anaamini benki, kuliko kampuni ya Vodacom.”

Tulizungumza pia na Justino Mabuiango<sup>308</sup>, aliyeanza kutumia huduma ya M-Pesa mwaka wa 2016. Kwake, programu ya M-Pesa ni salama kwa sababu “data yake haionekani na kila mtu”. Kama Gilberto, alisema kwamba mabadiliko makubwa yalifanyika mwaka wa 2020 wakati ambapo M-Pesa ilianza kutumia mfumo ambao, katika hali ya kutuma maelezo, programu huonyesha tu herufi za kwanza za jina la mteja. Mteja huyo alisema kwamba hatumii huduma ya Txuna mara kwa mara kwa sababu “si vyema kuwa na madeni.” Kila kitu anachojua kuhusu data ya binafsi kilitokana na uzoefu wake mwenyewe kama mtumiaji na alisema kwamba huwa hasomi hati yoyote ili kujisajili kwenye huduma kwa sababu kuna hakikisho la usalama.

## **Hitimisho**

Programu ya M-Pesa Txuna inafuchua kwamba ingawa huduma hiyo imekuwa nchini Msumbiji kwa zaidi ya miaka mitano, kiwango chake cha kutumika kwenye benki zingine bado kiko chini tunapozingatia kwamba Msumbiji ina zaidi ya benki kumi za biashara. Inatumika tu na benki mbili na hali hii inaweza kuzua baadhi ya maswali ambayo yanahitaji uchanganuzi zaidi. Kando na hayo, licha ya kufanya sheria na masharti ya matumizi yapatikane kwenye mfumo, ukosefu wa kusasishwa kwa hati hizi linabaki kuwa swali lisilo na jibu. Sera ya faragha haijachapishwa hadharani kwa wateja, hali inayomaanisha kuwa kuna hali za kutojumuishwa kwa vipengele fulani, kama ilivyotambulika katika mahojiano yote ambapo mtumiaji alitaja suala la kutumia huduma bila kuwahi kusoma hati yoyote kabla. Kwa kuhitimisha, kuna hali ya kutojumuishwa kwa vipengele fulani kuhusu jinsi M-Pesa hufanya kazi na Benki Kuu (Central Bank) ili kuomba data ya binafsi ya mteja.

# Namibia



## Maelezo ya Nchi

Ikiwa inapatikana katika eneo la pwani ya kusini magharibi mwa Afrika, Namibia inapakana na taifa la Angola upande wa kaskazini na Afrika Kusini upande wa kusini. Baada ya kuwa chini ya ukoloni wa Ujerumani na Afrika kusini kwa miaka 106, Namibia ilipata uhuru mnamo tarehe 21 Machi 1990, chini ya katiba ya kidemokrasia ya vyama vingi.<sup>309</sup> Jiji lake kuu ni Windhoek. Ina idadi inayokadiriwa ya karibu watu milioni 2<sup>310</sup> na GDP inayokadiriwa ya bilioni 10.56 kufikia mwaka wa 2020.<sup>311</sup>

309 <https://www.britannica.com/place/Namibia> > ilifikiwa tarehe 6 Septemba 2021.

310 <https://www.worldometers.info/world-population/namibia-population/> > ilifikiwa tarehe 5 Septemba 2021.

311 <https://www.statista.com/statistics/510122/gross-domestic-product-gdp-in-namibia/> > ilifikiwa tarehe 5 Septemba 2021.

## Ulinzi wa Data Nchini Namibia

Namibia haijatunga sheria ya ulinzi wa faragha ya data.<sup>312</sup> Nchi hii inatambua suala la faragha kama haki ya msingi ya binadamu chini ya Kifungu cha 13 cha Katiba ya Namibia.<sup>313</sup> Inaeleza kwamba hakuna mtu yeyote ambaye faragha yake ya nyumbani, maoni na mawasiliano inapaswa kuingiliwa. Sheria hii inaruhusu kuingiliwa kwa faragha ya mtu chini ya sheria, kwa maslahi ya usalama wa kitaifa, usalama wa umma au ustawi wa uchumi wa nchi, kwa ulinzi wa afya au maadili, kwa uzuiaji wa shughuli za ukiukaji wa sheria au uhalifu, au ulinzi wa haki au uhuru wa watu wengine.

Namibia imeidhinisha Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Umma na za Kisiasa (International Covenant on Civil and Political Rights ('ICCPR')).<sup>314</sup> Hatua hii inaimarisha Kifungu cha 12 cha sheria ya UDHR, ambacho kinaeleza kwamba "hakuna mtu yeyote ambaye faragha yake ya binafsi, ya nyumbani au ya mawasiliano inapaswa kuingiliwa kiholela au kinyume cha sheria, wala kushambuliwa kwa heshima na sifa yake kinyume cha sheria".

## Mfumo wa Fedha na Teknolojia ya Fedha Nchini Namibia

Utaratibu wa kisheria wa Mfumo Kitaifa wa Malipo (National Payment System) ulitolewa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mfumo wa Malipo (Payment System Management Act), ya 2003 (Sheria Nambari 18 ya 2003)<sup>315</sup> na kanuni zinazotolewa chini ya Sheria ya Usimamizi

312 <https://www.dlapiperdataprotection.com/index.html?t=law&c=NA> > ilifikiwa tarehe 6 Septemba 2021.

313 [http://www.kas.de/upload/auslandshomepages/namibia/constitution/const\\_en\\_contents.pdf](http://www.kas.de/upload/auslandshomepages/namibia/constitution/const_en_contents.pdf) > ilifikiwa tarehe 5 Septemba 2021.

314 <https://www.ohchr.org/en/professionalinterest/pages/ccpr.aspx> > ilifikiwa tarehe 5 Septemba 2021.

315 <https://www.bon.com.na/Bank/Payments-and-Settlements/Legal-Framework/Payment-System-Management-Act.aspx> > ilifikiwa tarehe 3 Septemba 2021.

wa Mfumo wa Malipo (Payment System Management Act), kama ilivyonekebishwa.<sup>316</sup> Benki ya Namibia (Bank of Namibia) ina Watoa Huduma za Fedha za Kielektroniki Walioihinishwa watano: Magnet Payment Solutions; Nam-mic Payment Solutions; NamPost; Virtual Technology Services na Vivo Energy Namibia.<sup>317</sup>

Mnamo Februari 2021, iliripotiwa<sup>318</sup> kwamba mwaka wa 2020 pekee, zaidi ya Dola za Namibia bilioni 40 (N\$40)<sup>319</sup> zilisambazwa kupitia mifumo ya fedha za kielektroniki kama vile eWallet, easyWallet na Blue Wallet na huduma zingine kama hizo za fedha. Mwaka mmoja kabla ya mwaka wa 2019, thamani hii ilikuwa N\$ bilioni 14,8<sup>320</sup>, ambayo imeongezeka kwa 177%, zaidi ya kiwango cha ukuaji katika thamani kilichosukumwa na shughuli za matumizi ya kadi za benki na huduma za fedha za kielektroniki.

Mwezi wa Aprili uliopita, Bank of Namibia (BON) iliitaka sekta ya benki kuzingatia teknolojia ya fedha ili kuboresha ufikiaji na huduma fedha.<sup>321</sup> Katika ripoti yake ya kila mwaka,<sup>322</sup> benki kuu ilisema kuwa kadri huduma za kufikia bidhaa na huduma za benki zinavyoongezeka, ndivyo wateja wengi watakavyofikiwa. Inaripotiwa kuwa bado Namibia ina watu na biashara nyingi ambazo hazina akaunti za benki na zinapendelea kufanya shughuli za kifedha za pesa taslimu.

Shughuli za kutuma na kupokea pesa kupitia simu za mkononi pia zimeongezeka kwa ghafla, kutoka chini ya shughuli milioni 10 mwaka wa 2015 hadi zaidi ya shughuli milioni 65 mwaka wa 2020.<sup>323</sup> BON ilizindua pia mpango wa Mkakati na Maono ya Mfumo wa Kitaifa wa Malipo wa Namibia (Namibia National Payment System Vision and Strategy) wa 2021-2025, ambao unajumuisha mipango ya kunahisisha shughuli ya kufanya malipo kwenye mifumo tofauti.<sup>324</sup> Kando na hayo, Bank of Namibia (BON) iko mbioni kukamilisha utafiti wake<sup>325</sup> kuhusu sarafu dijitali kufikia mwezi wa Aprili 2022, gavana wa benki kuu, Johannes Gaxab, alisema hivi karibuni.<sup>326</sup> Hata hivyo, gavana huyo alisisitiza kuwa sarafu dijitali si biashara halali kwa sababu hakuna kifungu chochote kwa sasa kuhusu matumizi ya sarafu dijitali katika sheria za nchi.

## **PayToday: Programu ya Simu za Mkononi ya Kukopesha Pesa**

PayToday<sup>327</sup> ni programu ya huduma ya kutuma na kupokea pesa kupitia simu ya Namibia ambayo inatoa huduma za malipo na mikopo kupitia akaunti za benki kwa watu na biashara. Wateja lazima wapakue Programu ya PayToday kwenye Apple App Store au Google Play Store na wakamilishe mchakato wa kujisajili ili kutumia programu. Wateja lazima watoa maelezo ya kadi na akaunti yao ya benki kama sehemu ya mchakato wa kujisajili. Maelezo ya kadi zao hutumika kufanya malipo.

Kwanza, programu ilizinduliwa kama StayToday, na Chris (Mhasibu Aliyehinshwa) na Naude (Mhandisi wa Masuala ya Elektroniki/Kielektroniki) mwaka wa 2013.<sup>328</sup> Mwaka wa 2017

316 <https://www.bon.com.na/Bank/Payments-and-Settlements/Legal-Framework/Payment-System-Management-Amended-Act.aspx> > ilifikiwa tarehe 3 Septemba 2021.

317 Mashirika ya Huduma za Fedha za Kielektroniki <https://www.bon.com.na/Bank/Payments-and-Settlements/E-Money-Institutions.aspx> > ilifikiwa tarehe 6 Septemba 2021.

318 Ripoti ya habari <https://allafrica.com/stories/202102240567.html> > ilifikiwa tarehe 3 Septemba 2021.

319 Karibu Dola 2 800 581 200

320 Karibu Dola 1 050 217 950

321 Ripoti ya habari <https://afcacia.com/2021/04/17/namibian-banks-urged-to-embrace-fintech/> > ilifikiwa tarehe 3 Septemba 2021.

322 <https://www.bon.com.na/getattachment/7923760d-1805-4265-906a-b424abafdef8/.aspx> > ilifikiwa tarehe 3 Septemba 2021.

323 Idem.

324 <https://www.bon.com.na/getattachment/2183fe04-8b8f-44d0-add9-4629d7ec86a5/19-02-2021-Namibia-National-Payment-System-Vision.aspx> > ilifikiwa tarehe 3 Septemba 2021.

325 Sheria za Namibia Kuhusu Sarafu Dijitali <https://freemanlaw.com/cryptocurrency-blockchain/namibia/> > ilifikiwa tarehe 6 Septemba 2021

326 Ripoti ya habari <https://news.bitcoin.com/namibia-central-bank-to-complete-crypto-study-by-april-2022-governor-says-current-laws-do-not-permit-use-of-digital-assets/> > ilifikiwa tarehe 4 Septemba 2021.

327 <https://site.paytoday.com.na> > ilifikiwa tarehe 4 Septemba 2021.

328 <https://www.offerzen.com/companies/paytoday> > ilifikiwa tarehe 4 Septemba 2021.

ilizinduliwa nchini Namibia. Huduma hii inawezeshwa kuitia kwa ushinkiano na Nedbank Namibia. Kadi nyingi za mikopo au benki kutoka kwenye Benki yoyote ya Namibia zinaweza kutumika kulipia mafuta kwenye programu ya PayToday.<sup>329</sup>

## Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali

PayToday <sup>330</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu
	Programu inaruhusu aina tatu tofauti za mipangilio ya Faragha na ruhusa <sup>331</sup> : Washiriki pekee (Mipangilio thabiti ya faragha): Watu ambao watumiaji wanawaomba pesa au kuwatumia pesa ndio tu watafahamu shughuli hiyo kifedha. Marafiki pekee (Mipangilio ya wastani ya faragha): Shughuli za kifedha zitashirikiwa tu marafiki wa watumiaji. Anwani zote za mawasiliano za mteja zilizo kwenye kifaa chake zinaeleza marafiki wa mtumiaji. Kila mtu (Mipangilio isiyothabiti ya faragha): Shughuli za kifedha (baina ya watu na ununuzi) zitashirikiwa kwenye Mipasho ya Namibia na Marafiki na kuonekana na kila mtu.
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji Jina; Nambari ya simu; Anwani ya barua pepe; Nambari ya kadi ya Mikopo/Benki na tarehe ya mwisho wa matumizi; Maelezo ya Benki; Nambari za kitambulisho; Majina ya kuingia katika akaunti; Manenosiri; Maelezo ya kifaa;
	Ufikiaji na urekebishaji wa maelezo ya binafsi Kusoma maudhui ya nafasi ya hifadhi ya USB ya mteja Kubadilisha au kufuta maudhui ya nafasi ya hifadhi ya USB ya mteja Maelezo yote ya binafsi ya mteja ambayo Programu hukusanya na kuhifadhi yanaweza kufikiwa na kubadilishwa na watumiaji wakati wowote.

329 <https://www.namibian.com.na/169678/archive-read/PayToday-introduces-mobile-fuel-payments> > ilifikiwa tarehe 4 Septemba 2021.

330 Maswali Yanayoulizwa Sana <https://site.paytoday.com.na/need-help/#FAQs> > ilifikiwa tarehe 4 Septemba 2021.  
331 <https://www.today.com.com.na/paytoday-privacy-policy> > ilifikiwa tarehe 3 Septemba 2021.

	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Data ya mahali (baada tu ya mteja kutoa idhini yake moja kwa moja); Maelezo ya anwani za mawasiliano za mteja zilizo kwenye simu (baada tu ya mteja kutoa idhini yake moja kwa moja) Programu ya PayToday hulinganisha data ya anwani za mawasiliano kwenye hifadhidata ya mteja aliyesajiliwa ili kufanya shughuli za kifedha na watumiaji wengine waliosajiliwa. Data yake ya mawasiliano huhifadhiwa kwenye Programu katika hifadhidata ya ndani kwa ajili ya kuakibishwa lakini si kwenye seva ya programu. Maelezo yote yanayohusiana na kila shughuli ya kifedha (maudhui ya ujumbe, saa, tarehe, mpokeaji na kiasi cha kila shughuli ya kifedha); Maelezo Yasiyo ya Binafsi Yanayoweza Kutambulika (Non-Personal Identifiable Information ("NPPI") – maelezo haya yanaweza kuhusiana na mtu au akaunti fulani lakini, yakiwa peke yake, hayatoshi kutambulisha, kuwasiliana au kutambua mahali mtu mahususi alipo.
	Maelezo yanayokusanywa kutokana na kutumia tovuti ya PayToday's	Mtumiaji anapoingia katika akaunti ya Programu ya PayToday au kufikia tovuti ya Today, zinaweza kutuma faili ndoto za data zinazojulikana kama "vidakuzi" kwenye kompyuta au kifaa cha kutumia kuingia katika akaunti. Tovuti za Today hutumia "vidakuzi" hivi kubonesha hali ya utumiaji, na watumiaji wana chaguo la kukataa matumizi ya "vidakuzi" hivi.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Hakuna maelezo yoyote
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	PayToday au mashirika husika au mali zake husika zinaweza kununuliwa na biashara nyingine au kuungana na biashara nyingine. Ikiwa tukio la kununuliwa au kuungana na biashara nyingine litatokea, mteja anapaswa kutarajia programu ya PayToday kushiriki baadhi au maelezo yote ya mtumiaji yanayoweza kumtambulisha mtu.
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Kama sehemu ya kutuma na kupokea pesa kutoka kwa watumiaji wengine wa programu ya PayToday, maelezo ya binafsi yafuatayo yatashirikiwa na watumiaji wengine ambao wateja wanafanya nao shughuli za kifedha: maelezo ya shughuli ya kifedha (kiasi cha pesa, saa, tarehe, washiriki wengine, picha ya wasifu ya mteja na jina la mtumiaji).

## Hitimisho

Inaonekana kuwa programu inatoa maelezo yanayohitajika kwa watumiaji kwenye tovuti yake. Hata hivyo, ukosefu wa sheria ya ulinzi wa data hauruhusu uchanganuzi thabiti ambao unahakikisha ulinzi wa data ya binafsi. Kwa mfano, katika sheria na masharti ya sera ya faragha, hakuna maelezo yoyote yaliyotolewa kuhusu jinsi mamlaka za usimamizi hushughulikia hali ambapo wamiliki wa programu wanakiuka haki za faragha za wateja wao. Tunatambua pia kwamba haitoi maelezo kuhusu uhusiano kati ya Programu na washirika wake (benki za biashara) katika kushiriki maelezo na wahusika wengine. Maelezo yaliyotolewa si dhahiri na yanaangazia tu Programu yenyewe wala si kuhusu wahusika wengine.

# Naijeria

## Maelezo ya Nchi

Ikiwa inapatikana katika eneo la Afrika Magharibi,<sup>332</sup> Naijeria, inayojulikana pia Shirikisho la Jamhuri ya Naijeria, inapakana na mataifa ya Nijeri (Niger), Chad, Kameruni na Ghuba ya Gine (Gulf of Guinea).<sup>333</sup> Ina ukubwa wa 923,768 km<sup>2</sup><sup>334</sup> na tabianchi ya ukame na unyevu wa kiikweta.<sup>335</sup> Ina makabila mbalimbali ya karibu 250, na lugha za Kihausa, Kiigbo na Kiyoruba zikiwa lugha maarufu zaidi.<sup>336</sup> Naijeria ni nchi iliyo na idadi kubwa zaidi ya watu barani Afrika, ikiwa na zaidi ya watu milioni 211.<sup>337</sup> Jiji lake kuu ni Abuja ingawa Lagos linabaki kuwa jiji kubwa zaidi lenye shughuli za kiuchumi.<sup>338</sup>

332 Naijeria <https://www.nationsonline.org/oneworld/nigeria.htm>

333 Naijeria <https://www.britannica.com/place/Nigeria>

334 (n1)

335 (n2)

336 Mambo 13 Uhayohitaji Kujua Kuhusu Naijeria [https://artsandculture.google.com/story/13-things-you-need-to-know-about-nigeria/\\_AQCgGgURLk8KA](https://artsandculture.google.com/story/13-things-you-need-to-know-about-nigeria/_AQCgGgURLk8KA)

337 Dashibodi ya Idadi ya Watu Duniani Naijeria <https://www.unfpa.org/data/world-population/NG>

338 (n1)

## Ulinzi wa Data Nchini Naijeria

Programu za mikopo dijitali nchini Naijeria zinatumika kwa wingi zaidi na watu na biashara ndogo na za wastani (SME) kwa sababu ya mchakato wake rahisi na haraka wa kutoa mikopo, kuliko benki ambapo shughuli ya kupata mkopo ni ngumu.<sup>339</sup> Matumizi ya programu hizi yameongezeka, hasa baada ya kutokea kwa janga la virusi vya korona, ambalo liliathiri zaidi uchumi wa dunia.<sup>340</sup> Tofauti na benki, programu hizi zinatoa njia rahisi ya kupata mikopo ndani ya kipindi kifupi cha muda bila kuhitaji dhamana. Hata hivyo, zinategemea sana data ya mtumiaji ili kutathmini hatari ya kutoa mkopo.

Mashirika yanayomiliki programu hizi lazima yasajiliwe na kupata leseni kutoka Benki Kuu ya Naijeria (Central Bank of Nigeria (CBN) chini ya Sheria ya Benki na Taasisi Nyingine za Fedha (Banks and Other Financial Institutions Act) ya 2020 (BOFIA)).<sup>341</sup> Sheria hii inaweka programu hizi chini ya usimamizi wa CBN na inaziweka katika aina ya "biashara za taasisi nyingine za fedha", ambazo zinajumuisha biashara za fedha zinazotekelizwa kidijitali, mtandaoni au kielektroniki.<sup>342</sup> Ni vyema kutambua kuwa mashirika haya (wakopeshaji) yanaweza pia kujisajili ndani ya sheria za majimbo ya Naijeria. Hata hivyo, chaguo hili linaweza

339 Uingiliaji wa Faragha wa Programu za Simu za Kukopesha Pesa nchini Naijeria <https://aanoip.org/the-intrusiveness-of-money-lending-apps-in-nigeria/>

340 Ibid

341 Kifungu cha 57 (1), Sheria ya Benki na Taasisi Nyingine za Fedha (Banks and Other Financial Institutions Act) ya 2020 (BOFIA) <https://www.cbn.gov.ng/Out/2021/CCD/BOFIA%202020.pdf>

342 Kifungu cha 57 (2)(j)(ix), Sheria ya Benki na Taasisi Nyingine za Fedha (Banks and Other Financial Institutions Act), 2020

kudhibiti shughuli za wakopeshaji. Udhibiti huu unatokana na sababu kwamba mkopeshaji ataruhusiwa tu kuendesha shughuli zake ndani ya jimbo alikosajiliwa. Watadhibitiwa pia kuhusiana na viwango vya riba wanavyoweza kutoza.<sup>343</sup>

Shughuli za uchakataji wa data za programu hizi zinasimamiwa na Sheria za Ulinzi wa Data za Naijeria (Nigeria Data Protection Regulations (NDPR), ambazo zinahitaji programu hizi kulinda haki ya faragha ya watumiaji.<sup>344</sup> Sheria hizi zinabainisha utaratibu ambao wadhibiti wa data wanapaswa kufuata ili kuhakikisha usalama wa wamiliki wa data (katika hali hii, wakopaji). Utafiti huu unalenga kuchunguza jinsi programu hizi zinavyotii kanuni za NDPR. Unaanza kwa kuchunguza data inayokusanywa na programu hizi na vile vile kuchanganua iwapo uchakataji huo unatii kanuni za NDPR.

## Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali

Carbon <sup>345</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	Huomba ruhusa ya kufikia: SMS Anwani za mawasiliano Programu zilizosakinishwa Historia ya kivinjari Kalenda Mahali- Maelezo ya mahali mahususi Programu hii pia inaweza kukusanya maelezo haya chinichini wakati ambapo mtumiaji haitumii.
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Maelezo ya mtumiaji yanayotakikana; jina, anwani, anwani ya barua pepe, nambari ya simu, maelezo ya kuingia katika mitando ya kijamii, maelezo ya fedha/ mikopo, maelezo ya binafsi, kazi ya sasa na ya zamani, elimu, majina ya wenzako, anwani za mawasiliano na marafiki, picha na onodha ya wanafamilia
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji/ Matumizi ya tovuti	Maelezo ya kiufundi: Anwani ya IP, maelezo ya kuingia katika akaunti, toleo na aina ya kivinjari, mipangilio ya saa za eneo, matoleo na aina za programu jalizi za kivinjari, mfumo wa uendeshaji na mfumo Shughuli ya mtumiaji ya kutembelea tovuti: Viungo vya URL unapovinjari tovuti; bidhaa zilizoangaliwa au kutafutwa; kasi za kufunguka kwa kurasa, hitilafu za upakuaji, kipindi cha muda wa kutembelea kurasa za tovuti, maelezo ya utumiaji wa ukurasa (upitiaji, mibofyo, misogezo ya kipanya); njia za kutumia kuvinjari; nambari ya simu iliyotumiwa kupiga simu kwa nambari ya huduma kwa wateja Data ya malipo
	Jinsi maelezo ya mtumiaji yanavyokusanywa	Anapojaza fomu kwenye tovuti (yaani., kujisajili na kuomba mkopo kwenye Programu) Anapotoa idhini ya kufikia mifumo ya mitando ya kijamii Kupitia mawasiliano yaani., barua pepe, simu nk

343 ICLG, Sheria ya Usimamzi wa Teknolojia ya Fedha ya Naijeria (Nigeria Fintech Law Regulation) ya 2021 <https://iclg.com/practice-areas/fintech-laws-and-regulations/nigeria>

344 Sheria ya Ulinzi wa Data ya Naijeria (Nigeria Data Protection Regulation) ya 2019 <https://ndpr.nitda.gov.ng/Content/Doc/NigeriaDataProtectionRegulation.pdf>

345 Sera ya programu ya Carbon <https://getcarbon.co.ke/privacy-policy.html>

	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Hupokea maelezo kutoka: Tovuti zingine zinazoendeshwa na Carbon, zinazotumiwa na mtumiaji Mitandao ya kijamii ambayo mtumiaji ameingia kupitia tovuti ya Carbon Wahusika wengine kama vile; wakandarasi wa biashara, wakandarasi wadogo, huduma za malipo na usafirishajii wa bidhaa, tovuti za mitandao ya kijamii, mitandao ya utangazaji, ofisi za usimamizi wa mikopo, watoa huduma za mikopo na wengineo
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Utekelezaji wa wajibu wa kimkataba kwa mtumiaji Kutoa za mikopo Kutoa maelezo kuhusu bdihaa na huduma za Carbon Matangazo Kutoa taarifa kuhusu mabadiliko ya huduma za Carbon Uchakataji zaidi wa maelezo kwa madhumuni ya kisayansi, kitakwimu au kiutafiti kulingana na maslahi ya umma,
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine/ Ufichuzi wa Maelezo	Hushiriki maelezo na wahusika wengine wafuatao: Mashirika yake tanzu, kampuni kuu Washirika wa kibashara, wauzaji wa bidhaa na wakandarasi wadogo Watangazaji na mitandao ya utangazaji Watoa huduma za takwimu na mitambo ya kutafutia Wahusika wengine, kutii wajibu wa kisheria au kutekeleza sheria na masharti yake ya matumizi. Hupokea maelezo ya mtumiaji kutoka: Kampuni washirika Watoa huduma za mtandao wa simu Kampuni za umeme Wajumlishaji wa data Ofisi za rekodi za mikopo Mifumo ya biashara za mtandaoni, na Taasisi nyingine za fedha  Haijabainishwa
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Teknolojia za ufuutiliaji/ vidakuzi vyatovuti	Watumiaji wanakubali kuwekwa kwa vidakuzi kwenye vivinjari vyao na barua pepe za HTML baada ya kutembelea tovuti
	Uhamishaji wa data kimataifa	Data inaweza kuhamishiwa/ kushirikiwa kati ya nchi ambazo Carbon inaendesha biashara yake
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Huhifadhi data kwenye seva zake kwa kutumia teknolojia ya JWT

	Ruhusa zinazotakikana	Huomba ruhusa ya kufikia: Orodha ya anwani za mawasiliano Rekodi za nambari za simu Rekodi za SMS Anwani za Facebook Orodha ya anwani za akaunti zingine za mitandao ya kijamii Picha, video au maudhui mengine dijitali Programu hupiga simu kwa anwani za orodha ya anwani za mawasiliano za mtumiaji, SMS au orodha ya simu ili kuthibitisha utambulisho wa mtumiaji
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Data ya binafsi: jina, umri, anwani ya barua pepe, nambari ya simu, maelezo ya anwani halisi, maelezo ya binafsi, picha, jina la mtumiaji, nenosiri, maelezo ya fedha/kadi ya mikopo, nambari za akaunti ya benki Data ya shughuli za kifedha: shughuli za mtumiaji kwenye Programu Mawasiliano: data iliyokusanywa kuititia mawasiliano na mtumiaji Maelezo ya ziada kwa madhumuni ya uthibitishaji
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Kitambulisho cha kifaa Aina ya kifaa Vitambulishi maalum vya kifaa; maelezo ya mahali, kompyuta, mfumo wa uendeshaji na maelezo ya muunganisho Anwani ya IP Maelezo ya kawaada ya faili za tovuti
	Jinsi maelezo ya mtumiaji yanavyokusanywa	Anapojaza fomu kwenye Programu Anapowasiliana na programu ya PalmCredit Anaposisajili kutumia Programu Anaposisajili kwenye huduma za PalmCredit Anaposhiriki data kuititia vipengele vya mitandao ya kijamii vya Programu Kuititia matangazo, mashindano au utafiti Anaporipoti matatizo yanayohusiana na Programu
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Data ya takwimu na utumiaji, Maelezo ya ukaguzi wa ustahiki wa kupokea mikopo, na Maelezo kutoka kwa ofisi ya usimamizi wa mikopo
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kutathmini kiasi cha juu cha mkopo Kutoa huduma ya kufikia Programu ya Carbon Kutatua migogoro Kuzuia ulaghai na utekelezaji wa sheria na masharti ya Programu Kufanya maudhui, matangazo na huduma zimfae mtumiaji Kutoa maelezo kuhusu huduma za Programu Kutoa matangazo mahususi Kuthibitishwa na wahusika wengine Kuwasiliana na mtumiaji

	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	-Programu hufichua maelezo ya mtumiaji kwa: Washirika wake wa kibashara wakati wa miungano na ununuzi wa biashara Washirika wake wa kibashara wakati wa kuuza au kununua biashara au mali zake Mashirika ya serikali na ya utekelezaji wa sheria Mashirika yake tanzu, kampuni kuu, nk Wahusika wengine wakati wa utekelezaji wa sheria na masharti yake au kuchapisha takwimu za matumizi ya Programu Ofisi za rekodi za mikopo Wahusika wengine wakati wa kutii maagizo ya kisheria au kiusimamizi au utekelezaji wa sera zake Haijabainishwa
	Teknolojia za ufuutiliaji/ vidakuzi vya tovuti	Programu ina: Vidakuzi vya kipindi ambavyo hufutwa kwenye kifaa cha mtumiaji baada ya mtumiaji kukamilisha kipindi cha matumizi ya Programu Vidakuzi vya wahusika wengine ambavyo vinatoka kwa watoa huduma wake Vidakuzi vya wahusika wengine (ambao si watoa huduma za Programu) ambavyo mtumiaji hukumbana navyo anapotembelea ukurasa tofauti wa wavuti kwenye Programu
	Uhamishaji wa data kmataifa/ Uhamishaji wa data nje ya nchi	Wakati ambapo data ya mtumiaji inapaswa kuhamishiwa kwenye nchi ambayo haipo kwenye Orodha ya Zinazoruhusiwa, Programu itahamisha tu data chini ya hali zifuatazo: Mtumiaji anapotoa idhini yake Wakati ambapo uhamishaji unahitajika kwa utekelezaji wa mkataba kati ya mtumiaji na Programu Wakati ambapo uhamishaji unahitajika ili kukamilishwa kwa mkataba kati ya Programu na mhusika mwengine kwa maslahi ya mtumiaji Wakati ambapo uhamishaji unahitajika kwa maslahi ya umma Wakati ambapo uhamishaji unahitajika kwa ajili ya kuanzisha au kutetea madai ya kisheria
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Data ya mtumiaji inaweza kuhifadhiwa au kuhamishwa nje ya nchi ya Naijeria. Inaweza pia kushughulikiwa na wafanyakazi wa nje ya nchi ya Naijeria
Branch	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	

	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Jina, tarehe ya kuzaliwa, nambari ya simu, anwani ya barua pepe, utaifa, nambari ya kitambulisho cha kodi, maelezo ya benki, nambari ya uthibitishaji wa benki, nambari ya kitambulisho, mahali, picha, anwani ya IP, anwani ya MAC, nambari ya IMEI, nambari ya IMSI. <sup>347</sup>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	
	Jinsi Programu ya Branch hukusanya maelezo	Kupitia fomu za ndani ya programu wakati wa kuomba mkopo Kupitia kifaa cha mtumiaji Kupitia mawasiliano na mtumiaji yaani.,barua pepe
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	
	Matumizi ya maelezo ya mtumiaji	Kutathmini hatari ya utoaji wa mkopo Kufanya uchunguzi wa historia ya mtumiaji Kutii Sheria Kwa madhumuni ya matangazo
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine  Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Teknolojia za ufuutiliaji/ vidakuzi vya tovuti	
	Uhamishaji wa data kimataifa	
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	
QuickCheck <sup>348</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	

347 Sera ya Ulinzi wa Data ya Programu ya Branch, ukurasa wa 5 <https://branch.co/documents/BranchDataProtectionPolicy-NG.pdf>  
 348 Sera ya Faragha ya Programu ya QuickCheck <https://quickcheck.ng/privacy-policy/>

Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Jina, anwani (ikijumuisha anwani ya zamani), barua pepe, nambari ya simu, maelezo ya mitandao ya kijamii, maelezo ya fedha, maelezo ya hali ya binafsi, maelezo ya kazi, maelezo ya kiwango cha elimu, anwani za mawasiliano za familia na maarifa, programu, ujumbe, anwani ya IP, aina ya kivinjari. <sup>349</sup>
Jinsi maelezo yanavyokusanywa kutoka kwa watumiaji	Unapojaza fomu kwenye Programu/ tovuti Unapotoa idhini ya kufikia akaunti za mitandao ya kijamii Kupitia mawasiliano, yaani, kupitia simu au barua pepe Kupitia maoni yanayotolewa na mtumiaji kwenye tovuti
Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	
Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	
Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kufanya maudhui yamfae mtumiaji Kutoa bidhaa na huduma Kutoa alama za mikopo Kutoa taarifa kuhusu mabadiliko kwenye bidhaa na huduma Mawasiliano, yaani, kupitia barua pepe na simu
Kuhifadhiwa kwa data ya mtumiaji	Kuhifadhiwa kwa maoni ya mtumiaji kwenye tovuti kwa kipindi kisicho julikana “Watumiaji wanaweza kuona, kubadilisha au kufuta data yao wakati wowote”. Hata hivyo, “hawawezi kubadilisha majina yao ya mtumiaji”.
Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine  Muda wa wahusika wengine kufikia data	
Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuzi vya tovuti	Aina ya vidakuzi: Vidakuzi vya mtu mfupi- hubainisha kukubaliwa kwa vidakuzi na kivinjari cha mtumiaji wakati wa kuingia Vidakuzi vya kuingia- Huhifadhi maelezo ya kuingia ya mtumiaji Vidakuzi huhifadhiwa kwenye vivinjari vya watumiaji wanapochapisha au kuhariri makala kwenye tovuti -Vidakuzi hutumiwa kwa madhumuni ya ufuatiliaji.

	Uhamishaji wa data kimataifa	
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	"Maelezo ya binafsi ya mtumiaji huhifadhiwa kwenye mitandao salama na yanaweza tu kufikiwa na watu wachache walio na haki maalum za ufikiaji wa mifumo hiyo na wanahitajika kudumisha usiri wa maelezo hayo. Kando na hayo, maelezo yote nyeti/ya mikopo yanayotolewa na watumiaji husimbwa kupitia teknolojia ya Secure Socket Layer (SSL) ...Shughuli zote za kifedha huchakatwa kupitia mto huduma za fedha na hazihifadhiwi au kuchakatwa kwenye seva zetu." <sup>350</sup>
Aella credit <sup>351</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Jina, anwani, anwani ya barua pepe, nambari ya simu, IMEI, maelezo ya SIM kadi, umri, jina la mtumiaji, nenosiri, maelezo ya fedha na mikopo (ikijumuisha maelezo ya akaunti ya mtumiaji ya huduma ya kutuma na kupokea pesa kupitia simu, maelezo ya akaunti ya benki, nambari ya uthibitishaji wa benki), maelezo ya binafsi na picha <sup>352</sup>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji/ Matumizi ya tovuti	Maelezo ya kiufundi: aina ya simu ya mkononi, vitambulishi maalum (IMEI au nambari ya kitambulisho), matumizi ya SIM kadi, mtandao wa simu, mfumo wa uendeshaji, aina ya kivinjari, data ya mahali ya kifaa na mipangilio ya saa za eneo, maelezo yaliyohifadhiwa kwenye kifaa (anwani, rekodi za nambari za simu, SMS, picha, video au maudhui mengine dijitali), maelezo ya matumizi ya Programu ya mhusika mwingine kwenye kifaa, maelezo ya matumizi ya Programu ya aella (ikijumuisha data ya trafiki na mahali, maelezo ya kuingia katika akaunti). <sup>353</sup> Maelezo ya mahali kupitia teknolojia ya GPS
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Hupokea maelezo kutoka: Ofisi za rekodi za mikopo Watoa huduma za mtandao wa simu
	Matumizi ya maelezo ya mtumiaji	Kufungua akaunti Kutii masharti ya mchakato wa Jua Mteja Wako (Know Your Customer (KYC)) Kutathmini ufaafu wa mtumiaji kustahiki kupata mkopo

350 Sera ya Faragha ya rogramu ya QuickCheck- Kifungu cha 'Jinsi tunavyolinda data yako'

351 Sera ya Faragha ya rogramu ya Aella credit <https://aellaapp.com/privacy-policy>

352 Sera ya Faragha ya Programu ya Aella credit- Kifungu cha 'Maelezo Yanayohitajika' <https://aellaapp.com/privacy-policy>

353 Sera ya Faragha ya Programu ya Aella Credit- Kifungu cha 3.2 Maelezo Yanayokusanywa

	Jinsi maelezo ya mtumiaji yanavyokusanya	Kupitia kujaza fomu wakati wa kuomba mkopo kwenye Programu au tovuti Kupitia mawasiliano na programu ya aella credit Kujisajili kwa matumizi ya tovuti ya aella Kupitia kupakua Programu Kujisajili kwenye huduma za aella Wakati wa kutafuta Programu au huduma Kuingia/ kushiriki maelezo kupitia vipengele vya mitandao ya kijamii vya programu ya aella credit Kujiunga kwenye mashindano ya Programu Wakati wa matangazo au tafiti Wakati wa kuwasilisha malalamiko kuhusu Programu, huduma au tovuti
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine/ Ufichuzi wa Maelezo	Programu ya Aella credit hushiriki maelezo na: Watoa huduma Washirika wa kibiasara, yaani., kampuni yake kuu, kampuni tanzu nk Kampuni zilizopewa kandarasi ya kutangaza bidhaa zake Kampuni zingine wakati wa michakato ya miungano, ununuzi, mauzo ya mali, kufilisiwa au kufilisika Mamlaka za sheria kwa uzuiaji wa madhara Mamlaka husika katika kutii maagizo ya mahakama, au kwa madhumuni ya kutetea madai ya kisheria au kutii sheria Ofisi za rekodi za mikopo wakati wa kuripoti wadeni au kwa uchapishaji wa takwimu kuhusu matumizi ya Programu
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	Hajabainishwa
	Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuzi vya tovuti	Matumizi ya vidakuzi na teknolojia za ufuatiliaji
	Uhamishaji wa data kimataifa	
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Data ya mtumiaji inaweza kuhifadhiwa na kuhamishwa nje ya nchi ya Naijeria na kuchakatwa na wafanyakazi wanaohudumu nje ya nchi ya Naijeria.

## Uchanganuzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu

### Kikomo cha Madhumuni

Programu za kukopesa pesa zinahitajika chini ya Sheria za Ulinzi wa Data nchini Naijeria (Nigeria Data Protection Regulations (NDPR) kuchakata data ya binafsi kwa madhumuni maalum, halali na ya kisheria kwa kutegemea idhini ya mmiliki wa data.<sup>354</sup> Sheria hizi pia zinaeleza kwamba uchakataji zaidi wa data ya binafsi na programu hizi unapaswa tu kufanywa kwa ajili ya madhumuni ya kuhifadhiwa, utafiti wa kisayansi, utafiti wa kihistoria au madhumuni ya kitakwimu kwa maslahi ya umma.<sup>355</sup>

Programu zinazochunguzwa, kama ilivyoonyeshwa hapo juu, zinabainisha madhumuni

<sup>354</sup> Kanuni ya 2.1. (1) (a) NDPR

<sup>355</sup> Kanuni ya 2.1 (1) (i) NDPR

ya ukusanyaji wa data ya binafsi, ambayo ni pamoja na. wala si tu, utoaji wa huduma (yaani., mikopo), kutoa alama za mikopo na matangazo. Hata hivyo, swali ni iwapo data inayokusanywa inahusiana na madhumuni ya ukusanyaji wa data. Uchunguzi wa sera za faragha za programu hizi (kama ilivyoonyeshwa hapo juu) unabainisha kuwa ni ya ziada na haihusiani na madhumuni ya utoaji wa mikopo dijitali. Hii inajumuisha data iliyoohifadhiwa kwenye kifaa cha mtumiaji kama vile orodha ya anwani za mawasiliano, rekodi za nambari za simu, picha na video; maelezo ya mitandao ya kijamii (ikijumuisha maelezo ya kuingia katika akaunti) na anwani za mitandao ya kijamii; maelezo ya binafsi ya mtumiaji; maelezo ya fedha na mikopo; wenzake; na orodha ya wanafamilia. Ukusanyaji wa aina hii ya maelezo ni wa kinyume na madhumuni na unakiuka haki ya faragha ya mmiliki wa data.

Aina hii ya maelezo hayahitajiki kwa madhumuni ya utoaji wa mikopo dijitali, na programu zinapaswa tu kuzingatia ukusanyaji wa data ya binafsi inayohitajika kwa utoaji wa mikopo.

## **Kuhifadhiwa kwa Data**

Sheria ya NDPR inahitaji programu hizi kubainisha moja kwa moja kipindi cha muda ambao zitahifadhi data yake na vigezo vinavyotumiwa kubainisha kipindi hicho.<sup>356</sup> Sheria zinazidi kueleza kwamba programu hizi zinapasa tu kuhifadhi data ya binafsi ya watumiaji kwa kipindi ambacho data hiyo inahitajika.<sup>357</sup>

Programu zinazochunguzwa zimeshindwa kutii kanuni hii. Baadhi ya programu zinaruhusu kufutwa kwa data baada ya data hiyo kutumiwa kwa madhumuni yake yaliyobainishwa. Hata hivyo, bado zinaweka kanusho kwa suala hili kinyume na kanuni ya ufutaji. Programu ya Carbon, kwa mfano, inaeleza kwamba data ya binafsi itafutwa baada ya madhumuni yake, yaani., ukopeshaji, kukamilika.<sup>358</sup> Hata hivyo, inaeleza kwamba licha ya kufutwa kwa data, data hiyo bado itahifadhiwa kwenye hifadhi yake rudufu au kumbukumbu kwa madhumini ya kisheria, kodi au usimamizi.<sup>359</sup> Hii bila shaka linamaanisha kwamba programu ya Carbon bado itakuwa na data ya mtumiaji licha ya kufutwa na kukamilika kwa madhumuni yake. Ni muhimu pia kutambua kwamba programu ya Carbon haibainishi vigezo vinavyotumiwa kubaini kipindi cha kuhifadhi data.<sup>360</sup>

Programu ya Palm Credit, kwa upande mwengine, inaendelea kiasi kuonyesha vigezo vinavyotumiwa kubainisha kipindi cha kuhifadhi data.<sup>361</sup> Hata hivyo, sera ya faragha ya Programu hii inabainisha kwamba hata ikiwa mtumiaji ataondoa Programu kwenye kifaa, bado Programu inaweza kuhifadhi data ya mtumiaji kwa muundo uliojumlishwa na kuondolewa data ya utambulisho.<sup>362</sup> Sera hiyo pia inaeleza kwamba bado Programu inaweza kuhifadhi data ya mtumiaji kwa madhumuni ya kutii wajibu wa kisheria na kutatua au kusuluhisha migogoro na utekelezaji wa mikataba yake.<sup>363</sup> Masuala haya pamoja yanabainisha kwamba data haitafutwa na bado itakuwa inahifadhiwa na Programu.

Programu ya Branch haina kifungu kuhusu kuhifadhiwa kwa data. Programu ya QuickCheck, kwa upande mwengine, inaruhusu watumiaji kuona, kubadilisha au kufuta data yao isipokuwa majina yao ya mtumiaji.<sup>364</sup> Programu ya Aella inabainisha kwamba data ya mtumiaji haitahifadhiwa kwa muundo ambao unawatambulisha kwa muda mrefu zaidi ya madhumuni ya ukusanyaji wa data.<sup>365</sup>

<sup>356</sup> Kanuni ya 2.13.6 (g), NDPR

<sup>357</sup> Kanuni ya 2.1. (1) (c) , NDPR

<sup>358</sup> Sera ya Faragha ya Programu ya Carbon; Kifungu cha Kuhifadhiwa kwa Data

<sup>359</sup> Sera ya Faragha ya Programu ya Carbon: Kifungu cha Kuhifadhiwa kwa Data

<sup>360</sup> Ibid

<sup>361</sup> Sera ya Faragha ya Programu ya Palm Credit: Kifungu cha Kuhifadhiwa kwa Data

<sup>362</sup> Sera ya Faragha ya Programu ya Palm Credit: Kifungu cha Kuhifadhiwa kwa Data

<sup>363</sup> Sera ya Faragha ya Programu ya Palm Credit: Kifungu cha Kuhifadhiwa kwa Data

<sup>364</sup> Sera ya Faragha ya Programu ya QuickCheck: Kifungu cha Kuhifadhiwa kwa Data

<sup>365</sup> Sera ya Faragha ya Programu ya Aella: Kifungu cha 1.4

## Usalama wa Data

Sheria ya NDPR inabainisha kanuni dhahiri ambazo programu hizi zinapaswa kufuata ili kuhakikisha usalama wa data ya binafsi ya mtumiaji. Inaeleza kwamba programu hizi zinapaswa kulinda data ya binafsi ya mtumiaji dhidi ya hatari na matukio yote ya ufhichuzi haramu wa data yanayoweza kutokea kama vile wizi, mashambulizi ya mtandaoni, mashambuzi ya virusi, kusambazwa, kuathiriwa au kuharibiwa.<sup>366</sup> Kwa kufanya hivyo, sheria ya NDPR inahitaji programu hizi ziweke mbinu za usalama kama vile; kulinda mfumo dhidi ya wadukuzi, kuweka kingamtandao, kuhifadhi data kwa usalama na kufikiwa na watu maalum waliodhinishwa, kutumia teknolojia za usimbaji wa data, kutunga sera ya shirika ya kushughulikia data ya binafsi, kulinda mifumo ya barua pepe na kukuza uwezo wa wafanyakazi.<sup>367</sup>

Mbinu hizi ni muhimu kwa kuzingatia wingi wa data ya inayokusanywa na programu hizi za kukopesha pesa. Hata hivyo, baadhi ya mbinu zinazohusiana na usalama wa data zinazotumiwa na programu hizi ni za kutiliwa shaka mno. Programu ya Carbon na Palm Credit, kwa mfano, haziwahakikishii watumiaji ulinzi wa data wanayotuma kwa Programu, yaani, manenosini wakati wa shughuli za kuingia katika akaunti.<sup>368</sup> Zinabainisha kuwa utumaji huo data ni kwa tahadhari ya mtumiaji.<sup>369</sup> Hili ni jambo la kusikitisha sana kwa mtumiaji ambaye anahitaji kupokea huduma za Programu kwa dharura. Programu hizi kulingana na sheria ya NDPR zinapaswa chini ya hali kama hizo kutumia teknolojia ya usimbaji wa data ili kulinda data ya binafsi ya mtumiaji inayotumwa kwa Programu wakati wa shughuli kama vile kuingia katika akaunti. Programu pekee ambazo zinatumia teknolojia ya usimbaji ni Branch na QuickCheck.<sup>370</sup>

Programu hizi zimeweka kiwango fulani cha usalama; hata hivyo, programu zingine zina mbinu thabiti za usalama ikilinganishwa na zingine. Hizi zinajumuisha; Programu ya Branch na QuickCheck.

## Idhini ya Mmiliki wa Data

Programu hizi zinahitajika chini ya sheria ya NDPR kuhakikisha kuwa shughuli zake za uchakataji ni halali. Programu hizi zinapaswa tu kuchakata data ya binafsi kwa kutegemea idhini ya mmiliki wa data na kwa madhumuni maalum ya kisheria.<sup>371</sup> Sheria ya NDPR inazidi kuzishurutisha programu hizi kuwafahamisha wamiliki wa data kuhusu madhumuni ya ukusanyaji wa data ili kuhakikisha kuwa wamiliki wa data wanatoa idhini yao kwa busana.<sup>372</sup>

Mwandishi huyu anaamini kuwa programu hizi haziwaruhusu watumiaji kutoa idhini yao kwa hiari. Hii ni kwa sababu huduma za programu hizi zinategemea idhini ya mtumiaji na ikiwa mtumiaji atakataa data yake isichakatwe, programu hizi hazimruhusu kupokea huduma.

Pili, sheria ya NDPR inaeleza kwamba wakati wa kuchunguza iwapo idhini imetolewa kwa hiari, itazingatiwa iwapo utoaji wa huduma unategemea kutolewa kwa idhini ya uchakataji wa data binafsi ambayo si muhimu au (ya ziada) kwa utekelezaji wa mkataba.<sup>373</sup>

Katika hali hii, ufikiaji wa huduma za mikopo kwenye programu unategemea programu kufikia data isiyohitajika na ya ziada ambayo inakiuka faragha ya mtumiaji. Programu hizi zinaomba kufikia data isiyohitajika kwa madhumuni ya ukopeshaji wa pesa, kama vile maelezo ya mitandao ya kijamii, orodha ya anwani za mawasiliano za mtumiaji na orodha ya

<sup>366</sup> Kanuni ya 2.1 (1) (d) NDPR

<sup>367</sup> Kanuni ya 2.6 NDPR

<sup>368</sup> Sera ya Faragha ya Programu ya Carbon na Palm Credit: Vifungu vya Usalama

<sup>369</sup> Ibid

<sup>370</sup> Vifungu vya Usalama vya Programu ya Branch na QuickCheck.

<sup>371</sup> Kanuni ya 2.2 (a) ya NDPR

<sup>372</sup> Kanuni ya 2.3 NDPR

<sup>373</sup> Kanuni ya 2.3 (2) (d) NDPR

wanafamilia, SMS, picha na video za mtumiaji na nyingineyo, ambayo inaingilia fanagha ya mtumiaji.

## **Upatikanaji na Uwazi wa Sera ya Faragha**

Chini ya Kanuni ya 2.5 ya sheria ya NDPR, kifaa chochote kinachochakata data ya binafsi kinahitajika kuonyesha sera ya fanagha dhahiri na rahisi ambayo kiwango cha wamiliki wa data wanaolengwa wanaweza kuelewa. Sera ya Faragha inapaswa kujumuisha:<sup>374</sup>

- Kinachounda idhini ya mmiliki wa data
- Maeleo ya data ya binafsi inayoweza kukusanywa
- Madhumuni ya ukusanyaji wa data ya binafsi
- Mbinu za kiufundi zinazotumiwa kukusanya na kuhifadhi maeleo ya binafsi na vidakuzi
- Ufikiaji wa maeleo ya binafsi na wahusika wengine na madhumuni ya ufikiaji
- Muhtasari wa kanuni za ulinzi wa data
- Mbinu zilizopo za kushughulikia matukio ya ufichuzi haramu wa data
- Kipindi cha muda wa ushughulikiaji

Programu ya Branch haina hili. Sera yake haina maeleo mengi kama inavyohitajika chini ya kanuni hii.

## **Uchakataji wa Data na Wahusika Wengine**

Sheria ya NDPR inahitaji shughuli ya uchakataji wa data na wahusika wengine isimamiwe na mkataba wa maandishi kati ya mhusika mwengine na Mdhibiti wa Data.<sup>375</sup> Inaeleza pia kwamba wadhibiti wa data wanaohusisha wahusika wengine katika uchakataji wa data ya binafsi ya watumiaji wanapaswa kuhakikisha kuwa wanatii sheria ya NDPR.<sup>376</sup>

Hakuna programu yoyote kati ya programu zilizochunguzwa ambayo iliweka mikataba na wahusika wengine ambao ilishiriki nao maeleo ya mtumiaji. Baadhi ya programu hizo, hasa programu ya QuickCheck na Branch, hazonyeshi wahusika wengine ambao zinashiriki nao maeleo haya. Suala la kutia wasiwasi zaidi ni kwamba programu hizi hazonyeshi hatua zitakazochukua ili kuhakikisha kuwa wahusika wengine ambao zinashiriki nao maeleo ya mtumiaji wanatii sheria ya NDPR.

## **Kuhamishiwa kwenye Nchi ya Kigeni**

Sheria ya NDPR inabainisha masuala muhimu ambayo yanapaswa kuzingatiwa kuhusiana na shughuli ya kuhamishia data kwenye nchi ya kigeni. Inaeleza kwamba shughuli hiyo ya uhamishaji inapaswa kufanyika kulingana na kanuni za sheria ya NDPR na usimamizi wa Mkuu wa Sheria Anayeheshimika wa Nchi (Honourable Attorney General of the Federation (HAGF).<sup>377</sup> Suala muhimu la kuzingatiwa ni kwamba nchi ya kigeni inapaswa kuwa na kiwango cha kutosha cha ulinzi wa data.<sup>378</sup> HAGF anapaswa kuchunguza mfumo wa sheria wa nchi ya kigeni kuhusiana na uongozi wa sheria na ulinzi wa haki za binadamu, na mengineyo.<sup>379</sup>

Kanuni ya NDPR inatoa hali maalum kuhusiana na suala hili.<sup>380</sup> Inaeleza kwamba data ya binafsi itahamishiwa katika nchi ya kigeni; ikiwa mmiliki wa data amekubali<sup>381</sup>, ambapo uhamishaji huo ni muhimu kwa utekelezaji wa mkataba kati ya mmiliki wa data na mdhibiti<sup>382</sup>. Mmiliki wa data anapaswa kufahamishwa kuhusu mbinu mwafaka za ulinzi wa data zinazotumika katika nchi ya kigeni.<sup>383</sup>

<sup>374</sup> Kanuni ya 2.5 ya NDPR

<sup>375</sup> Kanuni ya 2.7 ya NDPR

<sup>376</sup> Ibid.

<sup>377</sup> Kanuni ya 2.11 ya NDPR

<sup>378</sup> Kanuni ya 2.11 (a) ya NDPR

<sup>379</sup> Kanuni ya 2.11 (b) ya NDPR

<sup>380</sup> Kanuni ya 2.12 ya NDPR

<sup>381</sup> Kanuni ya 2.12 (a) ya NDPR

<sup>382</sup> Kanuni ya 2.12 (b) ya NDPR

<sup>383</sup> Kanuni ya 3.1 (8) ya NDPR

## Haki za Mmiliki wa Data

Sheria ya NDPR inawapa wamiliki wa data haki kuhusiana na uchakataji wa data yao.<sup>384</sup> Inaeleza kwamba kabla ya uchakataji wa data ya binafsi ya mmiliki wa data, mdhibiti wa data anapaswa kumfahamisha mmiliki wa data kuhusu utambulisho na maelezo ya mawasiliano ya mdhibiti wa data, maelezo ya mawasiliano ya Ofisa wa Ulinzi wa Data, madhumuni ya uchakataji, maslahi ya kisheria yanayolengwa kutimizwa na mdhibiti, wapokeaji wa data ya binafsi, nia ya kuhamishia data kwenye nchi nyingine, kipindi ambacho data ya binafsi itahifadhiwa na vigezo vya kubaini kipindi hicho, haki ya mmiliki wa data ya kuomba kufikia, kurekebisha au kufuta data ya binafsi, haki ya mmiliki wa data ya kuondoa idhini, uwepo wa mbinu ya kufanya maamuzi na kuweka rekodi ya mtumiaji kiotomatiki, maelezo kuhusu madhumuni ya uchakataji wa ziada, na maelezo kuhusu uhamishiaji wa data ya binafsi kwenye nchi ya kigeni.

Baadhi ya programu zilizochunguzwa, kama vile Programu ya Aella, QuickCheck na Carbon, hazitoi maelezo ya mawasiliano ya Ofisa wa Ulinzi wa Data, wala hazibainishi iwapo mashinika haya yana Maofisa wa Ulinzi wa Data. Programu ya Branch na Palm Credit ndizo programu pekee zilizo na Maofisa wa Ulinzi wa Data. Kama ilivyojadaliwa katika sehemu iliyotangulia, programu hizi zinabainisha madhumuni ya uchakataji wa data; hata hivyo, data inayochakatwa haihusiani na madhumuni ya ukopeshaji wa pesa.

Baadhi ya programu zilizochunguzwa zinawafahamisha watumiaji kuhusu wapokeaji wa data yao, na zingine haziwafahamishi. Programu hizo pia zinabainisha nia yake ya kuhamishia data ya binafsi kwenye nchi za kigeni lakini hazibainishi mbinu za ulinzi zilizowekwa ili kulinda data katika nchi za kigeni. Programu pekee ambayo inawapa watumiaji nafasi ya haki ya kuomba ufikiaji, urekebishaji na ufutaji wa data ni Palm Credit. Programu zingine zinadhibiti haki hii. Kwa mfano, programu ya Branch inawapa tu watumiaji haki ya kuomba urekebishaji wa maelezo wakati ambapo maelezo hayo si sahihi, na programu ya Carbon inawapa tu watumiaji haki ya kukataa data yao isichakatwe kwa madhumuni ya matangazo. Programu mbili pekee ndizo zinawaruhusu watumiaji kutekeleza haki yao ya kuhamishika kwa data, yaani, programu ya Quick Check na Palm Credit.<sup>385</sup>

## Uaibishwaji

Programu za mikopo dijitali nchini Naijeria zinafahamika zaidi pia kwa uaibishaji.<sup>386</sup> Programu hizo zina vifungu kwenye sera zake za faragha ambavyo vinazipa haki ya kuwasiliana na watu ambao mtumiaji huwasiliana nao kuhusu hali ya mtumiaji kushindwa kulipa deni.<sup>387</sup> Baadhi ya programu huchukua hatua hata zaidi ya kuchapisha wakopaji walioshindwa kulipa madeni kwenye mitandao ya kijamii na kuwafanya waonekane kama wahalifu.<sup>388</sup> Haya yote hufanywa ili kumfanya mkopaji alipe deni. Hata hivyo, vitendo kama hivyo vinakiuka faragha ya mkopaji na kuharibu sifa yake.

Programu zinazojulikana zaidi kwa vitendo hivi zinajumuisha OKash, Soko Loan, LCredit, Credit9ja na Fast Money.<sup>389</sup> Katika sera zake za faragha, programu hizi zinabainisha moja kwa moja kwamba zinaweza kutumia anwani za mawasiliano za mtumiaji ikiwa mtumiaji atashindwa kulipa deni. Vifungu kama hivyo vinakiuka sheria ya NDPR, ambayo hairuhusu uchakataji wa data ya binafsi kinyume cha sheria.<sup>390</sup> Shirika la Kitaifa la Maendeleo ya Mawasiliano (National Information Development Agency (NITDA) linapaswa kuchukua hatua

384 Kanuni ya 3.1. (7) ya NDPR

385 Sera ya Faragha ya Programu ya Quick Check: Kifungu cha Haki za Mtumiaji Sera ya Faragha ya Programu ya Palm Credit: Kifungu cha Haki za Mtumiaji

386 <https://twitter.com/EthanZ/status/1429845838751207432?s=19>

387 Uingiliaji wa Faragha wa Programu za Kukopesha Pesa nchini Naijeria <https://aanoip.org/the-intrusiveness-of-money-lending-apps-in-nigeria/>

388 Ukiukaji wa Haki za Dijitali nchini Naijeria <https://www.change.org/p/central-bank-of-nigeria-violation-of-digital-rights-of-nigerians>

389 Ukiukaji wa Haki za Dijitali Nchini Naijeria <https://www.change.org/p/central-bank-of-nigeria-violation-of-digital-rights-of-nigerians>

390 Kanuni ya 2.2, Sheria za Ulinzi wa Data za Naijeria

kuhusu mbinu hizi na kuhakikisha kuwa programu hizi zinachakata data ya binafsi kwa njia ya haki na halali. Shirika hilo hivi karibuni liliwekeea vikwazo programu ya Soko Loan kwa kuingilia faragha ya wakopaji baada ya kupokea malalamiko kuhusu ufichuzi wake wa maelezo ya binafsi ambao haujaidhinishwa, kushindwa kulinda maelezo ya binafsi ya watumiaji, na udhalilishaji wa watumiaji.<sup>391</sup>

## **Faragha kwa Chaguomsingi au Kimuundo**

Programu zinapaswa kubuniwa kiufundi ili kuzifanya zikusanye tu maelezo ambayo ni muhimu kwa madhumuni ya ukopeshaji pesa. Muundo wa kiufundi wa programu haupaswi kuziruhusu kufikia data ya siri ya watumiaji kwenye vifaa vyao, kama vile picha, video, orodha ya anwani za mawasiliano, SMS na maelezo ya mitandao ya kijamii. Wasanidi wa Programu wanapaswa kuibuni kwa njia ambayo inaheshimu faragha ya mtumiaji.

## **Hitimisho**

Programu zinazochunguzwa zinaweza kusemekana kuwa hazitii sheria ya NDPR. Programu hizi zinachakata data nyingi mno ya binafsi kutoka kwa wamiliki wa data ambayo hailingani na madhumuni ya utoaji wa mikopo dijitali. Ukusanyaji wa kiasi kama hicho cha data ni wa kinyume na madhumuni na unakiuka haki ya faragha ya wamiliki wa data. Programu hizi zinapaswa kutii kikamilifu sheria ya NDPR na kuchakata tu data ya binafsi ambayo ni muhimu kwa utoaji wa mikopo dijitali. Programu hizi pia hushiriki data hii na wahusika wengine. Baadhi ya programu hizi (kama ilivyotajwa hapo juu) hazibainishi wahusika wengine ambao zinashiriki nao data hii. Haziwafahamishi watumiaji muda ambao wahusika wengine watafikia data na mbinu ambazo zinaweka ili kuhakikisha kuwa data inayoshirikiwa na wahusika wengine inalindwa kwa usalama.

---

<sup>391</sup> Shirika la NITDA Laiwekea Vikwazo Programu ya Soko Loan kwa Uingiliaji wa Faragha <https://nitda.gov.ng/nitda-sanctions-soko-loan-for-privacy-invasion/>

# Afrika Kusini



## Maelezo ya Nchi

Afrika Kusini, ambayo pia inajulikana kama Jamhuri ya Afrika Kusini, inapatikana katika eneo la kusini kabisa mwa Afrika.<sup>392</sup> Inapakana na mataifa ya Namibia, Botswana, Zimbabwe na Eswatini<sup>393</sup> na ni mionganini mwa maeneo yanayotembelewa zaidi na watalii barani Afrika. Afrika Kusini inajulikana kwa mandhari yake ya kupendeza na utamaduni mbalimbali.<sup>394</sup> Nchi hii ina lugha 11 rasmi, yaani., Kiafrikana, Kiingereza, Kindebele, Kisotho cha Kaskazini, Kisotho, Kiswazi, Kiswana, Kisonga, Kivenda, Kihosa na Kizulu, ambapo Kizulu, Kihosa na Kiafrikana ndizo lugha zinazozungumzwa zaidi.<sup>395</sup> Ina miji mikuu mitatu, yaani., Pretoria, ambao ni makao ya Viongozi Wakuu; Cape Town, ambao ni makao ya Bunge; na Bloemfontein, ambao ni makao ya Mahakama.<sup>396</sup> Nchi hii ina idadi ya watu milioni 60<sup>397</sup> na ina ukubwa wa 1,221,037 km<sup>2</sup>.

392 Afrika Kusini <https://www.britannica.com/place/South-Africa>

393 Ibid

394 Ibid

395 Afrika Kusini [https://www.nationsonline.org/oneworld/south\\_africa.htm](https://www.nationsonline.org/oneworld/south_africa.htm)

396 Ibid

397 Idadi ya Watu Nchini Afrika Kusini 2021 <https://worldpopulationreview.com/countries/south-africa-population>

## Ulinzi wa Data nchini Afrika Kusini

Kenya, Naijeria na Afrika Kusini ni nchi zinazoongoza barani Afrika katika mfumo wa teknolojia ya fedha, zikiwa na kampuni 450 za teknolojia ya fedha.<sup>398</sup> Afrika Kusini ina kampuni 200 za teknolojia ya fedha<sup>399</sup> zilizovunjwa katika vipengele kadhaa, yaani., malipo, mikopo, akiba na amana, na nyaginezo.<sup>400</sup> Lengo letu kuu katika utafiti huu ni sekta ya mikopo, ambayo inakua kwa kasi ya juu zaidi.<sup>401</sup>

Sekta ya ukopeshaji wa pesa ina mifumo kadhaa, ikijumuisha Pollen Finance, ambao unachukuliwa kuwa mfumo mkubwa zaidi wa kukopesha pesa nchini,<sup>402</sup> ukifuatwa na Lulalend na Fundrr.<sup>403</sup> Sekta hii inapatikana chini ya usimamizi wa Sheria ya Kitaifa ya Mikopo

398 Afrika Kusini, Naijeria na Kenya: Vitovu Vikubwa Zaidi vya Teknolojia ya Fedha Barani Afrika <<https://fintechnews.africa/39379/kenya/south-africa-nigeria-and-kenya-africas-largest-fintech-hubs/>> Ilifikiwa tarehe 4/8/2021

399 Ibid

400 Uchanganuzi wa Upeo wa Teknolojia ya Fedha nchini Afrika Kusini

<[http://www.treasury.gov.za/comm\\_media/press/2020/WB081\\_Fintech%20Scoping%20in%20SA\\_20191127\\_final%20\(002\).pdf](http://www.treasury.gov.za/comm_media/press/2020/WB081_Fintech%20Scoping%20in%20SA_20191127_final%20(002).pdf)> Ilifikiwa tarehe 4/8/2021

401 (n1)

402 (n3) ukurasa wa 8 (n1)

403 (n1)

(National Credit Act), ya 2005, ambayo inatoa vifungu vya sheria vya usimamizi wa sekta ya mikopo na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kitaifa ya Udhibiti wa Mikopo (National Credit Regulator), ambayo inawajibika kimsingi kwa usimamizi na udhibiti wa sekta hii.<sup>404</sup> Sheria hii inahitaji watoa huduma za mikopo kujisajili na inatoa mamlaka kwa shirika la Huduma za Kitaifa za Mikopo (National Credit Provider) kusimamia usajili huo.<sup>405</sup> Inatoa pia utaratibu wa kina wa kusajili watoa huduma za mikopo wanapotuma maombi ya kusajili kwa shirika la Huduma za Kitaifa za Mikopo (National Credit Provider).<sup>406</sup>

Kuhusu shughuli za uchakataji wa data, mifumo ya kukopesha pesa lazima itii Sheria ya Ulinzi wa Maelezo ya Binafsi (Protection of Personal Information Act (POPI Act) ambayo inabainisha kanuni ambazo zinapaswa kufuatwa na mifumo hii ili kuhakikisha usalama wa data ya binafsi inayokusanya.<sup>407</sup> Ni muhimu kutambua kuwa utekelezaji wa POPI Act na Mamlaka ya Usimamizi wa Maelezo (Information Regulator) ulianza hivi karibuni mnamo tarehe 1 Julai 2020, na mashirika yalipewa kipindi cha msahama cha mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kuanza kutekelezwa, yaani, tarehe 1 Julai 2020, ili kutii Sheria hii.<sup>408</sup>

Kwa hivyo, mashirika (ikijumuisha mashirika yanayomiliki mifumo ya kukopesha pesa) lazima yahakikishe kuwa shughuli zake za uchakataji wa data zinalingana na Sheria ya POPI. Pamoja na hayo, utafiti huu unalenga kuchanganua mbinu za ulinzi wa data za mifumo hii. Unaanza kwa kuchunguza sera za mifumo hii ili kuangazia data inayokusanywa na mifumo. Kisha unafuata kwa kufanya utathmini wa data inayokusanywa dhidi ya vifungu vya Sheria ya POPI ili kutambua iwapo mifumo hii inatii sheria ya ulinzi wa data.

## **Mifumo ya Mtandaoni ya Kukopesha Pesa inayochunguzwa katika utafiti huu**

Mifumo ya mtandaoni ya kukopesha pesa inayochunguzwa katika utafiti huu hufanya kazi kupitia tovuti, hasa mfumo wa Pollen Finance, Lulalend na Fundrr. Mfumo pekee ambao hufanya kazi kupitia programu ni Niftycredit (GetBucks) ambayo inaweza kupakuliwa kwenye Google Play.

- Pollen Finance - Mojawapo ya mifumo mikubwa zaidi ya mtandaoni ya kukopesha pesa nchini
- Lulalend - Ukopeshaji
- Fundrr - Ukopeshaji
- Nifty Credit (GetBucks) - Ukopeshaji

## **Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali**

404 Sheria ya Kitaifa ya Mikopo, 2005 ( Sheria Nambari 34 ya 2005) [https://www.gov.za/sites/default/files/gcis\\_document/201409/a34-050\\_0.pdf](https://www.gov.za/sites/default/files/gcis_document/201409/a34-050_0.pdf)

405 Kifungu cha 14, Sheria ya Kitaifa ya Mikopo ya 2005

406 Aya ya 3, National Credit Act 2005

407 Sheria ya Ulinzi wa Maelezo ya Binafsi (POPI Act) <https://popia.co.za/act/>

408 Tarehe ya Kuanza Kutekelezwa kwa Sheria ya POPI au Tarehe ya Kuanza Kutumika kwa Sheria ya POPI <https://www.michalsons.com/blog/pop-i-commencement-date-pop-i-effective-date/13109>

Pollen Finance <sup>409</sup> (Sera ya Faragha na Sheria na Masharti)	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Maelezo ya jumla ya biashara Nambari za mawasiliano Anwani ya mtaa, na Anwani ya barua pepe
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji/ Kivinjani	Hukusanya kiotomatiki maelezo yafuatayo, ambayo huhifadhiwa kwenye rekodi zake za seva: Anwani ya IP Maelezo ya vidakuzi Ukurasa ulioombwa
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Maelezo ya mtumiaji hutumiwa kwa madhumuni yafuatayo: Kutuma mawasiliano na taarifa kuhusu tovuti au huduma za programu ya Pollen Finance Mfumo huu hutumia vidakuzi kufuatilia vipindi vya mtumiaji na kuvihifadhi kwenye diskii zake kuu. Anwani ya IP ya mtumiaji hutumiwa pia kutambua matatizo ndani ya tovuti na kuyashughulikia
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Pollen Finance hushiriki maelezo na wahusika wengine ili kutoa huduma ya matangazo na mawasiliano ya mtandaoni. Wahusika wengine hutumia data hiyo kutathmini aina ya huduma, ofa na matangazo ambayo yanaweza kuwavutia watumiaji wa mfumo. Hata hivyo, data inayoshirikiwa hujumlishwa na haihusishwi na mtumiaji ye yeyote wa mfumo. Mfumo huwapa watumiaji fursa ya kutekeleza haki yao ya kujiondoa ikiwa hawangependa data yao itumiwe katika kutoa huduma ya matangazo.
Muda wa wahusika wengine kufikia data		

	Ufichuzi wa Maelezo	Mfumo wa Pollen Finance hufichua maelezo ya mtumiaji kwa madhumuni yafuatayo: Takwimu za soko: Hufichua takwimu zilizojumlishwa kwa watangazaji na washirika wa kibiashara Maajenti na watoa huduma wengine: Mhusika mwengine hupaswa kutumia tu data hiyo kutoa huduma zilizoombwa Utekelezaji wa Sheria: Hufichua data wakati; inahitaji na sheria, kulinda usalama wa mtu na kuzuia ukiukaji wa sheria. Anwani ya IP inaweza pia kufichuliwa ikiwa inahitajika katika mchakato wa kisheria au ikihitajika na sheria Kubadilisha umiliki: Miungano, ununuzi au uuza ji wa mali ya biashara Wafanyakazi wa Pollen Finance
	Teknolojia za ufuutiliaji/ vidakuzi vya tovuti	Mfumo huu hutumia vidakuzi kufuutilia vipindi vya mtumiaji na kuvihifadhi kwenye diskii zake kuu. Anwani ya IP ya mtumiaji hutumiwa pia kutambua matatizo ndani ya tovuti na kuyashughulikia
	Kuhifadhiwa/ Usalama wa data	“Tovuti inaendeshwa katika mazingira salama ya seva ambayo hutumia kinga mtandao na mbinu zingine za usalama ili kuzuia kuathiriwa au kufikiwa na watu ambao hawajaidhinishwa.”
	Uhamishaji wa Data Nje ya Nchi	Pollen Finance inaweza kuhamishia data ya mtumiaji kwenye nchi zingine, ikijumuisha nchi ambazo hazina sheria (viwango) vinavyolingana vya ulinzi wa data.

Lulalend <sup>410</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Jina, nambari ya usajili/ tarehe ya kuzaliwa, anwani ya mahali na posta, anwani ya barua pepe, nambari ya simu, jinsia/ utaifa/ asili ya kikabila na kijamii/ umri, maelezo ya fedha, maoni ya binafsi/ mitazamo/ mapendeleo, mawasiliano ya siri yanayotumwa na mtumiaji, mitazamo/ maoni ya watu wengine kuhusu mtumiaji, maelezo ya mikopo na historia ya mtumiaji,
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Mtumiaji anapotembelea tovuti ya Lulalend, seva za tovuti hukusanya kiotomatiki maelezo ya kiufundi kuhusu shughuli ya mtumiaji kwenye tovuti na kompyuta. Maelezo haya yanajumuisha maelezo ya kompyuta ya mtumiaji, anwani ya IP, mfumo wa uendeshaji na aina ya kivinjari, data ya mahali na maelezo ya utumiaji.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	

	Matumizi ya maelezo ya mtumiaji/ madhumuni ya ukusanyaji wa data	Programu ya Lulalend hutumia data ya mtumiaji kwa madhumuni yafuatayo: Kuamua iwapo itaweka mkataba na mtumiaji Utekelezaji wa wajibu chini ya mkataba Kutii wajibu wa kisheria Kulinda maslahi ya kisheria ya mtumiaji Kutimiza maslahi ya kisheria ya huduma ya Lulalend Madhumuni ya kuripoti mikopo Madhumuni ya kuonyesha matangazo moja kwa moja Kuboresha na kuonyesha na kufanya maudhui kama vile bidhaa, makala, matangazo nk Kutuma maudhui kuhusu makala, bidhaa, matangazo nk Kujulisha watumiaji kuhusu mabadiliko kwenye tovuti
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine  Muda wa wahusika wengine kufikia data	Programu ya Lulalend hushiriki maelezo ya binafsi na wahusika wengine wafuatao: Benki za mtumiaji au taasisi za fedha Watoa huduma za ofisi za mikopo Watoa huduma za kitaalamu wanaotoa huduma za kisheria, uhasibu na ukaguzi Watoa huduma za utarishi na usafirishaji wa bidhaa Mtoa huduma za malipo Programu ya Lulalend inaweza kushiriki maelezo ya mtumiaji yaliyojumlishwa na mitindo ya matumizi ya wavuti kwa madhumuni ya matangazo

	<p>Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji/ Mbinu za ulinzi</p> <p>Programu ya.Lulalend inaahidi kulinda data ya binafsi dhidi ya kupotea, kuharibiwa au kufikiwa bila idhini</p> <p>Programu ya Lulalend hutambua hatari zinazoweza kujitokeza kwa data ya binafsi na kuweka mbinu za ulinzi ili kuilinda dhidi ya hatari hizo</p> <p>Programu ya Lulalend huhakikisha kuwa mikataba yake na wahusika wengine ina wajibu ufuatao:</p> <p>Wahusika wengine hawaruhusiwi kuchakata data ya binafsi bila idhini ya Lulalend</p> <p>Wahusika wengine wanapaswa kushughulikia data ya binafsi kama data ya siri na hawapaswi kuishiriki na wahusika ambao hawaajaidhinishwa</p> <p>Wahusika wengine wanapaswa kuweka mbinu za ulinzi za kiwango sawa kama cha Lulalend</p> <p>Wahusika wengine wanapaswa kujulisha Lulalend wakati ambapo wahusika ambao hawaajaidhinishwa wamefikia data ya binafsi</p> <p>Ikiwa mhusika mwengine anaishi katika nchi nyingine, anapaswa kutii sheria za ulinzi wa data za nchi hiyo</p> <p>Ikiwa mhusika mwengine anahitajika kisheria kufichua maelezo ya mtumiaji, anapaswa kujulisha Lulalend</p>
Uhamishaji wa Data ya Binafsi Nje ya Nchi	<p>Lulalend huhamishia data ya mtumiaji kwenye nchi nyingine kwa kutegemea ruhusa yake. Data huhamishwa kwa hali zifuatazo:</p> <p>Wakati ambapo uhamishaji huo ni muhimu kwa utekelezaji wa mkataba kati ya mtumiaji na Lulalend</p> <p>Wakati ambapo uhamishaji huo unahitajika kwa ajili ya kutimizwa kwa masharti ya kabla ya kuweka mkataba Uhamishaji huo ni kwa manufaa ya mtumiaji</p> <p>Mtumiaji ameidhinisha uhamishaji huo</p> <p>Ili kuhifadhi maelezo ya mtumiaji kielektroniki kwenye hifadhidata salama</p> <p>Watoa huduma za Lulalend wana haki ya kuhamishia data ya mtumiaji kielektroniki kwenye hifadhidata inayopatikana nje ya nchi ya Afrika Kusini mradi nchi hizo zina kiwango sawa cha ulinzi wa usalama, sera na kanuni kuhusu ulinzi wa data kama cha Lulalend</p>
Teknolojia ya Ufuutilaji na Vidakuvi	<p>Lulalend hutumia vidakuvi kwenye tovuti yake ili:</p> <p>Kutofautisha watumiaji</p> <p>Kufuatilia vipindi vya mtumiaji kwenye tovuti</p> <p>Kuhifadhi kuhusu mapendeleo ya mtumiaji</p> <p>Kukadiria idadi ya watumiaji wa tovuti na mitindo ya matumizi</p> <p>Kuongeza kasi ya utafutaji</p>

Fundrr <sup>411</sup>	Maelezo Yanayokusanya na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	
	Maelezo yanayokusanya kutoka kwa mtumiaji	Programu ya hukusanya maelezo yafuatayo kutoka kwa watumiaji: Anwani ya IP Maelezo ya mawasiliano Maelezo ya biashara Maelezo ya fedha, na Maelezo yoyote yanayohitajika na programu Fundrr
	Maelezo yanayokusanya kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Anwani ya IP (Internet Protocol) Anwani ya jina la kikoa Utambulisho wa huduma ya intaneti au mto huduma Aina ya programu ya kivinjari Mfumo wa uendeshaji wa kompyuta URL ya ukurasa uliotembelewa na mtumiaji kwenye tovuti Lugha ya kivinjari iliyochaguliwa na mtumiaji
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine/ Kushiriki maelezo ya binafsi	Programu ya Fundrr hushiriki maelezo na wahusika wengine katika hali zifuatazo: Wakati wa kuchakata maelezo kwa madhumuni ya kutoa ripoti ya mikopo Wakati wa kuunganisha huduma za mashirika washirika Wakati wa kuunganisha huduma za wahusika wengine ambao hutoa huduma kama vile; kutoa bili na ukusanyaji wa madeni, huduma zinazohusiana na mikopo (kama vile ufaafu wa kupokea mikopo, kutoa alama za mikopo, kuorodhesha walioshindwa kulipa madeni, nk) na mengineyo
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Teknolojia ya ufuutilaji na vidakuzi	Maelezo yanayokusanya na vidakuzi huhifadhiwa na kutumiwa kuunda wasifu wa watumiaji wa tovuti. Ripoti hii huwezesha Fundrr kujua mapendeleo ya mtumiaji, matumizi na shughuli za mazoea.
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji/ Ulinzi	Maelezo huhifadhiwa kwenye seva salama kwa kipindi kinachohitajika kisheria na Fundrr

Niftycredit (GetBucks) <sup>412</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	<p>Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji na programu ya Niftycredit yanajumuisha:</p> <p>Maelezo ya jumla: jina, nambari ya kitambulisho, jinsia, tarehe ya kuzaliwa, anwani ya makazi, maelezo ya mawasiliano kama vile barua pepe na nambari ya simu</p> <p>Maelezo ya ajira: historia ya ajira, elimu, vyeti, uzoefu, data ya takwimu za kijamii na kiuchumi, data ya mahali na maelezo ya mshahara</p> <p>Maelezo ya kuomba mkopo: Maelezo yanayotolewa wakati wa kuomba mkopo yanajumuisha mali, mapato na madeni</p> <p>Maelezo ya akaunti: maelezo ya akaunti ya benki, mkopo</p> <p>Maelezo ya shughuli za kifedha: Maelezo yanayohusiana na shughuli za kifedha na shughuli za akaunti kama vile masilio ya akaunti, historia ya malipo na matumizi ya akaunti</p> <p>Maelezo ya ripoti ya mtumiaji:</p> <p>Maelezo yaliyopatikana kutoka kwenye vidakuzi</p> <p>Rekodi za mazungumzo ya simu</p> <p>Mapendeleo ya mtumiaji ya matangazo</p> <p>Vitambulishi kama vile anwani ya IP (internet protocol)</p> <p>Maelezo hukusanywa kutoka kwa mtumiaji:</p> <p>Wakati wa kuvunjari tovuti ya Niftycredit</p> <p>Wakati wa kufungua akaunti/kuomba huduma za Niftycredit</p> <p>Wakati wa kuwasiliana na Niftycredit kuitia barua pepe, mitandao ya kijamii au simu</p> <p>Maelezo pia hupatikana kutoka kwa wahusika wengine ambao:</p> <p>Hufuatilia matumizi ya tovuti</p> <p>Hufanya utafiti wa soko, tafiti na biashara na uchanganuzi wa kitakwimu</p>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	

Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	<p>Programu ya Niftycredit hutumia maelezo ya mtumiaji kwa madhumuni yafuatayo:</p> <p>Kutoa bidhaa na huduma</p> <p>Kuwezesha shughuli za kifedha</p> <p>Kwa ukarabati, matengenezo au ukusanyaji wa akaunti</p> <p>Kutoa bidhaa na kutathmini ustahiki wa mtumiaji</p> <p>Kufanya utafutaji wa rekodi za mikopo au uthibitishaji</p> <p>Kutekeleza shughuli ya kutoa alama za mikopo na utathmini</p> <p>Kutekeleza utathmini wa hatari ya kutoa mkopo</p> <p>Kutoa ulinzi kwa watumiaji</p> <p>Kuthibitisha akaunti</p> <p>Kuthibitisha utambulisho wa mtumiaji</p> <p>Ukusanyaji wa madeni</p> <p>Kutii masharti ya kisheria na usimamizi, na mengineyo</p>
Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine/ Kushiniki maelezo ya binafsi	<p>Programu ya Niftycredit hushiriki maelezo na wanachama wa kikundi chake na wataalamu wa ushauri ili kupata ushauri wa kitaalamu na kutetea madai ya kisheria, na mengineyo.</p> <p>Hushiriki pia maelezo na wahusika wengine wafuatao:</p> <p>Watoa huduma za mifumo ya malipo, mashirika ya ukusanyaji wa madeni, mashirika ya ufuatiliaj na watoa huduma wanaofuatilia matumizi ya mitandao ya kijamii</p> <p>Watoa huduma za IT, wakaguzi, mashirika ya matangazo, watoa huduma za kodi nk</p> <p>Mashirika ya utekelezaji wa sheria</p> <p>Kampuni au mashirika ya sheria kwa madhumuni ya kutoa ushauri wa kisheria au uwakili</p> <p>Watoa huduma za utafiti</p> <p>Wasimamizi na mamlaka za serikali, wachunguzi maalum au mamlaka za kodi</p>
Teknolojia ya ufuatiliaj na vidakuvi	<p>Hutumia vidakuvi kwa madhumuni yafuatayo:</p> <p>Uthibitishaji wa watumiaji</p> <p>Kufuatilia hali ya matumizi ya tovuti na mtumiaji (yaani, ikiwa mtumiaji ameingia kwenye tovuti)</p> <p>Kufanya tovuti ifae watumiaji</p> <p>Kulinda akaunti ya mtumiaji na uzuaji wa shughuli za kilaghai za kuingia katika akaunti</p> <p>Kutoa matangazo</p> <p>Kufanya uchanganuzi wa utendakazi wa tovuti</p>
Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji/ Uhamishaji wa data nje ya nchi	<p>Huomba idhini ya mtumiaji katika matukio ambapo data inachakatwa nje ya nchi.</p> <p>Wakati ambapo seva au watoa huduma wanapatikana nje ya nchi, au wakati ambapo seva zinapatikana nje ya nchi ya Afrika Kusini, Niftycredit itaomba mmiliki wa data inayohamishwa akubali kanuni na desturi zake za faragha.</p>

## **Uchanganuzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu za Mifumo ya Mtandaoni ya Kukopesha Pesa**

### **Uwajibikaji**

Sheria ya Ulinzi wa Data ya Binafsi (Protection of Personal Information Act (POPI Act)<sup>413</sup> inahitaji mifumo ya mtandaoni ya kukopesha pesa, mionganini mwa mashirika mengine, ya kuchakata data ya binafsi ihakikishe uwajibikaji inapochakata data. Inahitaji hasa itii masharti yaliyobainishwa kwenye Sheria ya uchakataji halali wa data. Masharti haya lazima yatumike wakati wa kubainisha madhumuni na njia za uchakataji wa data ya binafsi.<sup>414</sup> Masharti haya yanajumuisha uwajibikaji, uzuiaji wa uchakataji, ubainishaji wa madhumuni, uzuiaji wa uchakataji wa ziada, ubora wa maelezo, uwazi, mbinu za ulinzi na kushirikishwa kwa mmiliki wa data, kama inavyobainishwa kwenye vifungu vifuatavyo.<sup>415</sup>

### **Uzuiaji wa Uchakataji**

Masharti haya yanahusisha kanuni kadhaa.<sup>416</sup> Kwanza, yanahitaji data ya binafsi kuchakatwa kisheria na kwa njia inayofaa, bila kuingilia haki ya faragha ya mmiliki wa data.<sup>417</sup> Pili, yanahitaji data ya binafsi kukusanya moja kwa moja kutoka kwa mmiliki wa data, isipokuwa katika hali maalum zilizobainishwa kwenye Sheria.<sup>418</sup> Tatu, yanahitaji data ya binafsi ichakatwe kwa madhumuni yanayohusiana na ukusanyaji wake na kuwa data hiyo inapaswa kuwa ya kutosha, inayohusika na isiyo ya ziada. Hatimaye, masharti haya yanahitaji kuwa ukusanyaji huo wa data utegemee idhini ya mtumiaji, na kutolewa kwa thibitisho thabiti la uchakataji. Mtumiaji ana haki ya kukataa uchakataji huo.<sup>419</sup>

Uchunguzi wa mifumo ya mtandaoni ya kukopesha pesa inayochunguzwa kwenye utafiti huu unabainisha kwamba kampuni za kutoa mikopo hukusanya kiotomatiki data ya binafsi mara tu mtumiaji anapotumia tovuti, kuwasilisha maelezo wakati wa kujisajili au kutumia bidhaa. Watumiaji wasioidhinisha/ kukataa data yao isichakatwe hushauriwa waache kutumia tovuti hizi na hunyimwa kiotomatiki uwezo wa kutumia bidhaa zinazotolewa na tovuti hizi. Katika hali hii, inaweza kusemekana kuwa mtumiaji hatoi idhini yake kwa hiani, lakini mtumiaji anahitaji kutumia bidhaa husika.

Baadhi ya mifumo inayochunguzwa hukusanya maelezo yasiyohusika na madhumuni ya uchakataji huo. Niftycredit, kwa mfano, hukusanya maelezo kama vile historia ya ajira ya mtumiaji, uzoefu, maelezo ya akaunti ya benki na rekodi za mazungumzo ya simu, ambayo hayahusiani na madhumuni ya huduma ya kutoa mikopo.<sup>420</sup> Lulalend, kwa upande mwingine, hukusanya maelezo kama vile asili ya kijamii ya mtumiaji, mitazamo/ maoni ya binafsi, na mitazamo/ maoni ya binafsi ya watu wengine kuhusu mtumiaji, ambayo hayahusiki na madhumuni.<sup>421</sup>

Lulalend inatii masharti ya kukusanya maelezo ya mtumiaji moja kwa moja kutoka kwa mtumiaji na inabainisha hali maalum zinazolingana na Sheria ya POPI ambapo huenda masharti yasifuatwe.<sup>422</sup>

### **Kuhifadhiwa kwa Data**

Mifumo ya mtandaoni ya kukopesha pesa inapaswa chini ya Sheria ya POPI kutohifadhi

413 Sheria ya Ulinzi wa Maelezo ya Binafsi (Protection of Personal Information Act (POPI Act), Sheria ya 4 ya 2013 <https://popia.co.za/>

414 Kifungu cha 4 (1) (a) cha Sheria ya POPI

415 Kifungu cha 4 cha Sheria ya POPI

416 Kifungu cha 4 (1) (b) cha Sheria ya POPI

417 Kifungu cha 4 (1) (9) cha Sheria ya POPI

418 Kifungu cha 12 cha Sheria ya POPI

419 Kifungu cha 11 cha Sheria ya POPI

420 Sera ya Faragha ya Programu ya Nifty Credit <https://niftycredit.co.za/za/terms-and-conditions>

421 Sera ya Faragha ya Programu ya Lulalend <https://www.lulalend.co.za/PrivacyPolicy>

422 Sera ya Faragha ya Programu ya Lulalend <https://www.lulalend.co.za/PrivacyPolicy>

data ya binafsi kwa muda mnefu kuliko jinsi inavyohitajika kwa ajili ya kutimiza madhumuni ya ukusanyaji.<sup>423</sup> Inaeleza kwamba kampuni itahifadhi tu data ya binafsi kwa muda mnefu zaidi ikiwa sheria inaihitaji. Ikiwa mfumo wa kukopesha pesa unaihitaji kwa madhumuni ya kisheria, mkataba kati ya wahusika unahuishisha data kuhifadhiwa au ikiwa mmiliki wa data ataidhinisha<sup>424</sup>.

Mifumo iliyokaguliwa kwenye utafiti huu inabainisha kanuni hii katika sera zake za faragha, inayobainisha moja kwa moja kuwa kampuni itafuta data ya watumiaji baada ya madhumuni ya ukusanyaji huo kutimizwa.<sup>425</sup> Hata hivyo, mifumo mingine kama vile Fundrr na Nifty Credit inahitaji watumiaji waombe kufutwa kwa maelezo yao. Kwa upande mwingine, mfumo wa Pollen Finance hautaji kanuni hii kwenye Sera yake Faragha, na si wazi iwapo inatii kanuni hii.

## **Mbinu za Ulinzi**

Sheria ya POPI inahitaji mifumo hii ya mtandaoni ya kukopesha pesa kudumisha uadilifu na usiri wa maelezo ya binafsi inayohifadhi kwa kuweka mbinu mwafaka, zinazofaa, za kiufundi na kishirika za kuzuia; kupotea, kuharibika au kuharibiwa kwa data ya binafsi bila idhini na ufikiaji wa maelezo ya siri kinyume cha sheria.<sup>426</sup> Pamoja na haya, inaongeza kwamba mifumo hii inapaswa kuweka mbinu zinazofaa za: kutambua hatari zote zinazoweza kujitekeza kwa maelezo ya binafsi, kudumisha mbinu za ulinzi zinazofaa dhidi ya hatari zilizotambulika, kuthibitisha kuwa mbinu hizo za ulinzi zinatekelezwa, na kuhakikisha kuwa mbinu hizo za ulinzi zinasasishwa mana kwa mara ili kushughulikia hatari mpya zinazojitekeza.<sup>427</sup> Wakati ambapo tukio la ufichuzi haramu wa data limetokea, mifumo hii inapaswa kujulisha Usimamizi na mmiliki wa data.<sup>428</sup> Kuhusu suala la uchakataji wa maelezo ya binafsi na wahusika wengine kwa niaba ya mifumo hii, Sheria inawahitaji; kuchakata data hiyo kwa idhini ya mifumo hii na kushughulikia data hiyo kama data ya siri.<sup>429</sup> Mifumo ya Lulalend na Nifty credit inaonekana kuwa imejumuisha mbinu hizi kwenye sera zake za faragha kati ya mifumo inayochunguzwa kwenye utafiti huu. Sera za faragha za mifumo ya Fundrr na Pollen Finance, kwa upande mwingine, zinaahidi tu kuhakikisha usalama wa data ya binafsi lakini hazibainishi kwa watumiaji mbinu za ulinzi ambazo mifumo hii itaweka ili kuhakikisha usiri wa maelezo yao ya binafsi.

## **Haki za Mtumiaji na Kushiriki**

Wamiliki wa data wamepewa haki kuhusiana na data yao. Kimahususi, wana haki ya kufikia maelezo yao ya binafsi<sup>430</sup> na haki ya kuomba yarekebishwe<sup>431</sup>. Sheria inatoa zaidi uwezo wa kufikia maelezo kama ilivyobainishwa kwenye vifungu vya Sheria ya Haki ya Kufikia Maelezo (Promotion of Access to Information Act (PAIA)).<sup>432</sup>

Mifumo hii inawapa watumiaji funsa ya kufikia, kurekebisha na kusasisha maelezo yao ya binafsi. Inatoa pia njia (yaani, maelezo ya mawasiliano) za jinsi ya kufanya hivyo. Mifumo hii inawaruhusu zaidi watumiaji kuelezea masuala yao na kuwasilisha malalamiko.

## **Chaguo la Kujiiondoa**

Kulingana na masharti ya kutoa idhini chini ya Sheria ya POPIA kuhusu kutoa matangazo kwa njia ya kielektroniki<sup>433</sup> Mifumo yote inayochunguzwa inawapa watumiaji chaguo la kujiiondoa kwenye huduma ya kupokea ujumbe wa matangazo.

423 Kifungu cha 14 cha Sheria ya POPI

424 Kifungu cha 14 (1) cha Sheria ya POPI

425 Sera ya Faragha ya Programu ya Lulalend <https://www.lulalend.co.za/PrivacyPolicy>

426 Kifungu cha 19 cha Sheria ya POPI

427 Kifungu cha 19 (2) cha Sheria ya POPI

428 Kifungu cha 22 (1) cha Sheria ya POPI

429 Kifungu cha 21 (1) cha Sheria ya POPI

430 Kifungu cha 23 cha Sheria ya POPI

431 Kifungu cha 24 cha Sheria ya POPI


432 Kifungu cha 25 cha Sheria ya POPI

433 Kifungu cha 69 cha Sheria ya POPI

## **Hitimisho**

Kwa kuhitimisha, Sera za Faragha za baadhi ya mifumo inayochunguzwa zinatii Sheria ya POPIA. Hata hivyo, utifufu huu unapatikana tu katika kiwango cha sera. Tunasubiri kuona iwapo mifumo hii itatii Sheria ya POPIA katika hali halisi, ikizingatiwa kuwa ilianza kufanya kazi mnamo tarehe 1 Juni.

# Tanzania



## Maelezo ya Nchi

Ikiwa inapatikana katika eneo la Afrika Mashariki, Muungano wa Jamhuri ya Tanzania unapakana na Bahari Hindi upande wa mashariki. Inapakana na nchi nane: (katika mzunguko wa kinyume cha saa kutoka kaskazini) Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (ukivuka Ziwa Tanganyika), Zambia, Malawi na Msumbiji. Nchi hii inajumuisha kisiwa cha Zanzibar (kisiwa kikuu cha Unguja, pamoja na Pemba na visiwa vingine vidogo).<sup>434</sup> Idadi ya watu katika nchi hii inakadiriwa kuwa 59,734,210 kufikia mwaka wa 2020.<sup>435</sup>

434 <https://www.eac.int/eac-partner-states/tanzania>

435 <https://data.worldbank.org/indicator/SP.POP.TOTL?locations=TZ>

## Ulinzi wa Data Nchini Tanzania

Mwaka wa 2014, kampuni ya Vodacom Tanzania ilikuwa kampuni ya kwanza kuanzisha mfumo wa teknolojia ya fedha nchini Tanzania. Mabadiliko haya yalitokea wakati kampuni hii iliposhirikiana na Benki ya Biashara ya Afrika (Commercial Bank of Africa) - CBA (Kwa sasa inajulikana kama NCBA), ili kuanzisha huduma ya MPawa, huduma mpya ya benki inayoruhusu wateja wa Vodacom kuweka akiba kupitia simu zao, kupata riba kutokana na akiba yao kisha hatimaye kupata mikopo midogo.<sup>436</sup>

Tangu wakati huo, mfumo wa teknolojia ya fedha nchini Tanzania umekuwa ukiimanika kwa kasi, hali ambayo imesababisha kuongezeka na umaarufu wa Programu za fedha kwa wateja.

Zaidi ya asilimia 54 ya idadi ya watu nchini Tanzania hutumia huduma za malipo ya simu na shughuli za kutuma na kupokea pesa kupitia simu za mkononi.<sup>437</sup>

Taasisi za kawaida za benki, taasisi zisizo za benki na Watoa Huduma za Mtando wa Simu (Mobile Network Operators - MNO (na pochi zao dijitali) wameanzisha Programu zao za simu za mkononi za mikopo dijitali baada ya muda. Hizi ni pamoja na, wala si tu; TigoPesa Nivushe,<sup>438</sup> Branch,<sup>439</sup> Halotel Haloyako,<sup>440</sup> nk.

436 <https://www.vodacom.co.tz/mpawa>

437 <https://www.statista.com/statistics/1082056/tanzania-mobile-money-transaction-value/>

438 <https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-nivushe>

439 <https://branch.co.tz>

440 <https://halotel.co.tz/package-mobile/1552657603579>

Tanzania ikiwa haina sheria ya Ulinzi wa Data na Faragha,<sup>441</sup> hali ya utekaji ya baadhi ya Programu hizi inaweza kuhatarisha faragha na data ya binafsi ya watumiaji.

## Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali

Vodacom MPawa <sup>442</sup>	Data inayokusanywa na kuchakatwa na Programu
Ruhusa za programu zinazotakikana	<p>Programu hii inaweza kufikia:</p> <p>Anwani za simu Data ya mahali (inayotokana na GPS na mtandao) SMS za mtumiaji Hali ya simu na utambulisho Maudhui ya hifadhi ya kifaa Kamera Kitambulisho cha kifaa na maelezo ya mazungumzo ya simu Miunganisho ya mitandao</p>
Data ya Mtumiaji Inayokusanywa	<p>Panapohitajika:</p> <p>Jina, anwani, nambari ya simu na ya simu ya mkononi, tarehe ya kuzaliwa, jinsia na anwani ya barua pepe; Maelezo ya kadi ya benki au mikopo, maelezo kuhusu akaunti ya benki na maelezo mengine ya benki</p>
Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	<p>Kitambulisho cha kifaa Data ya kutembelea tovuti. Data ya mahali; Data ya Global Positioning System (GPS) / mitandaopepe ya Wi-Fi /anwani ya IP au maelezo kama vile msimbo wa posta au jina la mji au jiji;</p>
Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Rekodi za mikopo
Jinsi programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	<p>Kushughulikia maagizo na kutoa bidhaa na huduma kwa mtumiaji Kuboresha na kubuni bidhaa na huduma Kuonyesha matangazo na kufanya huduma zimfae mtumiaji Kuchunguza historia (kwa madhumuni ya kutoa mikopo, ulaghai na usalama)</p>

441 <https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/usalama-taanifa-binafsi-shakani-3006726>

442 <https://www.vodacom.co.tz/mpawa>

	Kushiriki data na Wahusika wengine	Panapohitajika, Vodacom hushiriki maelezo na: Kampuni za Vodacom Group Washirika au maajenti wanaohusika katika utoaji wa bidhaa na huduma zilizoagizwa au zinazotumika; Kampuni zinazohusika katika utoaji wa huduma za, au kwa niaba ya, kampuni za Vodacom Tanzania Public Limited Company, Vodacom Group au Vodafone Group; Mashirika ya rekodi za mikopo, uzuiaji wa ulaghai au kutoa alama za biashara, au mashirika mengine ya kutoa alama za mikopo; Mashirika ya ukusanyaji wa madeni au mashirika mengine ya kudai madeni; Mashirika ya utekelezaji wa sheria, mashirika ya serikali, mashirika ya usimamizi, mahakama au mamlaka zingine za umma ikiwa ni lazima tufanye hivyo, au tumeidhinishwa na sheria; Mhusika mwengine au shirika ambapo ufichuzi huo unaohitajika ili kutimiza sheria yoyote husika au masharti mengine ya kisheria au usimamizi; Huduma za dharura (ukipiga simu ya dharura), ikijumuisha data ya mahali ambapo si mahususi; Wahusika wengine kwa ajili ya kutoa matangazo ya pamoja na wahusika hao;
	Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuzi vya tovuti	GPS / Vidakuzi vya tovuti
	Jinsi programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Data ya binafsi huhifadhiwa nchini Tanzania

TigoPesa Nivushe <sup>443</sup>	Data inayokusanywa na kuchakatwa na programu	
	Ruhusa za programu zinazotakikana	Programu hii inaweza kufikia:  Anwani za simu Data ya mahali (inayotokana na GPS na mtandao) SMS za mtumiaji Hali ya simu na utambulisho Maudhui ya hifadhi ya kifaa Kamera Kitambulisho cha kifaa na maelezo ya mazungumzo ya simu Miunganisho ya mitandao
	Data ya Mtumiaji Inayokusanywa	maelezo ya usajili: Jina kamili la mtumiaji, umri, nambari ya simu, anwani ya barua pepe, anwani ya barua, maelezo ya malipo, anwani ya malipo au jina la mtumiaji na nenosiri.

	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	maelezo kuhusu mahali mtumiaji alipo. Maelezo ya programu ya simu za mkononi hutokana na tovuti zilizotembelewa na programu zilizopakuliwa kutoka kwenye mtandao wa Tigo. Maelezo kuhusu matumizi ya Tovuti: anwani ya mtandao na mfumo wa uendeshaji wa kompyuta, aina ya kivinjari kilichotumiwa, tovuti ambayo mtu alitumia kuunganisha kwenye tovuti, shughuli za mtumiaji kwenye Tovuti, pamoja na historia ya kivinjari ya mtumiaji, saa na tarehe alipotembelea tovuti na kununua bidhaa na huduma kupitia Tovuti.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Rekodi za mikopo
	Jinsi programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kubainisha matumizi, kufanya matengenezo na maboresho ya huduma, Kutoa huduma kwa wateja, kufanya maudhui, huduma na bidhaa ziwafae watumiaji, kubuni mipango ya biashara, kutathmini hali ya kuridhishwa kwa wateja, kuunda hifadhidata, kufanya uchanganuzi wa maelezo na data, kubuni programu za viashirio vikuu vya utendaji (KPI), kutuma bili, kutoa ulinzi, kudhibiti ubora na, kwa ujumla, maelezo yote yanayohitajika ili kutii mikataba ya bidhaa au huduma za Tigo, pamoja na sheria na kanuni husika Kutoa ofa, matangazo, bidhaa, nafasi za kazi, mashindano ya bahati nasibu ya fedha, kampeni, mipango ya uaminifu, kudumisha wateja
	Kushiriki data na Wahusika wengine	Programu ya Tigo hushiriki data ya binafsi na: Wahusika wengine ambao hutoa huduma kwa Tigo kama vile huduma za kuhifadhi, kukamilisha agizo, ukusanyaji na usafirishaji wa bidhaa, kufanya tafiti, kutoa huduma kwa wateja au kutoa matangazo Mashirika ya utekelezaji wa sheria Mashirika mengine ya Tigo, au katika tukio la muungano, ununuza, uuzaaji wa mali za kampuni, au kuhamishia huduma kwa mtoa huduma mwengine Nchi zingine ambazo zina sheria za ulinzi wa data tofauti na zile zinazotumika nchini Tanzania, kwa agizo la maandishi la mamlaka ya kisheria inayotambulika au panaporuhusiwa kulingana na sheria
	Teknolojia za ufuatilaji/vidakuzi vya tovuti	GPS / Vidakuzi vya tovuti
	Jinsi programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Kimsingi data ya binafsi huhifadhiwa nchini Tanzania lakini inaweza kuhamishiwa kwenye nchi zingine ambazo zina sheria za ulinzi wa data tofauti na zile zinazotumika nchini Tanzania kwa agizo la maandishi la mamlaka ya kisheria inayotambulika au panaporuhusiwa kulingana na sheria.

Branch Tanzania <sup>444</sup>	Data inayokusanya na kuchakatwa na programu	
	Ruhusa za programu zinazotakikana	<p>Programu hii inaweza kufikia:</p> <p>Anwani za simu</p> <p>Data ya mahali (inayotokana na GPS na mtandao)</p> <p>SMS za mtumiaji</p> <p>Hali ya simu na utambulisho</p> <p>Maudhui ya hifadhi ya kifaa</p> <p>Kamera</p> <p>Kitambulisho cha kifaa na maelezo ya mazungumzo ya simu</p> <p>Miunganisho ya mitandao</p>
	Data ya Mtumiaji Inayokusanya	Jina, anwani, anwani ya barua pepe na nambari ya simu, nambari ya simu ya kifaa, maelezo ya SIM kadi, umri, jina la mtumiaji, nenosiri na maelezo mengine ya usajili, maelezo ya fedha na mikopo (ikijumuisha maelezo ya akaunti ya huduma ya kutuma na kupokea pesa kuititia simu, maelezo ya akaunti ya benki, na nambari ya uthibitishaji wa benki), maelezo ya binafsi na picha.
	Maelezo yanayokusanya kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	<p>Maelezo ya kiufundi, ikijumuisha aina ya simu, vitambulisho maalum vya kifaa (kwa mfano, IMEI ya Kifaa cha mtumiaji au nambari ya kitambulisho), maelezo kuhusu SIM kadi inayotumiwa na kifaa, maelezo ya mtandao wa simu, mfumo wa uendeshaji wa kifaa chako, aina ya kivinjani, au data ya mahali ya kifaa na mipangilio ya saa za eneo (Maelezo ya Kifaa);</p> <p>Maelezo yaliyohifadhiwa kwenye Kifaa cha mtumiaji, ikijumuisha orodha za anwani za mawasiliano, rekodi za nambari za simu, rekodi za SMS, marafiki wa Facebook, orodha za anwani za mawasiliano kutoka kwenye akaunti zingine za mitandao ya kijamii, picha, video au maudhui mengine dijitali (Maelezo ya Maudhui);</p> <p>Data inayotokana na matumizi ya programu nyingine yoyote ya mhusika mwingine kwenye Kifaa au Tovuti za Huduma</p>
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Mashirika ya rekodi za mikopo na watoa huduma za mtandao wa simu
	Jinsi programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	<p>Maelezo yanayokusanya hutumiwa kubainisha ustahiki wa mteja, kiasi cha mkopo husika, na sheria na masharti yanayotumika kwa mkopo huo.</p> <p>Panapohitajika:</p> <p>Kwa kutii agizo la Mahakama, Jopo la Upatanishi, Mahakama, Agizo au Amni ya Usimamizi au wajibu mwingine wowote wa kisheria au usimamizi</p>

	Kushiriki data na Wahusika wengine	Programu ya Branch hushiriki data ya binafsi na: Ofisi za rekodi za mikopo Mwanachama yeote wa kikundi cha Branch, yaani, mashirika tanzu, washirika, kampuni ya hisa na kampuni zake tanzu Mamlaka zozote za kisheria au usimamizi kama inavyotakikana
	Teknolojia za ufuatilaji/ vidakuvi vya tovuti	GPS / Vidakuvi vya tovuti
	Jinsi programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Data inaweza kuhamishiwa kwenye, na kuhifadhiwa katika, nchi nyingine (kama inavyohusika). Inaweza pia kuchakatwa na wafanyakazi wa nje ya nchi ya Tanzania (ipasavyo)
Halotel Haloyako <sup>445</sup>	Data inayokusanywa na kuchakatwa na programu	
	Ruhusa za programu zinazotakikana	Programu hii inaweza kufikia:  Anwani za simu Data ya mahali (inayotokana na GPS na mtandao) SMS za mtumiaji Hali ya simu na utambulisho Maudhui ya hifadhi ya kifaa Kamera Kitambulisho cha kifaa na maelezo ya mazungumzo ya simu Miunganisho ya mitandao
	Data ya Mtumiaji Inayokusanywa	Jina, tarehe ya kuzaliwa, anwani, aina na nambari ya hati ya kitambulisho, mahali pa kuzaliwa na utaifa, hali ya ndoa, maelezo ya akaunti, barua pepe nk.
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	maelezo kuhusu mahali mtumiaji alipo.
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Rekodi za mikopo

	Jinsi programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kushughulikia bidhaa na huduma zilizonuliwa kutoka kwenye Halotel Kutoa huduma au bidhaa husika kwa watumiaji Kutoza mtumiaji kwa kutumia bidhaa au huduma zetu. Kufahamisha mtumiaji kuhusu bidhaa na huduma zingine za kampuni ambazo zinaweza kumvutia Kufanya utafiti na uchanganuzi wa kitakwimu, ikijumuisha kufuatilia jinsi wateja wanavyotumia bidhaa na huduma kwa msingi wa kibinagsi au kutotambulishwa. Kuzuia na kugundua ulaghai au uhalifu mwингine, kudai madeni au kufuatilia wenyе madeni ya Halotel money. Kutoa ripoti zilizojumlishwa kwa wahusika wengine
	Kushiriki data na Wahusika wengine	Washirika au maajenti wanaohusika katika utoaji wa bidhaa na huduma ambazo umeagiza au unatumia; Washirika au maajenti ambaо hufanya tafiti za kutathmini kiwango cha kuridhishwa kwa wateja na tafiti zingine zozote zinazohusiana na bidhaa au huduma zinazotolewa kwa mtumiaji Kampuni ambazo zinahusika na utoaji wa huduma kwa ajili ya, au kwa niaba ya HaloPesa au Halotel Tanzania. Panapowezekana, mashirika ya nekodi za mikopo, uzuiaji wa ulaghai, mashirika ya kutoa alama za biashara au mashirika mengine ya kutoa alama za mikopo. Mashirika ya ukusanyaji wa madeni au mashirika mengine ya kudai madeni. Mashirika ya utekelezaji wa sheria, mashirika ya usimamizi, mahakama au mamlaka za umma ikiwa ni lazima tufanye hivyo, au tumeidhinishwa na sheria. Huduma za dharura (ikiwa simu ya dharura ya itapigwa)
	Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuzi vya tovuti	GPS / Vidakuzi vya tovuti
	Jinsi programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Data ya binafsi hushughulikiwa na shirika la Halotel nchini Tanzania lakini inaweza kuchakatwa na mashirika mengine yaliyo na wajibu wa kimkataba na shirika la HaloPesa au Halotel Tanzania kulingana na sheria.

## **Uchanganuzi wa Programu za Mikopo ya Kulipwa Siku ya Kupokea Mshahara kwa Kuzingatia Mfumo wa Usimamizi**

Ingawa Tanzania haina Sheria ya ulinzi wa data, Katiba ya Muungano wa Jamhuri ya Tanzania (Constitution of the United Republic of Tanzania), ya mwaka wa 1977 ("Katiba"), haitoi hakikisho la haki ya faragha na usalama wa binafsi.<sup>446</sup> Vifungu vya 98 na 99 vya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Barua (The Electronic and Postal Communications Act) ya mwaka wa 2010 ("EPOCA") inaweka wajibu wa kudumisha usiri wa maelezo kwa watoa huduma za mtandao waliodhinishwa na hairuhusu ufichuzi wa maelezo hayo bila idhini, vile vile.<sup>447</sup> Kwa upande wake, Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Barua (Ulinzi wa Mteja) za mwaka wa 2018 zinahitaji mtoa huduma aliyeidhinishwa kulinda maelezo ya mteja dhidi ya

446 Kifungu cha 16, Katiba ya Muungano wa Jamhuri ya Tanzania (Constitution of the United Republic of Tanzania (1977) <https://rsf.org/sites/default/files/constitution.pdf>

447 Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Barua (Electronic and Postal Communications Act) ya mwaka wa 2010 ("EPOCA") [https://www.tcra.go.tz/uploads/documents/sw-1619082940-The%20Electronic%20and%20Postal%20Communications%20Act,%202010%20\(Act%20No.%203%20out%20of%2010\).pdf](https://www.tcra.go.tz/uploads/documents/sw-1619082940-The%20Electronic%20and%20Postal%20Communications%20Act,%202010%20(Act%20No.%203%20out%20of%2010).pdf)

kufichuliwa kwa njia isiyofaa au bila kukusudiwa.<sup>448</sup>

Sheria ya Mifumo ya Kitaifa ya Malipo (National Payment Systems (NPS) ya mwaka wa 2015 na Sheria ya Benki ya Tanzania (Bank of Tanzania Act) ya mwaka wa 2006 inaipa mamlaka Benki ya Tanzania (Bank of Tanzania (BoT) kudhibiti na kusimamia huduma za mifumo ya malipo na bidhaa zinazotolewa na taasisi za benki na taasisi zisizo za benki chini Tanzania.<sup>449</sup>

## **Haki ya Faragha**

Kila Programu ya mikopo dijitali iliyochunguzwa huomba ruhusa ya kufikia anwani za simu za mtumiaji, data ya mahali, SMS za mtumiaji na ruhusa zingine. Ruhusa hizi huhatarisha faragha ya watumiaji wa Programu hizi ikiwa zitapatikana na wadhibiti laghai wa data.

## **Uwazi**

Ni dhahiri kwamba sera za faragha za Programu zina uwazi, kwa sababu zinabainisha kwa uwazi aina ya maelezo zinazokusanya kutoka kwa watumiaji, sababu ya ukusanyaji, zinaoshiriki nao data iliyokusanya na sababu, na iwapo data hiyo inashirikiwa ndani au nje ya nchi ya mtumiaji.

## **Haki ya Ufikiaji na Ufutaji wa Data ya Binafsi**

Ingawa watumiaji wa Programu hizi wanaweza kuomba data yao irekebishwe na wadhibiti wa data, suala la haki ya kufutwa kwa data yao si bayana katika baadhi ya Programu hizi.<sup>450</sup> Vodacom ndio kampuni pekee ambayo inajaribu kushughulikia suala la Haki ya Ufikiaji katika ratiba yake ya kipindi cha kuhifadhi data. Kulingana na kampuni ya Vodacom, maelezo ya mtumiaji huhifadhiwa kwa kipindi cha kutekelezwa kwa mkataba wa mtumiaji au kama inavyohitajika kisheria. Kisha kampuni ya Vodacom hufuta data ya mtumiaji baadaye.<sup>451</sup>

---

448 Kifungu cha 6 (1) na (2) [https://www.tanzania.go.tz/egov\\_uploads/documents/EPO%20consumer%20Protection%20Regulations%202011.pdf](https://www.tanzania.go.tz/egov_uploads/documents/EPO%20consumer%20Protection%20Regulations%202011.pdf)

449 <https://www.bot.go.tz/PaymentSystem>

450 Kifungu cha 93(4) cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Barua (Electronic & Postal Communications Act) [https://www.tcra.go.tz/uploads/documents/sw-1619082940\\_The%20Electronic%20and%20Postal%20Communications%20Act,%202010%20\(Act%20No.%203%20out%20of%2010\).pdf](https://www.tcra.go.tz/uploads/documents/sw-1619082940_The%20Electronic%20and%20Postal%20Communications%20Act,%202010%20(Act%20No.%203%20out%20of%2010).pdf)

451 <https://www.vodacom.co.tz/public/assets/files/Vodacom%20Tz-%20%20Customer%20Privacy%20Statement-retention-schedule.pdf>



# Uganda



## Maelezo ya Nchi

Ikiwa inapatikana katika eneo la Afrika Mashariki, Uganda ni nchi isiyo na bandari inayopatikana karibu na mstari wa ikweta. Inapakana na (mwelekeo wa saa kutoka kaskazini) Sudan, Kenya, Muungano wa Jamhuri ya Tanzania, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.<sup>452</sup> Nchi hii ina idadi inayokadiriwa ya watu milioni 39.0<sup>453</sup>

452 EAC <https://www.eac.int/eac-partner-states/uganda>  
 453 <https://www.eac.int/component/documentmananger/?task=download.document&file=bWFpbj9kb2N1bVVudHNfcGRmXOV2cFVzSHI3RUF6dUhnS2hXc3RkVkJNRUF DIEZhY3RzlEZpZ3VyZXMcMjAxOQ==&counter=575>

## Ulinzi wa Data Nchini Uganda

Uganda inajivunia sekta inayonawiri na kukua kwa haraka ya ICT, ambapo zaidi ya nusu ya idadi yake ya watu hutumia simu za mkononi. Uganda ina shirika huru la kisheria linalojulikana kama Mamlaka ya Kitaifa ya Teknolojia ya Mawasiliano-Uganda (National Information Technology Authority-Uganda (NITA-U), lilianzishwa chini ya Sheria ya NITA-U ya mwaka wa 2009. Jukumu lake ni kusimamia na kudhibiti huduma za Teknolojia ya Mawasiliano nchini Uganda. Data kutoka kwa shirika la NITA-U inaonyesha kuwa simu mahiri na simu za vipengele zenye uwezo wa kufikia intaneti moja kwa moja zinasalia kuwa kigezo cha wateja wapya kujisajili kwenye huduma za intaneti. Idadi ya usajili imeongezeka kutoka simu mahiri na simu za vipengele milioni 21.5 katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19 hadi karibu milioni 24.1 katika Mwaka wa Fedha wa 2019/20.<sup>454</sup>

Mikopo dijitali, dhana ambayo inakita mizizi kwa kasi katika eneo la Afrika Mashariki, imewezesha wateja wa simu za mkononi kufikia haraka kwa urahisi mashirika ya kutoa mikopo. MTN, ambayo ni kampuni kubwa zaidi ya huduma za mawasiliano ya simu za mkononi nchini, kwa ushirikiano na Benki ya Biashara ya Afrika (Commercial Bank of Africa (CBA) – ambayo kwa sasa inajulikana kama NCBA - ilianzisha huduma ya MoKash, huduma dijitali inayowezesha kupata mikopo kupitia simu za mkononi, mwaka wa 2016<sup>455</sup>.

Kutokana na mahitaji ya mteja ya kupata huduma zaidi za kuweka akiba na kupokea mikopo, MoKash alijifunza kutokana na huduma kama hizo zilizoanzishwa na mafanikio ya huduma ya M-shwari nchini Kenya mwaka wa 2012 na M-Pawa katika Muungano wa Jamhuri ya Tanzania mwaka wa 2014.<sup>456</sup>

454 NITA <https://www.nita.go.ug/publication/nita-u-statistical-abstract-2020>

455 <https://techweez.com/2016/08/10/cba-partners-mtn-launching-mokash-m-shwari-equivalent-uganda/> accessed 18 July 2021  
 456 <https://www.uncdf.org/article/2844/disrupting-savings-lending-market-uganda-mokash ilifikiwa tarehe 20 Jula 2021>

Baada ya kuanzishwa kwa huduma ya MoKash, wateja 83,000 walijisajili ndani ya saa 48 za kwanza, 650,000 baada ya mwezi mmoja na zaidi ya 1,000,000 ndani ya miezi mitatu,<sup>457</sup> na kushinda rekodi za awali zilizowekwa na huduma mwenzi za M-Shwari nchini Kenya (wateja 645,000 ndani ya siku 21 baada ya kuanzishwa) na M-Pawa katika Muungano wa Jamhuri ya Tanzania (wateja 250,000 ndani ya mwezi wa kwanza).<sup>458</sup>

Mfumo wa Teknolojia ya fedha unaonawini (Fintech) nchini Uganda umesababisha kufurika kwa Programu za mikopo ya kulipwa siku ya mshahara. Kando na Programu ya MoKash ya MTN, Programu zingine maarufu zinajumuisha Programu ya Wewole ya Airtel, Money Mate Uganda na Numida Business Loans miongoni mwa zingine.

### **Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali**

MTN MoKash <sup>459</sup>	Data inayokusanywa na kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa za programu zinazotakikana	Programu hii inaweza kufikia:  Anwani za simu Data ya mahali (inayotokana na GPS na mtandao) SMS za mtumiaji Hali ya simu na utambulisho Maudhui ya hifadhi ya kifaa Kamera Kitambulisho cha kifaa na maelezo ya mazungumzo ya simu Miunganisho ya mitandao
	Data ya Mtumiaji Inayokusanywa	Jina, nambari ya kitambulisho, anwani ya mahali, tarehe ya kuzaliwa, utaifa, anwani ya barua pepe, nambari za simu
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	nambari ya kitambulisho cha kituo cha simu Mfumo wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu (Global System for Mobile telecommunication (“GSM”))
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Rekodi za mikopo
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kushughulikia maagizo na kutoa bidhaa na huduma kwa mtumiaji Kuonyesha matangazo na kufanya huduma zimfae mtumiaji
	Kushiriki data na Wahusika wengine	Washirika au maajenti wanaohusika katika utoaji wa bidhaa na huduma; Mashirika ya rekodi za mikopo, uzuaji wa ulaghai au kutoa alama za biashara; Mashirika ya utekelezaji wa sheria, mashirika ya serikali, mashirika ya usimamizi, mahakama au mamlaka zingine za umma ikiwa inahitajika, au ikiwa imeidhinishwa na sheria;

457 <https://www.unCDF.org/article/1675/three-months-down-the-road-the-story-of-mokash-in-uganda-migration> ilifikiwa tarehe 20 Julai 2021

458 Ibid.

459 <https://www.mtn.co.ug/mtn-momo/>

	Teknolojia za ufuutiliaji/ vidakuzi vya tovuti	GPS / Vidakuzi vya tovuti
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Data ya binafsi huhifadhiwa nchini Uganda
AirtelMoney Wewole <sup>460</sup>	Data inayokusanywa na kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa za programu zinazotakikana	Programu hii inaweza kufikia:  Anwani za simu Data ya mahali (inayotokana na GPS na mtandao) SMS za mtumiaji Hali ya simu na utambulisho Maudhui ya hifadhi ya kifaa Kamera Kitambulisho cha kifaa na maelezo ya mazungumzo ya simu Miunganisho ya mitandao
	Data ya Mtumiaji Inayokusanywa	Jina, nambari ya kitambulisho, anwani ya mahali, tarehe ya kuzaliwa, utaifa, nambari ya simu
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Nambari Dijitali ya Huduma za Muunganisho wa Mteja wa Simu ya Mkononi (Mobile Subscriber Integration Services Digital Number), na nambari husika ya kitambulisho na PUK ya ufikiaji wa Mtandao wa Airtel
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Rekodi za mikopo
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kushughulikia maagizo na kutoa bidhaa na huduma kwa mtumiaji
	Kushiriki data na Wahusika wengine	Washirika na/au maajenti wanaohusika katika utoaji wa bidhaa na huduma; Mashirika ya utekelezaji wa sheria / usimamizi
	Teknolojia za ufuutiliaji/ vidakuzi vya tovuti	GPS / Vidakuzi vya tovuti
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Ingawa inapatikana nchini Uganda, haijabainishwa mahali ambapo data huhifadhiwa

MoneyMate Uganda <sup>461</sup>	Data inayokusanya na kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa za programu zinazotakikana	Programu hii inaweza kufikia:  Hali ya simu na utambulisho Miunganisho ya mitandao
	Data ya Mtumiaji Inayokusanya	Jina la mtumiaji, nambari ya mtumiaji wa simu, nambari ya kitambulisho, nambari ya simu ya mkononi, nambari ya simu ya jamii, anwani ya mawasiliano, Kampuni au Shinika Lililosajiliwa (kwa mashirika ya biashara)
	Maelezo yanayokusanya kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Kitambulisho cha kifaa
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Watoa huduma wasiojulikana
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kushughulikia maombi / kufanya shughuli za kifedha
	Kushiriki data na Wahusika wengine	Watoa huduma wasiojulikana
	Teknolojia za ufuutilaji/ vidakuzi vyatovuti	GPS / Vidakuzi vyatovuti
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Uganda

Numida - Business Loans <sup>462</sup>	Data inayokusanya na kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa za programu zinazotakikana	Programu hii inaweza kufikia:  Data ya mahali (inayotokana na GPS na mtandao) Maudhui ya hifadhi ya kifaa Kamera Kitambulisho cha kifaa na maelezo ya mazungumzo ya simu Miunganisho ya mitandao
	Data ya Mtumiaji Inayokusanya	Jina, kitambulisho, nambari ya simu/maelezo ya biashara (kwa biashara)

461 <https://play.google.com/store/apps/details?id=com.moneymateuganda.mmg>

462 [https://play.google.com/store/apps/details?id=com.numidatech.numida&hl=en\\_US&gl=US](https://play.google.com/store/apps/details?id=com.numidatech.numida&hl=en_US&gl=US)

Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	Kitambulisho cha Kifaa / Mfumo wa Uendeshaji (OS)
Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	Ofisi za rekodi za mikopo
Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Kutoa na kuboresha huduma zetu. Kutoa matangazo mahususi Kuwasiliana na mtumiaji
Kushiriki data na Wahusika wengine	Ofisi za rekodi za mikopo Wafanyakazi na wauzaji wa bidhaa
Teknolojia za ufuutiliaji/ vidakuzi vya tovuti	GPS / Vidakuzi vya tovuti
Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	Data ya binafsi huhifadhiwa nchini Uganda lakini inaweza kushirikiwa na, na kuchakatwa na wafanyakazi wa ndani au nje ya nchi ya Uganda

## Uchanganuzi wa Programu za Mikopo ya Kulipwa Siku ya Kupokea Mshahara kwa kuzingatia Mfumo wa Usimamizi

Katika kipindi kilichotangulia enzi ya ukuaji wa kasi wa mfumo wa Teknolojia ya Fedha nchini Uganda, wasimamizi walitunga sheria nyingi.

Hizi zinajumuisha Sheria za Shughuli za Kifedha za Kielektroniki (Electronic Transactions Act (2011),<sup>463</sup> Sheria ya kudhibiti matumizi, usalama, uvezeshaji na udhibiti wa mawasiliano na shughuli za kifedha za kielektroniki, kuhimiza matumizi ya huduma za serikali za mtandaoni na masuala husika; Sheria ya Matumizi Mabaya ya Kompyuta (Computer Misuse Act (2011),<sup>464</sup> Sheria inayodhibiti usalama na ulinzi wa shughuli za kifedha za kielektroniki na mifumo ya mawasiliano ili kuzuia ufikiaji wa kinyume cha sheria, matumizi mabaya au kutumiwa visivyo; Sheria ya Mikataba (Contracts Act (2010);<sup>465</sup> Sheria ya Sahihi za Kielektroniki (Electronic Signatures Act (2011);<sup>466</sup> na Mwongozo wa Huduma ya Kutuma na Kupokea Pesa Kupitia Simu za Mkononi wa Benki ya Uganda (Bank of Uganda (BoU) Mobile Money Guidelines (2013)<sup>467</sup>

Licha ya sheria hizi mbalimbali kutoweza kushughulikia vikwazo vya, au kuendeleza, shughuli za mifumo dijitali ya malipo au maendeleo ya baadaye, kinadharia, zilionekana kuwapa wadau namna fulani ya ‘ulinzi’.

Katika juhudzi za kutoachwa nyuma katika maendeleo ya kiteknolojia katika sekta ya dijitali, sheria za ziada zilizotungwa ili kudhibiti mfumo unaonawiri wa teknolojia ya fedha zimepitishwa hivi karibuni. Sheria ya Mfumo wa Kitaifa wa Malipo (National Payments System Act (2020)<sup>468</sup> inalenga kutoa ulinzi na ufanisi wa mifumo ya malipo, ili kuendeleza kazi za Benki

463 <https://ict.go.ug/2019/12/03/the-electronics-transactions-act-2011/>

464 <https://ict.go.ug/2019/12/03/the-computer-misuse-act-2011/>

465 <https://commons.laws.africa/akn/ug/act/2010/7/eng@2010-05-28.pdf>

466 <https://www.nita.go.ug/publication/electronic-signatures-act-2011-act-no-7-2011>

467 <https://www.bou.or.ug/bou/bouwebsite/FinancialInclusion/innovations.html>

468 [https://www.bou.or.ug/bou/bouwebsite/bouwebsitecontent/acts/supervision Acts\\_Regulations/Payment-Systems-Act/The-National-Payments-Systems-Act-2020.pdf](https://www.bou.or.ug/bou/bouwebsite/bouwebsitecontent/acts/supervision Acts_Regulations/Payment-Systems-Act/The-National-Payments-Systems-Act-2020.pdf)

Kuu (Central Bank) kuhusiana mifumo ya malipo. Sheria ya Maajenti wa Mifumo ya Kitaifa ya Malipo (National Payment Systems Agents Regulations (2021)<sup>469</sup> inalenga kulainisha sekta ya kutoa leseni kwa maajenti wa huduma ya kutuma na kupokea pesa kuitopia simu za mkononi. Sheria ya Mifumo ya Kitaifa ya Malipo (Majaribio) (National Payment Systems (Sandbox) Regulations (2021),<sup>470</sup> kwa upande mwine, inatoa mfumo wa mafaribio wa ‘kanuni ndogo’ kwa bidhaa na huduma bunifu za fedha, miundo ya biashara au mbinu za utoaji wa huduma katika mfumo wa mifumo ya malipo.

Sheria ya Faragha na Ulinzi wa Data (Data Protection and Privacy Act)<sup>471</sup> ilipitishwa mnamo tarehe 25 Februari 2019 lakini ilianza kutumika mnamo tarehe 3 Mei 2019. Sheria hii inadhibiti ukusanyaji na uchakataji wa maelezo ya binafsi. Inatumika kwa mtu, taasisi au shirika lolote la umma ambalo hukusanya, kuchakata, kuhifadhi au kutumia data ya binafsi ndani au nje ya nchi ya Uganda.

Kwa wahusika wanaoishi nje ya nchi ya Uganda, Sheria inatumika tu kwa data ya binafsi inayohusiana na naia wa Uganda.

## **Haki ya Faragha**

Kukiwa na kanuni mbalimbali zilizowekwa, kati yazo, Sheria ya Faragha na Ulinzi wa Data ya Uganda, kampuni za Programu za mikopo zinaonekana kuwa zimejumuisha kanuni za kuzingatia masuala ya faragha kuanzia mwanzo wa ubunifu wa bidhaa na huduma zao katika juhudui ya kudumisha faragha na usiri wa maelezo ya binafsi yanayokusanywa.

## **Uwazi**

Kampuni za Programu za mikopo zinabainisha kwa uwazi mbinu za ukusanyaji wa data binafsi; ukusanyaji, kuhifadhi, kushiriki na wahusika wengine na mbinu za usimamizi za kuhakikisha usalama wa data ya binafsi iliyokusanywa, hatua ambayo inatii kanuni ya utathmini wa athari ya ulinzi wa data.

## **Haki ya Kufikia na Kufuta Data ya Binafsi**

Kifungu cha 35 cha Sheria ya Faragha na Ulinzi wa Data (Data Protection and Privacy Acts) kinabainisha Haki ya ufikiaji wa maelezo ya binafsi yanayohifadhiwa na mdhibiti wa data. Mmiliki wa data ana haki ya kuomba kurekebishwa kwa data yake ipasavyo. Hata hivyo, (mmiliki wa data), lazima atimize masharti ya uthibitishaji wa utambulisho, ambapo mmiliki wa data anapaswa kutoa chochote kati vitu vifuatavyo - (a) kadi ya kitambulisho cha kitaifa au kadi ya kitambulisho cha mgeni; (b) pasipoti au hati yoyote ya usafiri; au (c) leseni ya udereva. Kwa upande wake, mdhibiti wa data anapaswa kujulisha mmiliki wa data kuhusu uamuzi ulioafikiwa ndani ya siku saba baada ya kupokea ombi.

Katika sheria na masharti yake ya mteja, kampuni ya MTN inaeleza kwamba mtu yeyote anayewasilisha maelezo yoyote kwa kampuni ya MTN kuitopia Mfumo wa Huduma ya Kutuma na Kupokea Pesa Kuitopia Simu za Mkononi (Mobile Money System) anaweza kupewa haki za maelezo hayo. Taarifa inaongeza kwamba kampuni ya ‘MTN imebuni mifumo ambayo inawezesha ufikiaji na kurekebishwa kwa maelezo yaliyowasilishwa kwa kampuni’.<sup>472</sup> Huduma zingine, Airtel Money, Money Mate na Numida, hazitoi maelezo yoyote kuhusu hatua zinazochukua kuhusiana na kanuni hii.

469 [https://www.bou.or.ug/bou/bouwebsite/bouwebsitecontent/acts/supervision\\_acts\\_regulations/Payment-Systems-Regulations/The-National-Payment-Systems-Agents-Regulations-2021.pdf](https://www.bou.or.ug/bou/bouwebsite/bouwebsitecontent/acts/supervision_acts_regulations/Payment-Systems-Regulations/The-National-Payment-Systems-Agents-Regulations-2021.pdf)

470 [https://www.bou.or.ug/bou/bouwebsite/bouwebsitecontent/acts/supervision\\_acts\\_regulations/Payment-Systems-Regulations/The-National-Payment-Systems-Sandbox-Regulations-2021.pdf](https://www.bou.or.ug/bou/bouwebsite/bouwebsitecontent/acts/supervision_acts_regulations/Payment-Systems-Regulations/The-National-Payment-Systems-Sandbox-Regulations-2021.pdf)

471 Sheria ya Faragha na Ulinzi wa Data Binafsi ya Uganda <https://ict.go.ug/wp-content/uploads/2019/03/Data-Protection-and-Privacy-Act-2019.pdf> <<https://www.nita.go.ug/sites/default/files/publications/Data%20Protection%20and%20Privacy%20Act%20No.%209%20of%202019.pdf>> ilifikiwa tarehe 23 Julai 2021.

472 <https://www.mtn.co.ug/wp-content/uploads/2019/10/MTN-MOBILE-MONEY-Consumer-Terms-and-Conditions-0519.pdf>

# Zimbabwe



## Maelezo ya Nchi

Zimbabwe, inayojulikana pia kama Jamhuri ya Zimbabwe, inapatikana katika eneo la Kusini mwa Afrika.<sup>473</sup> Inapakana na mataifa ya Afrika Kusini, Botswana, Zambia na Msumbiji.<sup>474</sup> Ina ukubwa wa 390,757 km na ina idadi ya watu milioni 15.<sup>475</sup> Jiji lake kuu ni Harare na lugha za Kiingereza, Kishona, Kindebele ndizo zinazozungumzwa sana.<sup>476</sup>

473 Britannica <https://www.britannica.com/place/Zimbabwe>

474 Britannica <https://www.britannica.com/place/Zimbabwe>

475 Zimbabwe <https://www.nationsonline.org/oneworld/zimbabwe.htm>

476 Zimbabwe <https://www.nationsonline.org/oneworld/zimbabwe.htm>

## Ulinzi wa Data Nchini Zimbabwe

Kuzuka kwa teknolojia kumesababisha maendeleo makubwa katika sekta ya fedha nchini Zimbabwe.

Kumezua teknolojia ya fedha, ambayo imebadilisha sekta hiyo na kusababisha uwezo wa kufikia huduma za fedha ambapo watu wasio na akaunti za benki wanaweza kupata huduma za fedha. Sekta ya huduma za mikopo ni kipengele muhimu katika mfumo wa teknolojia ya fedha, ambayo inawezesha kufikia haraka na kwa rahisi huduma ya mkopo mtandaoni bila dhamana.

Huduma ya mikopo dijitali nchini Zimbabwe, hata hivyo, bado hajathibitiwa. Sheria ya usimamizi wa mifumo ya fedha inashughulikia tu taasisi za fedha kama vile benki, mashirika ya ujenzi na kampuni za bima.<sup>477</sup> Sheria ya Benki (Banking Act) inadhibiti mamlaka ya Reserve Bank of Zimbabwe ya kutoa leseni, kusimamia na kudhibiti mashirika ya kupokea amana na kutoa mikopo.<sup>478</sup> Hatua hii inaacha pengo kubwa kuhusiana na udhibiti wa desturi za mifumo ya kukopesha pesa.

Hakuna pia sheria inayodhibiti mbinu za ulinzi wa data za mifumo dijitali ya kukopesha pesa. Kwa sasa Zimbabwe ina Mswada wa Sheria ya Ulinzi wa Data (Data Protection Bill) ambao bado haujapitishwa kuwa sheria. Seneti hivi karibuni ilipitisha Mswada huo lakini ulirejeshwa

477 Kifungu cha 2 (a)(iii), Sheria ya Marekebisho ya Sekta ya Benki (Banking Amendment Act), ya 2015 <https://www.rbz.co.zw/documents/acts/Banking%20Amendment%20Act,%202015.pdf>

478 Fsd Africa, Utafiti wa Mfumo wa Teknolojia ya Fedha Nchini Zimbabwe (Machi 2020) ukurasa wa 27 [https://www.fsdafrica.org/wp-content/uploads/2020/03/Zim-Fintech-Report-25.03.20\\_FINAL.pdf](https://www.fsdafrica.org/wp-content/uploads/2020/03/Zim-Fintech-Report-25.03.20_FINAL.pdf)

baadaye kwa bunge ili kufanyiwa manekebisho.<sup>479</sup> Haki ya fanagha imetolewa kwenye katiba na baadhi ya sheria za sekta, kama vile Sheria ya Uhuru wa Kuchapisha na Kupokea Maelezo (Freedom of Information Act), ambayo inasimamia mbinu za ulinzi wa data za mashirika ya umma.<sup>480</sup>

Ukosefu wa sheria ya ulinzi wa data nchini Zimbabwe unaacha mbinu za ulinzi wa data za programu za mikopo bila kudhibitiwa na unahatarisha zaidi watumiaji wa programu hizo. Utafiti huu unachunguza data inayokusanywa na programu tatu maarufu nchini Zimbabwe, yaani, GetBucks, MyBucks na eShagi. Unatoa pia mwongozo kuhusu mbinu za ulinzi wa data ambazo programu hizi zinapaswa kufuata kulingana na mbinu bora za kimataifa.

### **Muhtasari wa Data Inayokusanywa na Programu za Mikopo Dijitali**

GetBucks <sup>481</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	<p>Nambari ya kitambulisho, nambari ya mawasiliano, anwani ya mtaa, anwani ya barua pepe na anwani ya IP</p> <p>Mfumo huu hupokea na kurekodi maelezo ya mtumiaji yaliyochakatwa kutoka kwenye kivinjari cha mtumiaji kwenye seva zake baada ya mtumiaji kutumia tovuti. Maelezo haya yanajumuisha:</p> <p>Anwani ya IP</p> <p>Maelezo ya vidakuzi</p> <p>Ukurasa uliotafutwa na mtumiaji</p> <p>“Programu ya GetBucks inaweza pia kuzuia, kufuutilia, kuchuja, kusoma, kufuta na kufichua mawasiliano yoyote yanayofanywa kupitia mfumo wake wa mawasiliano. Hii ni pamoja na, wala si tu kufuutilia anwani za Internet Protocol (Anwani za IP) za watumiaji, na watumiaji wanakubali kwamba programu ya GetBucks inaweza kuomba maelezo yao ya binafsi kutoka kwa Watoa Huduma wao wa Intaneti (Internet Service Provider) kwa sababu yoyote ambayo tovuti inaona kuwa inafaa ili kuhakikisha uhusiano salama na wa kuaminika na mtumiaji”.</p>
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji/ Matumizi ya tovuti	<p>Mfumo huu hupokea na kurekodi maelezo ya mtumiaji yaliyochakatwa kutoka kwenye kivinjari cha mtumiaji kwenye seva zake baada ya mtumiaji kutumia tovuti. Maelezo haya yanajumuisha:</p> <p>Anwani ya IP</p> <p>Maelezo ya vidakuzi</p> <p>Ukurasa uliotafutwa na mtumiaji</p>

479 Zimbabwe Yakaribia Kupitisha Sheria ya Ulinzi wa Data <https://iapp.org/news/a/zimbabwe-on-the-cusp-of-finalizing-data-protection-law/#> Mswada Wenye Utata wa Sheria ya Ulinzi wa Faragha na Usalama wa Mtandaoni Nchini Zimbabwe Warudishwa Bungeni <https://www.grcworldforums.com/global/zimbabwe-controversial-cyber-security-and-privacy-bill-sent-back/2325.article>

480 Zimbabwe: Muhtasari wa Ulinzi wa Data <https://www.dataguidance.com/notes/zimbabwe-data-protection-overview>

481 Sera ya Faragha ya Programu ya GetBucks <https://zw.getbucks.com/site-policy>

	Jinsi maelezo ya mtumiaji yanavyokusanywa	Maelezo ya mtumiaji hukusanywa kutokana na matumizi ya tovuti
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	
	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine/ Ufichuzi wa Maelezo	Programu ya GetBucks hushiriki maelezo ya binafsi ya mtumiaji na wahusika wengine wafuatao: Watangazaji - hufichua maelezo ya mtumiaji kwa madhumuni ya kutoa matangazo Watoa huduma au maajenti - hufichua maelezo ya mtumiaji kwa watoa huduma kwa ajili ya kutoa huduma Mashirika ya utekelezaji wa sheria - hufichua maelezo ya mtumiaji panapohitajika kwa amri ya mahakama au sheria Inaweza kufichua anwani ya IP ya mtumiaji panapohitajika na sheria Washirika Washirika wa kibiashara katika hali za; kubadilishwa kwa umiliki, miungano, ununuzi au uuzaji wa mali za biashara Wafanyakazi - wanapofanya kazi zao Wahusika wengine wakati wa kutatua au kuchunguza malalamiko <sup>482</sup>
	Teknolojia za ufuatiliaji/ vidakuviya tovuti	
	Uhamishaji wa data kimataifa	Mfumo huu unaweza kutuma au kuhamishia data ya binafsi ya mtumiaji kwenye nchi zingine. Nchi hizi zinaweza kuwa na sheria za ulinzi wa data ambazo si kali zaidi.
	Kuhifadhiwa kwa maelezo/ ulinzi wa data	“Hutumia mbinu za ulinzi za kiwango cha juu ili kulinda data ya binafsi inayohifadhi.”
MyBucks <sup>483</sup>	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	

482 Sera ya Faragha ya Programu ya GetBucks: Kifungu cha Ufichuzi <https://zw.getbucks.com/site-policy>  
 483 Sera ya Faragha ya MyBucks <https://corporate.mybucks.com/privacy>

	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	Huchakata maelezo/ data ifuatayo ya mtumiaji: Data ya matumizi: Anwani ya IP, data ya mahali, aina ya kivinjari na toleo, mfumo wa uendeshaji, chanzo cha uelekezaji, muda wa kuvinjari tovuti, kurasa zilizotazamwa na njia za matumizi ya tovuti, kipindi cha matumizi, mara za mtumiaji kutembelea tovuti na mtindo wa matumizi ya huduma. <sup>484</sup> Data ya akaunti ya mtumiaji: jina la mtumiaji na anwani ya barua pepe Data ya wasifu wa mtumiaji: jina, anwani, nambari ya simu, anwani ya barua pepe, picha ya wasifu, jinsia, tarehe ya kuzaliwa, hali ya ndoa, mambo yanayokuvutia na unayopenda, maelezo ya elimu na maelezo ya ajira Data ya ajira ya mtumiaji: jina, anwani, nambari ya simu, anwani ya barua pepe, picha ya wasifu, jinsia, tarehe ya kuzaliwa, hali ya ndoa, mambo yanayokuvutia na unayopenda, historia ya ajira, elimu, vyeti, uzoefu, maelezo ya binafsi, mahali na maelezo ya mshahara Data ya huduma ya mtumiaji: data inayohusiana na jinsi mtumiaji anavyotumia huduma ya MyBuck Data ya machapisho: data inayotokana na maelezo yaliyochapishwa na mtumiaji kwenye tovuti ya MyBucks. Data ya maombi: data inayotokana na maombi ya mtumiaji kuhusu bidhaa, huduma au nafasi ya kazi ya MyBucks Data ya uhusiano wa mteja: Inajumuisha; jina, mwajiri, cheo cha kazi, maelezo ya mawasiliano, maelezo yaliyo kwenye mawasiliano yanayofanywa kati ya MyBucks na mtumiaji au mwajiri wa mtumiaji. Data ya shughuli za kifedha: maelezo yanayohusiana na shughuli za kifedha ambazo mtumiaji anafanya na MyBucks kupitia tovuti Data ya arifa: inajumuisha maelezo yanayohusiana na usajili wa mtumiaji kwenye huduma ya MyBucks ya kupokea arifa za barua pepe. Data ya mawasiliano: maelezo yanayohusiana na mawasiliano yanayofanywa kati ya mtumiaji na MyBucks Maelezo yanayochakatwa kupitia vidakuzi Rekodi za mazungumzo ya simu Mapendeleo ya mtumiaji ya matangazo Anwani ya IP ya mtumiaji
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	
	Jinsi maelezo ya mtumiaji yanavyokusanywa	
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	

	Jinsi Programu inavyotumia maelezo ya mtumiaji	Programu ya MyBucks hutumia maelezo ya mtumiaji kwa madhumuni yafuatayo: Kutoa huduma za MyBucks na shughuli zake za ndani Kutii wajibu wa kisheria na usimamizi Kutathmini uwezo wa mtumiaji wa kulipa mkopo Kuwapa watumiaji huduma zinazowafaa Kuwapa watumiaji huduma zinazowafaa za ubora wa juu Kuipa MyBucks ufahamu wa biashara yake na kuboresha huduma zake Kuhakikisha mifumo ya MyBucks inafanya kazi vizuri Kuhakikisha kuwa maelezo yanayochakatwa kuhusu watumiaji ni sahihi Kuzuia uhalifu kama vile ulaghai Kutoa huduma za malipo Kudai madeni Kudumisha nekodi za biashara Kutangaza bidhaa na huduma za MyBucks Kuboresha ubora wa huduma zinazotolewa na MyBucks Kuhakikisha mifumo ya MyBucks inafanya kazi vizuri Kulinda usalama wa mifumo ya MyBucks Kutatua malalamiko Kutetea madai ya kisheria Kutii wajibu wa kisheria <sup>485</sup>
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	Hufichua maelezo ya mtumiaji kwa wahusika wafuatao: Wanachama wa kikundi cha MyBucks Watoa huduma za bima na wataalamu wa ushauri Watoa huduma, yaani, watoa huduma za malipo, mashirika ya ukusanyaji wa madeni nk Watoa huduma za IT, wakaguzi, mashirika ya matangazo, washauri wa masuala ya kodi, watoa huduma wanaofutilia matumizi ya tovuti ya MyBucks Ajenti wa mtumiaji Benki au taasisi za fedha Mashirika ya utekelezaji wa sheria katika uchunguzi na uzuiaji wa uhalifu Kampuni/ mashirika ya sheria yanayotoa ushauni wa kisheria kwa MyBucks au kuiwakilisha katika kesi za mahakamani Watoa huduma za utafiti walioteuliwa kufanya utafiti wa soko Washirika wa kibiashara wakati wa mchakato wa kuuzwa, kuhamishwa au kununuliwa kwa biashara ya MyBuck Wasimamizi na mamlaka za serikali
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Teknolojia za ufuutiliaji/ vidakuzi vyatovuti	

	Uhamishaji wa data kmataifa/ Uhamishaji wa data nje ya nchi	MyBucks huhamishia data ya mtumiaji kwenye nchi zingine.
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	
eShagi <sup>486</sup>  -Programu ya eShagi haina sera ya faragha -Vile vile haina sheria na masharti	Maelezo Yanayokusanywa na Kuchakatwa na Programu	
	Ruhusa zinazotakikana	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwa mtumiaji	
	Maelezo yanayokusanywa kutoka kwenye kifaa cha mtumiaji	
	Jinsi Programu ya Branch hukusanya maelezo	
	Maelezo yanayopokewa kutoka kwa wahusika wengine	
	Matumizi ya maelezo ya mtumiaji	
	Maelezo yanayoshirikiwa na wahusika wengine	
	Muda wa wahusika wengine kufikia data	
	Teknolojia za ufuutiliaji/ vidakuzi vyatovuti	
	Uhamishaji wa data kimataifa	
	Jinsi Programu inavyohifadhi maelezo ya mtumiaji	

## Uchanganuzi wa Mbinu za Ulinzi wa Data za Programu

### Udhibiti wa Mtumiaji

Mifumo djijitali ya kukopesha pesa inapaswa kuruhusu watumiaji kuwa na uhuru wa kudhibiti data yao. Inapaswa kuwezesha watumiaji kujua aina ya data ya binafsi inayochakatwa,

jinsi maelezo hayo yanavyotumiwa, wahuksika ambao data itashirikiwa nao na jinsi itakavyoshughulikiwa.

Inapaswa pia kutoa njia za watumiaji kufikia data yao, kuomba kuinekebisha au kuisasisha na hata kuifuta. Hii ni muhimu kwa sababu watumiaji wana haki ya kudhibiti data yao, na hatua yoyote inayochukuliwa kwa data yao inapaswa kuchukuliwa kwa idhini yao. Programu ya mikopo ya GetBucks inaonekana kuwa haitoi hakikisho la kufurahia kikamilifu haki hii. Sera yake inaruhusu tu watumiaji kurekebisha au kusasisha data yao.<sup>487</sup> Hakuna njia ya watumiaji kufikia data yao au hata kuifuta wakati ambapo hawahitaji tena huduma. Watumiaji pia hawawezi pia kuomba kuhamisha data yao. Programu ya MyBucks, kwa upande mwengine, inawahakikishia watumiaji haki hizi. Chini ya sera yake, watumiaji wana haki ya kufikia, kurekebisha, kufuta na kuhamisha data yao.<sup>488</sup>

## **Idhini**

Watumiaji watoa idhini yao kwa sera za faragha kwa msingi wa ‘unaweza kukubali au kukataa’. Programu hizi hukusanya data ya ziada na kuwaacha watumiaji bila chaguo lingine bali kukubali sheria na masharti kwa sababu ya ‘haja’ yao ya kuhitaji huduma. Chukulia, kwa mfano, Sera ya Faragha ya GetBucks “Kifungu cha Kuzuia na Kufuatilia”. Kifungu hiki kinaleza kwamba mfumo “unaweza kuzuia, kufuatilia, kusoma, kufuta na kufichua mawasiliano yoyote yanayofanywa kupitia mfumo wake. Hii ni pamoja na, wala si tu kufuatilia anwani za Internet Protocol (anwani za IP) za mtumiaji, na kuomba maelezo ya binafsi ya mtumiaji kutoka kwa Mto Huduma wake wa Intaneti (Internet Service Provider) kwa sababu yoyote ambayo tovuti inaona kuwa inafaa ....”

## **Kikomo cha Madhumuni**

Programu za mikopo dijitali zinapaswa kubainisha kwa watumiaji madhumuni ya ukusanyaji wa data na matumizi yanayopendekezwa.<sup>489</sup> Zinapaswa pia kuhakikisha kuwa zinachakata tu data inayohitajika kwa utoaji wa huduma zake.<sup>490</sup> Kwa kufanya hivyo, zinapaswa kuhakikisha kuwa zinachakata data ya binafsi ambayo ni ya kutosha, inayohusika na isiyo ya ziada. Programu zilizochunguzwa inaonekana kuwa zinakusanya data nyingi kuliko inavyohitajika kwa madhumuni ya kutoa mikopo dijitali. Programu ya MyBucks huchakata maelezo ya mtumiaji kama vile mambo yanayovutia mtumiaji na anayopenda, hali ya ndoa, historia ya ajira, uzoefu wa kikazi na maelezo mengine ambayo hayahusiki kwa madhumuni ya kutoa mikopo dijitali.<sup>491</sup>

## **Uhamishaji wa Data Kimataifa**

Programu za kukopesha pesa zilizochunguzwa huhamishia data ya mtumiaji kwenye nchi zingine. Programu kama vile GetBucks, kwa mfano, huhamishia data ya binafsi ya mtumiaji kwenye nchi zingine ambazo hazina sheria kali za ulinzi wa data.<sup>492</sup> Uhamishaji huu unahatarisha zaidi usalama wa data ya mtumiaji.

Programu hizi zinapaswa kuhakikisha kuwa data ya binafsi inayohamishiwa nje ya nchi imelindwa. Kwa kufanya hivyo, zinapaswa kuweka mbinu mwafaka za ulinzi ili kulinda data na kuhakikisha kuwa data inahamishiwa kwenye nchi zilizo na sheria za kutosha za ulinzi wa data.

487 Sera ya Faragha ya Programu ya GetBucks <https://zw.getbucks.com/site-policy>

488 Sera ya Faragha ya Programu ya MyBucks: Kifungu cha 10 <https://corporate.mybucks.com/privacy>

489 Privacy International - ukurasa wa 39

490 Ripoti ya Kudhibiti Ukusanyaji wa Data (Data Minimization Report) - ukurasa wa 4

491 Sera ya Faragha ya Programu ya MyBucks: Kifungu cha 3 ‘Matumizi ya Data ya Binafsi’ <https://corporate.mybucks.com/privacy>  
Sera ya Faragha ya Programu ya GetBucks: Uhamishaji wa Data Nje ya Nchi <https://zw.getbucks.com/site-policy>

## Kushiriki Data ya Mtumiaji na Wahusika Wengine

Programu za mikopo dijitali zinapaswa kujulisha watumiaji wahusika wengine ambao zinakusudia kushiriki nao data yao. Zinapaswa kuweka wazi katika sera zake data ambayo zinakusudia kushiriki na wahusika wengine, kipindi ambacho wahusika wengine watafikia data, na mbinu za ulinzi zilizowekwa ili kulinda data inayoshirikiwa na wahusika wengine.

Programu zilizochunguzwa hazijabainisha suala hili katika sera zake za faragha. Programu ya Getbucks inabainisha tu wahusika wengine ambao inashiriki nao data na hakuna maelezo kuhusu data inayoshirikiwa na wahusika wengine, kipindi ambacho watafikia data au mbinu za ulinzi zilizowekwa.<sup>493</sup> Programu ya MyBucks, kwa upande mwingine, haielezi kwa uwazi wahusika wengine ambao inashiriki nao maelezo.<sup>494</sup> Programu ya eShagi haina sera ya faragha, hali ambayo inawaacha watumiaji bila maelezo kuhusu wahusika wengine ambao hufikia data yao.

## Kuhifadhiwa kwa Data ya Mtumiaji

Programu zinazochunguzwa katika utafiti huu hazibainishi vigezo ambavyo zinatumia kubaini kipindi ambacho zitahifadhi data ya mtumiaji. Hazielezi pia watumiaji muda mahususi ambao zitahifadhi data yao. Maelezo haya ni muhimu kwa watumiaji wa programu hizi ili kuwasaidia kujua muda ambao programu hizi zitafikia data yao na njia ambazo wanaweza kutumia ili kuondoa data yao kwenye programu hizi.

---

<sup>493</sup> Sera ya Faragha ya Programu ya GetBucks: Kifungu cha Ufichuzi <https://zw.getbucks.com/site-policy>

<sup>494</sup> Sera ya Faragha ya MyBucks <https://corporate.mybucks.com/privacy>

# Hitimisho

Si siri kwamba programu dijitali za fedha zimeimarika na kuzidi kupanya katika mashirika ya benki, hasa katika maeneo ya mashambani ya nchi za Kiafrika. Hata hivyo, katika hali ya programu dijitali za mikopo, huduma hii inaonekana kuwa zawadi isiyo ya kutegemewa, kwa sababu programu hizi hukusanya kiasi kikubwa cha data ya binafsi bila kubainisha wazi jinsi zitakavyoishughulikia, na wadhibiti wanaonekana kuwa wameshindwa au hawana habari kuhusu jinsi ya kudhibiti ukusanyaji na matumizi ya data.

Katika nchi za kwanza zilizoanzisha kanuni za ulinzi wa data kama vile Kepuvede (Cape Verde), sekta ya fedha huchunguzwa jinsi inavyoshughulikia data ya wateja. Hata hivyo, hatua hii haijakomesha matumizi mabaya ya data hii kwa sababu hakuna uwazi kuhusu kiwango cha mamlaka ya udhibiti ambacho Shirika la Ulinzi wa Data limepewa ili kudhibiti programu dijitali. Sasa imekuwa muhimu zaidi kwa sheria katika nchi zote za Afrika kuonyesha uwazi na maelezo kuhusu:

Iwapo programu dijitali za fedha zinapaswa kufuata viwango sawa vya ushughulikiaji wa data kama vya benki za kawaida;

Mfumo wa udhibiti unaohitajika ili kusaidia na kulinda data ya mtumiaji kutokana na sekta bunifu na ya inayozidi kukua ya teknolojia ya fedha.

Shirika la Paradigm Initiative linaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhimiza suala la faragha na ulinzi wa data, na kuchangia katika kubuni mbinu za kufunga mianya katika nchi zilizoangaziwa, nakala za ripoti hii zitatolewa kwa Mashirika ya Ulinzi wa Data yanayohusika ili kuchukua hatua, na kwa washirika wengine kwa kazi inayohitajika ya uhamasishaji.

